

Historia ya kushushwa Qur-an 96:1 - 5, inatukumbusha na kutufunza kuwa Mtume (s.a.w) alianza kushushiwa wahy kwa kupewa amri ya kusoma. Hivyo, hapana shaka kabisa kuwa Elimu ndio Faradhi ya kwanza inayopaswa kutekelezwa na kila Muislamu tangu zama za Mtume (s.a.w) hadi sasa.


Kusoma au kutafuta elimu kumefanya kuwa Faradhi ya kwanza ili kumuezesha mja kumjua Mola wake na kumpatia ujuzi wa kutosha juu ya kanuni na sheria alizoziweka Allah (s.w) zikifuatwa katika kila kipengele cha maisha ya kila siku, hupatikana uadilifu na amani ya kweli katika jamii.

Hii ni juzu ya Saba ya maarifa ya Uislamu katika mfululizo wa juzu 7 za masomo kwa Darasa la Watu Wazima unaokusudia kumuwezesha mja na jamii kufikia kilele hicho.

Mfululuzo huu wa masomo katika juzu ya 7 ni:

1. Lengo la Maisha ya Mwanadamu
2. Nguzo za Uislamu
3. Qur-an na Sunnah
4. Familia ya Kiislamu
5. Jamii ya Kiislamu
6. Historia ya Kuhuisha Uislamu
7. Kuhuisha Uislamu katika Jamii

KUHUISHA UISLAMU KATIKA JAMII



Maarifa ya Uislamu

Darasa la Watu Wazima

Juzuu 7
(Toleo la Pili)

KUHUISHA UISLAMU KATIKA JAMII

Islamic Propagation Centre

Maarifa ya Uislamu
Darasa la Watu Wazima
Juzuuy ya 7 :Kuhuisha Uislamu katika Jamii

©Islamic Propagation Centre (IPC)

Waandishi/Wasambazaji
Islamic Propagation Centre (IPC)
S.L.P 55105, Dar es Salaam, Tanzania.

Toleo la Pili, 29, May, 2009
Nakala 1000

Mchapaji: Afroplus Industries(Ltd)
P.O.Box 32427, Tel 022-2773751
Dar es salaam Tanzania.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

NENO LA AWALI

Shukrani zote anastahiki Allah (s.w), Bwana Mlezi wa Walimwengu wote. Rehma na Amani zimuendee Muhammad (s.a.w) na wale wote wanaofanya jitihada za makusudi za kuudhihirisha na kuutawalisha Uislamu katika jamii pamoja na kuchukia kwa Washirikina.

Tunamshukuru tena Allah (s.w) kwa kutuwezesha kutoa toleo hili la pili la Juzu 7: **“KUHUISHA UISLAMU KATIKA JAMII”**, inayokamilisha mfululizo huu wa somo la Maarifa ya Uislamu Darasa la Watu Wazima. Toleo hili la pili lina mabadiliko makubwa kimpangilio na kimaudhui. Pamoja na Utangulizi juzuuhii ya toleo la pili itakuwa na Mada kuu zifuatazyo:

1. Haja ya Kusimamisha Uislamu katika jamii.
2. Kuandaliliwa Mtume (s.a.w) na Mafunzo yatokanayo.
3. Sifa za Mwanaharakati wa Kiislamu.
4. Maandalizi ya Kundi la Harakati.
5. Mbinu za Kulingania na Kusimamisha Uislamu katika jamii.
6. Mipango katika Harakati za Kiislamu.
7. Uongozi Bora katika Harakati za Kiislamu.
8. Mwongozo wa Kujifunza na Kuujua Uislamu kwa Wepesi.
9. Mbinu za Kufundisha kwa Lengo la Kumuandaa Khalifa wa Allah (s.w).

Ni tumaini letu kuwa, kwa Tawfiiq ya Allah (s.w), Mada hizi zikipitiwa kwa makini kinadharia na kisha zikaingizwa katika

utendaji hatua kwa hatua, zitawawezesha Waumini kuudhihirisha na hatimaye kuutawalisha Uislamu katika jamii yetu na jamii ya Ulimwengu kwa ujumla.

رَبَّنَا آءَنَا مِنْ لُذْنَكَ رَحْمَةً وَهَيْئَ لَنَا

مِنْ أَمْرِنَا رَشَدًا

“.....*Mola wetu! Tupe rehema zinazotoka kwako
na tutengenezee uongofu
katika kila jambo letu*”
(18:10)

YALIYOMO

| | |
|---|-------|
| Neno la awali | (iii) |
| Utangulizi: Dhana ya kuhuisha Uislamu katika Jamii | (x) |
| | |
| Sura ya kwanza | 1 |
| Haja ya kusimamisha Uislamu katika Jamii | 1 |
| | |
| Utangulizi | 1 |
| Maana ya kusimamisha Uislamu katika jamii | 3 |
| Umuhimu wa kusimamisha Uislamu katika Jamii | 6 |
| Kwanini ni muhimu kusimamisha | |
| Uislamu katika jamii | 14 |
| Ugumu wa kusimamisha Uislamu katika | |
| jamii uko wapi? | 26 |
| Kwanini Makafiri wanafanikiwa katika mambo yao | 30 |
| Kanuni ya Allah(s.w) kuhusu uongozi katika jamii | 34 |
| Zoezi la kwanza | 36 |
| Sura ya Pili | 37 |
| Kuandaliwa Mtume(s.a.w)namafunzo yatokanayo | 37 |
| | |
| Utangulizi | 37 |
| Zama za Jahiliyyah | 38 |
| Kuandaliwa Mtume(s.a.w) | 40 |
| Maandalizi ya Ki-ili-hamu | 41 |
| Mafunzo yatokanayo na maandalizi ya ki-ili-hamu | 48 |
| Maandalizi ya kimafunzo | 49 |
| Mafunzo yatokanayo na maandalizi ya kimafunzo | 53 |
| Zoezi la Pili | 61 |

| | |
|---|-----|
| Sura ya Tatu: | 62 |
| Mwanaharakati wa kiislamu | 62 |
| Utangulizi | 62 |
| Sifa za mwanaharakati wa kiislamu | 64 |
| Ujuzi sahihi juu ya Uislamu | 64 |
| Imani thabiti juu ya Uislamu | 65 |
| Tabia Njema (tabia ya utendaji) | 67 |
| Kusimamisha Uislamu kuwe ndio lengo kuu la maisha | 69 |
| Kutarajia malipo kutoka kwa Allah(s.a.w) | 70 |
| Kuwa na Subira | 72 |
| Kuwa na Hekima | 76 |
| Mafunzo na mazoezi ya kumuaanda mwanaharakati | 76 |
| Zoezi la tatu | 80 |
| Sura ya Nne | 81 |
| Kundi la Harakati za Kiislamu | 81 |
| Ni lipi kundi la Harakti | 81 |
| Umuhimu wa kuwepo kundi la Harakati | 81 |
| Sifa za kundi la Harakati | 83 |
| Kila mwanakundi kujipamba na sifa za Mwanaharakati | 84 |
| Mshikamano wa udugu na upendo | 84 |
| Kushauriana | 99 |
| Nidhamu | 102 |
| Kukusoana kwa nia njema na kwa njia nzuri | 102 |
| Kujiepusha na kujiona | 104 |
| Kujiepusha na Ria | 106 |
| Kuwa na Subira | 107 |
| Kuwa na Hekima | 108 |

| | |
|--|-----|
| Kuanzisha kundi la Harakati kama alivyofanya | |
| Mtume(s.a.w) | 108 |
| Nini Darasa Duara | 109 |
| Kazi za Darasa Duara | 110 |
| Mtaala wa Darasa Duara | 110 |
| Uongozi wa Darasa Duara | 112 |
| Kazi za viongozi wa Darasa Duara | 113 |
| Zoezi la Nne | 114 |
| Sura ya Tano | 116 |
| Mbinu za kulingania na kusimamisha | |
| Uislamu katika Jamii | 116 |
| Dhana ya kulingania Uislamu | 116 |
| Dhana ya kusimamisha Uislamu katika Jamii | 117 |
| Jukumu la kulingania na kusimamisha | |
| Uislamu katika jamii ni Amana kuu | 117 |
| Mbinu za kulingania Uislamu | 119 |
| Kuwepo mlinganiaji mwenye sifa stahiki | 119 |
| Kuwepo kundi la walinganiaji | |
| lenye sifa stahiki | 121 |
| Wawepo wenyе kulinganiwa | 125 |
| Kulingania kwa Hekima | 128 |
| Kulingania kwa mawaidha mazuri | 129 |
| Kujadiliana na watu kwa namna iliyo bora | 131 |
| Kutowakatia tamaa unaowalingania | 132 |
| Kuwafahamu maadui wa | |
| Uislamu na mbinu zao | 133 |
| Makafiri na Washirikina | 134 |
| Mayahudi na Wakristo | 139 |
| Wanafiki | 147 |
| Sheitwaani | 157 |
| Zoezi la Tano | 167 |

| | |
|---|-----|
| Sura ya Sita | 169 |
| Mipango katika Harakati za kiislamu | 169 |
| Maana ya mipango (Planning) | 169 |
| Umuhimu wa kuweka mipango | 169 |
| Aina ya mipango | 171 |
| Hatua za kufuata katika kupanga | 172 |
| Vigezo vya mpango madhubuti | 173 |
| Mipango ya kistratejia(strategic Planning) | 179 |
| Uoni na mwelekeo (Vision and Direction) | 184 |
| Zoezi la Sita | 186 |
| Sura ya saba: | |
| Uongozi Bora katika Harakati za Kiislamu | 187 |
| Nani kiongozi | 187 |
| Nani mtawala | 187 |
| Dhana ya Uongozi kwa mtazamo wa Uislamu | 187 |
| Uongozi wa Allah(s.w) | 189 |
| Uongozi wa Twaghuti | 189 |
| Sifa za kiongozi wa Kiislamu | 190 |
| Sifa za msingi za kiongozi wa kiislamu | 191 |
| Sifa za ziada za kiongozi Bora | 192 |
| Zoezi la Saba | 199 |
| Sura ya Nane | 200 |
| Muongozo wa kujifunza na kujua | |
| Uislamu kwa wepesi | 200 |
| Utangulizi | 200 |
| Kuweka ratiba ya kujisomea | 201 |
| Kujisomea kwa lengo kwa kufata Mtaala | 203 |
| Kusoma kwa njia ya mjadala(darasa duara) | 204 |
| Kujiunga na Elimu ya Kiislamu kwa Posta(EKP) | 205 |

| | |
|---|------------|
| Kusoma Qur'an kwa mazingatio | 206 |
| Zoezi la Nane | 208 |
| Sura ya Tisa: | 209 |
| Mbinu za kufundisha Uislamu kwa lengo la kumuandaa Khalifa | 209 |
| Utangulizi | 209 |
| Mbinu za kumuandaa Khalifa | 210 |
| Kuliweka bayana lengo la Elimu | 211 |
| Kutumia lugha nyepesi inayofahamika kwa wanafunzi | 213 |
| Kufafanua mada kwa aya au Hadith | 214 |
| Kutoa na kutumia mifano na vielelezo vyta kiislamu | 214 |
| Kuleta mazingatio ya Allah(s.w.) kupitia mada unazofundisha | 215 |
| Kukosoa Nadharia Potofu | 216 |
| Zoezi la Tisa | 217 |

Utangulizi

DHANNA YA KUHUISHA UISSLAMU KATIKA JAMII

Tunaposema **kuhuisha Uislamu katika jamii** hatuna maana ya kuongeza idadi ya Waislamu katika jamii. Waislamu wanaweza kuwa asilimia 99.99 lakini bado Uislamu usiwepo katika jamii. Kwa mfano nchi nyingi za Uarabuni ikiwemo Saudi Arabia ilipo Ka'abah, idadi kubwa ya wakazi wa nchi hizo, zaidi ya asilimia 99 ni Waislamu lakini bado Uislamu haujasimama katika nchi hizo. Tusiende mbali, turudi hapa Tanzania, asilimia 99 na zaidi ya wakazi wa Zanzibar ni Waislamu. Vile vile hapa Tanzania kuna idadi kubwa ya Waislamu ukilinganisha na watu wengine katika mikoa yote ya Pwani, Tabora na Kigoma. Aidha, idadi ya Waislamu ni kubwa sana takribani katika miji yote mikubwa ya mikoa ya Tanzania; kielelezo ni wingi wa misikiti katika miji hiyo na kufurika kwake katika siku za Ijumaa na hasa katika mwezi wa Ramadhani, lakini bado kijamii hapaoneshi kuwepo Uislamu katika mikoa na miji hiyo ya Waislamu.

Kinyume chake, Waislamu wanaweza kuwa wachache katika jamii kama asilimia (10%) tu hivi lakini bado wakaweza kudhihirisha Uislamu katika jamii yao. Mhadhiri maarufu wa "Biblia" duniani (wa ulinganisho wa Uislamu na Ukristo) duniani Al-marhuum Sheikh, Ahmed Deedat, wa Afrika ya Kusini, alishangazwa sana na hali ya Waislamu wa Tanzania, alipotembelea hapa mwaka 1981. Alishangaa kuona kuwa pamoja na wingi wa Waislamu, hasa Zanzibar, Uislamu haukuwa na athari yoyote katika jamii. Kwa mfano, wakati Sheikh Deedat anaonesha mshangao wake, alishikilia gazeti la "Daily News" lililokuwa na orodha ya wanaojiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo cha Ardhi na Chuo cha Maji. Alionesha kuwa katika wale wote waliochaguliwa kujiunga na Vyuo hivyo Waislamu walikuwa chini ya

asilimia(10%). Baada ya kutuonesha udhaifu huo, Sheikh Deedat alitugeukia tuliokuwa pale msikitini Mwembe chai katika hadhara ile na kutushangaa. “Waislamu wa Tanzania mnatatizo gani! Mmebakia kujivunia wingi lakini hamna athari yoyote katika jamii!! Sisi Afrika ya Kusini Waislamu ni asilimia mbili (2%) tu lakini jamii inahisi kuwepo kwetu!” Hivi ndivyo ilivyo katika historia ya Waislamu wa kweli. Kila walipokuwepo pamoja na uchache wao, athari yao ilionekana katika jamii hata kama hawajafikia uwezo wa kusimamisha Dola ya Kiislamu. Athari ya Mtume (s.a.w) na Maswahaba wachache aliokuwa nao katika kipindi cha Makka ilikuwa bayana katika jamii ya Maquraysh. Rejea maelezo ya Ja’affar mbele ya Mfalme Najash:

“Ewe Mfalme, sisi tulikuwa waovu na majahili, tukiabudu masanamu na kula nyamafu hata mizoga ya wanyama waliokufa wenyewe. Tulifanya kila aina ya matendo machafu na ya aibu na hatukuwa wenyewe kuwajibika kwa jirani na jamaa zetu. Wenyewe nguvu miongoni mwetu waliwakandamiza wanyonge. Kisha Allah akamleta mtume miongoni mwetu ambaye tulimfahamu vema kwa nasaba yake, utukufu wake na uzuri wa tabia yake tukufu. Alituuta tumuabudu Mungu mmoja tu na akatukataza kuabudia masanamu na mawe. Alitufundisha kusema ukweli, kutunza amana, kuwaangalia ndugu na jamaa na kuwafanya wema na kuacha maovu, alituamrisha kusimamisha swala na kutoa Zakat. Alituamrisha kujiepusha na maovu na kujiepusha na umwagaji damu. Alitukataza zinaa, kusema uwongo, kula mali ya yatima na kuwasiningizia uovu wanawake watoharifu. Alitufundisha Qur-an. Tulipomuamini na kuishi kulingana na mafundisho yake mazuri, watu wetu walianza kutupinga na kututesa wakidhania kuwa tutaiacha dini yetu na kurudia Ibada ya masanamu. Ukatili wao dhidi yetu ulipokithiri ndipo tukaja kujihami katika nchi yako kwa ruhusa ya Mtume wetu (s.a.w)”(A. Guillaume: *The life of Muhammad*, Uk. 151 - 252)

Hivyo, tunaposema kuhuisha Uislamu katika jamii tuna maana ya kuweka mikakati itakayowawezesha Waislamu kutekeleza wajibu wao wa kuamrisha mema na kukataza maovu na hatimaye kusimamisha Ukhilifa (Uongozi wa Allah (s.w)) katika jamii

ambao utawaelekeza na kuwafanya watu wafuate utaratibu anaouridhia Allah(s.w)katika kukiendea kila kipengele cha maisha na hatimaye kupatikana utulivu na amani ya kweli katika jamii.

Katika kuweka mikakati ya kuhuisha Uislamu katika jamii hatuna budi kwanza kuwa na Waislamu walio waumini wa kweli. Waumini wa kweli watapatikana kwa kutoa elimu sahihi ya Uislamu kwa Waislamu na wasiokuwa Waislamu. Baada ya watu kupata elimu sahihi juu ya Uislamu, watakaokhiyari kuwa Waislamu, wataudhihirisha Uislamu wao kibinagsi na kijamii. Pamoja na hali ya hatari iliyokuwepo katika kipindi cha mwanzo wa utume cha **kwanza** kuulingania Uislamu Makka, Mtume (s.a.w), baada ya kuwadarasisha Maswahaba pale Darl-Arqam, na kuwapa tafsiri sahihi ya Shahada katika maisha ya kila siku, mara moja wakaanza kutekeleza. Rejea tena maelezo ya Ja'affar kwa Mfalme Najash wa Uhabeshi. Ili kuweza kupata jamii ya Waislamu wa aina hii ni lazima tuanze kuandaa wanaharakati watakaokuwa walimu na mfano wa kuijwa kinadharia na kimatendo. Juzuuhii inaainisha maandalizi haya na yakifuatiliwa vilivyo Inshaa-Allah, itakuwa ndiyo sababu ya kuhuisha na kusimama uislamu katika jamii yetu ya Tanzania na ulimwengu na kwa ujumla.

Sura ya Kwanza

HAJA YA KUSIMAMISHA UISLAMU KATIKA JAMII

Utangulizi:

Kusimamisha Uislamu katika jamii ndio lengo kuu la kuletwa Mtume(s.a.w) kama inavyobainika katika Qur'an:

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ
عَلَى الْأَدِينَ كُلِّهِٰ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ ﴿٢٣﴾

“Yeye (Allah) ndiye aliyemtuma Mtume wake kwa uongofu na dini ya haki (Uislamu) ili aijaalie kushinda dini zote, ijapokuwa watachukia washirikina.” (9:33, 61:9)

Kwa mujibu wa aya hii ambayo imerudiwa katika sura mbili tofauti, lengo la kuletwa Mtume Muhammad (s.a.w), na mitume wote kwa ujumla, ni kuutawalisha Uislamu juu ya mifumo yote ya maisha katika jamii ya binaadamu.

Katika kipindi cha miaka 23, Mtume (s.a.w) na waumini aliokuwa pamoja nao, walifanikiwa kufikia lengo hili na Allah (s.w) anashuhudia hili katika aya ifuatayo:

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الْأَدِينَ كُلِّهِٰ
وَكَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا ﴿٢٨﴾

“Yeye ndiye aliyemtuma, (aliyemleta) Mtume wake kwa uwongofu na dini iliyo ya haki, ili aishindishe juu ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Shahidi”. (48:28).

“.....Na Allah (s.w) atosha kuwa shahidi” ina maana kubwa mbili:

Kwanza, Allah (s.w) anashuhudia kuwa Mtume wake alifikia lengo la kuletwa kwake baada ya miaka 23 ya kazi ngumu. Tukirejea historia, ushuhuda huu anautoa Allah (s.w) pale Mtume (s.a.w) na kundi lake la waumini walipowashinda maadui zao wote, ikiwemo dola ya Kirumi iliyokuwa “**Super power**” ya nyakati hizo. Maadui wengine walikuwa Mayahudi, Wanafiki, Makafiri wa Kiquraish na Makabila mengine ya Waarabu. Maadui wote hawa walikatishwa tamaa na nguvu ya Dola ya Kiislamu, kama Allah (s.w) alivyombainishia Mtume wake, alipokuwa Arafa katika Hija ya kuaga (Hijjatul-Wadaa) 9Dhul Hija 10A.H, kuwa:

الْيَوْمَ يِسَّ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ دِينِكُمْ فَلَا تَخْشُوْهُمْ وَأَخْشُونَ الْيَوْمَ
أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَنْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيَتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِيَنًا

“.... *Leo waliokufuru wamekata tamaa katika Dini yenu, basi msiwaogope, bali niogopeni Mimi. Leo nimekukamilishieni Dini yenu, na kukutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni Uislamu uwe Dini yenu* ” (5:3).

Aya hii inatoa ushahidi wa wazi kuwa Uislamu ulikuwa juu ya mifumo yote ya maisha ya jamii wakati wa Mtume (s.a.w).

Pili, Allah (s.w) pia anashuhudia kuwa wakati wowote Waislamu watakapoamua kusimamisha Uislamu katika jamii yao kwa kufuata baraabara mwenendo wa Mtume (s.a.w) na maswahaba zake, wataweza kusimamisha Uislamu katika jamii kama Allah (s.w) anavyoahidi katika aya ifuatayo:

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ ظَاهَرُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفُنَّهُمْ فِي
 الْأَرْضِ كَمَا أَسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَيَكُنَّ لَّهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي
 أَرْتَقَنَّ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلُنَّهُمْ مِنْ بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْ أُمَّا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي
 شَيْئًا وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٦٦﴾

“Mwenyezi Mungu Amewaaahidi wale walioamini mionganoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, kuwa Atawafanya makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya makhalifa wale waliokuwako kabla yao, na kwa yakini Atawasimamishia dini yao Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wawe wananiaabudu, hawanishirikishi na chochote. Na watakaokufuru baada ya hayo, basi hao ndio mafasiki (wavunjao amri zetu)”. (24:55).

Maana ya kusimamisha Uislamu katika Jamii

Uislamu utakuwa umesimama katika jamii pale Waislamu katika jamii hiyo watakapoweza kuendesha kila kipengele cha maisha yao ya **binafsi** na ya **jamii** kwa kufuata baraabara mwongozo wa Qur'an na Sunnah.Yaani Uislamu utakuwa umesimama katika jamii pale Waislamu watakapoweza kumuabudu Mola wao katika uchumi, siasa, utamaduni na kila nyanja ya maisha ya jamii kama wanavyomuabudu katika Swala, Zakat, Swaum na Hijja.

Katika hali ya kawaida ya utaratibu wa maumbile aliouweka Allah (s.w), haitatokea Waislamu kujikuta tu wapo katika mazingira mazuri ya kumtii Mola wao na kukiendea kila kipengele cha maisha yao ya binafsi na ya jamii kwa wepesi tu bila ya kipingamizi chochote kama viumbe wengine walioko mbinguni na ardhini wanavyomtii Mola wao kama inavyobainika katika ya ifuatayo:

أَفَغَيْرَ دِينِ اللَّهِ يَبْعُدُونَ وَلَهُ أَسْلَمَ مَنْ فِي السَّمَاوَاتِ
 وَالْأَرْضِ طَوْعًا وَكَرْهًا وَإِلَيْهِ يُرْجَعُونَ

Je! Wanataka dini isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu na hali kila kilichomo mbinguni na ardhini kinamtii Yeye, kikipenda kisipende? Na Kwake watarejeshwa wote". (3:83).

Aya hii inabainisha wazi kuwa binadamu ana hiari ya kumtii Allah (s.w.) au kumuasi, lakini viumbi vyote vinalazimika kimaumbile kumtii Allah (s.w.) katika kila nukta ya maisha yao. Vilevile aya zifuatazo, zinatufahamisha kuwa si katika Sunnah (kawaida) ya Allah (s.w.) kuwalazimisha binadamu na majini kumtii wakipenda wasipende:

وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ لَآمِنَ مَنْ فِي الْأَرْضِ كُلُّهُمْ جَمِيعًا أَفَأَنْتَ تُكْرِهُ النَّاسَ حَتَّىٰ
 يَكُونُوا مُؤْمِنِينَ

Na kama angalitaka Mola wako (kuwalazimisha kwa nguvu kuamini) bila shaka wangaliamini wote waliomo katika ardhi (asibaki hata mmoja). (Lakini Mwenyezi Mungu hataki kuwalazimisha watu kwa nguvu) Basi je, wewe utawashurutiza (watu kwa nguvu hata wawe Waislamu?) (10:99)

وَلَوْ شِئْنَا لَأَتَيْنَا كُلَّ نَفْسٍ هُدًى هَا وَلَكِنَّ حَقَّ الْقَوْلِ مِنِّي
 لِأَمَلَانَ جَهَنَّمَ مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسُ أَجْمَعُونَ

"Na tungalitaka Tungempa kila mtu uongofu wake (kwa lazima, lakini binadamu amepewa uhuru wa kufanya alitakalo lilo jema au baya), lakini imehakikika kauli iliyotoka kwangu: Kwa yakini Nitaijaza Jahannamu kwa wote hawa, majini na watu" (32: 13)

Kutokana na uhuru waliopewa na pamoja na kuumbwa kutokana na asili moja, (Baba mmoja - Adamu na mama mmoja - Hawa) wanaadamu wamegawanyika katika makundi makubwa mawili yanayohasimiana **Makafiri** na **Waumini**:

هُوَ الَّذِي حَقَّكُمْ فَمِنْكُمْ كَافِرٌ وَمِنْكُمْ مُؤْمِنٌ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ

“Yeye ndiye aliyekuumbeni (nyote) na kuna wengine wenu makafiri na wengine wenu ni waumini. Na Mwenyezi Mungu anayaona (yote) mnayoyafanya”. (64:2)

Lakini ilivyo, Ukafiri ni **Giza** na Uislamu ni **Nuru**. Katika hali ya kawaida ya maumbile nuru na giza haviwezi kuishi pamoja bali giza likizidi nuru, nuru inatoweza na kinyume chake ni sahihi. Kwa mantiki hii ukafiri ukiwa na nguvu ya kuitawala jamii Uislamu utatoweza katika jamii hiyo hata kama Waislamu watakuwepo. Kwa maana nyingine, pale ambapo jamii huongozw a kwa sheria na sera zinazopingana na sheria na utaratibu aliouweka Allah (s.w.) katika kuendea uchumi, siasa, utamaduni na vipengele vingine vya maisha ya jamii, jamii hiyo itakuwa inaongozwa kikafiri; na Waislamu katika jamii hiyo watakuwa wanaishi kikafiri hata kama watabakia kuiita waislamu na kufanya matendo binafsi ya Kiislamu kama vile kuswali, kufunga, kuhiji, n.k. Kwa mantiki hii vilevile, ili Waislamu waweze kuufuata Uislamu wao katika kila kipengele cha maisha ya jamii hawana budi kuutawalisha Uislamu katika jamii, yaani, hawanabudi kuusimamisha Uislamu katika jamii kwa kuhakikisha kuwa sharia na mwongozo wa Allah (s.w.) ndio unaotawala kila kipengele cha maisha ya jamii.

Kihalisia, si jambo jepesi kusimamisha Uislamu katika jamii, kwani daima makafiri huja juu dhidi ya jambo hili. Makafiri wanapenda kubakia katika giza ili waendeleze maovu katika jamii kwa manufaa yao huku wakiyaita mema. Hivyo makafiri hawako tayari kumulikwa na kuadhiriwa na nuru ya Uislamu. Nia ya makafiri ya kuzima nuru ya Uislamu inabainishwa na Allah (s.w.):

يُرِيدُونَ لِيُطْفِئُوا نُورَ اللَّهِ بِأَفْوَاهِهِمْ وَاللَّهُ مُتِمٌ ثُورِيهِ
وَلَوْ كَرِهَ الْكَافِرُونَ

“Wanataka kuzima nuru ya Mwenyezi Mungu (Uislamu) katika jamii kwa vinywa vyao, hakika Mwenyezi Mungu atakamilisha nuru yake ijapokuwa makafiri watachukia.” (61 :8)

Kama ilivyo Sunnah (kawaida) yake, Allah (s.w.) hatausimamisha Uislamu katika jamii kwa kuwahilikisha makafiri wote katika jamii au kuwalazimisha watu wote wawe waumini, bali anaahidi kutimiza nuru yake kwa kuwasaidia waumini dhidi ya makafiri pale watakapokuwa tayari kujitoa muhanga kwa mali zao na nafsi zao kupigania uhuru wao wa kufuata Uislamu katika kila kipengele cha maisha ya jamii.

Umuhimu wa kusimamisha Uislamu katia Jamii

Umuhimu wa kusimamisha Uislamu katika jamii unadhihirini katika vipengele vifuatavyo:

- (i) Kusimamisha Uislamu ni faradh (lazima) kwa waumini.
- (ii) Msamaha na Pepo ya Allah (s.w) imeahidiwa kwa wenye kufanya juhud za makusudi za kusimamisha Uislamu.
- (iii) Allah (s.w) ameshusha chuma (silaha) kwa lengo la kusimamisha Uislamu katika jamii.
- (iv) Kusimamisha Uislamu katika jamii ndio lengo kuu la maisha ya muumini.

(i) Kusimamisha Uislamu katika jamii ni faradh:

Kwa Waislamu, suala la kusimamisha Uislamu katika jamii limefaradhishwa kwao kama ilivyo faradhishwa Swala, Zakat, Swaumu na Hijja, kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

كُتِبَ عَلَيْكُمُ الْقِتَالُ وَهُوَ كُرْهٌ لَّكُمْ وَعَسَى أَن تَكُرْهُوا شَيْئاً
 وَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ وَعَسَى أَن تُحِبُّوا شَيْئاً وَهُوَ شَرٌّ لَّكُمْ وَاللَّهُ يَعْلَمُ
 وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ

“Mmelazimishwa kupigana vita (kwa ajili ya dini). Nalo ni jambo zito kwenu. Lakini huenda mkachukia kitu, nacho ni kheri kwenu. Na huenda mkapenda kitu nacho ni shari kwenu. Na Mwenyezi Mungu ndiye anayejua, (lakini) nyinyi hamjui”. (2:216)

Neno “**Kutiba**” (Mmelazimishwa) lililotumika katika aya hii ndilo hilo hilo lililotumika katika kufaradhishwa Swaumu Ramadhani kwa waumini.

يَتَأَيَّهَا الَّذِينَ ظَاهَرُوا مِنْ قَبْلِكُمْ لَعْنَكُمْ أَصْنَامٌ كَمَا كُتِبَ
 عَلَى الَّذِينَ مِنْ قَبْلِكُمْ لَعْنَكُمْ تَتَّقُونَ

“Enyi mlionamini! Mmelazimishwa kufunga (Saumu) kama walivyolazimishwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu.”. (2:183).

Hivyo kimantiki, kupigana vita vya jihadi ili kusimamisha Uislamu katika jamii au ili kuuhami Uislamu usiangushwe na maadui baada ya kusimama ni jambo la **faradh** (la lazima) kwa Waislamu kama ilivyo faradh kufunga mwezi wa Ramadhani. Neno hili “**Kutiba**” kwa maana hii ya kufaradhisha (kulazimisha) waumini limetumika tena katika sura hii ya Al-Baqara katika aya (2:178) na (2:180). Jambo la kushangaza ni kwamba, Waislamu walio wengi wanajihimu kwa “**kutiba**” moja tu ya Swaumu (2:183) na hawanahabari kiutekelezaji na “**kutiba**” tatu zilizobakia!

Pia amri ya Allah (s.w) ya kuupigania Uislamu kaitka jamii inabainika katika aya ifuatayo:

..... وَجَنَهُدُوا فِي اللّٰهِ حَقًّا جِهَادٍ

“Na ipiganieni dini ya Mwenyezi Mungu kama inavyostahiki kupiganiwa...” (22:78)

Kuipigania Dini ya Allah katika haki ya kuipigania au kama inavyostahiki kupiganiwa, maana yake ni kudhamiria, kuweka mikakati na kufanya jitihada za makusudi za kusimamisha Uislamu katika jamii.

(ii) Pepo hupatikana kwa kupigania kusimama kwa Uislamu katika jamii

Allah (s.w), pamoja na kufaradhisha jihadi kwa waumini kama alivyo faradhisha Swala, Zakat, Swaumu na Hija, ameahidi pepo moja kwa moja kwa **Mujahidina**. Ilivyo ni kuwa lengo la kusimamisha Swala, Zakat, Swaumu na Hija na faradhi nyinginezmo pamoja na utekelezaji wa sunna mbali mbali ni kumuwezesha muumini kuwa **Mujahidina**. Kama muislamu atatekeleza ibada mbali mbali za **faradh** na **Sunnah** bila kuwa **mujahidina**, amali zake zitakuwa zimeruka patupu. Hivyo, Allah (s.w) **anawapa** motisha waumini wafanye jitihada za makusudi katika kupigania Dini yake kwa malipo ya pepo kama inavyodhahirika katika aya zifuatazo:

﴿إِنَّ اللّٰهَ أَشْتَرَى مِنَ الْمُؤْمِنِينَ أَنفُسَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ بِأَنَّ لَهُمُ الْجَنَّةَ﴾

﴿يُقَدِّلُونَ فِي سَبِيلِ اللّٰهِ فَيَقْتُلُونَ وَيُقْتَلُونَ وَعَدًا عَلَيْهِ حَقًّا فِي التَّورَةِ﴾

﴿وَالْأَنْجِيلِ وَالْقُرْءَانِ وَمَنْ أَوْفَى بِعَهْدِهِ مِنَ اللّٰهِ فَأَسْتَبِرُوا بِبَيِّنَكُمْ﴾

﴿الَّذِي بَأْتُمُوهُنَّا بِهِ وَذَلِكَ هُوَ الْفُورُ الْعَظِيمُ﴾

“Mwenyezi Mungu amenunua kwa waumini nafsi zao na mali zao (watoe nafsi zao na mali zao katika kupigania dini) ili na yeye awape Pepo. Wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu; wanauua na wanauawa. Hii ndiyo ahadi

aliyojilazimisha (*Mwenyezi Mungu*) katika Taurati na Injili na Qur'an. Na ni nani atekelazaye zaidi ahadi yake kuliko *Mwenyezi Mungu?* Basi furahini kwa biashara yenu mliyofanya naye (*Mwenyezi Mungu*). Na huko ndiko kufuzu kukubwa". (9:111)

Pia Allah (s.w) anawahamasisha wafanye biashara naye kwa malipo ya pepo katika aya zifuatazo:

﴿فَلَيُقْتَلُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ الَّذِينَ يَشْرُونَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا بِالْآخِرَةِ وَمَنْ

﴿يُقْتَلُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيُقْتَلُ أَوْ يَعْلَمُ فَسَوْفَ نُؤْتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا﴾

"Basi nawapigane katika njia ya *Mwenyezi Mungu* wale wanaouza maisha (yao) ya dunia kwa (kununua) ya Akhera. Na anayepigana katika njia ya *Mwenyezi Mungu* kisha akauawa au akashinda, tutampa ujira mkuu". (4:74)

Pia Allah (s.w) anatangaza biashara hii katika Suratus-Saff:

﴿يَأَيُّهَا الَّذِينَ ظَاهَرُوا هَلْ أَذْكُرُمْ عَلَىٰ تَجَزِّرٍ تُنْجِيْكُمْ مِّنْ عَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿١﴾ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَتُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ يَأْمُوْلُكُمْ وَأَنْفُسُكُمْ ذَلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٢﴾ يَغْفِرُ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَيُدْخِلُكُمْ جَنَّتِ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَرُ وَمَسَكِنَ طَيِّبَةً فِي جَنَّتِ عَدْنٍ ذَلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿٣﴾ وَأُخْرَىٰ تُحِبُّونَهَا نَصْرٌ مِّنَ اللَّهِ وَفَتْحٌ قَرِيبٌ وَبَشِّرِ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٤﴾﴾

*Enyi mliaoamini! Je! Nikujulisheni biashara itakayokuokoeni na adhabu iumizayo? (Basi biashara yenewe ni hii): - Muaminini *Mwenyezi Mungu* na Mtume wake, na piganieni dini ya *Mwenyezi Mungu* kwa mali zenu na nafsi zenu, haya*

ni bora kwenu; ikiwa mnajua (kuwa ni bora, basi fanyeni). (Mkifanya haya) Atakusameheni dhambi zenu na atakuingizeni katika Mabustani yapitayo mito mbele yake na (atakupeni) maskani mazuri mazuri katika Bustani za milele: huku ndiko kufuzu kukubwa”. Na (atakupeni) kingine mnachokipenda: Nay o ni nusura itokayo kwa Mwenyezi Mungu na ushindi ulio karibu! Na wapashe habari njema Waumini”. (61:10-13).

Katika kuwapa motisha zaidi waumini wasonge mbele katika kupigania Uislamu usimame katika jamii, Allah (s.w) anakataza kuwaita wafu wale waliokufa katika Jihadi:

وَلَا تَقُولُوا لِمَنْ يُفْتَلُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَمْوَاتٌ بَلْ أَحْيَاءٌ وَلَكِنْ لَا تَشْعُرُونَ

Wala msiwaite wale waliouawa katika njia ya Mwenyezi Mungu wafu, bali wahai lakini nyinyi hamtambui”. (2:154).

وَلَا تَحْسِبَنَّ الَّذِينَ قُتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَمْوَاتًا بَلْ أَحْيَاءٌ عِنْدَ رَبِّهِمْ يُرْزَقُونَ

فَرِحِينٌ بِمَا أَتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ وَيَسْتَبْشِرُونَ

بِالَّذِينَ لَمْ يَلْحَقُو بِهِمْ مِنْ خَلْفِهِمْ لَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ

يَخْرُزُونَ

* يَسْتَبْشِرُونَ بِنِعْمَةٍ مِنَ اللَّهِ وَفَضْلٍ وَأَنَّ اللَّهَ لَا

يُضِيعُ أَجْرَ الْمُؤْمِنِينَ

(W)

Wala usiwadhani wale waliouawa katika njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni wafu (maiti). Bali wahai, wanaruzukiwa kwa Mola wao”. Wanafurahia aliyowapa Mwenyezi Mungu kwa fadhila Zake; na wanawashangilia wale ambao hawajajiunga nao, walio nyuma yao, (wako ulimwenguni, bado hawajafa); ya kwamba haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika. Wanashangilia neema na fadhila za Mwenyezi Mungu, na kwamba Mwenyezi Mungu hapotezi ujira wa wanaoamini”. (3:169-171).

Pia Allah (s.w) anawapa motisha waumini katika aya ifuatayo:

وَلِئِنْ قُتِلُّتُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَوْ مُتُّمْ لَمَغْفِرَةٌ مِّنَ اللَّهِ وَرَحْمَةٌ خَيْرٌ

مِمَّا يَجْمَعُونَ ١٥٧

Na kama mkiuawa katika njia ya Mwenyezi Mungu au mkifa (si khasara kwenu) kwani msamaha na rehema zinazotoka kwa Mwenyezi Mungu ni bora kuliko vile wanavyokusanya (hapa ulimwenguni)". (3:157).

Vinginevyo, Allah (s.w.) anawakatisha tamaa kabisa wale Waislamu wanaojiweka mbali na **Jihad** kwa dhana kuwa Swala, Zakat, Swaumu, Hija na Ibada zao nyingine za kibinafsi kama hizo, zitawaingiza peoponi kilaini. Allah (s.w.) anatutanabahisha:

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَّا يَأْتِكُمْ مَّثُلُ الَّذِينَ خَلَوْ مِنْ قَبْلِكُمْ

مَسْتَهْمُ الْبَاسَاءُ وَالضَّرَاءُ وَرُزِّلُوا حَتَّىٰ يَقُولَ الْرَّسُولُ وَالَّذِينَ ظَاهَرُوا مِنْ أَمْنُوا

مَعَهُ وَمَنِي نَصْرًا اللَّهُ لَا إِنْ تَصْرُّ اللَّهُ قَرِيبٌ ٣٦٤

"Mnadhani kuwa mtaingia Peponi, na hali hamjajiwa na mfano wa wale waliopita kabla yenu? Yaliwapata mashaka na madhara na wakatetemeshwa sana hata Mitume na walioamini pamoja nao wakasema: "Nusura ya Mwenyezi Mungu itafika lini?" Jueni kuwa nusura ya Mwenyezi Mungu iko karibu. (2:214)"

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَّا يَعْلَمَ اللَّهُ الَّذِينَ جَنَدُوا مِنْكُمْ

وَيَعْلَمُ الصَّابِرِينَ ٣٦٥

Je! Mnadhani mtaingia Peponi (hivi hivi tu), hali Mwenyezi Mungu hajawapambanua wale waliopigania dini ya Mwenyezi Mungu mionganoni mwenu, na kuwapambanua waliofanya subira? (Sharti yaonekane kwanza haya hapa ulimwenguni). (3: 142)

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تُشْرَكُوا وَلَمَا يَعْلَمَ اللَّهُ الَّذِينَ جَاهَدُوا مِنْكُمْ وَلَمْ يَتَّخِذُوا
منْ دُونِ اللَّهِ وَلَا رَسُولِهِ وَلَا الْمُؤْمِنِينَ وَلِيَحْجُّ وَاللَّهُ خَيْرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿١٦﴾

Je, mnadhani kuwa mtaachwa, na hali Mwenyezi Mungu hakuwabainisha wale waliopigania dini mionganoni mwenu na wasiwafanye rafiki wa moyo isipokuwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake na waumini (wenziwe)? Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za yote mnayoyafanya". (9:16)

(iii) Allah(s.w)ameshusha silaha kwa lengo la kusimamisha Uislamu katika Jamii.

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلًا إِلَيْبِنَتٍ وَأَنْزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ
لِيَقُومَ النَّاسُ بِالْقِسْطِ وَأَنْزَلْنَا الْحَدِيدَ فِيهِ بَأْشَ شَدِيدٌ وَمَنْتَفِعٌ لِلنَّاسِ
وَلَيَعْلَمَ اللَّهُ مَنْ يَنْصُرُهُ وَرُسُلُهُ بِالْغَيْبِ إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٢٥﴾

Kwa hakika Tuliwapeleka Mitume Wetu kwa dalili waziwazi na Tukaviteremsha Vitabu na mizani pamoja nao, ili watu wasimamie uadilifu. Na tumekiteremsha chuma chenyenuguvi nydingi na manufaa kwa watu; na ili Mwenyezi Mungu Ajulishe anayemnusuru na Mitume yake, na hali ya kuwa hawamuoni Mwenyezi Mungu. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu mwenyewe kushinda". (57:25).

Katika aya hii tunajifunza kuwa lengo la kuletwa Mitume wa Allah (s.w) ni kusimamisha haki na uadilifu katika jamii kwa kufuata vitabu vya Allah (s.w) vyenye mwongozo, sheria na hukumu. Kisha Allah (s.w) akashusha chuma chenyenuguvi (silaha) ili Mitume na walioamini pamoja nao wakitumie kuzima nguvu za wapinzani wa haki na uadilifu, wanaopendelea kudhulamu watu na kufanya ufisadi katika ardhi.

(iv) Kusimamisha Uislamu ndio lengo kuu la Maisha ya Waumini.

Allah (s.w) ameweka bayana kuwa hayuko radhi na yule atakayekuwa na lengo lingine la maisha lisilokuwa la kusimamisha Uislamu katika jamii kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

يَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَشْرِدُوا أَبَاءَكُمْ وَإِخْوَانَكُمْ أَوْ لِيَاءَ إِنِّي أَسْتَحِبُّ
الْكُفَّارَ عَلَى الْإِيمَانِ وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ

(٣٤)

Enyi mlionmini! Msiwafanye baba zenu na ndugu zenu kuwa vipenzi (vyenu) ikiwa wanastahabu(wanapenda) ukafiri kuliko Uislamu. Na katika nyinyi atakayewafanya hao kuwa ndio vipenzi vyake, basi hao ndio madhalimu (wa nafsi zao) (9:23)

فُلِّ إِنْ كَانَ عَابَاؤُكُمْ وَأَبْنَاؤُكُمْ وَإِخْوَانُكُمْ وَأَزْوَاجُكُمْ وَعَشِيرَتُكُمْ
وَأَمْوَالُ افْتَرَفُتُمُوهَا وَتِجَارَةً تَخْشُونَ كَسَادَهَا وَمَسَكِنَ تَرْضُونَهَا
أَحَبَّ إِلَيْكُم مِّنْ أَلَّهِ وَرَسُولِهِ وَجِهَادٍ فِي سَبِيلِهِ فَتَرَبَّصُوا حَتَّىٰ يَأْتِيَ
الَّلَّهُ بِأَمْرِهِ وَالَّلَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ

(٣٥)

Sema: "Kama baba zenu na wanawenu na ndugu zenu na wake zenu na jamaa zenu na mali mlizochuma na biashara mnazoogopa kuharibikiwa, na majumba mnayoyapenda; (ikiwa vitu hivi) ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kupigania dini yake, basi ngojeni mpaka Mwenyezi Mungu alete amri yake; na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu maasi (njia iliyonyooka)". (9:24).

Kwa mujibu wa aya hizi tunajifunza kuwa chochote tutakacho kipenda au kukifanya, tukipende au tukifanye kwa lengo la kumridhisha Allah (s.w), Mtume wake na kusimamisha Dini yake katika jamii.

Kwa nini ni muhimu kusimamisha Uislamu katika Jamii ?

Kusimamisha Uislamu kumefaradhishwa kwa waumini ili yapatikane yafuatayo:

- (i) Waumini waweze kumuabudu Allah (s.w) ipasavyo.
- (ii) Kuleta amani ya kweli katika jamii.
- (iii) Waumini waweze kuamrisha mema na kukataza maovu.
- (iv) Kuikinga jamii na majanga mbali mbali.

(i) *Waumini kuweza kumuabudu Mola wao ipasavyo*

Allah (s.w.) amewaumba majini na watu kwa lengo moja tu la kumuabudu

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونَ ﴿٥١﴾

“Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu.” (51:56)

Kumuabudu Allah (s.w.) kwa mnasaba wa lengo la kuumbwa watu, ni watu kuishi katika kila kipengele cha maisha yao kwa kufuata baraabara kanuni, sharia na mwongozo wa Allah (s.w.). Kimantiki Allah (s.w) ndiye pekee anayestahiki kuabudiwa au kutiwi na binaadamu kwa unyenyekevu katika kukiendea kila kipengele cha maisha yake ya kibinagsi na kijamii kwa kuwa ye ye ndiye aliyemuumba binaadamu na maumbile yote yaliyomzunguka pamoa na kumtunukia neema mbali mbali kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

يَتَائِفُهَا النَّاسُ أَعْبُدُوا رَبَّكُمْ الَّذِي خَلَقَكُمْ وَالَّذِينَ مِنْ
قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّبَعُونَ ﴿٢١﴾ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ
الْأَرْضَ فِرَشًا وَالسَّمَاءَ بَنَاءً وَأَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَآءً فَأَخْرَجَ بِهِ
مِنَ الْثَّمَرَاتِ رِزْقًا لَكُمْ فَلَا تَجْعَلُوا لِلَّهِ أَنْدَادًا وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٢٢﴾

Enyi mliaoamini! Mwabuduni Mola wenu ambaye amekuumbeni nyinyi na wale wa kabla yenu; ili mpate kuokoka.(Mwenyezi Mungu) Ambaye amekufanyieni hii ardhi kuwa kama busati (mliotandikiwa mstarehe), na mbingu kuwa kama paa, na akateremsha maji kutoka mawinguni; na kwa hayo akatoa matunda yawe riziki zenu. Basi msimfanyizie Mwenyezi Mungu washirika, na hali nyinyi mnajua (kuwa hana mshirika)".(2:21-22)

Pia aya ifuatayo inaonesha kuwa Allah (s.w), Ndiye anayestahiki kutoa amri na kutiwa pasina hoja kwa kuwa ndiye aliyeumba:

إِنَّ رَبَّكُمْ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سَتَةِ أَيَّامٍ
ثُمَّ أَسْتَوَى عَلَى الْعَرْشِ يُغْشِي الْيَوْمَ الْهَارَ يَطْلُبُهُ وَحَشِيشًا
وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ وَالنُّجُومَ مُسْخَرًا بِإِمْرَةِ الْخَلْقِ وَالْأُمُرِ
تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَلَمِينَ ﴿٣٤﴾

Hakika Mola wenu ni Mwenyezi Mungu aliyezumba mbingu na ardhi kwa siku sita. Kisha akatawala juu ya Arshi yake. Huufunika usiku kwa mchana, uufuatiao upesi upesi, (na huufunika mchana kwa usiku uufuatiao upesi upesi). Na (ameliumba) jua na mwezi na nyota. (Na vyote) vimetiishwa kwa amri Yake. Fahamuni, Kuumba (ni Kwake tu Mwenyewe Mwenyezi Mungu) na amri zote ni zake (Mwenyezi Mungu). Ametukuka kabisa Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote". (7:54)

Makafiri ambao, wamekanusha kuwepo kwa Allah (s.w.), lengo hili la kuumbwa binaadamu hawalitambui na huishi hapa duniani kwa lengo tu la kustarehe. Hivyo, wale makafiri wanaoshika hatamu ya uongozi katika jamii, huwawekea raia wao kanuni na sheria zitakazowawezesha (watawala hao) kuishi kwa starehe bila ya kujali maslahi ya raia. Kwa hiyo, raia waumini chini ya utawala wa kitwaaghut (kikafiri) nao watalazimika kufuata kanuni na sheria za twaaghut zinazopingana na kanuni na sheria za Allah (s.w.) katika kuendea kila kipengele cha maisha ya kijamii, kama vile uchumi, siasa, utamaduni, n.k. Hivyo, waumini wa sampuli hii, hata kama watakuwa **wanaswali**, **wanatoa zakat**, **wanafunga**, **wanahiji** na kufanya Ibada nydingine kama hizi za kibinagsi, sehemu kubwa ya maisha yao watakuwa wanaishi nje ya lengo la kuumbwa kwao. Waumini wa sampuli hii, wanaoridhika kuishi chini ya utawala wa twaaghut, mbele ya Allah (s.w.) ni washirikina kama inavyobainika katika aya ifuatayo:-

اَتَخَذُواْ اَحْبَارَهُمْ وَرُهْبَنَتِهِمْ اَرْبَابًا مِّنْ دُونِ اللَّهِ وَالْمُسِيَّحَ اُبْنَ مَرْيَمَ
وَمَا اَمْرُوْ اِلَّا لِيَعْبُدُوْ اِلَّاهًا وَاحِدًا لَا إِلَهَ اِلَّا هُوَ سُبْحَانُهُ وَعَمَّا يُشْرِكُونَ

Wamewafanya wanavyuoni wao na watawa wao kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu, na (wamemfanya) Masihi mwana wa Maryamu (pia Mungu) hali hawakuamrishwa isipokuwa kumuabudu Mungu mmoja, hakuna anayestahiki kuabudiwa ila Yeye. Ametakasika na yale wanayomshirikisha nayo. (9:31)

Mayahudi na Wakristo, katika aya hii wanalaumiwa kuwa wamewafanya viongozi wao (Mapadre na Mafarisayo) kuwa miungu badala ya Allah (s.w.). Katika kuitafsiri aya hii Mtume (s.a.w.) aliwafahamisha waumini kuwa, kuwafanya viongozi miungu badala ya Allah (s.w.), ni pale viongozi watakapotiiwa na kufuatwa kinyume na sheria na mwongozo wa Allah (s.w.).

Vile vile waumini wanaoishi kwa raha mustarehe chini ya utawala wa twaaghut, maadamu tu wana uhuru wa kuswali, kutoa zaka, kufunga na kuhiji na uhuru wa kufanya ibada nyingine kama hizi za kibinagsi, uumini wao hautambuliki mbele ya Allah (s.w.) kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

..... أَفَتُؤْمِنُونَ بِعَيْنِ الْكِتَابِ وَتَكُفِّرُونَ بِبَعْضٍ

..... فَمَا جَزَ آءُ مَن يَفْعَلُ ذَلِكَ مِنْكُمْ إِلَّا خِرْقَىٰ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۖ وَيَوْمَ

..... الْقِيَمَةُ يُرَدُّونَ إِلَى أَشَدِ الْعَذَابِ ۚ وَمَا اللَّهُ بِغَافِلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٤٥﴾

“.....Je! Mnaamini baadhi ya kitabu na kukataa baadhi (yake)? Basi hakuna malipo kwa mwenye kufanya haya katika nyinyi ila fedheha katika maisha ya dunia, na siku ya kiyama watapelekwa katika adhabu kali. Na Mwenyezi Mungu si mwenye kughafilika na yale mnayoyatenda.” (2:85)

Katika hali halisi, waislamu walioridhika na uongozi wa kikafiri watakuwa wanaamini baadhi ya Qur-an kwa kutekeleza amri ya **Swala, Zakat, funga, Hija** na Ibada nyingine za aina hii za kibinagsi na watakuwa wamekataa baadhi palewatakapo kuwa radhi kufuata mfumo wa maisha ya kijamii katika siasa, uchumi, utamaduni, n.k. unaongozwa kikafiri. Waislamu wa sampuli hii wameahidiwa kudhalilika duniani na huko akhera wanangojewa na adhabu kali. Je! waislamu hivi leo hatuko dhalili katika ulimwengu? Hatunyanyaswi na Mayahudi walio milioni 18 tu na hali sisi tuko billioni 1.6 (millioni 1,600) na bado tunajidhania ni ummah bora?

Waumini wa kweli ni wale tu wanaomuabudu Allah (s.w.) katika kila kipengele cha maisha yao ya kibinagsi na kijamii kama Allah anavyowahimiza:

يَتَأَكَّلُهُ الَّذِينَ ظَاهَرُوا أَدْخَلُوا فِي الْسَّلَمِ كَافَّةً وَلَا تَشَبَّهُوا
 بِخُطُوطِ الشَّيْطَانِ إِنَّهُ دُلُكٌ عَدُوٌّ مُّبِينٌ

Enyi mliao mini! Ingieni katika hukumu za Uislamu zote, wala msifuate nyayo za Shetani; kwa hakika yeye kwenu ni adui dhahiri. (2:208)

Waumini wataweza kumtii Allah (s.w.) katika kila kipengele cha maisha ya jamii pale tu watakapochukua hatamu za uongozi wa jamii. Kihalisia, waumini kuchukua hatamu za uongozi wa jamii si jambo la lele mama. Daima viongozi wa kitwaaghut (kikafiri) hawako radhi kuwaachia (kuwaridhia) Waumini uongozi wa jamii kwa kuchelea kukosa maslahi yao waliyokuwa wakiyapata kwa njia ya kuwadhlumu raia zao. Hivyo, historia inaonesha kuwa hapana njia ya mkato na nyepesi kwa waumini kuchukua uongozi wa jamii ila kwa mapambano makali dhidi ya uongozi wa kitwaaghut (kikafiri) uliopo madarakani. Hii ndio mantiki ya Allah (s.w.) kuwaamrisha waumini kupigana na makafiri:

وَقَدْ تُلُوهُمْ حَتَّىٰ لَا تَكُونَ فِتْنَةً وَيَكُونُ الَّذِينَ لِلَّهِ فِيْنَ أَنْتَهُوْ فَلَا
 عُدُوَّنَ إِلَّا عَلَى الظَّالِمِينَ

“Na piganeni nao (makafiri) mpaka kusiwe na mateso (wao kuwatesa Waislamu bure) na dini iwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu. Na kama wakiacha basi usiwepo uadui ila kwa madhalimu”. (2: 193).

Anaongeza Allah kwa kusisitiza:

وَمَا لَكُمْ لَا تُقْتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَالْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ الرِّجَالِ وَالِّيَاسِأَرْ
وَأَلْوَدَنِ الَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا أَخْرِجْنَا مِنْ هَذِهِ الْقَرْيَةِ الظَّالِمِ أَهْلُهَا
وَاجْعَلْ لَنَا مِنْ لَدُنْكَ وَلِيَّا وَاجْعَلْ لَنَا مِنْ لَدُنْكَ نَصِيرًا

Na mna nini hampigani katika njia ya Allah na (katika kuwaokoa) wale walio madhaifu katika - wanaume na wanawake na watoto ambao husema: "Mola wetu! Tutoe katika mji huu ambao watu wake ni madhalimu, na tujaalie mlinzi anayetoka kwako, na tujaalie tuwe na wa kutunusuru anayetoka kwako. (4: 75)

الَّذِينَ ظَاهَرُوا يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَالَّذِينَ كَفَرُوا
يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ الظَّلْفِ وَمَنْ أَوْلَيَ اللَّهَ شَيْطَانٍ إِنَّ
كَيْدَ الشَّيْطَانِ كَانَ ضَعِيفًا

Wale walioamini wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu, lakini waliokufuru wanapigana katika njia ya Shetani. Basi piganeni na marafiki wa Shetani. Hakika hila za Shetani ni dhaifu. (4:76)

وَقَاتِلُوهُمْ حَتَّىٰ لَا تَكُونَ فِتْنَةٌ وَيَكُونَ الَّذِينُ كُلُّهُو لِلَّهِ فَإِنِّي أَنْتَهُو
فِإِنَّ اللَّهَ بِمَا يَعْمَلُونَ بَصِيرٌ

Na piganeni nao (makafiri) mpaka yasiweko mateso (nyinyi kuteswa na wao kwa ajili ya dini kama wanavyokuteseni sasa); na dini iwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu (asikatazwe mtu kuabudu dini anayoitaka). Lakini wakiacha, basi hakika Mwenyezi Mungu anayaona wanayoyatenda.

Kama hamtakwenda atakuadhibuni kwa adhabu inayoumiza, na atawaleta watu wengine badala yenu, wala

hamtamdhuru (Mungu) chochote (mkitopigania dini yake); na Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu. (8:39)

يَأَيُّهَا الَّذِينَ ءامَنُوا مَا لَكُمْ إِذَا قِيلَ لَكُمْ أَنْفِرُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ
أَنْقَلْتُمْ إِلَى الْأَرْضِ أَرْضِيْتُمْ بِالْحَيَاةِ الدُّنْيَا مِنَ الْآخِرَةِ فَمَا مَنَعَ
الْحَيَاةِ الدُّنْيَا فِي الْآخِرَةِ إِلَّا قَلِيلٌ ﴿٣٨﴾

Enyi mlionamini! Mna nini mnapoambiwa “Nendeni (kupigana) kwa ajili ya dini ya Mwenyezi Mungu” mnajitia uzito katika ardhi? Je, mumekuwa radhi na maisha ya dunia kuliko ya Akhera? Lakini starehe za maisha ya dunia kwa mkabala wa maisha ya akhera ni kidogo tu. (9:38)

Waislamu watakapoitikia wito huu wa kupigana na makafiri, Allah (s.w.) ameahidi kuwasaidia na kuwapa ushindi na uongozi juu ya makafiri.

..... وَلَيَصُرَّنَ اللَّهُ مَنْ يَنْصُرُهُ وَإِنَّ اللَّهَ لَقَوِيٌ عَزِيزٌ ﴿٤٠﴾

.....Na bila shaka Mwenyezi Mungu humsaidia yule anayesaidia dini yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mwenye kushinda. “ (22:40)

(ii) Kuondoka khofu na kupatikana amani na furaha ya kweli:

Waumini watakaposhika hatamu ya uongozi wa jamii, khofu itatoweka na utulivu na amani ya kweli itachukua nafasi yake. Hii inawezekana kwa sababu waumini ambao ni Makhalifa wa Allah (s.w.) hufuata kanuni, sheria na mwongozo wa Allah (s.w.) ulioainishwa katika vitabu vyake na Sunnah ya Mitume wake. Mitume na Vitabu vyya Allah vivilivoambatanishwa nao, hawakuletwa kwa lengo lingine lolote ila kusimamisha na kusimamia uadilifu katika jamii.

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلًا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنْزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمُيَزَانَ
 لِيَقُولُوا النَّاسُ بِالْقِسْطِ وَأَنْزَلْنَا الْحَدِيدَ فِيهِ بَأْسٌ شَدِيدٌ وَمَنَافِعٌ لِلنَّاسِ
 وَلِيَعْلَمَ اللَّهُ مَنْ يَنْصُرُهُ وَرُسُلُهُ بِالْغَيْبِ إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ
 ﴿٢٥﴾

Kwa hakika Tuliwapeleka Mitume Wetu kwa dalili wazi wazi na tukaviteremsha Vitabu na mizani pamoja nao, ili watu wasimamie uadilifu. Na Tumekiteremsha, (tumekiumba) chuma, chenye nguvu nydingi na manufaa kwa watu; na ili Mwenyezi Mungu Ajulishe anayemnusuru na Mitume yake, na hali ya kuwa hawamuoni Mwenyezi Mungu. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mwenye kushinda. (57:25)

Aya hii pamoja na kutufahamisha lengo la kuletwa Mitume pamoja na vitabu vya Allah (s.w.), pia inatufahamisha kuwa Allah (s.w.) ameumba “Chuma” chenye nguvu nydingi na manufaa kwa watu”, ili Mitume na Waumini watumie chuma hicho kwa silaha na matumizi mengineyo ili kuunda Dola yenyeye nguvu itakayowawezesha kuwa na mamlaka ya kusimamia uadilifu katika jamii. Panapokuwa na usimamizi imara wa uadilifu, kila raia katika jamii atapata haki yake anayostahiki na atakuwa huru kutumia uhuru wake binafsi aliopewa na Allah (s.w.).

Vile vile jamii inayoendeshwa katika mfumo wa kutii sheria na mwongozo wa Allah (s.w) katika kila kipengele cha maisha huwa katika amani kwa sababu itakuwa inaendana na sheria za maumbile. Kwa mfano Allah (s.w.) ameharamisha ulevi, riba na kamari kwa sababu vitu hivi vina madhara makubwa kiuchuni kwa watu binafsi na kwa jamii kwa ujumla. Miiongoni mwa madhara yanayosababishwa na ulevi, riba na kamari ni uvivu, uharibifu wa mali, ubadhirifu, wizi, umwinyi, unyonyaji, ukandamizaji, utapeli, rushwa, n.k. Hivyo mfumo wa uchumi wa Kiislamu ambao umeviharamisha vitu hivi na kuvipiga marufuku katika jamii, ndio pekee unaoweza kunawirisha uchumi na kujenga mazingira ya

Enyi mliaoamini! Bila shaka ulevi na kamari na kuabudiwa (na kuombwa) asiyekuwa Mwenyezi Mungu, na kutazamia kwa mishare ya kupigia ramli (na kwa vinginevyo); (yote haya) ni uchafu (ni) katika kazi ya Shetani. Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufaulu (kutengenekewa). (5:90)

إِنَّمَا يُرِيدُ الشَّيْطَانُ أَنْ يُوقَعَ بِيَدِكُمُ الْعَدَوَةَ وَالْبُغْضَاءَ فِي الْخَمْرِ
وَالْمَيْسِرِ وَيَصْدُدُ كُمْ عَنِ ذِكْرِ اللَّهِ وَعَنِ الْصَّلَاةِ فَهَلْ أَنْثُمْ مُّنْتَهُونَ ﴿٩١﴾

Hakika Shetani anataka kukutilieni uadui na bughudha baina yenu kwa ajili ya ulevi na kamari na anataka kukuzuilieni kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kusali. Basi je, mtaacha (mabaya hayo)? (5:91)

Matwaghuti huita maovu hayo kuwa ni njia za uchumi endelevu na huwasakama waumini wanaopiga vita maovu haya na kuwapachika majina ya siasa kali, magaidi mujahidina,n.k.

Nuru, katika aya (2:257) inaashiria maisha ya utulivu, furaha na amani, ambapo giza, linaashiria maisha ya khofu, dhulumu na machafuko ya kijamii ya aina mbali mbali. Hivyo, kutohana na aya hii tunajifunza kuwa utulivu, furaha na amani halisi vitapatikana katika jamii pale tu Waislamu watakapochukua hatamu za uongozi wa jamii au pale tu Waislamu watakapo chukua nafasi yao ya **Ukhalifa**.

(iii) Waumini kuweza kuamrisha mem na kukataza maovu

Pia Waislamu wanapochukua hatamu ya uongozi wa jamii, hudumisha mazingira ya utulivu na amani kwa kufanya kazi ya ziada ya kuwaamrisha watu kufanya mema yenyе manufaa na jamii na kuwakataza kufanya maovu yenyе kuihilikisha jamii. Majukumu makuu ya viongozi wa Kiislamu yameainishwa katika aya ifuatayo:

uadilifu ambapo kila raia atapata haki yake na mahitaji muhimu ya maisha. Kwa hiyo, mfumo huu wa uchumi ndio pekee unaoiwezesha jamii kuishi kwa utulivu na amani.

Kwa upande mwingine, pale ambapo ulevi, riba na kamari, vimehalalishwa na kuingizwa kwenye mfumo wa uchumi wa jamii, madhara yake yatauathiri uchumi na kujenga mazingira ya dhuluma na chuki na kuigawanya jamii kwenye matabaka ya walionacho na wasionacho, wavya jasho na mabwenyenyenye, watawala na watawaliwa, mabwana na watwana, n.k. Ni muhali kupata utulivu na amani kwenye jamii ya sampuli hii. Allah (s.w.) anatuweka wazi juu ya matokeo ya uongozi wa Kiislamu na uongozi wa kikafiri:

اللَّهُ وَلِئِنَّ الَّذِينَ ءامَنُوا يُخْرِجُوهُم مِّنَ الظُّلْمَاتِ إِلَى النُّورِ
وَالَّذِينَ كَفَرُوا أُولَئِكُمُ الظَّاغِنُونَ يُخْرِجُونَهُم مِّنَ النُّورِ إِلَى
الظُّلْمَاتِ أُولَئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَلِيلُونَ

“Mwenyezi Mungu ni Mlinzi (kiongozi) wa wale walioamini. Huwatoa katika giza na huwaingiza katika nuru. Lakini waliokufuru, walinzi (viongozi) wao ni Matwaghuti. Huwatoa katika nuru na kuwaingiza katika giza. Hao ndio watu wa motoni, humo watacaa milele.” (2:257)

Katika aya hii, matwaaghuti ni viongozi wa jamii wanaochupa mipaka ya Allah (s.w.) katika maongozi yao. Wanawawekea raia zao sheria na sera zinazokwenda kinyume na sheria za Allah (s.w.). Kwa mfano, Allah (s.w.) anapowakataza waache ulevi na kamari, kama zinavyoagiza aya zifuatazo:

يَأَيُّهَا الَّذِينَ ءامَنُوا إِذَا الْخَمْرُ وَالْمَيْسِرُ وَالْأَنْصَابُ وَالْأَرْلَمُ رِجْسٌ مِّنْ
عَمَلِ الشَّيْطَانِ فَاجْتَبَيْهُ لَعَلَّكُمْ تُفَلِّحُونَ

الَّذِينَ إِنْ مَكَنُوهُمْ فِي الْأَرْضِ أَقْمُوا الصَّلَاةَ وَإِنْ تَوْلُوا الْكَوَافِرَ وَأَمْرُوا
 بِالْمَعْرُوفِ وَنَهُوا عَنِ الْمُنْكَرِ وَلِلَّهِ عِدْقَبَةُ الْأُمُورِ

“Wale ambao tukiwamakinisha (tukiwapa mamlaka) katika ardhi husimamisha swala na wakatoa zaka na wakaamrisha yaliyo mema na wakakataza yaliyo mabaya. Na marejeo ya mambo ni kwa Mwenyezi Mungu.” (22:41).

Jamii ya Kiislamu imekuwa bora mbele ya Allah (s.w.) kuliko jamii nyingine kwa sababu ya kuiweka jamii katika hali ya utulivu na amani kwa kuamrisha mema na kukataza maovu.

كُنْتُمْ خَيْرًا مِّنْ أُمَّةٍ أُخْرِيَ حَتَّى لِلَّاتِي تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ
 عَنِ الْمُنْكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ

“Nyinyi ndio umma bora kuliko umma zote zilizodhahirishiwa watu (Ulimwenguni) - mnaamrisha yaliyo mema na mnakataza yaliyo maovu, na mnamuamini Mwenyezi Mungu” (3: 110)

Waumini, hata kama hawajafikia uwezo wa kuwa na Dola ya Kiislamu, hawanabudi kuamrisha mema na kukataza maovu kwa kadiri ya uwezo wao. Mtume (s.a.w.) amesisitiza hili katika Hadith zifuatazo:

Abu Said Al-Khudri (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: “Yeyote mionganini mwenu atakayeona jambo ovu na aliondoe kwa mkono wake, kama hawezi (kuliondoa kwa mkono) na aliondoe kwa ulimi na kama hawezi kuliondoa kwa ulimi na achukie moyoni mwake na huku kuchukia kwa moyo tu ni kiwango cha chini cha imani.” (Muslimu)

(iv) Kuikinga jamii na majanga mbali mbali.

Hudhaifa (r.a.) ameелеza kuwa Mtume wa Allah amesema: “Naapa kwa yule ambaye mikononi mwake yako maisha yangu, mtaamrisha mema na kukataza maovu, vinginevyo ni hivi karibuni tu adhabu ya Mwenyezi Mungu itakuwa juu yenu. Kisha mtamuomba Allah (s.w.) lakini hamtajibiwa.” (Tirmidh).

Katika Hadith nyiningine imesimuliwa kuwa:

Jabir bin ‘Abdullah (r.a.) ameèleza: Nimemsikia Mtume wa Allah akisema: “Hapana mtu ambaye anafanya maovu mbele ya watu ambao wana uwezo wa kumzuia, lakini wasijali kufanya hivyo, ila Mwenyezi Mungu atawaadhibu wote hapa duniani kabla hawajafa.” (Abu Daud, Ibn Majah).

Kutokana na Hadithi hizi, waumini popote walipo katika jamii, hata chini ya maongozi ya Twaaghuti, wanawajibika kukataza au kukemea maovu, kwani athari ya uovu katika jamii haiishii kwa wale waovu peke yao, bali jamii nzima kama Allah (s.w.) anavyotutanabahisha:

وَأَنْقُوا فِتْنَةً لَا نُصِيبَنَّ أَذِينَ ظَلَمُوا مِنْكُمْ خَاصَّةً وَأَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ شَدِيدٌ

الْعِقَاب

Na iogopeni adhabu ya (Mwenyezi Mungu ya hapa duniani) ambayo haitawasibu peke yao wale waliodhulumu nafsi zao mionganu mwenu (bali itawasibu hata walionyamaza wasiwakataze, bali na wengineo pia): na jueni ya kuwa Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu. (8:25)

Naye, Mtume (s.a.w.), katika kutuweka wazi juu ya aya hii anatupigia mfano wa yule anayefanya uovu na yule anayeshuhudia uovu katika Hadith ifuatayo:

Nu'maan bin Bashir (r.a.) ameелеza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Mfano wa yule asiyelekemea maovu na yule anayefanya maovu ni sawa na watu wanaosafiri kwenye meli. Wengine wako katika sehemu ya juu na wengine wako chini. Walioko chini hupata maji kutoka kwa walio juu, na kwa hiyo walikuwa wakiwasumbua sumbua (kwa kuwataka wawape maji kila wanapohitajia), hivyo waliamua kutoboa sehemu ya chini ya meli. Kisha wale wa juu waliwajia na kuwauliza, "Imekuwaje (mbona mnatoboa meli)?" Walijibu, "Mmetusumbua (na maji yenu) kwa hiyo tumeona hapana namna nyingine ya kupata maji ila kutoboa tundu yaingie." Kama (wale wa juu) watawakataza wasiendelee na kitendo hicho (cha kutoboa meli) watakuwa wamewaokoa wale wa chini na kujikoka wao wenyewe. Vinginevyo, wakiwaachia waendelee kutoboa watakuwa wamejiangamiza wao wenyewe pamoja na hao wenyeye kutoboa." (Bukhari).

Ugumu wa kusimamisha Uislamu katika Jamii uko wapi?

Tumekwishaona umuhimu wa Uislamu kuyaongoza maisha ya binaadamu katika sura zake zote. Tumezingatia pia nini maana ya kusimamisha Uislamu katika jamii; lengo la kuletwa mitume duniani; na wajibu wetu wa kuhakikisha kuwa siku zote jamii inaongozwa na mafundisho yaliyoletwa na mitume wa Allah (s.w). Ikiwa yote hayo tunayajua na kuyakubali, kwanini hatujaweza kuusimamisha Uislamu katika jamii yetu? Ugumu uko wapi.?

Kushika mamlaka ya dola na kuyatumia hayo kutekeleza maamrisho ya Allah (s.w) ni kazi inayohitaji jitihada kubwa, kujitolea mali na nafsi kwa kiwango kikubwa sana na subira. Kwa sababu ya ugumu wa kazi yenyewe, baadhi yetu tumetafuta njia za mkato au nyepesi za kuikwepa kazi hiyo huku tukijidanganya kuwa tunaifanya kazi hiyo. Hivi sasa Waislamu tumegawanyika katika makundi makubwa matatu.

Kundi la kwanza ni la Waislamu ambao wanahalalisha hali iliyopo kwa hoja kuwa Waislamu ni dhaifu. Waislamu wanakubali kutawaliwa na taratibu za kitwaaghuti kwa sababu hiyo ndiyo hali halisi, na kwamba Uislamu hauwezi kuwa juu ya taratibu hizi za kitwaghuti.

Kundi la pili ni la Waislamu ambao wanachukizwa sana na maisha ya kitwaghuti yanayotawala katika jamii lakini wamekata tamaa na hivyo wameamua kuwa ufumbuzi ni kujitoa katika uhalisia wa maisha ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ya hapa duniani na kujitenga au kujitoa katika maisha ya kijamii kwa kutojihusisha na chochote na badala yake kutafuta kujikurubisha kwa Allah (s.w) kwa dhikri na nyiradi. Yaani wameamua kuwa **watawa**.

Kundi la tatu ni la Waislamu ambao wanaona kuwa hapana haja ya Waislamu kujishughulisha na mamlaka ya dola, badala yake wafanye kazi tu ya kuhimiza na kulingania Uislamu kwa watu binafsi kwa hoja kuwa kila mtu akifuata Uislamu basi Uislamu utakuwa umesimama katika jamii hata kama dola itaendeshwa kitwaaghuti.

Ukweli wa mambo ni kuwa Allah (s.w) amejaalia kuwa ulimwengu huu hauendi ila kwa kufuata zile kanuni au taratibu alizoziweka na yeye Allah (s.w) ndiye Muumba wa vyote vilivyomo. Haiwezekani kwa watu kuzikiuka kanuni alizoziweka Allah (s.w) kisha wakatarajia mafanikio katika mambo yao. Kwa mfano, kwa kanuni alizoziweka Allah (s.w) za namna mwili wa binaadamu unavyofanya kazi, kama mtu atatenganishwa kichwa na kiwiliwili basi mtu huyo atakufa. Hata kama watu hao watakuwa milioni moja au milioni kumi au zaidi; au hata kama watakuwa wacha Mungu au watu waovu; raia au wafalme, wakikatwa vichwa vyao watakufa. Kutarajia kuwa wataendelea kuishi ni kutarajia miujiza. Hali kadhalika, katika maisha ya kijamii Allah (s.w) ameweke kanuni. Moja ya kanuni hizo ni kuwa **mtu asitarajie kupata**

jambo bila ya kufanya juhudi yoyote. Si katika utaratibu wa Allah (s.w) kuwa watu wakavuna mazao mengi na mazuri kwa kucheza bao au karata. Allah (s.w) anasema:

وَأَن لَّيْسَ لِلْإِنْسَنِ إِلَّا مَا سَعَى

“Na ya kwamba hatapata mtu ila aliyoafanya mwenyewe”
(53:39).

Kanuni nyingine ya Allah ni kuwa:

..... إِنَّمَا يُعَذِّبُ مَا يَقُومُ بِهِنَّ يُغَيِّرُوا مَا بِأَنفُسِهِمْ

“.....Hakika ye ye Allah habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili wao yaliyomo nafsini mwao.....” (13: 11)

Kwa kanuni hii iliyotajwa katika Qur'an (13: 11) tunajifunza kuwa kila mmoja wetu amejaaliwa nafsi yenyе nguvu (power) kubwa sana na Allah (s.w). Nguvu ambayo hakuna mja anayeweza kuichezea bila ya ridhaa ya mtu mwenyewe. Ndio maana Allah (s.w) anatuamrisha tusiwatii makafiri pamoja na maguvu waliiyonayo:

يَتَأَكَّلُهَا الظَّبْئِ أَثْقِ الْلَّهَ وَلَا تُطِعِ الْكُفَّارِينَ وَالْمُنَافِقِينَ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْهَا حَكِيمًا ① وَاتَّبَعَ مَا يُوَحَّى إِلَيْكَ مِن رَّبِّكَ إِنَّ اللَّهَ كَانَ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرًا ② وَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ وَكَفَى بِاللَّهِ وَكِيلًا ③

“Ewe Nabii! Mche Allah wala usiwatii makafiri na wanafiki. Hakika Allah ni Mwenye kujua, Mwenye hikima. Na fuata uliyofunuliwa kwa wahayi kutokana na Mola wako Mlezi. Hakika Allah anazo khabari za mnayoyatenda. Na mtegemee Allah. Na Allah anatosha kuwa wa kutegemewa. “ (33: 1-3)

Ametuamuru hilo kwa sababu anajua kuwa uwezo wa kukataa kuwatii makafiri tunao kwa sababu yeye ndiye aliyetujaalia uwezo huo, lakini ikiwa sisi wenyewe tutakuwa tayari kuitumia nguvu hiyo aliyatupatia. Utii hauwezi kupatikana mpaka mtu mwenyewe aamue kumtii huyo anayedai kutiwa. Binaadamu yejote, awe mwanaume au mwanamke, awe huru au mtumwa, raia au mfalme, akikataa kumtii binaadamu mwenzake, basi hakuna anayewenza kumlazimisha kumtii. Sana sana kinachowezza kufanyika ni kumtesa au kumwua. Maswahaba walikuwa wakilazimishwa watoke katika Uislamu na makafiri, walipokataa hawakuwa na lakufanya zaidi ya kuwatesa au kuwauwa. Lakini ikiwa ilitaka kumtawala mtu, kisha mtu huyo akakataa kutawaliwa; nawe kwa ghadhabu ukamwua, bado utakuwa hujamta wala mtu huyo. Kilichotokezea ni kuwa mtu huyo kafanikiwa kuishi hadi kufa bila ya kutawaliwa na wewe.

Tafsiri yake ni kuwa **mtu hawezi kuwa dhalili mbele ya kiumbe mwenzake bila ya ridhaa yake mwenyewe**. Ndio maana kwa mujibu wa mafundisho ya Qur'an siku ya Kiyama Allah hatayapa uzito wowote madai kuwa mtu aliwati makafiri kwa sababu walimlazimisha au kumshinikiza.

Ipo mifano mingi. Huko Rufiji, kuna kisa cha mwanamke mmoja ambaye hakuwa na silaha yoyote zaidi ya jembe. Lakini aliweza kupambana na simba aliye kuwa anataka kumla mwanawewe. Angeweza kusema kuwa sikuwa na la kufanya kwa kuwa mimi ni mwanamke, nilikuwa peke yangu na sikuwa na silaha yoyote. Lakini alimwokoa mwanawewe kwa sababu ndani ya nafsi yake alikwishaamua kuwa liwe litakalokuwa, lakini siwezi nikamwacha mwanangu aliwe na simba nami nikiangalia. Ama nitamwokoa mwanangu au nife nikimtetea mwanangu. Hiyo ndio nguvu ya binaadamu. Halikadhalika hakuna mtu anayekukataza wewe kuswali, kufunga au kuvaahijabu, ikiwa ndani ya nafsi yako umekwishaamua kufanya hivyo.

Ikiwa mtu, ye ye mwenyewe atajiambia na kuamini kuwa hawezi kufanya jambo lolote, basi mtu huyo hawezi kunusuriwa kwa namna yoyote mpaka kwanza ye ye mwenyewe aamini kuwa ye ye ni binaadamu kama binaadamu wengine na kwamba ana uwezo wa kuamua na kuteke1eza analolitaka.

Kwa nini Makafiri wanafanikiwa katika mambo yao?

Kama tulivyotangulia kusema, ulimwengu huu na vyote vilivyomo vimeumbwa na Allah (s.w). Naye amejaalia kuwa vyote vinafuata taratibu au kanuni alizoziweka. Hivyo basi, ili mtu afanikiwe, hana budi kuzijua na kuzifuata kanuni hizo. Hakuna jambo litakalofanikiwa ama kwa kutamani tu, au kwa kuwa na nia njema, au kwa sababu tu ya kuomba dua wakati jambo lenyewe limefanywa kwa kukiuka kanuni za Allah (s.w). Kwa mfano, mkulima hata akiwa mcha Mungu kiasi gani, hata kama atakuwa akimtaja Allah kila wakati na amehifadhi Qur'an yote kifuani hawezi kupata mazao kama katika kulima kwake hafuati majira ya mvua, au hafuati kanuni za kilimo bora. Mlevi anayefuata kanuni hizo atavuna mazao bora kuliko huyo mcha Mungu. Halikadhalika msikiti uliojengwa kwa kuyakusanya tu matope ovyo ovyo utaanguka, na danguro la kufanya ufuska litakuwa imara kama ujenzi wake utafuata kanuni za ujenzi.

Binaadamu anazo sehemu mbili: mwili na roho. Utukufu wake unategemea namna anavyoitekeleza amana yake kama **Khalifa** wa Allah (s.w) hapa duniani. Yaani namna anavyotumia uhuru na uwezo wake wa uchaguzi kufanya mambo yanayoitakasa nafsi yake na jamii pia. Hivyo kuinuka au kuanguka kwa utukufu wa binaadamu kunategemea sana kuimarika au kuzorota kwa kanuni za kimaadili (moral laws) kuliko kanuni za kimaada (physical laws). Kanuni za kimaadili zimegawanyika katika sehemu kuu mbili:

(i) Maadili ya kibinaadamu na (ii) Maadili ya Kiislamu.

(i) Maadili ya Kibinaadamu

Maadili ya kibinaadamu ni yale maadili ya kimsingi kabisa ambayo ni lazima yapatikane ili binaadamu apate mafanikio katika yale anayoyafanya yawe ya kheri au ya shari. Maadili hayo ya kibinaadamu hayana uhusiano wowote kama mtu anamwamini Allah (s.w) au la; anaamini mitume wa Allah (s.w) au la; anaamini kuwepo kwa siku ya Mwisho au la; mcha Mungu au twaghuti, ana nia njema au la; anafanya kheri au la. Yaani ili mtu afanikiwe katika hilo alilolikusudia liwe zuri au baya zipo sifa za kimaadili ambazo lazima awe nazo. Sifa hizo ni:

- (a) Dhamiri madhubuti ya kuliendeja jambo.
- (b) Uwezo wa kufanya maamuzi.
- (c) Shauku na nia ya kuling'a'ng'ania jambo.
- (d) Subira na ujasiri.
- (e) Kufanya kazi kwa bidii usiku na mchana.
- (f) Kulipenda lengo na kuwa tayari kujitolea kwa chochote, iwe juhudhi, mali au wakati.
- (g) Uangalifu na busara katika kuliendeja jambo.
- (h) Uwezo wa kupanga na kuhamasisha watu.
- (i) Nidhamu na kuyarekebisha makosa yanapotokea.

Watu watakaokuwa na maadili hayo ya kibinaadamu, watafanikiwa katika kutimiza malengo yao waliyoyapanga. Hata kama malengo yenyehe hayatakuwa na kheri katika jamii. Na hilo ndilo jawabu la lile swalii letu. Kwanini makafrii wanafanikiwa katika mambo yao? Kwanini wasifanikiwe ikiwa usiku na mchana wanafanya kazi na wanatumia juhudhi kubwa na kujitolea mali na nafsi zao ili wapate malengo yao?

Hebu tuangalie mifano halisi inayotuhusu sisi Waislamu wa Tanzania. Waislamu tunajua Mtume (s.a.w) amesema nini kuhusu

umuhimu wa watu kuisoma Qur'an, kuielewa, kuizingatia, kuifundisha na kuitekeleza. Zipo Hadith nyingi, hatuna haja ya kuzinukuu.

Marekani kwa kupitia aliyekuwa Waziri wa Mambo ya nchi za nje wa zamani Bw. Collin Powell, na Waziri wa Ulinzi Bwana Donald Rumsfed wamesema kuwa umadhubuti wa Waislamu unatokana na wao kuisoma, kuifundisha, kuiamini na kuifuata Qur'an. Hivyo ufumbuzi wa kudumu ni kuwatoa Waislamu katika Uislamu wao kwa kuingilia mafundisho ya Qur'an. Na njia nzuri ni kuanzia kwenye madrasa zao. Kampeni hiyo iwe dunia nzima. Hapa tutaangalia tu wanayoyafanya Tanzania na mafanikio yao ukilinganisha na yetu sisi wanaharakati.

Njia ya kwanza waliona ni kutoa misaada kwenye madrasa ili iwe ni mwanya na hatimaye kubadilisha mitaala ya madrasa. Huko Kenya wakaenda kwa pupa kwa balozi wa Marekani kutoa rundo la misaada ya vitabu na pesa kwa madrasa. Waislamu wakashituka na wakakataa. Makafiri hawakukata tamaa wakajifunza kosa lao. Hapa Tanzania, wakaamua kuwa kwanza kabisa waanze na utafiti utakaowajulisha ukweli halisi juu ya madrasa. Na wakaona Marekani wasionekane waziwazi. Wakawatumia watu wengine, yaani shirika la Kijerumanii liitwalo **Konrad Adeneur Stiftung**. Mwezi Mei/Juni 2003 walifanya utafiti wao waliouita "**Qur'an Madrasa Baseline Survey**." Yaani utafiti wenye lengo la kujua hali halisi ya Madrasa kwa mkoa wa Dar es Salaam. Waliyagundua mengi, lakini kwa sasa tuseme tu kuwa baadhi ya waliyoyajua ni kuwa karibu nusu ya walimu wa madrasa wanapata mshahara wa chini ya shilingi 10'000/= kwa mwezi. Na wengine hawalipwi kabisa. Theluthi mbili ya madrasa zinamilikiwa na watu binafsi na zipo vibarazani. Wazazi na viongozi wa Kiislamu hawana taarifa wala hawataki kufuatilia kinachoendelea kwenye hizo madrasa. Baada ya kuupata ukweli huo Marekani ikaamua kuanza kuingilia madrasa kwa kuanzia Zanzibar.

Kwa ufupi ni kuwa Serikali ya Marekani kwa kupitia Shirika lake liitwalo USAID linasaidia madrasa huko Zanzibar. Waislamu tunasaidiwa kwa kupitia mifuko mikubwa minne. **Mfuko wa Rais Bush wa Elimu ya Waislamu** (President Bush's Muslim Education Initiative); **Mfuko wa Rais Bush wa Kupambana na Ugaidi Afrika Mashariki** (President Bush's East Africa Counter-terrorism Initiative); **Skolaship za Balozi kwa Wasichana** (The Ambassador's Girls' Scholarship Program) na **Mfuko wa Elimu Afrika** (Africa Education Initiative). Wanazitumia pesa hizo kuwasomeshea walimu wa Kiislamu, kuandaa mitaala na vitabu, kuwalipa mishahara walimu, na viongozi wa jamii, na kuwasaidia pia kipesa watoto Masikini. Wameanzisha pia Kituo cha Vitabu vy'a Rejea vy'a madrasa Zanzibar (The Zanzibar Madrasa Resource Centre). Kwa misaada hiyo Marekani kwa kupitia mradi wa MKEZA (Mradi wa Kuendezeza Elimu Zanzibar) imekwisha kujenga madrasa 16. Moja ya madrasa hizo ni ile aliyoitembelea mke wa Bush, Laura, Julai 2005. Na kwa mujibu wa USAID wenywewe hivi sasa Marekani ndiye mfadhili mkubwa kuliko wengine wote katika nyanja zote za elimu huko Zanzibar.

Na mionganoni mwa mafanikio ya hizo madrasa zao ni kuwa hivi sasa watu wengi wanajiunga nazo wakiwemo Wakristo. Wanasema USAID kuwa hiyo ni ishara kuwa wanatoa elimu nzuri inayopendwa na watu wa dini zote! Kwa upande wa Tanzania Bara USAID kwa kushirikiana na Bakwata wametoa kitabu cha Mwongozo wa Kufundishia Waalimu wa Kiislamu. USAID pia ilitoa mafunzo kwa walimu 54 wa madrasa ya kuwafundisha watoto wa kiislamu namna ya kupambana na ukimwi. Mwongozo huo wa vitabu 2,500 uligawanywa kwa walimu wa madrasa Dar es Salaam na Iringa. (Taarifa hizi zote tumezipata kutoka katika tovuti ya USAID /Tanzania.)

Ikumbukwe kuwa mwaka 1990 Padre mmoja wa Kanisa Katoliki aliomba Bakwata imruhusu awasomeshe watoto wa madrasa Qur'an na lugha ya Kiaarabu, ili waweze kusoma kwa muda mfupi kabisa. Bakwata walikataa. Kwa sababu watoto wa Kiislamu hawawezi kufundishwa dini yao na mtu anayeichukia na kuipiga vita dini hiyo.

Leo, yale yale waliyoyakataa Bakwata wakati ule yanafanyika tena kwa shangwe na vifijo. Swali: Hivi kwanini leo Wamarekani wanaowauwa Waislamu wenzetu huko Afghanistan, Iraq na Palestina wakawa ndio wafadhili pekee wa madrasa huko Zanzibar kwenye asilimia 99 ya Waislamu? Kwanini makafiri hawa wanafanikiwa? Al-jawab. "**Wamefuata zile kanuni za maadili ya kibinadamu**" tulizozitaja hapo juu. Watu hawawezi kuijua na kuifuata Qur'an kwa sababu tu sisi tunatamani, na ilhali hatupo tayari kutumia mali zetu, nafsi zetu, wakati wetu na juhud zetu kuhakikisha hilo linafanyika. Huko Zanzibar, USAID imekwishatumia **mamilioni** ya shilingi ili kufikia malengo yake.

(ii) Maadili ya Kiislamu

Maadili ya Kiislamu ni yale yale ya kibinaadamu isipokuwa kinachobadilika ni mwelekeo na matumizi ya maadili hayo. Maadili ya kibinaadamu yanapoongozwa na Tawhiid na yakawa lengo lake wakati wote ni kupata radhi za Allah (s.w) basi yatakuwa ni maadili ya Kiislamu. Maadili ya Kiislamu yanakuwa ni bora zaidi kwa sababu wakati wote yanatumika katika kusimamisha uadilifu katika jamii.

Kanuni ya Allah kuhusu uongozi katika jamii

Kanuni aliyoiweka Allah (s.w) kuhusu nani wawe viongozi katika jamii ni hii:

Uongozi wa watu katika jamii siku zote huchukuliwa na wale watu ambao wamechanganya maadili ya kibinadamu na yale ya Kiislamu. Ikiwa hakuna wenyе sifa hiyo basi uongozi utakwenda kwa wale wenyе maadili ya kibinaadamu, hata kama hawatakuwa

waadilifu. Lakini watu wen`ye maadili ya Kiislamu na ya kibinadamu, hata kama hawatakuwa na rasilimali za kutosha watawashinda wale wenyе rasilimali lakini hawana maadili ya Kiislamu. Rejea Qur'an:

يَتَأْلِمُهَا النَّبِيُّ حَرَّضَ الْمُؤْمِنِينَ عَلَى الْقِتَالِ إِن يَكُن مِّنْكُمْ عَشْرُونَ
صَابِرُونَ يَعْلَمُوْا مِائَتَيْنِ وَإِن يَكُن مِّنْكُمْ مِّائَةٌ يَعْلَمُوْا أَلْفًا مِّنَ
الَّذِينَ كَفَرُوا بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا يَفْقَهُوْنَ ﴿٦٥﴾

Ewe Mtume (wa Mwenyezi Mungu)! Wahimize walioamini wende vitani. Wakipatikana kwenu watu ishirini wanaosubiri watashinda mia mbili. Na kama wakiwa watu mia moja kwenu watashinda elfu moja ya wale waliokufuru, maana hao ni watu wasiofahamu (uhai wa Akhera) (8:65)

Hivyo, ukweli unabakia kuwa ugumu wa kusimamisha Uislamu upo katika nafsi zetu. Na kwamba hatuko tayari na hatuna ujasiri wa kupambana ili kubadilisha mfumo wa kitwaaghut uliopo.

Zoezi la Kwanza

1. (a) Kwa kurejea Qur'an(57:25)bainisha lengo kuu la kuletwa Mitume wa Allah(s.w.)
(b) Kwa kurejea Qur'an bainisha lengo kuu la kuletwa Mtume Muhammad(s.a.w) kisha onesha kuwa Mtume(s.a.w) alilifikia lengo hilo.
2. Nini maana ya kusimamisha Uislamu katika Jamii?
3. (a) Ni upi umuhimu wa kusimamisha Uislamu katika Jamii?
(b) Kwanini ni muhimu kusimamisha Uislamu katika jamii?
4. Pamoja na idadi ya waislamu kuwa kubwa katika jamii kwanini Uislamu haujasimama hivi leo?
Kwanini Makafiri wanafanikiwa katika harakati zao za kuuhilikisha Uislamu katika jamii?
6. Waislamu wafanyeje ili waweze kusimamisha Uislamu katika jamii.



Sura ya Pili

KUANDALIWA MTUME(S.A.W) NA MAFUNZO YATOKANAYO

Utangulizi

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ
عَلَى الْأَدِيْنِ كُلِّهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ ﴿٣﴾

“Yeye ndiye aliyemleta Mtume wake kwa uongofu na Dini ya haki ili aijaalie kushinda Dini zote ijapokuwa washirikina watachukia.” (9:33, 61:9)

Aya hii inatufahamisha kuwa lengo kuu la kuletwa Mtume Muhammad (s.a.w) ni kusimamisha Dola ya Kiislamu kama alivyofanya. Nasi Waumini tunalazimika kufuata nyayo za Mtume (s.a.w) na kuhakikisha kuwa Uislamu unasimama katika jamii zetu kama inavyosisitizwa katika Qur-an:

لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِمَنْ كَانَ يَرْجُوا اللَّهَ وَالْيَوْمَ
الْآخِرَ وَذَكَرَ اللَّهَ كَثِيرًا ﴿٢١﴾

Bila shaka mnao mfano mwema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, kwa mwenye kumuogopa Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, na kumtaja Mwenyezi Mungu sana” (33:21)

Kumuigiza Mtume (s.a.w) ni kufuata Sunnah ya Mtume (s.a.w) kwa kutekeleza yale aliyotuamrisha na kuacha aliyotukataza na kuiga tabia yake adhimu katika kuendesha maisha yetu ya kila siku ya kibinagsi, kifamilia na ya kijamii. Sunnah kuu ni ile ya kumuigiza Mtume (s.a.w) katika kuliendea lengo kuu aliloletwa kwalo la kusimamisha Uislamu na kuufanya utawale maisha yote ya jamii.

Hatutaweza kumuigiza Mtume(s.a.w) katika kusimamisha Uislamu bila ya kujiandaa kama yeye alivyoandaliiwa na Mola wake au bila ya kuzingatia na kuyatia vitendoni mafunzo tunayopata kutokana na kuandaliwa kwake.

Zama za Jahiliyyah

Zama za jahiliyyah ni zile zama ambazo watu walikuwa wakiendesha maisha yao ya kibinagsi na kijamii kwa kufuata matashi yao kinyume na muongozo wa Allah(s.w.) na Mitume wake. Wakati Mtume (s.a.w) anazaliwa katika karne ya Sita (570 A.D) dunia ilikuwa katika giza totoro la ujahili. Wakazi wa Bara Arab, katika kipindi hicho walikuwa chini sana kimaadili. Ubabe, unyanganyi na uporaji mali ya misafara ya biashara yalioneckana matendo ya kishujaa na ya kujivunia. Wanyonge hawakuwa na haki, wanawake walinyanyaswa na kudhalilishwa hadi kufikia watoto wa kike kuzikwa wangali hai na wanawake kurithiwa kwa nguvu kama ilivyorithiwa mali.

Kwa muhtasari hali ya Bara Arab wakati huo wa Jahiliya ilikuwa kama alivyoeleza Jaffari bin Abu Twalib mbele ya Mfalme Najash kwa niaba ya waislamu aliwaongoza katika hijira ya Uhabeshi::

"Ewe Mfalme, sisi tulikuwa waovu na majahili, tukiabudia masanamu na kula nyamafu hata mizoga ya wanyama waliokufa wenyewe. Tulifanya kila aina ya matendo machafu na ya aibu. Hatukuwa wenyewe kuwajibika kwa jirani na jamaa zetu. Wenyewe nguvu mionganoni mwetu waliwakandamiza wanyonge. Kisha Allah akamleta Mtume mionganoni mwetu ambaye tulimfahamu vema kwa nasaba yake, utukufu wake na uzuri wa tabia yake adhimu. Alituita tumuabudu Mungu mmoja tu na akatukataza kuabudia masanamu na mawe. Alitufundisha kusema ukweli kutunza amana,

kuwaangalia ndugu na jamaa na kuwafanyia wema na kuacha maovu. Alituamrisha kusimamisha swala na kutoa Zakat. Alituamrisha kujiepusha na maovu na kujiepusha na umwagaji damu. Alitukataza zinaa, kusema uwongo, kula mali ya yatima na kuwasiningizia uovu wanawake watwaharifu. Alitufundisha Qur-an... ”
(A.H. Siddiqui – The life of Muhammad uk.78).

Hali hii ya ujahili haikutawala Bara Arab peke yake, bali katika karne hii ya 6 A.D ulimwengu wote, Mashariki na Magharibi, ulizama katika giza totoro la uovu na ujahili. Ulimwengu katika zama hiso, wanyonge na watu wa chini walikandamizwa na kudhulumiwa pasina chembe ya huruma na wenye uwezo na watukufu mionganoni mwao.

Katika kipindi hicho, hata wale waliodai kufuata mafundisho ya Mitume wa Mwenyezi Mungu, Mayahudi na Wakristo, walikuwa katika giza hilo hilo la uovu na ujahili, Mayahudi waliacha mafundisho ya Mtume wao na wakaamua kuishi kulingana na matamanio ya nafsi zao. Walipotokea Mitume walifanyiwa maovu mengi kama ilivyobainishwa katika Qur-an. Wakristo nao waliacha mafundisho sahihi ya Nabii Issa (a.s) badala yake wakafuata Ushirikina wa Kirumi. Walileta uzushi mwingi juu ya Dini ya Allah (s.w) kama tunavyojifunza katika Qur-an:

وَقَالَتِ الْيَهُودُ عُزَيْرٌ أَبْنُ اللَّهِ وَقَالَتِ النَّصَارَى الْمُسِيَّخُ أَبْنُ اللَّهِ ذَلِكَ
 قَوْلُهُمْ بِأَفْوَاهِهِمْ يُضَاهِئُونَ قَوْلَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ قَبْلِ قَتْلَهُمُ اللَّهُ
 أَنَّى يُؤْفَكُونَ

“Na Mayahudi wanasema: Uzeiri ni Mwana wa Mwenyezi Mungu’ na Wakristo wanasema; ‘Masihi ni Mwana wa Mwenyezi Mungu’; haya ndiyo wayasemayo kwa vinywa vyao. Wanayaiga maneno ya wale walokufuru kabla yao, Mwenyezi Mungu awaangamize. Wanageuzwa namna gani hawa!(9:30)

أَتَخْذُوا أَحْبَارَهُمْ وَرُهْبَانَهُمْ أَرْبَاتًا مِّنْ دُونِ اللَّهِ وَالْمُسِيحَ أُبْنَى مَرْيَمَ
وَمَا أُمِرْتُ إِلَّا يَعْبُدُوا إِلَهًا وَاحِدًا لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ سُبْحَانُهُ وَعَمَّا يُشْرِكُونَ

Wamewafanya Wanavyuoni wao na Watawa wao kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu, na wamemfanya Masihi Mwana wa Maryamu (pia Mungu) hali hawakuamrishwa isipokuwa kumuabudu Mungu mmoja, hakuna anayestahiki kuabudiwa ila Yeye. Ametakasika na yale wanayomshirikisha nayo.” (9:31).

﴿ يَتَأَيَّهَا الَّذِينَ ظَاهَرُوا إِنَّ كَثِيرًا مِّنَ الْأَحْبَارِ وَالرُّهْبَانِ لَيَأْكُونُ أَمْوَالَ

الَّذِينِ بِالْبَطْلِ وَيَصُدُّونَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ وَالَّذِينَ يَكْبِزُونَ الْذَّهَبَ

وَالْفِضَّةَ وَلَا يُنِيقُونَهَا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَبَشِّرُهُمْ بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴾٩٣﴾

“Enyi Mlioamini! Wengi katika Makasisi(Wanavyuoni wa Mayahudi na wakristo) na Watawa (wao) wanakula mali za watu kwa batili na kuwazulia njia ya Mwenyezi Mungu... ”
(9:34)

Katika kipindi hicho cha historia utawala wa Kikristo Ulaya Magharibi uliwakandamiza na kuwanyonya wanyonge kama utawala wa kishirikina ulivyokuwa ukifanya huko Mashariki ya Kati na Mashariki ya mbali. Katika kipindi hiki wanasyansi walioibuka na ugunduzi ulio kinyume na maelezo ya Wakuu wa Kanisa walisulubiwa na kuuliwa kinyama.

Kuandaliwa Mtume(s.a.w)

Mitume huzaliwa Mitume. Mitume wa Allah wamekusudiwa kuwa walimu na viigizo katika jamii zao. Hivyo Allah (s.w) Mjuzi Mwenye Hekima, aliwaandaa kuanzia mbali kabisa, ili kuwawezesha kufikia lengo kuu lililo kusudiwa na ili kuifanya kila hatua ya maisha yao iwe ni funzo kwa Umma zao na Umma zilizofuatia.

Tukirejea historia, tunaona kuwa Mtume Muhammad (s.a.w) alipata maandalizi ya aina mbili, Maandalizi ya Ki-il-hamu na Maandalizi ya kufunzwa na kuelekezwa moja kwa moja.

Maandalizi ya Ki-il-hamu

Ni maandalizi yaliyompitia Mtume (s.a.w) katika kipindi cha miaka 40 kabla ya kupewa Utume rasmi. Katika maandalizi haya hapana mafunzo rasmi yanayotolewa bali tunajifunza kutokana na matukio na mazingira kuwa palikuwa na mpango maalum uliopangwa kumuaanda Mtume(s.a.w). Ili tuone maandalizi haya hebu tuzingatie matukio machache katika maisha ya Muhammad (s.a.w) kabla ya kupewa Utume ikiwa ni pamoja na:

- (i) Kuzaliwa Makka katika kabilia tukufu la Quraish
- (ii) Kupewa jina la Muhammad
- (iii) Malezi bora aliyoyapata
- (iv) Tabia njema isiyo na mfano wake
- (v) Ndoa yake na Bibi Khadija
- (vi) Kuchukia maovu na kujitenga pangoni

(i) Kuzaliwa Makka katika kabilia la Quraish

Mtume (s.a.w) kuzaliwa Makkah katika kabilia tukufu la Quraysh, chini ya ulezi wa Babu yake Abdul-Muttalib, aliyekuwa kiongozi wa Maquraysh, ni kielelezo kuwa alistahiki kuchaguliwa kuwa kiongozi wa watu wake. Kabilia la Quraish ni katika kizazi cha Nabii Ibrahim (a.s) kupitia kwa Ismail (a.s). Mtume (s.a.w) kuwa Mtume na kiongozi wa Dola ya Kiislamu ni jibu la dua ya Nabii Ibrahim baada ya kukamilisha kazi ya kujenga upya Ka'abah:

وَإِذْ يَرْفَعُ إِبْرَاهِيمُ الْقَوَاعِدَ مِنَ الْبَيْتِ وَإِسْمَاعِيلُ رَبِّنَا تَقَبَّلْ
مِنَّا إِنَّكَ أَنْتَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ

Na (kumbukeni khabari hii pia) Ibrahimu alipoinua kuta za nyumba (hiu ya Al-Kaaba) na Ismail (pia); (wakaomba

wakasema) “Ee Mola wetu! Tutakabalie (amali yetu hii ya kujenga huu msikiti). Hakika wewe ndiye Mwenye kusikia, na Mwenye kujua.” (2:127

رَبُّنَا وَأَبْعَثْ فِيهِمْ رَسُولًا مِّنْهُمْ يَشْتُرُ عَلَيْهِمْ ءَايَاتِنَاكَ وَيُعَلِّمُهُمْ الْكِتَابَ

وَالْحِكْمَةَ وَيُرِكِّبُهُمْ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

“Ee, Mola wetu! Walettee Mtume anayetokana na wao, awasomee Aya Zako, na kuwafundisha Kitabu (chako) na hikima na awafundishe kujitakasa (na kila mabaya). Hakika Wewe ndiye Mwenye nguvu, na ndiye Mwenye hikima. (2:129)

(ii) Kupewa jina la Muhammad (s.a.w)

Kuzaliwa kwa Mtume (s.a.w) na kupewa jina la Muhammad na Babu yake, lilito na maana sawa na lile la Ahmad alilooteshwa mama yake ni jambo jingine linalothibitisha maandalizi haya. Jina la Ahmad lilitabiriwa katika Taurat na Injili kama tunavyojifunza katika Qur-an:

وَإِذْ قَالَ عِيسَى أَبْنُ مَرْيَمَ يَدْبَيْتَ إِسْرَائِيلَ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ

إِلَيْكُمْ مُّصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيِّ مِنَ النُّورَةِ وَمُبَشِّرًا بِرَسُولٍ يَأْتِي مِنْ

بَعْدِي أَسْمُهُ وَأَحْمَدُ فَمَمَا جَاءَهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ قَالُوا هَذَا سِحْرٌ مُّبِينٌ

“Na (wakumbushe) aliposema Issa bin Maryamu, ‘Enyi wana wa Israil! Mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu, nisadikishaye yaliyokuwa kabla yangu katika Taurat, na kutoa habari njema ya Mtume atakayekuja nyuma yangu ambaye jina lake litakuwa Ahmad. Lakini alipowajia kwa hoja zilizowazi walisema, ‘huu ni udanganyifu uliodhahiri’. (61:6).

(iii) Malezi bora aliyoyapata

Pamoja na kuwa Muhammad (s.a.w) alizaliwa akiwa yatima, alipata malezi bora na ya huruma kupitia kwa mama yake wa kunyonya- Bibi Halima bint Abi-Dhuaby. Mama huyu wa kabila la

Bani Khawaizin ambalo lina sifa ya usafi na lugha fasaha ya Kiarabu alitokea Taifu mji wenyewe hali nzuri ya hewa kwa kulelea watoto. Mtume alipata bahati ya kukaa miaka mine badala ya miwili kutokana na magonjwa ya milipuko yaliyojitokeza Makkah jambo ambalo lilimuwezesha kuzungumza kiarabu kwa ufasaha zaidi kuliko watu wengine wa Makkah. Mama yake Amina bint Wahhab alimlea mpaka alipofikisha umri wa miaka 6 akafariki. Babu yake Abdul-Muttalib aliendelea kumlea na alipofikisha umri wa miaka 8 akafariki. Kisha alilelewa na ‘Ami yake Abu Talib ambaye aliendelea kuwa naye mpaka alipopewa utume na aliquwa akimlinda mpaka alipofariki Mtume(s.a.w) akiwa na miaka kumi ya utume. Hii haikutokea tu kwa bahati nasibu, bali tunafahamishwa katika Qur-an kuwa ni maandalizi maalum aliyoyapanga Allah (s.w).

اللَّمْ يَجِدُكَ يَتِيمًا فَقَوْيِ
①

*Je! Hakukukuta yatima akakupa makazi (mazuri ya kukaa)?
(93:6).*

(iv) Tabia yake njema isiyo na mfano wake

Tabia nzuri ya Mtume (s.a.w) haikuishia utotoni mwake tu iliendelea katika umri wake wote. Tunajifunza katika historia kuwa hata alipokuwa mtoto hakuwahi kufanya vitendo vya kipuuzi vya kitoto na aliquwa ni mwenye haya sana. Wakati fulani kuta za Ka'abah zilifanyiwa ukarabati. Wavulana wadogo wadogo nao wakashiriki katika kazi ya ukarabati. Wavulana hawa walizitoa nguo zao zakiunoni na kuziweka mabegani ili kubebea mawe. Abu Talib alimshauri Mtume (s.a.w) naye ajiunge na watoto wensiwe. Mtume (s.a.w) alikubaliana na ushauri wa Ami yake, lakini aliquwa na haya sana hata katika umri ule wa utotoni. Hivyo, alipojaribu naye kuvua nguo yake na kubaki uchi, alishikwa na bumbuazi (butwaa) na kuanguka chini.

Mtume (s.a.w) tangu utotoni mwake aliepukana na tabia zote chafu zenye kuchukiza watu kwa ujumla. Pia aliepushwa na matendo yote maovu yenye kumchukiza Allah (s.w) ambayo

yalionekana mazuri mbele za watu wa jamii yake. Kwa mfano katika umri wa ujana wake aliazimia mara mbili kuhudhuria mikesho ya ngoma za harusi za rafiki zake wawili lakini Allah (s.w) alimwepusha na mikesha hiyo kwa kumpa usingizi mzito mpaka asubuhi kwa safari zote mbili.

Tangu utotoni mwake Mtume (s.a.w) alichukia sana Ibada ya masanamu. Hakupata kuhudhuria hata mara moja ibada za masanamu wala hakupata kula kilichoandalowi kwa ajili ya masanamu. Moyo wake pia ulichukia maovu yote mengine yaliyofanywa matendo ya kawaida na watu wa jamii yake kama vile ulevi, uzinifu, uchezaji kamari, ulaji riba, udhalimu, ulaji wa vyakula vya haramu, n.k.

Tangu utotoni mwake, Muhammad (s.a.w) alisifika kwa kila sifa nzuri zilizobainishwa katika Qur'an. Bibi 'Aisha (r.a) alipoulizwa juu ya tabia ya Mtume (s.a.w) alijibu kuwa tabia yake ni Qur'an. Yaani Mtume (s.a.w) amejipamba na vipengele vyote vya tabia njema vilivvobainsihwa katika Qur'an tangia utotoni mwake. Qur'an yenyewe katika mionganini mwa aya zake za mwanzo mwanzo kushuka, inamsifu Mtume (s.a.w) kwa tabia yake tukufu:

وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ حُكْمٍ عَظِيمٍ

“Na bila shaka unatabia njema kabisa” (68:4)

Aya hii haielezi kuwa tabia yake ilikuwa njema tu pale alipopata utume bali inaashiria kuwa tabia yake njema anayo tangu utotoni mwake. Muhammad (s.a.w) tangu utotoni mwake tumeona kuwa alikuwa mpole, mtulivu, mwenye huruma, mwenye haya na mwenye sifa zote nzuri zilizowapendeza watu na kuwavutia. Alikuwa mashuhuri Bara Arab nzima kwa ukweli na uaminifu wake. Alikuwa mkweli mno mpaka akapewa jina la “As-Sadiq” – “mkweli” na alikuwa mwaminifu mno mpaka akapewa jina la Al-Amin. Muhammad (s.a.w) alikuwa haitwi ila kwa jina la **As-Sadiq**

Al-Amin. Wakubwa na wadogo walimheshimu na walimpa amana zao kuwawekea hata baada ya kupewa Utume. Tabia yake njema isiyo na mfano wake katika jamii yake ni uthibitisho kuwa Mutme (s.a.w) aliandaliwa ki-il-hamu kabla hajapewa utume.

Tabia yake njema isiyo na mfano wake kuanzia utotoni hadi utuuzima wake inaashiria wazi kuwa hakuwa zao la jamii yake, bali aliandaliwa na Mola wake awe vile ili awe kiigizo chema kwa watu wa Umma wake.

(v) Ndoa yake na Bibi Khadija

Umaarufu wa Muhammad (s.a.w) kutokana na tabia yake tukufu ulienea Bara Arab nzima. Bibi Khadijah, mwanamke mjane miongoni kwa matajiri wakubwa wa Makkah, alivutiwa na tabia ya Muhammad (s.a.w). Bibi Khadijah alimtaka Muhammad ampelekee bidhaa zake Yemen kwa ujira wa ngamia wawili. Muhammad (s.a.w) alikubali na alirejea na faida kubwa zaidi kuliko matazamio ya Bibi Khadijah. Bibi Khadijah alivutika kwa faida hiyo kubwa na ikambidi tena amuombe Muhammad (s.a.w) ampelekee bidhaa zake Sham(Syria)kwa malipo ya ngamia wanne. Katika msafara huu, Muhammad (s.a.w) alimletea Bibi Khadijah faida kubwa zaidi ya mategemeo yake. Khadijah alikuwa hajawahi kupata faida kubwa kiasi kile tangu aanze kufanya biashara katika misafara ya Sham. Pamoja na furaha ya kupata faida kubwa kiasi hicho, Bibi Khadija alizidi kufurahi na kuvutiwa na Muhammad aliposikia sifa zake za ajabu kutokana na taarifa ya mtumishi wake Maisarah waliyeongozana naye. Kutokana na alivyovutika Bibi Khadijah hakuweza kustahamili kukaa mbali na Muhammad (s.a.w) Hivyo alimtaka radhi Muhammad na kuomba amuo. Bibi Khadijah wakati huo alikuwa mjane mwenye umri wa miaka 40, aliyewahi kuolewa mara mbili na kujaaliwa kupata watoto watatu – wawili wanaume na mmoja mwanamke. Kabla ya hapo matajiri na machifu wengi wa Makkah walipeleka posa zao kwa Bibi

Khadijah lakini aliwakatalia. Muhammad (s.a.w) akiwa na umri wa miaka 25, alikubali ombi la Bibi Khadijah baada ya kushauriana na ami yake, bila ya kujali tofauti kubwa ya umri iliyokuwepo.

Baada ya kuoana, Bibi Khadijah alimuingiza Muhammad kwa ukamiifu katika biashara, akiwa si mwajiriwa tena kama ilivyokuwa katika safari mbili za mwanzo, bali baba na kiongozi wa familia. Muhammad (s.a.w) alifika sehemu mbali mbali za Bara Arab kwa shughuli ya biashara ikiwa ni pamoja na Bahrain na Yemen. Muhammad (s.a.w), kwa kushauriana na mkewe, alitumia sehemu ya utajiri wao katika kuwakomboa watumwa na vijakazi waliokuwa wakifanyiwa ukatili na mabwana zao. Bibi Khadijah alimzawadia Mtume (s.a.w) mtumwa wake aliyeitwa Zaid bin Harith. Mtume (s.a.w) alimpa Zaid uhuru wake na kumfanya mtoto wake wa kupanga. Pia walitumia utajiri wao katika kuwasaidia maskini na kuwalipia madeni wale waliokuwa hawana uwezo wa kulipa madeni yao.

Mtume (s.a.w) na mkewe Khadijah waliishi maisha mazuri ya kifamilia yaliyokuwa mfano bora wa kuigwa. Upendo, huruma na wema wa Mtume (s.a.w) kwa kila mtu, licha kwa familia yake, unafahamika. Bibi Khadijah naye, kwa kumjua Mtume (s.a.w) kuwa ni mtu mtukufu hata kabla hajatangaziwa utume rasmi, alikuwa ni kiliwazo cha Mtume kabla na baada ya utume. Alimfariji na kumpa ushauri mzuri kwa kila gumu lililomfika Mtume(s.a.w) katika maisha yote walipokuwa pamoja. Katika watoto saba wa Mtume (s.a.w), watoto sita wamezaliwa na Khadijah nao ni: Qasim, Zaynab, Ruqiyah, Umm Kulthum, Fatimah na ‘Abdullah. Watoto wote isipokuwa ‘Abdullah, walizaliwa kabla ya utume. Wanawe wa kiume walifariki wakiwa bado watoto katika kipindi cha utume cha Makkah. Mtoto wa saba wa Mtume (s.a.w) ni Ibrahim aliyezaliwa na mjakazi wake, Mariam bint Kibtiyah katika kipindi cha utume cha Madinah. Naye alifariki angali mtoto.

Hivyo ndoa ya Mtume (s.a.w) na Bibi Khadija haikutokea kwa bahati nasibu tu, bali ulikuwa mpango madhubuti wa Allah (s.w) ili kumtajirisha Mtume ili aweze kutoa mchango wake katika kuwahurumia na kuwasaidia madhaifu katika jamii yake, na ili awe mfano wa kuigwa na matajiri katika kutoa mali kwa ajili ya Allah katika kuwahurumia wanajamii. Qur-an inatufahamisha:

وَوَجَدَكَ عَلَيْلًا فَأَغْنَى

Na akakukuta fakiri akakutajirisha?” (93:8)

Muhammad (s.a.w) alikuwa fakiri kabla ya kumuoa Khadija na kuwa tajiri mkubwa baada ya kumuoa Khadija

(vi) Kuchukia maovu na kujitenga pangoni

Kuchukia maovu na kujitenga pangoni, ni tukio lingine linaloonesha kuandaliwa kwa Mtume (s.a.w). Muhammad (s.a.w) tangu angali kijana alijihuisha mno na masuala ya kijamii na alikuwa akikereka sana kuona wanyonge wakidhulumiwa. Akiwa na umri wa miaka 20 alijunga na Chama cha kuwatetea wanyonge dhidi ya Madhalimu. Mtume (s.a.w) alikosa usingizi kwa Sababu ya matatizo ya wengine na alikuwa na shauku kubwa ya kutafuta njia ya kuitoa jamii yake kwenye uovu na upotofu na kuipeleka kwenye wema na uongofu. Katika hali hiyo ilibidi ajitenge pangoni ili kutafuta msaada kwa Muumba Wake na aliupata kwa njia ya ndoto na baadaye kutumiwa Malaika Jibril. Allah (s.w) anamkumbusha Mtume wake juu ya maandalizi haya:

أَلْمَنْتَرِحُ لَكَ صَدْرُكَ ① وَوَضَعْتَا عَنْكَ وِزْرَكَ ② الَّذِي أَنْقَضَ

ظَهُرَكَ ③

“Je! Hatukukupanulia kifua chako. Na tukakuondolea mzigo wako (mzito) uliovunja mgongo wako?” (94:1-3)

وَوَجَدَكَ ضَلَالًا فَهَدَى

“Na akakukuta hujui kuongoza njia akakuongoza?” (93:7).

Mzigo uliovunja mgongo wa Muhammad (s.a.w) kipindi kile si mwingine ila ile hali ya udhalimu na uovu iliyoshamiri katika jamii yake. Alikuwa na ari kubwa ya kuiondoa ile hali na kusimamisha uadilifu katika jamii lakini hakujua ni vipi atafanikisha hilo.

Mafunzo yatokanayo na maandalizi ya ki-il-hamu

Kutokana na matukio haya yanayoashiria kuandaliwa kwa Mtume (s.a.w) kabla ya kupewa Utume rasmi, tunajifunza kuwa katika kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii hatuna budi kuzingatia haya yafuatayo:

Kwanza, hatunabudi kuwaandaa watoto wetu kuwa Makhalfa wa Allah (s.w) mapema kabla hata hawajazaliwa. Maandalizi haya yanawezekana pale wazazi wote wawili watakapokuwa na mtazamo huo wa Ukhalfa. Kisha baada ya watoto kuzaliwa tuwaadhini na kuwakimia, tuwafanyie aqika na kuwapa majina mazuri, tuwalee kwa mapenzi na huruma na kuwafunza tabia njema tangu wangali wachanga. Tuwasomeshe watoto wetu katika shule na vyuo vyenye kufuata mfumo wa elimu wa Kiislamu wenye lengo la kuandaa Makhalfa wa Allah(s.w).

Pili, hatunabudi kuandaa Waalimu na Madaiyah watakao fundisha Uislamu na taaluma nyingine kwa lengo la kusimamisha Ukhalfa katika jamii.

Tatu, Mume na Mke (Baba na Mama) katika familia hawanabudi kushirikiana na kusaidiana kwa huruma na mapenzi ili kupata uwezo wa kuwalea watoto viliyyo na kupata wasaa wa kuyaendea masuala ya jamii.

Nne, Wanawake wa Kiislamu, hawanabudi kumfanya Bibi Khadijah, Mkewe Mtume (s.a.w), kuwa kiigizo chao katika kuwasaidia na kuwaliwaza waume zao hasa wanapokuwa katika harakati za kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii.

Tano, hatunabudi kuchukia maovu na dhulma wanazofanyiwa wanyonge na madhaifu wengine katika jamii na kuwa tayari kuondoa maovu na dhulma kwa mikono yetu pale tunapoweza. Na pale ambapo hatuna uwezo wa kutumia mikono, tutoe makemeo, vinginevyo tuingie “pangoni Hira” tutafute msaada wa Allah (s.w).

Sita, hatunabudi kujipamba na tabia njema kwa kadiri iwezekanavyo. Mtu mwema hutambulika na kukubalika kwa watu kwa urahisi.

Saba, hatunabudi kuimarisha uchumi, kwani uchumi ndio nyenzo kuu ya kuusimamisha Uislamu katika jamii.

Nane, Katika kuchagua viongozi wa jamii hatunabudi kuzingatia historia zao pamoja na kuzingatia sifa nyingine za kiongozi bora.

Maandalizi ya Kimafunzo

Ni maandalizi yaliyompitia Mtume (s.a.w) pale alipoanza kuletewa wahyi na Malaika Jibril (a.s). Maandalizi haya tunayapata katika Qur-an katika wahay wa mwanzo mwanzo kumshukia Mtume (s.a.w) katika Suratul 'Alaq (96:1-5), Suratul-Muzzammil (73:1-10) na Suratul-Muddaththir (74:1-7).

(i) Suratul-A'laq (96:1-5)

أَقْرَأْ بِإِسْمِ رَبِّكَ الَّذِي خَلَقَ ① خَلَقَ الْإِنْسَانَ مِنْ عَصِيقٍ ② قَرَأْ وَرَبُّكَ
الْأَكْرَمُ ③ الَّذِي عَلِمَ بِالْقَلْمَنْ ④ عَلِمَ الْإِنْسَانَ مَا لَمْ يَعْلَمْ ⑤

“Soma kwa jina la Mola wako aliyeumba Aliyemuumba mwanaadamu kwa a'laq. Soma na Mola wako ni karimu sana. Ambaye amefundisha kwa msaada wa kalamu. Amefundisha mwanaadamu mambo aliyokuwa hayajui.” (96:1-5)

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa Amri ya kwanza aliyopewa Mtume (s.a.w), na kwa hiyo waumini wote wa Ummah wake, ni kusoma au kutafuta elimu kwa ajili ya Allah (s.w). Kusoma kwa jina la Allah ni kusoma kwa lengo la kumuwezesha muumini kumjua na kumuabudu Mola wake viliyvo kisha kusimamisha Ukhalifa katika jamii.

Katika mazingira ya kupewa amri hii ya kwanza, pale pangoni Hira katika kilima cha Nuur (Jabal-Nuur), Mtume (s.a.w) alishinikizwa kusoma na Malaika Jibril kwa kumbana (kumkumbatia kwa nguvu) mara tatu pale alipojitetea kuwa hajui kusoma. Kubanwa huku kwa Mtume (s.a.w) na Malaika Jibril kunaashiria kuwa elimu kwa waumini ni amri ya kwanza inayotakiwa kutekelezwa kwa **hima** na kwa **taklifu** kubwa.

Hivyo Elimu ni amri ya kwanza inayotakiwa itekelezwe kwa juhudhi na bidii zote. Ndiyo silaha kuu itakayowawezesha waumini kupata ushindi wa kusimamisha Uislamu katika jamii. Tukirejea nyuma katika historia, takrima ya kwanza aliyofanyiwa Adam (a.s) na Mola wake, ili kuandaliwa kuwa khalifa wa Allah (s.w) hapa duniani ni kufundishwa majina ya vitu vyote. Bimaana fani zote za Elimu anazohitajia binaadamu ili aweze kuwa kiongozi wa dunia kwa niaba ya Allah (s.w). Pia tunajifunza kuwa chanzo cha fani zote za elimu ni Allah (s.w).

(ii) ***Suratul-Muzzammil (73:1-10)***

يَتَأْيِهَا الْمُرْزِّمُونَ ① ۝ فَمِنْ أَلَيْلٍ إِلَّا قَلِيلًا ۝ بِصَفَةٍ ۝ وَأَنْقُضُ مِنْهُ قَلِيلًا ۝
أَوْ زِدْ عَلَيْهِ وَرَقَّلِ الْقُرْءَانَ تَرْتِيلًا ۝ ③

“Ewe uliyejifunika maguo simama usiku kucha (kuswali) ila muda mdogo (tu hivi). Nusu yake au upunguze kidogo au uzidishe na soma Qur-an viliyvo. (73:1-4)

إِنَّا سَلَّقْنَا عَلَيْكَ قَوْلًا ثَقِيلًا ﴿٦﴾ إِنْ فَاتِيَّةَ الْلَّيْلِ هِيَ أَشَدُ وَطْأَةً وَأَفْوَمُ
 قِيَالًا ﴿٧﴾ إِنَّ لَكَ فِي الْنَّهَارِ سَبْحًا طَوِيلًا ﴿٨﴾ وَأَذْكُرْ أَسْمَ رَبِّكَ وَتَبَّئْلُ
 إِلَيْهِ تَبَّئْلًا ﴿٩﴾

Hakika sisi tutakuteremshia kauli nzito. Hakika kuamka usiku kunawafikiana zaidi na moyo na maneno yake yanatuwa zaidi. Hakika mchana unashughuli nyingi. Na litaje jina la Mola wako na ujitupe kwake kwa kweli. (73:5-8)

رَبُّ الْمَسْرِقِ وَالْمَغْرِبِ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ فَانِّي خَذْهُ وَكِيلًا ﴿١﴾ وَأَصْبِرْ عَلَى مَا
 يَقُولُونَ وَأَهْجِرْهُمْ هَجْرًا جَمِيلًا ﴿٢﴾

(Yeye Ndiye)Mola wa mashariki na magharib, Hapana Mola ila yeye, basi mfanye kuwa mlinzi wako. Na subiri juu ya hayo wayasemayo na uwaepuke mwepuko mwema.” (73:9-10)

Aya ya kwanza ya sura hii inaashiria kuwa huu ni wahyi wa mwanzo mwanzo uliofuatia wahyi wa kwanza. Katika Hadith iliyosimuliwa na Bibi Aysha (r.a), tunafahamishwa kuwa Mtume (s.a.w) alistushwa sana na lile tukio la Pangoni Hira, la kulazimishwa kusoma na Malaika Jibril ambaye ilikuwa ni mara yake ya kwanza kukutana naye. Mtume(s.a.w) alirudi nyumbani akiwa anatetemeka kama mtu mwenye homa kali. Alimuomba mkewe Khadija amfunike nguo. Baada ya muda hali ile ya khofu iliisha na kuweza kumhadithia mkewe yale yaliyomtokea. Alipomuona tena Jibril (a.s) anamjia kumletea wahay uliomo mwanzoni mwa sura hii (73:1-10) Mtume (s.a.w) alistuka tena na kujaribu kujihami asijefikwa na yale yaliyo mfika pangoni kwa kujifunika tena nguo. Lakini bado Jibril alimuendea Mtume (s.a.w) katika hali ile ile ya kujifunika na kumfikishia ujumbe huu wenye kumuamrisha kufanya yafuatayo:

1. Kusimama kwa swala ya usiku kwa kitambo kirefu – kati ya saa 4 au theluthi ($\frac{1}{3}$) hadi saa 8 au theluthi mbili ($\frac{2}{3}$) za usiku.
2. Kusoma Qur-an kwa mazingatio.
3. Kumdhukuru au kumkumbuka Allah (s.w) kila wakati.
4. Kujitupa kwa Allah kikweli.(kumtii Allah kwa unyenyekevu)
5. Kumfanya Allah kuwa mlinzi (wakili) pekee.
6. Kufanya subira juu ya yale wayasemayo makafiri na kuwaepuka mwepuko mwema.

Imebainishwa wazi kuwa Mtume (s.a.w) amepewa amri hizi ili iwe maandalizi ya kupokea **kauli nzito**. Kauli nzito si nyingine ila lile lengo aliloletwa kwalo la kusimamisha Uislamu katika jamii.

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ وَبِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظَهِّرَهُ وَعَلَى الْدِينِ كُلِّهِ
وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ

﴿٣﴾

Yeye ndiye aliyemleta Mtume wake kwa uongofu na Dini ya haki ili aijaalie kushinda (Dini hii) Dini zote, ijapokuwa watachukia hao washirikina. “(9:33)

Kuchukia kwa washirikina kunaashiria mapambano.

(iii) *Suratul-Muddaththir (74:1-7)*

يَتَأْيِهَا الْمُدَّثِّرُ ﴿١﴾ قُلْمَ فَانِدِرُ ﴿٢﴾ وَرَبَّكَ فَكَبِّرُ ﴿٣﴾ وَثِيَابَكَ فَطَهِرُ

وَالرُّجْزَ فَاهْجُرُ ﴿٤﴾ وَلَا تَمْنُنْ تَسْتَكِثُرُ ﴿٥﴾ وَلَرِبِّكَ فَاصْبِرُ ﴿٦﴾

Ewe uliyejifunika maguo. Simama uonye (viumbe). Na Mola wako umtukuze. Na nguo zako uzisafishe. Na Mabaya yapuuze, (endelea kuyapuuza). (74:1-6)

وَلَا تَمْنُنْ تَسْتَكِثُرُ ﴿١﴾ وَلَرِبِّكَ فَاصْبِرُ ﴿٦﴾

Wala usiwafanyie ihsani (viumbe) ili upate kujikithirishia (wewe hapa duniani). Na kwa ajili ya Mola wako fanya subira (kwa kila yatakayokufika). (74:6-7)

Muda mfupi baada ya kupewa amri sita zilizomo katika suratul-Muzzammil (73:1-10) na kuanza kuzitekeleza, Mtume (s.a.w) akiwa katika hali ile ile ya kujifunika funika aliamrishwa tena na Mola wake, ili kumalizia kazi ya maandalizi, kufanya yafuatayo:

1. Kusimama na kuonya – kulingania Uislamu.
2. Kumtukuza Allah.
3. Kutakasa nguo.
4. Kupuuza mabaya.
5. Kufanya ihsani kwa ajili tu ya kutafuta radhi za Allah (s.w).
6. Kufanya subira kwa ajili ya Allah.

Mafunzo yatokanayo na maandalizi ya kimafunzo

Kutokana na maandalizi haya ya awali aliyopewa Mtume (s.a.w) mwanzoni mwanzoni mwa Utume wake tunajifunza kuwa ili tuweze kusimamisha Uislamu katika jamii kama alivyofanikiwa Mtume (s.a.w) na maswahaba zake kuusimamisha, tunajifunza yafuatavyo:

(i) Elimu katika Fani zote, ukiacha ila ya uchawi iliyoharamishwa, ndio nyenzo ya msingi ya kutuwezesha kusimamisha Uislamu katika jamii. Hivyo Waislamu hawanabudi kutilia mkazo suala la elimu na kuandaa mitaala na mazingira yatakayowezesha kuielimisha jamii kwa lengo la kusimamisha Ukhilifa katika ardhi.

(ii) Kisimamo cha usiku, ni nyenzo kuu ya pili inayofuata katika maandalizi ya kusimamisha Uislamu katika jamii. Allah (s.w) anatubainishia kuwa hekima ya kupewa amri ya

kisimamo cha usiku (Qiyamullayl) ni ili tupate maandalizi ya “**Ukomandoo**” (Ujasiri wa nafsi) yatakayotuwezesha kukabiliana na suluba (misuko suko) ya kusimamisha Uislamu katika jamii. Allah (s.w) anabainisha pia kuwa maandalizi haya hayafai mchana ila usiku kwa sababu kuna mazingira mazuri ya utulivu yatakayompelekea huyu askari wa Allah kuwa na **khushui** (unyenyekevu) ya hali ya juu inayohitajika kuomba hidaya na msaada kutoka kwa Allah (s.w). Pia kuamka usiku na kukatisha utamu wa usingizi katika theluthi ya mwisho ya usiku, humpa Muislamu zoezi la uvumilivu na subira. Hivyo, ni wazi kuwa, **kisimamo cha usiku**, kikitekelezwa viliyyo, kinauwezo mkubwa wa kumfanya Muislamu awe na ujasiri wa kusimamisha Uislamu katika jamii kwa hali yoyote iwayo. Hivyo kwa waumini wa kweli, wanaojua kuwa wanadhima ya kuusimamisha Uislamu katika jamii na kuuhami usiporomoke baada ya kusimama, **kisimamo cha usiku**, si jambo la khiari kwao kama Mola wao anavyowatanabahisha:

أَمْنٌ هُوَ قَدِيرٌ عَلَيْهِ اللَّهُ سَاجِدًا وَقَلِيمًا يَحْذِرُ الْآخِرَةَ وَيَرْجُوا رَحْمَةَ

رَبِّهِ فُلْهَلْ يَسْتَوِي الَّذِينَ يَعْلَمُونَ وَالَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ

أُولُو الْأَلْبَابِ ﴿٣﴾

Je, afanyae Ibada nyakati za usiku kwa kusujudu na kusimama na kuogopa Akhera na kutarajia rehema ya Mola wake (ni sawa na asiyefanya hayo)? Sema: “Je, wanaweza kuwa sawa wale wanaojua na wale wasiojua?” Wanaoatanabahi ni wale wenye akili tu. “(39:9)

(iii) **Kusoma Qur-an kwa mazingatio**, kwa lengo la kuifanya kuwa dira pekee ya maisha yetu ya kila siku, ni nyenzo nyingine itakayotuwezesha kusimamisha Uislamu katika jamii. Uislamu ni mfumo wa maisha wa kutii na kufuata utaratibu wa kuendesha maisha ya kibinagsi na ya kijamii anaouridhia Allah (s.w).

Utaratibu huu wa maisha anaouridhia Allah (s.w) umeainishwa na Qur-an, kitabu chake cha mwisho. Hivyo, waumini wa kweli; ili waweze kusimamisha Uislamu katika jamii, hawanabudi kuisoma Qur-an kwa mazingatio kiasi cha kuweza kuielewa vivilivo na kufanya mwongozo wa kukiendea kila kipengele cha maisha ya kibinafsi na kijamii. Vile vile jamii ya Waislamu hainabudi kuandaa mtaala wa kufundisha Qur-an kwa lengo la kuwaandaa wasomaji wa rika zote kuwa Makhalifa wa Allah (s.w).

(iv) **Kumdhukuru na kumtukuza Allah (s.w)**, ni nyenzo nyingine muhimu itakayowawezesha waumini kusimamisha Uislamu katika jamii. Ili Waislamu wawe na msimamo thabiti, hawanabudi kuwa na yakini juu ya kuwepo Allah (s.w) na sifa zake tukufu. Imani ya kweli juu ya Allah (s.w) inathibitishwa na matendo ya Muumini ya kila siku pale atakapofuata maagizo na kuchunga mipaka ya Allah (s.w) katika kukiendea kila kipengele cha maisha yake.

(v) **Kujitupa kwa Allah kwa kweli** au kumtii Allah (s.w) kwa unyenyekevu, ni nyenzo nyingine ya kumuwezesha Muumini kusimamisha Uislamu katika jamii. Pamoja na kuwa kusimamisha Uislamu ni “kauli nzito” (jambo zito), Muumini mwenye kujitupa kwa Allah kwa kweli, hatamchelea yejote awaye au lolote zito liwalo, katika kutekeleza amri ya Allah (s.w) iliyombele yake.


(vi) **Kumfanya Allah kuwa Mlinzi Pekee**, ni nyenzo nyingine inayompa Muumini ujasiri wa kusimamisha Uislamu katika jamii. Kuwa tegemezi kwa Allah (s.w) ambaye ni **Al-qahharu** (mwenye nguvu juu ya kila kitu) humfanya Muislamu asichelee kizuizi au nguvu yoyote inayozuia Uislamu kusimama.

(vii) *Kusimama na kuonya* ni amri ya kuwafahamisha watu juu ya upweke wa Allah (s.w) kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah na kisha kuwafahamisha namna ya kumuabudu Allah (s.w) pekee katika kila kipengele cha maisha. Baada ya kufikisha ujumbe huu wa Tawhiid, kwa hekima na mawaidha mazuri (rejea Qur-an 16:125), Mtume na Waumini kwa ujumla wanaamrishwa kuwaonya watu juu ya adhabu kali itakayowafika wale wote watakaoishi kinyume cha Tawhiid – katika maisha ya akhera.

Pia amri hii ya kuwaonya watu inakwenda sambamba na kuwabashiria malipo mema watakayopata wasimamishaji wa Tawhiid katika maisha ya akhera. Kuufundisha Uislamu na kuweka wazi faida itakayopatikana kwa wale watakaoufuata vilivyo na hasara itakayowafika wale watakaoukanusha, ni hatua muhimu na ya msingi mno katika harakati za kusimamisha Uislamu katika jamii.

(viii) *Kutakasa nguo*, ni amri inayoashiria kuwa mwenye kulingania Uislamu anatakiwa awe mfano wa kuigwa kwa tabia njema. Pamoja na mlinganajji kutekeleza amri ya kutakasa nguo zake na mwili wake ili awe kivutio kwa watu atakaokutana nao katika harakati za kulingania Uislamu, anatakiwa awe na tabia njema itakayovuta usikivu wa watu. Katika kutekeleza amri hii Mtume (s.a.w) alikuwa akipendelea vazi jeupe na kujipaka manukato ili asiwe kero kwa watu kutokana na harufu mbaya inayotokana na nguo chafu na majasho.

Sambamba na usafi huu wa nguo na mwili, Mtume (s.a.w) alikuwa na tabia njema kabisa.



“Na bila shaka una tabia njema kabisa.” (68:4)

Mlinganiaji kuwa kiigizo kwa tabia inasisitizwa katika aya zifuatazo:

يَتَأْكِلُهَا الَّذِينَ عَمِلُوا لِمَ تَقُولُونَ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٧﴾ كَبُرَ مَفْعَلًا عِنْدَ اللَّهِ أَنْ
تَقُولُوا مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٨﴾

Enyi mlionamini! Mbona, (kwa nini) mnasema msiyoyatenda? Ni chukizo kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu kusema msiyoyatenda. (61:2-3)

(ix) Kupuuza Mabaya, ni pamoja na kutojali au kutokatishwa tamaa na mabaya unayofanyiwa na maadui wa Uislamu. Pia amri hii ya kupuuza mabaya ni pamoja na kujiepusha kuyafanya, kutoyathamini maovu hatakama yanafanywa na watu maarufu na kuyachukia. Kupuuza mabaya ni nyenzo nyingine muhimu katika kusimamisha Uislamu. Kama muumini hatakuwa na tabia ya kupuuza mabaya anayofanyiwa na maadui wa harakati za kusimamisha Uislamu, atafikishwa mahali pa kumkatisha tamaa na kususa harakati.

(x) Kufanya ihsani kwa ajili tu ya kutafuta radhi za Allah (s.w), ni amri inayowataka wanaharakati wa kuhuishwa na kusimamisha Uislamu katika jamii wasitegemee malipo ya kazi hii kutoka kwa watu bali wategemee malipo yao kutoka kwa Allah (s.w). Kazi ya kusimamisha Uislamu katika jamii, Allah (s.w) ameifananisha na biashara kati yake na waumini ambapo waumini wanamuuzia Allah (s.w) **mali** zao na **nafsi** zao, naye Allah awalipe malipo makubwa yanayobainishwa katika aya zifuatazo:

* إِنَّ اللَّهَ أَشْتَرَى مِنَ الْمُؤْمِنِينَ أَنْفُسَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ بِإِنَّ لَهُمُ الْجَنَّةَ
يُقْتَلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيُقْتَلُونَ وَيُغَتَّلُونَ وَعَدًا عَلَيْهِ حَقًّا فِي الْتَّورَةِ
وَالْإِنجِيلِ وَالْقُرْآنِ وَمَنْ أَوْفَى بِعَهْدِهِ مِنَ اللَّهِ فَأَسْتَبِّشُوا بِيَتَعَبُّكُمْ
الَّذِي بَأْتُمُوهُمْ وَذَلِكَ هُوَ أَفْوَزُ الْعَظِيمِ ﴿١٠﴾

Mwenyezi Mungu amenunua kwa Waumini nafsi zao na mali zao (watoe nafsi zao na mali zao katika kupigania Dini) ili na yeye awape Pepo. Wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu; wanaua na wanaauawa. Hii ndiyo ahadi aliyojilazimisha (Mwenyezi Mungu) katika Taurati na Injili na Qur-an. Na ni nani atekelerezaye zaidi ahadi yake kuliko Mwenyezi Mungu? Basi furahini kwa biashara yenu mliyofanya naye (Mwenyezi Mungu). Na huko ndiko kufuzu kukubwa. “(9:111)

يَتَأْيِهَا الَّذِينَ عَمَّا وَهَلْ أَدْلُكُمْ عَلَىٰ تِجَارَةٍ ثُنِيجِيْكُمْ
 مِّنْ عَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٦﴾ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَتُجَاهِدُونَ فِي
 سَبِيلِ اللَّهِ بِأَمْوَالِكُمْ وَأَنفُسِكُمْ ذَلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ

Enyi mlioamini! Je! Nikujulisheni biashara itakayokuokoeni na adhabu iumizayo?

(Biashara yenye we ni hii) Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na piganieni Dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zenu na nafsi zenu. Haya ni bora kwenu ikiwa mnajuba (61:10-11)

(xi) Kufanya Subira kwa ajili ya Allah, ni nyenzo nyingine ya msingi itakayowawezesha Waumini kusimamisha Uislamu katika jamii. Katika harakati za kusimamisha Uislamu katika jamii, kuna kero na bughudha nyingi zinazoandalisha na kusimamiwa na wapinzani wa Uislamu. Ukrejea historia ya Mtume (s.a.w), kero hizi huanza na kujenga mazingira ya kukatisha tamaa. Katika mazingira hayo, Mtume (s.a.w) aliitwa mwongo, mwenda wazimu, mtunga mashairi, mchawi, aliyepagawa, mkatikiwa na kheri (Abtari), n.k.

Katika mazingira ya sasa makafiri wanajitahidi kuwa katisha tamaa wanaharakati kwa kuwaita siasa kali (fundamentalist),

mashabiki wa Kidini (fanatics), magaidi (terrorists), n.k. Allah (s.w) anatuamrisha tusubiri juu ya hayo wayasemayo dhidi yetu na tuwaepuke mwepuko mwema. Kuwaepuka mwepuko mwema ni kuyapuuza hayo wayasemayo dhidi yetu na tusilumbane nao wakajatutoa kwenye agenda yetu. Jibu la tusi kwa muungwana ni “hewala” na jibu la muumini kwa jahili ni “salama”.

وَعِبَادُ الرَّحْمَنِ مِنَ الظِّينَ يَمْشُونَ عَلَى الْأَرْضِ هَوَّا وَإِذَا خَاطَبُهُمْ

الْجَاهِلُونَ قَالُوا سَلَامًا

“Na waja wa Rahmani, ni wale wanaokwenda ulimwenguni
kwa unyenyekevu; na majahili wakisema nao (maneno
mabaya) huwajibu (maneno ya) salama.” (25:63).

Tukirejea historia, baada ya makafiri kushindwa kuzuia harakati za kusimamisha Uislamu kwa maneno ya kukatisha tamaa, waliandaa nguvu za kuzuia Uislamu kwa matendo kama vile kutesa, kufunga gerezani, kufukuza nchini na kuua. Haya ndiyo mazingira halisi katika harakati za kusimamisha Uislamu na ndiyo sunnah ya harakati aliyoiweka Allah (s.w) kama anavyotukumbusha:

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ أَنْتَيْ عَدُوًّا شَيْطَنَيْنِ إِلَيْنِسِ وَالْجِنِّ يُوْجِي بَعْضُهُمْ

إِلَيْ بَعْضٍ زُخْرُفَ الْقَوْلِ غُزْرَوْرًا وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ مَا فَعَلَوْهُ فَذَرْهُمْ وَمَا


يَفْتَرُونَ

Na namna hii tumemfanyia kila Nabii maadui; (nao ni)
mashetani katika watu na (mashetani katika) majini. Baadhi
yao wanawafunulia wenziwao maneno ya kupambapamba
ili kuwadanganya. Na kama Mola wako angalipenda
wasinalifanya hayo, (angewalazimisha kwa nguvu kutii).
Basi waache na uwongo wao. (6:112)

Hivyo waumini hawanabudi kuwa na subira ya hali ya juu ya kuhimili vitimbi vya maadui wa harakati za Uislamu. Tukumbuke kuwa kusimamisha Uislamu ni kazi ngumu (kauli nzito) yenyeye vikwazo na mitihani mingi kama tunavyokumbushwa.

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَا يَأْتِكُم مَّثْلُ الَّذِينَ خَلَوْا مِنْ قَبْلِكُم
مَّسَّتُهُمُ الْبُشَاءُ وَالضُّرُّ أَعْوَزُ لَرُؤْلَوْا حَتَّىٰ يَقُولُ الرَّسُولُ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا
مَعَهُ وَمَتَىٰ نَصْرُ اللَّهِ إِلَّا إِنَّ نَصْرَ اللَّهِ قَرِيبٌ


Mnadhani kuwa mtaingia Peponi, na hali hamjajiwa na mfano wa (yale yaliyowajia) wale waliopita kabla yenu? Yaliwapata mashaka na madhara na wakatetemeshwa sana hata Mitume na walioamini pamoja nao wakasema: "Nusura ya Mwenyezi Mungu itafika lini?" Jueni kuwa nusura ya Mwenyezi Mungu iko karibu. (2:214)

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَا يَعْلَمِ اللَّهُ الَّذِينَ جَاهَدُوا مِنْكُمْ وَيَعْلَمُ


Je! Mnadhani mtaingia Peponi hali Mwenyezi Mungu hajawapambanua wale waliopigania Dini ya Mwenyezi Mungu mionganoni mwenu, na kuwapambanua waliofanya subira? (Sharti yaonekane kwanza haya hapa ulimwenguni). (3:142)

Zoezi la Pili

1. (a) Mtume Muhammad(s.a.w) alizaliwa zama za Jahiliyyah.
Ni zipi zama za Jahiliyyah ?

(b) Katika zama za Jahiliyyah maadili ya wakazi wa Bara
Arabu yalikuwaje ?
(c) Je, maadili ya Ahlal kitaab(mayahudi na wakristo),
waliodai kuwa wafuasi wa Mitume, yalitofautianaje na yale
ya wakazi wa Bara Arab?
2. Mtume(s.a.w) aliandaliwa kabla na baada ya kupewa utume
ki-il-hamu na ***kimafunzo***. Toa ufanuzi juu ya maandalizi
haya.
3. Bainisha matukio yanayoonesha kuwa Mtume(s.a.w)
aliandaliwa ***Ki-il-hamu***.
4. Kwa kurejea Al ‘Alaq(96:1-5), Al-Muzzammil(73:1 - 10) na
Al-Muddaththiri (74:1 - 7), bainisha maelekezo ya
kimaandalizi.
5. Ainisha mafunzo yatokanayo na kuandaliwa Mtume(s.a.w):

(a) Ki-il-hamu
(b) Kimafunzo



Sura ya Tatu

MWANAHARAKATI WA KIISLAMU

Utangulizi:

Dai'ah au Mwanaharakati ni Muislamu anayefanya jitihada za makusudi za kusimamisha Uislamu katika jamii.

Da'awah au kazi ya kulingania Uislamu ndiyo kazi ya Mitume wote hivyo mitume wote walikuwa Wanaharakati. Kila Muumini wa kweli anawajibika kuwaiga mitume katika kazi ya Da'awah,kazi ya kuwaita watu kwenye Uislamu ili waufuate viliyyo na kuusimamisha katika jamii.Katika Hija ya kuaga (Hijjatul-Wadaa), Mtume Muhammad (s.a.w) alimuagiza kila Muislamu kuufikisha ujumbe wa Uislamu kwa kadri ya uwezo wake angalau aya moja anayoifahamu.Mwishoni mwa Khutba yake alisema:

*“Na afikishe aliyekuwepo kwa yule asiyekuwepo.Kwani
watu wengi wanaofikishiwa ujumbe wanaweza kuwa wenye
kuufuata (wenye kuuzingatia) kuliko walioupata moja kwa
moja kwa mtoaji ujumbe”.*

Kutokana na maelezo hayo ni dhahiri kuwa kila Muislamu anawajibika kuufikisha ujumbe wa Uislamu kwa wengine kwa kadri ya uwezo wake. Akianzia na watu wa nyumbani kwake,jamaa zake, rafiki zake na kisha jamii yake kuanzia ngazi ya mtaa hadi taifa na Mataifa.

Mitume wa Allah (s.w) hawakuifanya kazi hii kinadharia tu, bali walikuwa katika mstari wa mbele katika utekelezaji wake. Waliwavutia wafuasi wao si kwa maneno tu, bali tabia zao na mienendo yao mizuri iliathiri jamii zao kwa kiasi kikubwa. Hivyo yejote yule aliyeitikia wito wa kuifanya kazi hii takatifu ya

kulingania Uislamu na kuusimamisha katika jamii hana budi kujipamba na tabia njema ilioyelekezwa katika Quran na kufafanuliwa kwa nadharia na vitendo na Mtume (s.a.w).

Ifahamike wazi kuwa mtu muovu (fasiq) kamwe hawezi kufanikiwa katika kazi hii takatifu, kazi ya Mitume wa Allah (s.w). Atakayefanikiwa ni yule atakayejisalimisha ki kwelikweli kwa Allah (s.w) kwa maneno yake na matendo yake kama tunavyofahamishwa katika Quran:

وَمَنْ أَحْسَنْ قَوْلًا مِّمْنَ دَعَا إِلَى اللَّهِ وَعَمِلَ صَلِحًا
وَقَالَ إِنِّي مِنَ الْمُسْلِمِينَ

“Nani asemaye kauli bora zaidi kuliko yule aitaye(watu) kwa Allah na mwenyewe akafanya uitendo uizuri na husema (kwa maneno yake na uitendo uyake) hakika mimi ni mionganoni mwa Waislam”. (41:33)

Katika maisha yetu ya kila siku tunaona kuwa kazi zote muhimu na nzito katika jamii kama vile uongozi wa nchi, urubani wa ndege, uhandisi, udaktari n.k huendeshwa na watu wenye sifa zinazostahiki. Sifa hizi zinapatikana baada ya kisomo cha muda mrefu na uzoefu mwingi. Kazi ya Harakati za kulingania Uislamu ni kazi muhimu, nyeti na nzito kuliko zote katika jamii. Ni kazi ya kuiokoa jamii kutokana na matatizo ya kila aina na kuiongoza kwenye njia ya maisha iliyonyooka ambayo ndiyo pekee itakayoiwezesha jamii hiyo kuishi maisha ya amani na furaha.Bila jamii kuifahamu njia hii na kuifuata vilivyo, maisha ya furaha na amani hapa ulimwenguni na ya huko akhera huwa ni ndoto.Hivyo ili Harakati za kulingania Uislamu zifanikiwe Wanaharakati hawana budi kuwa na sifa zinazostahiki.

Sifa za Mwanaharakati wa Kiislamu

Zifuatazo ni sifa kuu anazostahiki kusifika kwazo Mwanahara kati wa Kiislamu:

1. Ujuzi sahihi juu ya Uislamu
2. Imani thabiti juu ya Uislamu
3. Tabia njema (tabia ya utendaji)
4. Kusimamisha Uislamu kuwa ndio lengo kuu la Maisha.
5. Kutarajia malipo kutoka kwa Allah (s.w) tu.
6. Kuwa na subira
7. Kuwa na Hekima

1. Ujuzi sahihi juu ya Uislamu

Waislamu walio wengi wameridhika na Elimu ya Fiq-hi inayowawezesha kutekeleza Ibada maalum tu kama vile: Swala, Zakat, Swaumu, Hija, Ndoa, Talaka, Mirathi n.k. Kwa hiyo Waislamu walio wengi hawajui uchumi wa Kiislamu ukoje, mtazamo wa Uislamu juu ya siasa ni upi, Uislamu unautazamaje utamaduni n.k. Kwa ujumla Waislamu walio wengi hawana mtazamo sahihi wa Uislamu juu ya vipengele mbalimbali vyta maisha ya jamii. Hivyo Mwanaharakati hana budi kuufahamu Uislamu kwa upana wake. Haina maana kuwa kila mtu anayetaka kulingania Uislamu katika jamii ni lazima awe amebobea kitaaluma katika kila kipengele muhimu cha maisha ya jamii ya Kiislamu bali hana budi kuwa na kiwango cha ujuzi kitakachomuwezesha kuishi Kiislamu katika kila kipengele cha maisha yake ya kibinagsi na yakijamii.

Kwa maana nyingine ili kuhuishwa Uislamu katika jamii na yapatikane mfanikio yanayotarajiwa Mwanaharakati hana budi kuwa na Elimu ya msingi juu ya:

- Lengo na Hadhi ya binaadamu hapa ulimwenguni
- Mtazamo wa Uislamu juu ya Elimu
- Mtazamo wa Uislamu juu ya Dini.

- Maana ya kislamu na matunda yake katika jamii.
- Imani ya Kislamu na tafsiri yake katika utendaji wa maisha ya kila siku.
- Lengo la nguzo za Uislamu.
- Maisha ya Familia ya Kiislamu.
- Uislamu katika kila kipengele cha Maisha ya jamii.
- Historia ya kuhuishwa Uislamu kuanzia Nabii Adam (a.s) hadi hivi leo.

Ili kupata elimu ya msingi juu ya Uislamu, msomaji anashauriwa asome Juzuu 7 za Maarifa ya Uislamu Darasa la Watu Wazima zinazotolewa na Islamic Propagation Centre (IPC) Zimeandaliwa kwa kufuata mtaala maalumu wenyewe lengo la kuandaa Makhalfa wa Allah(s.w.)

2. Imani thabiti juu ya Uislamu.

Kazi hii takatifu ambayo wakati mwingine inamtaka Mwanaharakati atoe uamuzi wa kujitoa muhang'a kwa mali yake na nafsi yake, haiwezekani ikafanywa kwa ufanisi na mtu mwenye imani haba juu ya Uislamu au mwenye imani ya kuyumbayumba. Yeyote yule anayejitoa mbele kufanya kazi hii, hana budi kuwa na **imani thabiti** juu ya kuwepo Allah (s.w) pamoja na sifa zake na utukufu wake, pia hana budi kuwa na **imani thabiti** juu ya kuwepo siku ya Hukumu na maisha ya Akhera.

Mwanaharakati lazima awe na yakini kuwa njia sahihi pekee ya maisha ni ile tu iliyofundishwa na kuelekezwa na Mtume (s.a.w). Chochote kisichokuwa katika njia hii ni kiovu na batili. Kipimo pekee cha kupimia usahihi wa maoni au jambo jipya lililowakilishwa na yeyote yule ni **Kitabu cha Allah(s.w) na Sunnah ya Mtume** wake.

Hivyo Mwanaharakati atakapokuwa na Imani thabiti juu ya vipengele vya nguzo za Imani ndipo atakapoweza kuuhuisha na

kuusimamisha Uislamu katika Jamii. Atakuwa tayari kufanya biashara na Allah (s.w) kama inavyobainishwa katika aya ifuatayo:

﴿ إِنَّ اللَّهَ أَشْتَرَى مِنَ الْمُؤْمِنِينَ أَنفُسَهُمْ وَأَمْوَالُهُمْ بِأَنَّ لَهُمُ الْجَنَّةَ
يُقْدِتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيَقْتُلُونَ وَيُقْتَلُونَ وَعَدًا عَلَيْهِ حَقًّا فِي الْتَّورَةِ
وَالْإِنْجِيلِ وَالْقُرْءَانِ وَمَنْ أَوْفَى بِعِهْدِهِ مِنَ اللَّهِ فَاسْتَبِشُوا وَأَبْتَغِعُكُمْ
الَّذِي بَأْتُكُمْ بِهِ وَذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴾ ١١١

“Mwenyezi Mungu amenunua kwa waumini nafsi zao na mali zao (watoe nafsi zao na mali zao katika kupigania dini) ili na yeye awape Pepo. Wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu; wanaua na wanaauawa. Hii ndiyo ahadi aliyojilazimisha (Mwenyezi Mungu) katika Taurati na Injili na Qur'an. Na ni nani atekelerezaye zaidi ahadi yake kuliko Mwenyezi Mungu? Basi furahini kwa biashara yenu miliyofanya naye (Mwenyezi Mungu). Na huko ndiko kufuzu kukubwa”. (9:111).

Pia mwanaharakati mwenye imani thabiti hatamchelea yoyote anayekuwa kipingamizi cha kusimamisha Uislamu katika jamii hata akiwa mtu wake wa karibu kinasaba. Kama inavyobainsihwa katika Qur'an:

لَا تَجِدُ قَوْمًا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ يُوَادُونَ مَنْ حَادَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ
وَلَوْ كَانُوا أَبَاءَهُمْ أَوْ أَبْنَاءَهُمْ أَوْ إِخْرَانَهُمْ أَوْ عَشِيرَتَهُمْ أَوْ لَتَّلِكَ كَتَبَ
فِي قُلُوبِهِمْ إِلَيْمَدَنَ وَأَيَّدَهُمْ بِرُوْجَ مَنْهُ وَيُدْخِلُهُمْ جَنَّتِ تَجْرِي مِنْ
ثَحْتِهَا الْأَنْهَرُ خَلِيدِينَ فِيهَا رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ أَوْ لَتَّلِكَ
حِزْبُ اللَّهِ أَلَا إِنَّ حِزْبَ اللَّهِ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴾ ١١٢

“Huwapati (huwaoni) watu wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, kuwa wanawapenda wale wanaompinga Mwenyezi Mungu na Mtume wake; hata wakiwa ni baba zao au watoto wao au ndugu zao au jamaa zao. Hao ndio ambao (Mwenyezi Mungu) ameandika (amethibitisha kweli kweli) nyoyoni mwao imani na akawatia nguvu kwa Roho itokayo kwake; na atawaingiza katika Mabustani yapitayo mito mbele yake humo watakaa daima. Mwenyezi Mungu amekuwa radhi nao, na wao wamekuwa radhi Naye. Hao ndio kundi la Mwenyezi Mungu. Sikilizeni! Hakika kundi la Mwenyezi Mungu ndilo linalofaulu”. (58:22)

3. Tabia Njema (Tabia ya utendaji)

Sifa hii ni kuwa maneno ya Mwanaharakati yawe ni kioo cha matendo yake. Hana budi kutenda vivilvyo lile analolikubali kuwa ni sahihi, na hana budi kujiepusha na lile analoliona kuwa si sahihi. Yaani kabla hajafikia hatua ya kuwaamrisha wengine kufanya mema na kuwakataza kufanya maovu, hana budi ye ye mwenyewe kujihimu kufanya mema na kujiepusha kufanya maovu. Tabia yake njema iwavutie watu zaidi kuliko maneno yake. Mwanaharakati mwenye tabia hii ya utendaji ndiye pekee atakayefanikiwa katika kazi hii kama anavyotuthibitishia Allah (s.w) katika Quran:

وَمَنْ أَحْسَنْ قَوْلًا مِّنْ دَعَا إِلَى اللَّهِ وَعَمِلَ صَلِحًا

وَقَالَ إِنَّمَا مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿٣﴾

Na nani asemaye kauli bora zaidi kuliko yule aitaye (watu) kwa Allah na akafanya vitendo vizuri na husema (kwa maneno yake na vitendo vyake hakika mimi ni mionganii mwa Waislamu. (41 :33)

Mwanaharakati hana budi kufahamu kwamba hataweza kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii, wakati ye ye

mwenyewe tabia yake ni ya kuuangusha na kuuhilikisha. Ni vibaya mno mbele ya Allah (s.w) mtu kusema asiyoyatenda kama Allah (s.w) anavyotuasa:

يَتَأْيَهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لِمَ تَقُولُونَ مَا لَا تَفْعَلُونَ ﴿٢﴾ كَبُرُّ مَقْتَنًا عِنْدَ اللَّهِ
أَنْ تَقُولُوا مَا لَا تَفْعَلُونَ ﴿٣﴾

Enyi mliao mini! Mbona mnasema msiyoyatenda? Ni chukizo kubwa mbele ya Allah kusema msiyoyatenda. (61 :2-3)

Pia Allah (s.w.) anatutanabahisha katika Aya ifuatayo:-

﴿أَتَأْمُرُونَ النَّاسَ بِالْبِرِّ وَتَنْسَوْنَ أَنفُسَكُمْ وَأَنْثُمْ تَتَلَوَّنَ الْكِتَابَ أَفَلَا
تَعْقِلُونَ﴾

“Je, mnawaamrisha watu kutenda mema na mnajisahau nafsi zenu, hali mnasoma kitabu Basi je, hamna akili? (2:44)

Kutokana na mafundisho haya ya Qur'an, si tu kwamba Mwanaharakati wa maneno matupu hatafanikiwa katika kazi yake bali anangojewa na adhabu kali mbele ya Allah (s.w) kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

“Usamah bin Zaid (r.a) ameeleza kuwa, Mtume wa Allah amesema: Mtu ataletwala siku ya Kiyama kisha atatumbukizwa motoni, matumbo yake yatamwagika motoni na kusagwa sagwa (yawee kama unga) kisha wakazi wa huko motoni watamzunguka na kisha watamuuliza, “Ewe mtu kitu gani kilichokutokea? Hukuwa unatuamrisha mema na kutukataaza maovu? Atajibu, Nilikuwa nikikuamrishi mema ambayo mimi mwenyewe sikuwa ninayafanya, na nilikukatazeni maovu ambayo mimi mwenyewe nilikuwa ninayafanya” (Bukhari na Muslim)

Mwanaharakati hana budi kujiepusha mbali na maneno ya kishetani ya wale wahubiri wasemao “**Tusikilizeni na kufuata maneno yetu lakini msifuate matendo yetu**”. Kwa kawaida mwanaadam huvutiwa zaidi na vitendo vya mtu kuliko maneno yake. Kwa hiyo maneno yanayopingana na matendo ya mlinganiaji yanakuwa chukizo kubwa mbele ya Allah (s.w) na wasikilizaji.

4. Kusimamisha Uislamu kuwe ndio lengo kuu la maisha.

Mwanaharakati wa Kiislamu hana budi kufahamu nafasi ya waumini katika jamii kuwa ni **makhalifa** wa Allah (s.w). Hivyo lengo kuu la kila muumini ni kusimamisha Uislamu katika jamii, kuuendeleza na kuulinda. Endapo Muislamu atajivekeea malengo mengine ya maisha au akazifanya shughuli zake za kutafuta maslahi ya maisha ya dunia kuwa ndio lengo kuu la maisha yake, basi ajue kuwa amestahiki ghadhabu za Allah(s.w) kama inavyobainishwa katika aya ifuatayo:

قُلْ إِنَّكَانَ عَابِرٌ كُمْ وَأَبْنَاؤُكُمْ وَإِخْوَانُكُمْ وَأَزْوَاجُكُمْ وَعَشِيرَتُكُمْ
وَأَمْوَالٍ أَقْرَبْتُمُوهَا وَتِجَارَةً تَحْسُنُونَ كَسَادَهَا وَمَسَكِينٌ تَرْضُوْهُنَّا
أَحَبَّ إِلَيْكُم مِّنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَجِهَادٍ فِي سَبِيلِهِ فَتَرَبَّصُوا حَتَّىٰ يَأْتِيَنَّا
اللَّهُ بِأَمْرِهِ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ



“Sema: kama baba zenu na wana wenu na ndugu zenu na wake zenu na jamaa zenu na mali mlizochuma na biashara mnazoogopa kuharibikiwa na majumba mnayoyapenda (ikiwa vitu hivi) ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kupigania Dini yake, basi ngojeni mpaka Mwenyezi Mungu alete Amri yake. Na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu maasi. “(9:24)

Muislamu wa kweli hatakiwi akathamini kitu chochote au jambo lolote lisilomfikisha kwenye kusimamisha Uislamu na kuudumisha

katika jamii. Kila shughuli anayoifanya katika harakati za maisha yake ya kila siku iwe na lengo la kumuwezesha kusimamisha Uislamu na kuufanya uwe juu ya mifumo mingine yote ya maisha. Hili ndilo lengo kuu la kuletwa Mtume (s.a.w) kama inavyobainishwa katika Qur'an:

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ
عَلَى الْأَدِينَ كُلِّهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ ﴿٣٣﴾

Yeye ndiye aliyemleta Mtume wake kwa uongofu na Dini ya haki, ili aijaalie kushinda dini zote ijapokuwa watachukia washirikina (9:33,61 :9)

5. Kutarajia malipo kutoka kwa Allah (s. w) tu.

Mwanaharakati wa Kiislamu hana budi kulifahamu vema lengo hili kuu la kusimamisha Uislamu katika jamii na awe na yakini kuwa kwa kuliendea lengo hili anafanya biashara na Allah (s.w) kama inavyobainishwa katika Qur'an:

﴿ إِنَّ اللَّهَ أَشْتَرَى مِنَ الْمُؤْمِنِينَ أَنفُسَهُمْ وَأَمْوَالُهُمْ بِأَنَّ لَهُمُ الْجَنَّةَ يُقْدِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيُقْتَلُونَ وَيُقْتَلُونَ وَعَدَ اللَّهُ عَلَيْهِ حَقًا فِي التَّوْرَةِ وَالْإِنْجِيلِ وَالْقُرْءَانِ وَمَنْ أَوْفَى بِعِهْدِهِ مِنَ اللَّهِ فَأَسْتَبِرُوا بِيَعِكُمْ الَّذِي بَأَيْعُثُمْ بِهِ وَذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴾

Mwenyezi Mungu amenunua kwa waumini nafsi zao na mali zao ili naye awape pepo. Na wanapigana katika njia ya Allah. Wanaua na wanauawa. Hii ndiyo ahadi aliyojilazimisha (Mwenyezi Mungu) katika Taurati,Injili na Quran.Na ni nani atekelerezaye zaidi ahadi kuliko Mwenyezi Mungu? Basi furahini kwa biashara mliyofanya naye. Na huko ndiko kufuzu kuliko kukubwa.(9: 111)

يَتَأْكِلُونَ الَّذِينَ ظَاهَرُوا مِنْهُمْ عَلَىٰ تَجَرَّدٍ ثُبُجِيْكُمْ
 مِّنْ عَذَابِ أَلِيمٍ ﴿١﴾ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَشُجَّعْهُدُونَ فِي
 سَبِيلِ اللَّهِ بِأَمْوَالِكُمْ وَأَفْسِكُمْ ذَلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ
 ﴿٢﴾ يَغْفِرُ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَيُدْخِلُكُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا
 الْأَنْهَارُ وَمَسَكِنٌ طَيِّبَةٌ فِي جَنَّاتٍ عَدْنٍ ذَلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿٣﴾
 وَأُخْرَىٰ تُحِبُّونَهَا نَصْرٌ مِّنَ اللَّهِ وَفَتْحٌ قَرِيبٌ وَبَشِّرِ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٤﴾

Enyi mliaoamini! Je! Nikujulisheni biashara itakayokuokoeni na adhabu iumizayo? (Basi biashara yenewe ni hii): Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na piganieni dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zenu na nafsi zenu, haya ni bora kwenu; ikiwa mnajua (kuwa ni bora, basi fanyeni). (Mkifanya haya) Atakusameheni dhambi zenu na atakuingizeni katika Mabustai yapitayo mito mbele yake na (atakupeni) maskani mazuri mazuri katika Bustani za milele: huku ndiko kufuzu kukubwa. Na (atakupeni) kingine mnachokipenda: Nayo ni nusura itokayo kwa Mwenyezi Mungu na ushindi ulio karibu! Na wapashe habari njema Waislamu.” (61:10-13)

Mwanaharakati wa Kiislamu daima ayaweke mbele malipo haya ya hakika na asifanye kazi hii kwa kutaraji malipo mengine yoyote isipokuwa hayo. Anatakiwa ajitumbukize kwa dhati katika biashara hii aliyatangaziwa na Allah(s.w) kwa mali yake na nafsi yake.

Pia akumbuke usia huu kutoka kwa Mola wake.

وَلَا تَمُنْ تَسْتَكِنُ ﴿٥﴾

“Wala usiwafanyie watu ihsani ili upate kujikithirishia. (74:6)

Mwanaharakati atakapojiingiza katika kazi hii ya Mitume kwa matarajio ya kupata maslahi ya kidunia, kamwe asitarajie kufikia lengo la kuusimamisha Uislam katika jamii.

6. Kuwa na Subira

Subira ni kipengele cha tabia njema chenye maana pana. Hapa tutaona miongoni mwa maeneo ya subira anayotarajiwa kuyapitia mwanaharakati:

(i) Kutokuwa na haraka katika kutoa maamuzi. Mwanaharakati anatakiwa anapopata jambo asilitolee uamuza haraka haraka kabla ya kufikiri vya kutosha na kupata ushauri wa kutosha kutoka kwa watu anaowategemea kwa ujuzi wao na uadilifu wao. **Uamuza wa jazba** hautakikani katika harakati za kuhuisha na kuusimamisha Uislamu katika jamii.

(ii) Kutokuwa na haraka ya kupata matunda ya harakati. Mwanaharakati asiwe na haraka ya kutaka kuona mabadiliko ya haraka haraka katika jamii kutokana na kazi yake. Anatakiwa kuifanya kazi hii kwa muda wote wa maisha yake kwa lengo la kuusimamisha Uislamu bila ya kukatishwa tamaa na chochote. Mwanaharakati bila ya kuwa na msimamo huu, kazi hii itamshinda na atakuwa miongoni mwa waliokata tamaa na Rehma ya Allah (s.w).

وَلَا تَأْيِسُوا مِنْ رَّوْحِ اللَّهِ إِنَّهُ وَلَا يُيَئِسُ مِنْ رَّوْحِ اللَّهِ.....

إِلَّا الْقَوْمُ الْكَافِرُونَ ﴿٨٧﴾

“..... wala msikate tamaa na Rehema ya Mwenyezi Mungu Na hawakati tamaa na rehma ya Mwenyezi Mungu isipokuwa makafiri”.(12:87)

(iii) Ni katika subira vile vile mtu kubakia na uamuza wake mwema mpaka hatua ya mwisho. Mwanaharakati anatakiwa awe na msimamo thabiti katika kazi yake hii ya

kulingania Uislamu. Asiwe ni mwenye mashaka mashaka na wala asirudi nyuma kwa hali yoyote itakayokuwa mpaka mwisho wa uhai wake.

(iv) Mwanaharakati anatakiwa awe tayari kupambana na magumu mbalimbali katika kuifanya kazi hii takatifu. Historia inatufahamisha wazi kuwa Mitume wa Allah (s.w) na wale walioamini pamoja nao walikabiliwa na magumu mbalimbali, lakini hawakukata tamaa. Bali walisubiri na walizidi kuwa imara na thabiti kila matatizo yalipoongezeka. Hii ndio tabia ya waumini wa kweli kama Allah (s.w) anavyobainisha katika Quran:

وَلَمَّا رَءَا الْمُؤْمِنُونَ الْأَحْرَابَ قَالُوا هَذَا مَا وَعَدَنَا اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَصَدَقَ
اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَمَا زَادُهُمْ إِلَّا إِيمَانًا وَتَسْلِيْمًا

Na waumini walipoyaona majeshi (ya makafiri) walisema: (Haya ndiyo aliyotuhadi Mwenyezi Mungu na Mtume wake (kuwa tutapata misukosuko kisha tutashinda). Mwenyezi mungu na Mtume wake wamesema kweli na jambo hili halikuwazidishia ila Imani na utii.(33:22)

Pia Allah (s.w) anatukumbusha kuwa kamwe tusitarajie mafanikio ya kusimamisha Uislamu na kupata malipo ya Peponi pasina kuwa tayari kupambana na matatizo mbalimbali kama yale yaliyowasibu waliopita kabla yetu.

أَخَسِبَ النَّاسُ أَنْ يُشْرَكُوا أَنْ يَقُولُوا عَامَّا وَهُمْ لَا يُفْتَنُونَ ﴿٢﴾ وَلَقَدْ فَتَنَّا
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ فَلَيَعْلَمَنَّ اللَّهُ الَّذِينَ صَدَقُوا وَلَيَعْلَمَنَّ الْكَاذِبِينَ ﴿٣﴾

Je! watu wanadhani wataachwa (wasitiwe katika misukosuko) kwa kuwa wanasema (Tumeamini?) Basi ndiyo wasijaribiwe (wasipewe mitihani)? Hapana, bila shaka tuliwatia katika taabu wale waliokuwa kabla yao, na kwa yakini Mwenyezi Mungu atawatambulisha wale walio wakweli na atawatambulisha (wale walio) waongo.(29:2-3)

وَكَائِنٌ مِّنْ نَّبِيٍّ قَدْ شُلِّ مَعَهُ رِبِّيُّونَ كَثِيرٌ فَمَا وَهَنُوا لِمَا أَصَابَهُمْ
فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَمَا ضَعُفُوا وَمَا أَسْتَكَانُوا وَاللَّهُ يُحِبُّ الصَّابِرِينَ

Na Manabii wangapi walipigana na maadui, na pamoja nao kulikuwa na watakatifu wengi. Hawakulegea kwa yale yaliyowasibu katika njia ya -Mwenyezi Mungu, wala hawakudhoofika wala hawakudhalilika. Na Mwenyezi Mungu anawapenda wafanyao subira (3: 146)

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَا يَأْتِكُمْ مَّثُلُ الَّذِينَ خَلُوا مِنْ قَبْلِكُمْ
مَّسْتَهُمُ الْبَاسَاءُ وَالضَّرَاءُ وَزُلُّوا حَتَّىٰ يَقُولَ الرَّسُولُ وَالَّذِينَ ءامَنُوا
مَعَهُ وَمَتَّنِي نَصْرُ اللَّهِ إِلَّا إِنَّ نَصْرَ اللَّهِ قَرِيبٌ

Mnadhani kuwa mtaingia Peponi, na hali hamjajiwa na mfano wa (yale yaliyowajia) wale waliopita kabla yenu? Yaliwapata mashaka na madhara na wakatetemeshwa sana hata Mitume na walioamini pamoja nao wakasema: “Nusura ya Mwenyezi Mungu itafika lini?” Jueni kuwa nusura ya Mwenyezi Mungu iko karibu. (2:214).

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَا يَعْلَمِ اللَّهُ الَّذِينَ جَاهَدُوا مِنْكُمْ

وَيَعْلَمُ الصَّابِرِينَ

Je! Mnadhani mtaingia Peponi, hali Mwenyezi Mungu hajawapambanua wale waliopigania dini ya Mwenyezi Mungu mionganoni mwenu, na kuwapambanua waliofanya subira? (Sharti yaonekane kwanza haya hapa ulimwenguni). (3:142).

(v) Kuwa mvumililivu juu ya maudhi ya kila namna yanayotolewa na maadui wa Uislamu. Historia inatuonesha kuwa maadui wa Uislamu kabla hawajafikia hatua ya kuuzuia Uislamu kwa nguvu, huanza mapambano yao kwa maneno ya kashfa na dharau na kueneza propaganda za uongo dhidi ya Uislamu na Waislamu. Kwa mfano

makafiri wa Kiquraishi walimwita Mtume(s.a.w) mchawi, mkiwa (abtar), mwendawazimu, mwenye kupagawa na shetani na mwenye kurogwa.Pia walimbeza na kumfanyia stihizai za kila namna.Mtume (s.a.w)hakuwajali bali aliendelea na ujumbe wake na watu wakawa wanazidi kusilimu siku baada ya siku.Ilikuwa hivyo kwa sababu Mtume (s.a.w) alifuatilia kwa makini maelekezo ya awali aliyopewa na Mola wake ya kufanya subira katika Al-Muzzammil (73:10) na Al-Muddathir (74:7).

Mwanaharakati hana budi kutambua kuwa yaliyomsibu Mtume (s.a.w) na walioamini pamoja naye katika kazi ya kusimamisha Uislamu ni lazima naye yamfike au mfano wake. Katika jamii ya leo maneno ya kashfa dhidi ya Uislamu na Waislamu si mageni kwetu. Waislamu wenyewe siasa kali,wanaochanganya dini na siasa, waislamu wanaotumiwa na maadui, waislamu wenyewe kuleta uchochezi ili kuvuruga amani na usalama, magaidi, n.k.Mwanaharakati hana budi kumuiga Mtume (s.a.w) kwa kudharau kashfa, matusi na propaganda zote na aendelee na kazi yake ili asije akatolewa katika lengo.

(vi) Kusubiri katika misukosuko ya kawaida ya maisha. Kama Allah (s.w) anavyotuasa katika Qur'an:

وَلَنَبْلُونَكُم بِشَيْءٍ مِّنَ الْخَوْفِ وَالْجُوْعِ وَنَقْصٍ مِّنَ الْأُمُوْلِ
وَالْأَنْفُسِ وَالثُّمَرَاتِ وَبَشَّرَ الصَّابِرِينَ ﴿١٥٥﴾
أَصَبَّتُهُمْ مُصِيْبَةً قَالُوا إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ ﴿١٥٦﴾ أَوْلَئِكَ
عَلَيْهِمْ صَلَوَاتٌ مِّنْ رَبِّهِمْ وَرَحْمَةٌ وَأَوْلَئِكَ هُمُ الْمُهَتَّدُونَ ﴿١٥٧﴾

Na tutakutieni katika msukosuko wa (baadhi ya mambo haya); hofu na njaa na upungufuwa mali na wa watu na wa matunda. Na wapashe habari njema wanaosubiri". Ambao uwapatapo msiba husema: "Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake

Yeye tutarejea (atatupa jaza yake)".

Hao juu yao zitakuwa baraka zitokazo kwa Mola wao na rehema; na hao ndio wenye kuongoka". (2:155-157).

7. Kuwa na Hekima

Hekima ni miongoni mwa sifa kuu muhimu anayotakiwa awe nayo Mwanaharakati.Kamwe mafanikio hayatapatikana pasi na kutumia hekima. Kutumia hekima katika Harakati ni maamrisho ya Allah (s.w.) kama anavyotuagiza katika aya ifuatayo:

اَذْعُ إِلَى سَبِيلِ رَبِّكَ بِالْحِكْمَةِ وَالْمُوعِظَةِ الْحَسَنَةِ وَجَدِلُهُمْ بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ يَمَنِ ضَلَالًا عَنْ سَبِيلِهِ وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمَهَدِيدِينَ

Waite (watu) katika njia ya Mola wako kwa Hekima na mawaidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola wako ndiye anayemjua aliyepotea katika njia yake, naye ndiye anayewajua walioongoka. (16:125)

Hekima ni kipengele cha tabia njema chenye maana pana. Hekima kwa ujumla ni kufanya jambo la sawa sawa kwa namna ya sawasawa kwa wakati wa sawa sawa katika mazingira ya sawa sawa.

Mafunzo na mazoezi ya kumuandaa mwanaharakati

Mwanaharakati baada ya kuzifahamu hizo sifa saba za msingi, hanabudi kufanya jitiahada za makusudi za kuijiandaa kama alivyo andaliwa Mtume (s.a.w). Tunajifunza katika historia kuwa Mtume (s.a.w) aliandaliwa **ki-il-hamu** na **kimafunzo**.

Pamoja na kuzingatia mafunzo yatokanayo na maandalizi ya Mtume (s.a.w) ya ki-il-hamu, hatunabudi pia kuzingatia mafunzo ya ujumbe wa wahy wa mwanzo mwanzo alioshushiwa Mtume (s.a.w) katika kukabidhiwa dhima ya utume katika:

• A'laq (96:1-5)

أَفْرَأَ يَا سِمِّ رَبِّكَ الَّذِي خَلَقَ ① خَلَقَ الْإِنْسَانَ مِنْ عَلَقٍ ② أَفْرَأَ وَرَبُّكَ
الْأَكْرَمُ ③ الَّذِي عَلِمَ بِالْقُلُمِ ④ عَلِمَ الْإِنْسَانَ مَا لَمْ يَعْلَمْ ⑤

• Muzzammil (73:1-10)

يَتَأَيَّهَا الْمُزَّمِّلُ ① قُمْ الْيَلَ إِلَّا فَلِيَلَا ② نِصْفُهُ وَأَوْ نِصْفُهُ مِنْهُ قَلِيلًا
أَوْ زِدْ عَلَيْهِ وَرَبِّلِ الْقُرْءَانَ شَرِّيَلَا ④ إِنَّا سَنُثْقِنِي عَلَيْكَ
قَوْلًا ثَقِيلًا ⑤ إِنَّ نَاسَةَ الْيَلِ هِيَ أَشَدُّ وَطْأً وَأَقْوَمُ قِيلًا ⑥ إِنَّ لَكَ فِي
النَّهَارِ سَبْعًا طَوِيلًا ⑦ وَأَذْكُرِ اسْمَ رَبِّكَ وَتَبَّلِ إِلَيْهِ تَبَّيَلًا
رَبُّ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ فَاتَّخِذْهُ وَكِيلًا ⑧
وَأَصْبِرْ عَلَىٰ مَا يَقُولُونَ وَأَهْجِرْهُمْ هَجْرًا جَمِيلًا ⑨

• Muddathir (74:1-7)

يَتَأَيَّهَا الْمُدَثِّرُ ① قُمْ فَانِدِرُ ② وَرَبِّكَ فَكِيرُ ③ وَثِيابَكَ فَطَهِيرُ
وَالرُّجْزَ فَاهْجُرُ ⑤ وَلَا تَمْنُنْ تَسْتَكْشِرُ ⑥ وَلِرَبِّكَ فَأَصْبِرُ ⑦

Kwa kuzingatia mafunzo tuyapatayo kutokana na maandalizi haya ya Mtume (s.a.w) mwanaharakati hanabudi kujiandaa kwa kupitia mafunzo na mazoezi yafuatayo:

1. Kusoma Elimu sahihi juu ya Uislamu

Kwa kufuata mtaala wa Darasa la Watu Wazima – Juzu 1-7 na kupitia vitabu vya wanaharakati mashuhuri kama akina A.A Maudud, Shahiid Sayyid Qutub na Shahiid Hassan Al-Bannah (Rehemaa za Allah ziwe juu yao).

2. Kujiipamba na tabia njema

Kama ilivyoelekezwa katika Qur'an na Sunnah. Soma vipengele vya tabia njema kama vilivyo ainishwa katika:

- (i) Juzuuy ya Pili – Sura ya kwanza – Maisha ya Shahada.
- (ii) Juzuuy ya Tatu – Sifa za Waumini kama zilivyo ainishwa kaitka Qur'an.
- (iii) Vitabu vya Hadith kama vile Riyadhus – Swalihiiin, na vinginevyo.

3. Kusoma Mbinu za Kulingania na Kuufundisha Uislamu.

Kila mwanaharakati anapaswa kujifunza mbinu za kulingania na kuufundisha Uislamu ili awe mlinganiasi na mwalimu bora atakayeweza kufikisha ujumbe kwa ufanisi.

4. Kuitakasa nafsi na kujijengea msimamo na ujasiri kwa kufanya yafuatayo:

- (i) Kutekeleza nguzo zote za Uislamu kama ipasavyo na kujitahidi kufikia lengo tarajiwa kwa kila nguzo.
- (ii) Kujizatiti kutekeleza maamrishi yote ya Allah na kuacha makatazo yake yote kwa kadiri ya uwezo.
- (iii) Kujizatiti kumtii Mtume (s.a.w) na kufuata mwenendo wake na kujitahidi kutekeleza matendo yote ya Sunnah aliyoinishwa katika ibada maalumu kama vile swala na funga za Sunnah na katika mwenendo mzima wa maisha ya kila siku.
- (iv) Kujitahidi kusimamisha swala ya usiku (Tahajjud) kila siku katika maisha yote ya mwanaharakati ili kupata ujasiri na ukomandoo (ujasiri na ukakamavu) wa nafsi.
- (v) Kusoma Qur'an kwa mazingatio. Mwanaharakati ajiwekee ada ya kuipitia tafsiri ya Qur'an na sherehe yake ili kupata ujumbe uliokusudiwa katika kila aya na

kuiingiza katika utekelezaji wa maisha yake ya kila siku. Awe na ada ya kupitia Qur'an yote kwa namna hii kuanzia sura ya mwanzo (Al-Faati'ha)mpaka sura ya mwisho (An-Naas)na kuanza tena mzunguko huo dumu daima. Katika kupitia Qur'an kwa namna hii, mwanaharakati awe na daftari maalumu la kunukuu mafunzo maalumu atakayo yapata. Ni kawaida, kila utakapoipitia Qur'an, hutaacha kupata mafunzo mapya kulingana na mazingira na wakati uliopo.

- (vi) Kuwa na ada ya kumdhukuru (kumkumbuka) na kumtukuza Allah (s.w) mara kwa mara kwa kuleta dhikiri asubuhi na jioni na katika kufanya matendo maalumu kama vile kulala na kuamka, kuanza na kumaliza kula na kadhalika, kama alivyofanya Mtume (s.a.w). Rejea Darasa la Watu Wazima Juzuu ya tatu – sura ya tano.
- (vii)Kumtegemea Allah (s.w) na kumfanya mlinzi pekee. Mwanaharakati hatamchalea au kumuogopa yejote anayemsalitisha na Allah (s.w) na Mtume wake.
- (viii)Kuwa na tabia ya kujihesabu na kuleta toba ya kweli pale anapogundua amemkosea Allah (s.w) na Mtume wake. Kuwa na kawaida ya kuleta stighfar mara 100 au zaidikila siku.

5. Kujihusisha na masuala ya kijamii kwa kufanya yafuatayo:

- (i) Kuwa mwepesi wa kuwatendea wema na kutoa huduma kwa wanaadamu wenzake kila inapohitajika.
- (ii)Kuwa mstari wa mbele katika kazi za kujitolea za kuendeleza Uislamu na jamii ya binaadamu kwa ujumla kwa kutarajia malipo kutoka kwa Allah (s.w) tu.
- (iii)Kuwa mwepesi wa kutoa mali kwa ajili ya kuendeleza harakati za Kiislamu na kuwasaidia wenye matatizo (wenye kuhitajia msaada) kwa kutarajia malipo kutoka kwa Allah (s.w) tu.

- (iv) Kuchukia maovu na udhalimu na kufanya jitihada za makusudi za kuyaondoa au kuyakemea kwa kadiri ya uwezo.
- (v) Kuwa na hamu na shauku ya kupigania Dini ya Allah na kufa shahidi.
- (vi) Kujitahidi kulingania na kuufundisha Uislamu kwa jamii akianzia kwa familia yake kisha kwa ndugu, jamaa na marafiki wa karibu na mbali.
- (vii) Kujiunga pamoja na watu binafsi, vikundi au taasisi zenye lengo kuu la kusimamisha Uislamu katika jamii.

Zoezi la Tatu

1. *Nani asemaye kauli bora kuliko yule aitaye(watu) kwa Mwenyezi Mungu na mwenyewe akafanya vitendo vizuri na kusema (kwa maneno yake na vitendo vyake), hakika mini ni mionganini mwa waislamu”(41:33)*

Chambua mafunzo makubwa matatu (3) yatokanayo na aya hii.

2. (a) Nani mwanaharakati wa Kiislamu ?
 (b) Chambua sifa anazostahiki kujipamba nazo mwanaharakati wa kiislamu.
3. “*Na kwa ajili ya Mola wako fanya Subira”* (74:7)

Subira ni kipengele cha tabia njema chenye maana pana. Bainisha maeneo makuu matano (5) yanayompasa mwanaharakati kuleta subira.

4. “*Waite (watu) katika njia ya Mola wako kwa Hekima na mawaidha mema*” (16:125)

Nini Hekima ?



Sura ya Nne

KUNDI LA HARAKATI ZA KIISLAMU

Ni lipi kundi la Harakati

Kundi la Harakati ni kundi lililo anzishwa na wanaharakati kwa lengo la kulingania na kusimamisha Uislamu katika jamii.

Umuhimu wa kuwepo Kundi la Harakati

Kila Muislamu lazima afahamu kuwa, hakuna Uislamu wa mtu binafsi. Kama Uislamu haujasimamishwa katika jamii mtu mmoja mmoja hawezi kuufuata Uislamu katika kukiendea kila kipengele cha maisha yaki kibinafsi na kijamii kama anavyoagiza Allah (s.w):

يَٰٰيُّهَا أَلٰذِينَ ءَامَنُوا ادْخُلُوْفِي الْسَّلَمِ كَافَةً وَلَا تَشْعُرُوْ
 حُطُّوْاتِ الشَّيْطَنِ إِنَّهُ لَكُمْ عَدُوٌّ مُّبِينٌ

(2:208)

“Enyi mlionami! Ingieni katika Uislamu wote (kwa kufuata hukumu zote) wala msifuate nyayo za Sheitwan, kwa hakika yehe kwenu ni Adui dhahiri” (2:208)

Mtu mmoja hawezi kuuingia Uislamu wote kwa sababu kuna vipengele vingi vya kijamii ambavyo mtu binafsi hawezi kuvitekeleza kwa kufuata mwongozo wa Qur-an na Sunnah, bali inabidi afuate nyayo za Shetani kwa kufuata utaratibu wa maisha uliowekwa na “matwaghuti” au wachupaji mipaka ya Allah (s.w). Kwa mfano, katika miongozo ya “Kitwaghuti” uchumi umejengwa juu ya misingi ya riba, kamari, ulevi, hongo, ulaghai, dhulma, ulanguzi, n.k. Waislamu binafsi wanaoishi katika jamii hizo hawana namna ya kujivua na uchumi huo haramu wakiwa katika hali ya mtu mmoja mmoja na kwa vyovoyote vile kipato chao kwa njia moja au nyingine kitatokana na Riba, Kamari,

Hongo, Dhulma, Ulevi, n.k. Huo ni mfano mmoja tu wa uchumi, kuna masuala ya Sheria na Hukumu za Kijahili, Utamaduni wa Kijahili, Siasa za Kitwaghuti na mifumo mingine ya Kitwaghuti katika kila fani ya maisha ya jamii.

Kutokana na hali hii ipo haja ya kuusimamisha Uislamu katika jamii ili kuwawezesha Waislamu kukiendea kila kipengele cha maisha ya kibinagsi na kijamii kwa kufuata baraabara muongozo wa Qur-an na Sunnah.

Kazi ya kusimamisha Uislamu katika jamii haiwezi kamwe kufanikishwa na nguvu ya mtu mmoja mmoja. Mitume wa Allah (s.w) hawakuweza wao wenyewe kufanikisha mpaka walipopata wafuasi waliosaidiana nao bega kwa bega. Hivyo jukumu la kuusimamisha na kuuendeleza Uislamu liko juu ya mabega ya waumini wote katika jamii.

Waislamu wataweza kutekeleza jukumu hili endapo tu watakuwa wameungana pamoja na kuwa umma mmoja au endapo tu watatekeleza amri ya Allah (s.w) ifuatayo:

وَأُنْتَصِمُوا بِحَبْلِ اللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَقْرَفُوا

“Na shikamaneni kwa kamba (dini) ya Allah nyote wala msifarikiane...” (3:103)

Bila shaka Waislamu wakitekeleza hili watakuwa umma wenye nguvu na uwezo wa kusimamisha Uislamu katika jamii kama Allah (s.w) anavyotuthibitishia:

كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجْتُ لِلّٰهِي تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَنَهَايُونَ
عَنِ الْمُنْكَرِ وَتَوْمِئُونَ بِاللَّهِ

“Nyinyi ndio umma bora kuliko umma zote zilizodhahirishiwa watu (ulimwenguni) mnaamrisha yaliyo mema na mnakataza yaliyo maovu na mnawamini Mwenyezi Mungu.....” (3:110)

Katika hali halisi ni vigumu kupatikana umma wa Kiislamu kutokana na jamii ya kijahili pasi na maandalizi. Uwezekano wa kuunda umma huo utakaosimamisha Uislamu katika jamii utakuwepo tu pale Waislamu wachache watakapotanabahi na kuunda kundi lililosikamana barabara likajizatiti katika **kulingania Uislamu, kuamrisha mema na kukataza maovu** katika jamii kama alivyojizatiti Mtume (s.a.w) na maswahaba wake. Kuhusu kundi hili Allah (s.w) anaagiza:

وَلْتَكُن مِّنْكُمْ أُمَّةٌ يَدْعُونَ إِلَى الْخَيْرِ وَيَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَنَهَاوْنَ عَنِ
الْمُنْكَرِ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ

﴿١٠٤﴾

“Na wawepo katika nyinyi watu wanaolingania kheri (Uislamu) na wanaoamrisha mema na kukataza maovu na hao ndio watakaotengenekewa.” (3:104).

Sifa za kundi la harakati

Si kila kundi litakalojitokeza na kudai kuwa linalingania Uislamu katika jamii litakuwa lile lililoagizwa katika Qur-an (3:104). Vikundi vingi tunavyovifahamu vilivyojitangazia kuwa ni vikundi vya Harakati vimeishia katika kuwafarakanisha Waislamu na kuzidi kuwapa mwanya maadui wa Uislamu wazidi kuuangamiza. Tukumbuke kuwa kazi hii ni kazi takatifu iliyofanywa na Mitume wa Allah (s.w) na wale walioamini pamoja nao. Hivyo, mafanikio katika kazi hii yatapatikana tu kama kundi la Harakati litaigiza vilivyo mwenendo wa Mitume na walioamini pamoja nao katika kufanya kazi hii.

Kundi la Harakati ili liweze kufanikiwa katika kuhuishwa Uislamu na kuusimamisha katika jamii linalazimika kwa ujumla wake liwe na sifa za msingi zifuatazo:

1. Kila mwanakundi kujipamba na sifa za mwanaharakati.
2. Mshikamano wa udugu na upendo.
3. Kushauriana.
4. Nidhamu.
5. Kukosoana kwa nia njema na kwa njia nzuri.
6. Kuepukana na kujiona.
7. Kujiepusha na Ria.
8. Kuwa na Subira
9. Kuwa na Hekima

1. Kila mwanakundi kujipamba na Sifa za Mwanaharakati.

Asiruhusiwe mtu (kujiunga) kuingia ndani kabisa ya kundi mpaka awe muislamu wa maneno na vitendo (awe na sifa saba za Mwanaharakati). Mtu atakuwaje mwanaharakati wa kusimamisha Uislamu na huku ni mvunjaji mkubwa wa Uislamu katika mwenendo wake wa maisha yake ya kila siku? si kila mtu atakayejiita Muislamu au mwanaharakati wa Kiislamu tumchukulie kuwa yuko hivyo, mtu huyo atathibitika kuwa yuko hivyo katika mwenendo wake na utendaji wake katika kuziendea harakati mbali mbali za Kiislamu.

2. Mshikamano wa udugu na Upendo.

Kundi la Waislamu litakalofanikiwa kuulingania Uislamu na kuusimamisha katika jamii ni lile tu litakaloshikamana pamoja kwa udugu na upendo. Kila mmoja katika kundi akawa anawapenda wenzake na kuwahurumia kwa undani na akawa tayari kujitoa muhanga kwa ajili ya wenzake. Kundi la Harakati lenye mshikamano huu ndilo litakalofanikiwa katika kulingania na kuisimamisha Dini ya Allah (s.w) katika jamii, kwani msaada wa Allah (s.w) na radhi zake ziko juu yao:

إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الَّذِينَ يُقْدِلُونَ فِي سَيِّلِهِ، صَفَا كَانُهُمْ بُنْيَنٌ مَرْضُوصٌ

“Kwa yakini Mwenyezi Mungu anawapenda wale wanaopigana katika njia yake safu safu (mkono mmoja) kama kwamba wao ni jengo lililokamatana barabara.” (61:4)

Kundi hili litapatikana pale tu Waislamu walioamua kujiingiza katika kazi ya kupigania dini ya Allah (s.w) watakapokamatana baraabara kwa ushirikiano, umoja, udugu na upendo. Mshikamano au mkamatano wa aina hii ni muhali kupatikana pasi na kila mwanakundi kuzingatia na kutekeleza yafuatayo:

- (a) Kuwa na lengo moja tu.
- (b) Kuwafanyia wema wanakundi na
- (c) Kutowafanyia mabaya wanakundi.

(a) Kuwa na lengo moja tu

Kila mlinganiaji hana budi kufahamu vyema kuwa lengo lililo mbele yake ni kuhakikisha kuwa dini ya Allah (s.w) inasimama katika jamii na kuwa juu ya dini zote kama lengo hili lilivyobainishwa katika Qur-an:

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ وَبِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَ رَءُوفًا

عَلَى الْدِّينِ كُلِّهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ ﴿٣﴾

“Yeye (Allah) ndiye aliyemtuma Mtume wake kwa uongofu na dini ya haki ili kuifanya ishinde dini zote ijapokuwa washirikina watachukia.” (9:33, 61:9)

Maana ya Uislam kuwa juu ya dini nyingine zote ni kwamba pamoja na kuwepo taratibu nyingine za maisha katika jamii, utaratibu wa maisha aliouweka Allah (s.w) kupitia kwa Mitume yake, yaani Uislamu, ndio pekee utakaofuatwa na Waislamu katika kuendesha maisha yao ya kibinagsi na ya kijamii.

Mwanaharakati atakapoliweka machoni pake lengo hili la kusimamisha Uislamu na kuufanya uwe juu ya taratibu zote za maisha katika jamii, na akawa analiendea lengo hili kwa hali na mali atafurahi sana kuungana na kushirikiana na wengine walio tayari kama yeze kuliendea lengo hili.

Waislamu wanapoungana kwa ajili ya kuliendea lengo hili moja tu, daima hawafarakani, kwani huwa wepesi kusamehe na kudharau tofauti zozote zitakazotokea baina yao ambazo hazihusiani na lengo na ambazo endapo wataziendekeza zitawafarakanisha na kuwatoa kwenye lengo au kuwachelewesha kufikia lengo.

Waislamu wakiungana pamoja kwa madai kuwa wao ni kundi la kupigania au kusimamisha Dini ya Allah (s.w) katika jamii, lakini miongoni mwao wakawa na malengo mengine ya kibinafsi, kamwe hapawezi kuwa na ushirikiano na mshikamano katika kundi hilo. Itafikia kipindi harakati hizo zitafika njia panda kwa kila mwanakundi kufuata njia halisi inayolingana na lengo lake. Kundi likifika hapo ni lazima mfarakano utokee kutokana na chuki, fitna, bughudha na uadui utakaokuwepo miongoni mwa wanakundi. Hali hii inatokea kwa sababu wale wenye malengo mengine kama vile maslahi mbali mbali ya kidunia wanayotaraji kuyapata kutokana na kundi hawatakubali kuyakosa maslahi hayo na wakati huo huo hawataweza kubainisha malengo yao hayo au unafiki wao mbele ya vikao vya kawaida vya wanakundi. Hivyo itabidi watumie vikao vya fitna na uchochezi ili kujenga hali ya chuki na uadui katika kundi dhidi ya wale wote wanaosimama imara kuhakikisha kuwa lengo bayana la kundi linafikiwa.

Waislamu hatuna budi kuwa macho mno wakati tunapokusanyana kuanzisha vikundi vya harakati za kusimamisha Uislamu katika jamii. Tumeona vikundi vingi vilivyojiita vya “Harakati za Kiislamu” ambavyo vilizimika vikawa kama kwamba

havikuwepo baada ya kutokea mfarakano na wanakundi kutawanyika kwa uadui na uhasama. Mifarakano hii katika vikundi hutokea pale baadhi ya wanakundi walipoona hawapati maslahi yao waliyoyatarajia. Tusithubutu kuanzisha vikundi ambavyo vitaruhusu wanafiki kuingia kwa urahisi na kutufarakanisha kabla hatujafika popote na kutufanya tushindwe kufikia lengo. Wanakundi hawana budi kuwa ni wale wenye sifa zinazostahiki ikiwa ni pamoja na kulifahamu vyema lengo la harakati.

Tuwe macho sana na wanafiki wenye kudai kuwa wanasimamisha Uislamu kumbe wana ‘malengo mengine.’ “Hawa ndio wavurugaji wakubwa wa harakati za Kiislamu.”

(b) Kufanyiana Wema

Udugu na upendo utakaoleta mshikamano na ushirikiano kati ya wana kundi utakuwepo pale kila mwanakundi atakapojizatiti katika kuwatendea wenzake wema. Kutendea wengine wema ni jambo pana linalohusu mambo mengi ikiwa ni pamoja na kuhurumiana na kusaidiana wakati wa shida na matatizo, kupeana zawadi mara kwa mara, kukaribishana na kutembeleana mara kwa mara, kujumuika pamoja katika furaha na misiba, kutembelea wagonjwa, kupeana salaam na kuchangamkiana kila mkutanapo.

Kufanyiana wema ni jambo la msingi linaloleta na kupalilia upendo mionganini mwa Waislamu na wanaadamu wote kwa ujumla na limepewa msisitizo mkubwa katika Uislamu. Hivyo, udugu na upendo utakaoleta mshikamano kati ya wanakundi utakuwepo pale tu kila mwanakundi atakapojizatiti katika kuwatendea wenzake wema. Kuwatendea wengine wema ni jambo pana linalohusu mambo mengi ikiwa ni pamoja na:

(i) Kuhurumiana na kusaidiana wakati wa shida na matatizo.

Allah (s.w) anatutanabahisha katika aya ifuatayo:

﴿لَيْسَ الْبِرُّ أَنْ تُؤْلِمُ وَجْهَكُمْ قَبْلَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغَرِبِ
وَلَكِنَّ الْبِرُّ مَنْ ظَاهَرَ مَعَ الْمُتَّقِينَ
وَأَنْلَبَّى الْمَالَ عَلَى حُبِّهِ، ذَوِي الْقُرْبَى وَالْيَتَامَى وَالْمَسَاكِينَ
وَأَبْنَى السَّبِيلَ وَالسَّابِلِينَ وَفِي الرِّقَابِ وَأَقَامَ الصَّلَاةَ وَءَاتَى الْزَكَوَةَ
وَالْمُؤْفُونَ بِعَهْدِهِمْ إِذَا عَاهَدُوا وَالصَّابِرِينَ فِي الْبَأْسَاءِ وَالصَّرَاءِ
وَحِينَ الْبَأْسِ أُوتِّبِكَ الَّذِينَ صَدَقُوا وَأُوتِّبِكَ هُمُ الْمُنَقَّبُونَ﴾

Sio wema (peke yake) kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa Mashariki na Magharibi. Bali wema hasa (ni wa wale) wanaomwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii na wanawapa mali juu ya kuwa wanayapenda, jamaa na mayatima na maskini na wasafiri (walioharibikiwa) na waombao na katika (kuwakomboa) watumwa, na wakawa wanasmamisha swala na kutoa zakat, na watekelezao ahadi zao wanapoahidi, na wavumiliao wakati wa shida na dhara na wakati wa vita, hao ndio waliosadikisha (Uislamu wao) na hao ndio wamchao Mungu. (2:177)

Aya hii imeeleza kwa upana kuwa mwema hasa ni Muumini mwenye kutekeleza vivilyo maamrisho yote ya Uislamu ikiwa ni pamoa na kuwahurumia na kuwasaidia wenye kuhitajia msaada kwa kadri ya uwezo wake. Kuhurumiana na kusaidiana kunajenga udugu na upendo wa ndani mionganoni mwa wahusika kama tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

Nu'man bin Bashir (r.a) amesema kuwa Mtume wa Allah amesema: “utawaona waumini wakifanyiana wema, wakipendana na kuhurumiana kama mwili mmoja. Wakati kiungo kimoja kikiugua, mwili mzima huhisi homa na hukesha (kwa maumivu). (Bukhari na Muslim)

Aidha katika Hadith nyingine,

Nu'uman bin Bashir (r.a) amesema kuwa Mtume wa Allah amesema: “Waumini ni sawa na mwili mmoja. Kama macho yanauma (yana matatizo), mwili mzima unauma (una matatizo), kama kichwa chake kinauma basi mwili mzima unauma”. (Muslim).

Hadith hizi zinatufahamisha na kutukumbusha kuwa tatizo la Muislam mmoja ni tatizo la Waislamu wote, kwa hiyo hawana budi kushirikiana pamoja kwa hali na mali katika kuondoa tatizo hilo.

(ii) Kutekelezeana wajibu

Kila Muislamu anawajibika kumtendea Muislamu mwenziwe mambo sita yaliyoelezwa katika Hadith ifuatayo:

Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Haki za Muislamu kwa Muislamu mwengine ni sita. Ikaulizwa ni zipy hizo ewe Mtume wa Allah? Akajibu: (1) Ukikutana naye msalimie; (2) Akikuita mwitikie; (3) Akitaka ushauri mpe; (4) Akipiga chafya na akasema Al-hamdu lillah mwitikie (mrehemu kwa kusema Rahmakallaah); (5) Anapokuwa mgonjwa, nenda kamtazame na (6) Anapokufa fuata jeneza lake (mzike). (Muslim)

(iii) Kuchangamkiana

Kuchangamkiana kila mnapokutana ni jambo linalopalilia udugu na upendo nyoyoni mwa Waislamu. Jambo hili linatiliwa mkazo na Hadith ifuatayo:

Jabir (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: “Kila kitendo kizuri ni sadaqa, na ni mionganini mwa kitendo chema kuwa unakutana na ndugu yako (Waislamu) kwa uso mchangamfu, na kwamba unamimina kutoka kwenye ndoo yako kwa ndoo ya ndugu yako”. (Ahmed, Tirmiz).

(iv) Kupeana zawadi

Kupeana zawadi mara kwa mara ni jambo linalojenga udugu na upendo nyoyoni mwa Waislamu. Umuhimu wa kupeana zawadi unabainika katika Hadithi ifuatayo:-

Aysha (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: “Peaneni zawadi kwani zawadi inaondoa chuki”. (Tirmidh)

(v) Kusuluuhishana

Waislamu wanapoingiliwa na Shetani wakagombana, mara baada ya kutulia, wanalahizimika wasuluuhishane na kusameheana. Kila wakati Waislamu wanatakiwa wawe katika upendo na amani kama Hadithi ifuatayo inavyosisitiza:

Abu Hurairah (r.a) amesema kuwa Mtume wa Allah amesema: “Hamtaingia Peponi mpaka muamini; na hamtakuwa wenye kuamini mpaka mpendane. Je, nisikufahamisheni jambo ambalo mkilifanya mtaweza kupendana? Enezeni (dumisheni) amani mionganini mwenu. (Muslim).

Kwa mujibu wa mafundisho ya Mtume (s.a.w) Waislamu hawaruhusiwi kununiana kiasi cha kutotoleana salaam kwa zaidi ya siku tatu.

Pia ni wajibu kwa Waislamu kuingilia kati na kusuluhisha wawili waliogombana kama tunavyoamrishwa katika Qur-an:

وَإِنْ طَالِبُكُمْ تَنَانٍ مِّنَ الْمُؤْمِنِينَ أَفْتَرْلُوْا فَأَصْلِحُوهُ بَيْنَهُمَا فَإِنْ بَغَثُ إِحْدَاهُمَا عَلَى الْأُخْرَى فَقَدِيلُوا أَنَّهُمْ تَبْغُونَ حَسْنًا تَقْرِئُهُ إِلَى أَمْرِ اللَّهِ فَإِنْ فَاءَتْ فَأَصْلِحُوهُ بَيْنَهُمَا بِالْعَدْلِ وَأَقْسِطُوهُ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ ﴿٤٩﴾

Na ikiwa makundi mawili katika Waislamu wanapigana, basi fanyeni suluhu baina yao, na ikiwa moja la hayo linamdhulumu mwenzive, basi lipigeni lile linalooneea mpaka lirudi katika amri ya Mwenyezi Mungu. Na kama likirudi, basi yapatanisheni baina yao kwa uadilifu. Na hukumuni kwa haki. Hakika Mwenyezi huwapenda wanao hukumu kwa haki (49:9).

(vi) Kushirikiana pamoja katika furaha na misiba

Miongoni mwa wema unaojenga udugu na upendo miongoni mwa watu ni mtu kumpendelea mwenzive lile analolipenda na kuchukia lisimfikie mwenzive lile analolichukia. Aidha Waislamu wanalahimika kujumuika na Waislamu wenzao kwenye sherehe na furaha na kushiriki nao pia kwenye misiba na huzuni.

(vii) Kuzuia vinavyodhuru visimfikie mwenzio

Pamoja na Muislamu kuchukia baya lisimfikie Muislamu mwenzive, pia Muislamu atumie juhudhi kadri ya uwezo wake kuzuia kwa hali na mali mabaya yasimfikie Muislamu mwenzive. Tunajifunza msisitizo wa jambo hili katika Hadith ifuatayo:

Abu Barzata (r.a) ameeleza: “Nilisema: ‘Ee Mtume wa Allah! Nifundishe jambo ambalo litaninufaisha’. Alisema (Mtume): “Ondo vitu vibaya (kama vile miba uchafu, n.k.) katika njia ya Waislamu”. (Muslim).

Hadith hii pia inamuhimiza Muislamu kumsaidia ndugu yake aliyedhulumiwa mpaka apate haki yake.

Haya yote tuliyoyaorodhesha, ikiwa ni kushauriana na kusaidiana wakati wa matatizo, kutekelezeana wajibu, kuchangamkiana, kupeana zawadi, kuzuia kinachodhuru kisimfike ndugu yako, kumsaidia mwenye kudhulumiwa, kupeana ushauri mzuri, kukatazana maovu, n.k. ni mionganoni mwa mambo mema ambayo wanakundi wanatakiwa wajizatiti katika kutendeana ili kuhuisha na kudumisha udugu na upendo mionganoni mwao na mionganoni mwa Waislamu wote kwa ujumla; upendo utakao wawezesha kushikamana pamoja katika kuhuisha na kusimamisha dini ya Allah (s.w) kama tunavyoamrishwa:

وَأَغْتَصِمُوا بِحَبْلِ اللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفْرُقُوا وَأَذْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ
كُنْتُمْ أَعْدَاءً فَالَّذِي بَيْنَ قُلُوبِكُمْ فَاصْبَحْتُمْ بِنِعْمَتِهِ إِخْرَاجًا وَكُنْتُمْ عَلَى
شَقَا حُفْرَةٍ مِّنَ الْتَّارِ فَانْقَذَكُمْ مِّنْهَا كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ عَابِرَتِهِ لَعْلَكُمْ

تَهْتَذُونَ ﴿٤٧﴾

Na shikamaneni kwa kamba (dini) ya Allah nyote, wala msiachane. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyojuu yenu. (Zamani) mlikuwa maadui; naye akaziunganisha nyoyo zenu; hivyo kwa neema yake mkawa ndugu. Na mlikuwa ukingoni mwa shimo la moto (wa Jahannam), naye akakuokoeni nalo. Namna hivi Mwenyezi Mungu anakubainishieni aya zake ili mpate kuongoka. (3:103)

Pamoja na aya hii kuwaamrisha Waislamu washikamane pamoja katika kuipigania Dini ya Allah, inatuelekeza vile vile turejee historia tuone jinsi gani lile kundi la Waislamu lililokuwa pamoja na Mtume (s.a.w) lilivyoshikamana kwa udugu na upendo baada ya kuwa Waislamu. Historia inatufahamisha kuwa kabla ya

Uislamu kuingia Madina, makabila ya Ausi na Khazraj yalikuwa maadui kati yao. Walipigana na kuuana hata bila ya kuwa na sababu yoyote ya msingi. Lakini mara tu baada ya kuukubali Uislamu walishikamana pamoja kwa kalima ya “***Laailaaha illallah Muhammad-Rasuulullah***”na kuwa ndugu walioheshimiana,kushirikiana na kuhurumiana.Uislamu haukuwaunganisha watu wa Madina tu bali ulijenga udugu na upendo kati ya Waislamu waliohamia kutoka Makka, Muhajiriin na Waislamu wenyiji wa Madina, Answar. Waislamu hawa kutoka miji miwili tofauti waliunganishwa na Uislamu na kujenga udugu baina yao ambao ulikuwa na nguvu kuliko udugu wa damu.

Muhajiriin walipohama waliacha ndugu zao, mali zao, majumba yao na kila kilichokuwa chao. Hivyo katika makazi haya mapya walikuwa maskini wenyewe kuhitajia msaada.

Answar walifahamu vyema dhima yao juu ya ndugu zao hawa **Muhajiriin** na kutokana na mapenzi ya Kiislamu, hawakusubiri mpaka Muhajiriin wawanyooshee mkono wa kuomba. Walijitolea mali zao ikiwa ni pamoja na majumba yao, mashamba yao, na kila kilichokuwa muhimu kuwa nacho ndugu zao. Aidha walikuwa tayari kuwaacha wake zao (walikuwa na mke zaidi ya mmoja) ili baada ya eda waolewe na ndugu zao Muhajiriin.

Imesimuliwa katika sahihi Bukhari kuwa Sa'd bin Rabiah (r.a) ambaye alikuwa tajiri mkubwa sana mionganoni mwa Answar, alimwambia Abdul-Rahman bin Auf kwamba yeye Sa'd yupo tayari na atafurahi sana ampe Abdul-Rahman nusu ya mali yake. Na kisha kwa vile ana wake wawili, basi yupo tayari amuache mmoja ili baada ya kipindi cha eda kupita Abdul-Rahman amuo. Abdul-Rahman alikataa kupokea chochote badala yake akamwomba Sa'd amwonyeshe mahali penye soko ambapo atawezwa kwenda kushughulika na kupata chochote cha kumsaidia kuendesha maisha yake.(Bukhari)

Udugu, mapenzi na huruma baina ya Waislamu hawa wa kundi la Mtume (s.a.w) uliwawezesha Waislamu kushikamana pamoja na kufikia lengo la kusimamisha Uislamu katika jamii yao pamoja na upinzani mkubwa wa maadui wa Uislamu uliokuwapo. Allah (s.w) anawasifu Waislamu hawa kama ifuatavyo:

مُحَمَّدٌ رَسُولُ اللَّهِ وَالَّذِينَ مَعَهُ وَأَشْدَاءُ عَلَى الْكُفَّارِ رُحْمَاءُ بِيَنَهُمْ
 تَرَبَّهُمْ رُكُوعًا سُجَّدًا يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِنَ اللَّهِ وَرِضْوَانًا سِيمَاهُمْ فِي
 وُجُوهِهِمْ مِنْ أَثْرِ السُّجُودِ ذَلِكَ مَثَلُهُمْ فِي النَّورَةِ وَمَثَلُهُمْ فِي الْإِنْجِيلِ
 كَزَرْعٍ أَخْرَجَ شَطْعَهُ فَقَازَرَهُ فَاسْتَغْلَظَ فَاسْتَوَى عَلَى سُوقِهِ يُعْجِبُ
 الْرُّزْرَاعَ لِيَغِيظَ بِهِمُ الْكُفَّارُ وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ ظَمَّنُوا وَعَمِلُوا الْصَّلَاحَاتِ
 مِنْهُمْ مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ عَظِيمًا



Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na walio pamoja naye ni wenyе nyoyo thabiti mbele ya makafiri na wenyе kuhurumiana wao kwa wao. Utawaona wakiinama na kurukuu na kusujudu (pamoja) wakitafuta fadhila za Mwenyezi Mungu na radhi (yake). Alama zao zi katika nyuso zao, kwa taathira ya kusujudu. Huo ndio mfano wao katika Taurati. Na mfano wao katika Injili; Kuwa wao ni kama mmea uliota matawi yake; kisha (matawi hayo) yakautia nguvu, ukawa mnene ukasimama sawa sawa juu ya kigogo chake, ukawafurahisha walioupanda; ili awakasirishe makafiri kwa ajili yao. Mwenyezi Mungu amewaaahidi walioamini na kutenda mema katika wao msamaha na ujira mkubwa. (48:29)

Kundi la kuhuisha na kusimamisha Uislamu halina budi kuiga kundi hili.

(c) Kutofanyiana Mabaya

Sumu kali inayoua mshikamano wa udugu na upendo mionganoni mwa Waislamu na kuzaa mfarakano unaotokana na uadui na chuki ni kufanyiana mambo maovu. Mionganoni mwa mambo maovu yanayovunja udugu na upendo na kuwafarakanisha Waislamu ni kudhulumiana, kusengenyana, kudhaniana vibaya, kuchunguzana, kuchukiana pasina sababu ya msingi, kudharauliana, kutukanana, kuvunjiana heshima na kuzuliana. Hebu turejee makemeo ya maovu haya katika Qur-an na Hadith:

(i) Kudhulumiana

Dhulma ni kitendo kibaya mno kinacholeta chuki na uadui baina ya watu. Kamwe watu hawawezi kushikamana kwa udugu na upendo pale penye kudhulumiana. Katika Hija ya Kuaga Mtume (s.a.w) alisisitiza:

Enyi watu! Hakika damu yenu, vitu vyenu (mali zenu) na heshima yenu ni vitakatifu na havitaingiliwa mpaka mkutane na Mola wenu, kama ilivyo takatifu siku yenu hii, mwezi wenu huu na mji wenu huu. Hakika mtakutana na Mola wenu hivi punde na mtakuwa mas-uli juu ya matendo yenu.

Katika hutuba hii ya Mtume (s.a.w) tunajifunza kuwa maisha ya mtu, mali yake na heshima yake ni haki zake ambazo hazitaingiliwa na yejote. Mwenye kuingilia haki hizi atakuwa amefanya dhulma kubwa. Pia Mtume (s.a.w) amesisitiza katika Hadith zifuatazo:

Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Muislamu ni ndugu wa Muislamu. Hatamkosea, wala hatamvunja heshima, (hatamhuzunisha), wala hatamchukia. Ucha Mungu uko hapa (akiwa anaashairia kwa kidole kifuanini kwake mara tatu). Kumdharaau ndugu yake Muislamu yatosha kuwa kitendo kiovu kwa mtu. Kila damu ya Muislamu, mali yake na heshima yake ni takatifu kwa Muislamu. (Muslim).

(ii) Kusengenya, kudhaniana vibaya na kupekuana

Kusengenya ni jambo ovu mno linalovuruga upendo na udugu katika kundi la Waislamu. Kusengenya ni kuongea juu ya ndugu yako yale ambayo asingaliyapendelea kuyasikia kama angelikuwepo, hata kama hayo yanayoongelewa ni ya kweli.

Abu Hurairah amesimulia kuwa Mtume wa Allah aliuliza: Wote mnajua kusengenya ni nini? Walijibu (Waislamu) Allah na Mtume wake ndio wajuzi zaidi. Akasema: maongezi juu ya ndugu yako ambayo hayapendi. Aliulizwa: Je, kama kile kinachozungumzwa ni kweli juu ya ndugu yangu? Akajibu: Kama hilo unalomsengenya kwalo analo, bado utakuwa umesengenya, na kama hilo unalosema hanalo, basi utakuwa umemzulia. (Muislamu).

Uislamu umekemea vikali kusengenya kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

وَيُلِّمُ كُلَّ هُمَرَةٍ لِّمَرَّةٍ ﴿١﴾

Adhabu kali itamthubutikia kila mwenye kulamba kisogo, msengenya... (104:1)

يَأَيُّهَا الَّذِينَ ظَاهَرُوا أَجْنَبُوا كَثِيرًا مِّنَ الظُّنُنِ إِنَّ بَعْضَ الظُّنُنِ إِنَّمَا
وَلَا تَجَسَّسُوا وَلَا يَعْتَبِرُ بَعْضُكُمْ بَعْضًا أَيُّهُبْ أَحَدُكُمْ أَنْ يَأْكُلَ لَحْمَ
أَخِيهِ مَيْتًا فَكَرِهُتُمُوهُ وَأَنْتُمُ الَّذِينَ تَوَأَّمُونَ رَحِيمٌ ﴿٢﴾

Enyi mliaoamini! Jiepusheni sana na dhana (mbaya) kwani dhana ni dhambi. Wala msipeleleze (habari za watu). Wala baadhi yenu wasiwasesenye wengine. Je! Mmoja wenu anapenda kula nyama ya nduguye aliyekufa? La, hapendi. Na Mcheni Mwenyezi Mungu. Bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba, Mwingi wa kurehemu. (49:12)

Pia katika aya hii (49:12) tunaonywa kuwa tujiepushe na kuwadhania watu vibaya na kupeleze mambo ya watu. Haya nayo ni matunda maovu yanayofitinisha watu walioungana na kuwafarakanisha.

(iii) Kudharauliana na Kutukanana

Dharau na matusi ni mionganoni mwa maovu yanayovuruga mshikamano na upendo baina ya watu. Maovu haya yanakemewa katika aya ifuatayo:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ عَامَنُوا لَا يَسْخَرُ قَوْمٌ مِّنْ قَوْمٍ عَسَى أَنْ يَكُونُوا خَيْرًا
مِّنْهُمْ وَلَا نِسَاءٌ مِّنْ نِسَاءٍ عَسَى أَنْ يَكُنَّ خَيْرًا مِّنْهُنَّ وَلَا تَلْمِزُوهُنَّ
أَنفُسُكُمْ وَلَا تَنابِرُوهُنَّ بِالْأَلْقَبِ بِئْسَ الْأَسْمُ الْفُسُوقُ بَعْدَ الْإِيمَانِ وَمَنْ لَمْ
يَتُبْ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿١١﴾

Enyi mlionmini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao, huenda wakawa bora kuliko wao; wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao, huenda wakawa bora kuliko wao. Wala msitukanane kwa kabilia, wala msitikanane kwa majina mabaya (ya kejeli). Jina baya la kuambiwa mtu ni “asi” baada ya kuwa ni Muislamu. Na wasiotubu basi hao ndio madhalimu. (49:11).

(iv) Kumchukia Muislamu pasina sababu ya msingi

Ni katika uovu kumchukia Muislamu bila ya sababu ya msingi. Kupenda kwa Muislamu na kuchukia kwake watu kuwe kwa ajili ya Allah (s.w) tu.

(v) Kuvunjiana heshima na kuzuliana

Kuvunjiana heshima na kuzuliana ni mionganoni mwa maovu ambayo husababisha chuki na uhasama baina ya watu.

Hapana shaka kuwa kundi la Harakati na Waislamu wote kwa ujumla watashikamana pamoja na kuwa umma mmoja endapo kila mmoja atakuwa na lengo la kusimamisha Uislamu katika jamii na endapo kila mmoja atajitahidi kuwatendea ndugu zake wema na kujitahidi kujiepusha na kuwatendea maovu. Baada ya kuwa Waislamu wameungana na kushikamana pamoja, pasitokee mtu wa kuwafarakanisha. Mwenye kuwafarakanisha Waislamu ni adui mkubwa mbele ya Allah (s.w) na anastahiki kupigwa vita kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

Usamah bin Shariik (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: “Yeyote yule atakayejitokeza kuwagawanya Waislamu, mkateni kichwa chake”. (Nisai).

Pia Muislamu haruhusiwi kujitenga na ummah wa Kiislamu kwa vyovyote vile itakavyokuwa. Mwenye kujitenga na Ummah wa Kiislamu atakuwa amejitenga na Uislamu hata kama ataendelea kuswali, kufunga, kuhiji, na kadhalika, kama tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

Ibn Abbas (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: “Yeyote atakayeona jambo lisilompendeza kwa Kiongozi wake awe na subira, kwani hapana yeyote atakayejitenga na Jumuiya (Ummah) ya Kiislamu hata kiasi cha kimo cha kiganja cha mkono, ila akifa anakufa kifo cha wakati wa ujahili. (Bukhari na Muslim).

Ibn Umar (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: “Allah (s.w) hatawaunganisha wafuasi wangu (Waislamu) katika mambo ya upotofu, na mkono wa Allah uko juu ya watu walioshikamana; na atakayejitenga (na Ummah) atatengwa katika moto wa Jahannam.” (Tirmidh)

Abu Zarr (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: “Anayejitoa kwenye ummah (jumuiya ya Kiislamu) hata kiasi cha upana wa kiganja cha mkono, hakika atakuwa ameitoa kamba ya Uislamu shingoni mwake”. (Ahmad, Abu Daud).

Hadith zote hizi zinasisitiza kuwa mwenye kujitenga na jumuiya ya Kiislamu iliyojengwa na inayoendeshwa kwa misingi ya Uislamu atakuwa pia amejitenga na Uislamu hata kama ataendelea kujiita Muislamu au mwanaharakati wa kusimamisha Uislamu. Hali kadhalika Mwanaharakati aliyejiunga katika kundi la Harakati lililojengwa na linaloendeshwa katika misingi ya Uislamu atashikamana na kundi hilo mpaka mwisho wa maisha yake. Atakayejitoa kwenye kundi bila ya sababu za msingi atakuwa amejitoa katika Rehema ya Allah(s.w).

3. Kushauriana

Sifa nyingine ya kundi la Harakati ni kuwa na tabia ya kushauriana katika kuendesha shughuli za Harakati ili kujenga hisia za umoja na ushirikiano kwa lile wanadolifanya katika kuendea lengo. Suala la kushauriana ni suala la kidemokrasia linalositisizwa mno katika Uislamu kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

فِيمَا رَحْمَةٌ مِّنْ اللَّهِ لِيُتَ لَهُمْ وَلَوْ كُنْتَ فَظُلاً غَلِيلَظَ الْقُلُوبِ لَانْفَضُوا مِنْ
حَوْلِكَ فَأَعْفُ عَنْهُمْ وَأَسْتَغْفِرُ لَهُمْ وَشَارِرُهُمْ فِي الْأَمْرِ فَإِذَا عَزَّمْتَ
فَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُتَوَكِّلِينَ

104

Basi kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu umekuwa laini kwao (ewe Muhammad). Na kama ungelikuwa mkali na moyo mgumu, bila shaka wangelikukimbia. Basi wasamehe wewe na waombee msamaha (kwa Mwenyezi Mungu) na **ushauriane** nao katika

mambo. Na ufungapo nia mtegemee Mwenyezi Mungu tu (ufanye hilo uliloazimia). Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wamtegemeao. (3:159).

Katika aya hii tunajifunza kuwa kiongozi wa Kiislamu anatakiwa awe mpole na laini mwenye huruma na upendo kwa wale anaowaongoza na awe ni mwenye kushauriana nao katika kuendesha mambo. Pia tunajifunza katika aya hii kuwa Waislamu wanapoazimia kufanya jambo baada ya kushauriana, wasizembee wala kusita bali walitekeleze mara moja huku wakimtegemea Mwenyezi Mungu.

Pia tunajifunza katika Qur-an kuwa watakaofuzu na kustahiki malipo mema ya akhera ni pamoja na wale wanaoshauriana katika kuendesha mambo yao ya kheri:

فَمَا أُوتِيْتُم مِّنْ شَيْءٍ فَمَنْتَهُ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا وَمَا عِنْدَ اللَّهِ خَيْرٌ وَأَبْقَى
لِلَّذِينَ آمَنُوا وَعَلَى رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٢٣﴾ وَالَّذِينَ يَجْتَنِبُونَ كَثِيرًا
إِلَّا إِثْمٌ وَالْفَوَاحِشَ وَإِذَا مَا غَصِبُوا هُمْ يَغْفِرُونَ ﴿٢٤﴾ وَالَّذِينَ أُسْتَجَابُوا
لِرَبِّهِمْ وَأَقامُوا الصَّلَاةَ وَأَمْرُهُمْ شُورَى بَيْنَهُمْ وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنْفِقُونَ

Basi vyote hivi mlivyopewa ni starehe ya maisha ya dunia tu, lakini kilichoko kwa Mwenyezi Mungu ni bora na cha kudumu(milele). Watakistahiki wale walioamini na wakawa wanamtegemea Mola wao. Na wale wanaojiepusha na madhambi makubwa na mambo mabaya, na wale ambao wanapokasirika husamehe.

Na wale waliomuitikia Mola wao (kwa kila amri zake) na wakasimamisha Sala, na wanashauriana katika mambo yao na wanatoa katika yale tuliyowaruzuku.(42:36:38)

Faida za kushauriana

Kuna faida nyingi zinazopatikana kutokana na kushauriana kwa kila uamuzi unaohusu shughuli za kundi la Harakati na faida mbili zifuatazo ziko wazi:

Kwanza, kushauriana hutoa fursa kwa kila mwanakundi kutoa mawazo yake juu ya uendeshaji wa shughuli za Da'wah. Mchango wa mawazo kutoka kwa kila mwanakundi kutauwezesha uamuzi juu ya utekelezaji wa jambo, uwe ni wa hakika zaidi. Kwani kila mtu ana kipaji chake ambacho hakipo kwa mwingine - akili ni nyewe kila mmoja ana zake.

Pili, kwa kumpa kila mwanakundi nafasi ya kutoa ushauri wake juu ya jambo, uamuzi utakao fikiwa utakuwa ni wa kundi na kila mwanakundi atakuwa tayari kutekeleza kwa moyo mkunjufu maamuzi yaliyofikiwa. Hata utekelezaji ukiwa mgumu kiasi gani, hakuna atakayeona kuwa amepachikwa jukumu asiloafikiana nalo. Bali kila mwanakundi ataifanya shughuli yoyote atakayopewa mpaka aione hatima yake.

Masharti ya kushauriana

Katika kushauriana yafuatayo ni muhimu yazingatiwe.

Kwanza, kila mmoja anatakiwa awe huru kutoa maoni yake juu ya jambo linalojadiliwa bila ya kusita wala kuficha chochote. Mawazo yake yasiathiriwe na upendeleo wala chuki.

Pili, baada ya uamuzi kutolewa kutokana na kuzingatia mawazo ya kila mtu wale waliokuwa na maoni tofauti na uamuzi uliotolewa unaotokana na maoni ya wengi, hawana budi kwa moyo mkunjufu kukubaliana na uamuzi wa wengi hata kama hawajabadilisha mawazo yao.

Tatu, uamuzi au maoni ya wengi hayataangaliwa kama yamekiuka Qur'an na Sunnah.

Nne, kila mwanakundi hutekeleza shughuli kama ilivyoamuliwa na Shura.

Tano, kikao chochote baada ya shura, dhidi ya maamuzi ya shura ni unafiki na ni haramu.

4. Nidhamu

Sifa nyingine muhimu ya kundi la Harakati ni nidhamu. Kundi la Harakati ili lifanikiwe ni lazima liwe na nidhamu ya hali ya juu. Kila mwanakundi anawajibika kuwa na nidhamu na utii wa hali ya juu. Ahudhurie popote anapotakiwa, ahudhurie bila ya kukosa na katika muda uliopangwa; atekeleze majukumu yake yote kwa kufuata utaratibu uliowekwa na muda uliopangwa; ashirikiane na wenzake bega kwa bega katika shughuli waliyopangiwa pamoja na kumtii kiongozi wake kila atakapomuelekeza vilivyo katika kuendea lengo.

Pia kundi lenyewe linatakiwa liwe na nidhamu ya hali ya juu. Kundi la Harakati halina budi kuwa na uongozi imara unaoeleweka; liwe na mipango mizuri na imara ya muda mfupi na muda mrefu na njia au hatua za utekelezaji ziwe wazi. Utekelezaji wa mipango ya kundi hauna budi kufanyika mara moja baada tu ya uamuzi kupitishwa. Kundi la Harakati linatakiwa liongee kwa vitendo zaidi kuliko maneno. Kundi lijiepushe na kutangaza mipango yake kabla ya kuitekeleza. Ushabiki na kujionyesha ni sumu kubwa kwa kundi la Harakati.

Udhibiti wa siri zote zinazohusu kundi la Harakati na shughuli zake ni kipengele muhimu mno cha nidhamu. Mwanaharakati hatatoa siri za harakati kwa yoyote asiyehusika.

5. Kukosoana kwa nia njema na kwa njia nzuri

Sifa nyingine muhimu inayotakikana ipatikane katika kundi la Harakati ni hii ya kujikosoa na kukosoana kwa nia ya kujirekebisha na kurekebishana pale mwanakundi au kundi zima

linapoteleza na kwenda nje ya lengo. Kundi linaweza kujikuta halipati matunda yaliyokusudiwa pamoja na nia yake safi, lengo sahihi na muelekeo sahihi wa kuliendea lengo, kutokana na makosa yaliyojiingiza bila ya kung'amuliwa na kurekebishwa. Hivyo ili kundi la Harakati liepukane na makosa yanayojipenyeza mara kwa mara katika harakati, halina budi kuwa na utaratibu maalumu wa kukosoana kwa mwanakundi mmoja mmoja na kundi lote kwa ujumla.

Katika kukosoana inatakiwa kuchukua tahadhari kubwa, kwani endapo patafanyika kosa katika kufanya kazi hii, inawezekana ikawa ni sababu ya kuharibu zaidi kuliko kutengeneza. Kukosoa kuepukane kabisa na sura ya kudhalilishana, kudharauliana, kulaumiana, kuvunjiana heshima, n.k. Kukosoana kuwe kwa nia ya kumrejesha mwanakundi au kundi lote kwenye njia sahihi ya kuliendea lengo baada ya kuridhika kuwa mwana kundi au kundi kwa ujumla, linakwenda kinyume kidogo na lengo. Mkosoaji hana budi kuonesha huruma na upendo kwa huyo anayemkosoa na hana budi kutumia lugha nzuri na hekima kubwa katika kumkosoa. Mkosoaji mwenye nia nzuri kabisa, asiyetumia lugha nzuri na hekima, huweza kuingiza doa jeusi katika kundi na kudhoofisha mshikamano wa kundi na hatimaye kulifarakanisha. Pamoja na nia yake njema, mkosoaji huyu asiyetumia hekima na lugha nzuri katika kukosoa, hana tofauti na wale wanao wakosoa wenzao kwa kuwazulia makosa ili tu wawadhalilishe na kuwavunzia hadhi na heshima yao ili wao waonekane kuwa ndio bora na wanaofaa zaidi.

Kwa upande mwingine mwenye kukosolewa kwa nia njema na kwa utaratibu unaotakikana awetayari kukosolewa na kujirekebisha kwa moyo mkunjufu. Mwenye kukosolewa kwa nia njema hana budi kuona kuwa amefanyiwa ihsani na mkosoaji kwa kumrudisha katika njia sahihi ya kuendea lengo. Mkosolewaji anatakiwa amuone ndugu yake anayemkosoa kama kioo ambacho

hakilaumiwi kwa kuonesha alama ya uchafu usoni. Ni juu ya mwenye kujitazama kiono (mkosolewaji) kuundoa uchafu huo usoni mwake.

6. Kujiepusha na kujiona

Kujiona na majivuno ni mionganoni mwa vipengele veya tabia ambayo humtoa mtu katika njia ya Allah (s.w). Makemeo ya Allah (s.w) yako wazi juu ya wenye kujiona na kujivuna katika ardhi. Hebu turejee aya chache zifuatazo:

وَلَا تُصْعِرْ خَدَّاكَ لِلنَّاسِ وَلَا تَمْسِحَ فِي الْأَرْضِ مَرَحًا إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ كُلَّ

مُخْتَالٍ فَخُورٍ

Wala usiwatazame (watu) kwa upande mmoja wa uso, wala usiende katika nchi kwa maringo, hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila ajivunaye, ajifaharishaye. (31:18)

وَلَا تَمْسِحَ فِي الْأَرْضِ مَرَحًا إِنَّكَ لَنْ تَخْرِقَ الْأَرْضَ وَلَنْ تَبْلُغَ الْجِبَانَ

طُولًا

Wala usitembee(usiende)katika ardhi kwa maringo. Hakika wewe huwezi kupasua ardhi wala huwezi kufikia urefu wa milima(Basi unajivuna nini). (17:37).

Aya hizi zinatufahamisha wazi kuwa Allah (s.w) hawapendi wanaojivuna na kujifaharisha. Hivyo mwenye tabia hii mbaya hana radhi mbele ya Allah (s.w) katika maisha haya ya dunia na katika maisha ya Akhera.

Mwanaharakati na kundi la Harakati kwa ujumla, ili lipate mafanikio katika kazi yake ya kulingania na kusimamisha Uislamu katika jamii halina budi kujiepusha na kila aina ya kiburi. Pasiwe na namna yejote ile ya kujiona kuwa wao ni bora kuliko wengine wala wasijivunie mafaniko yoyote watakayopata.

Kundi la Harakati halina budi kuwa macho sana, kwani ni rahisi mno kutumbukia ndani ya majivuno na kujifaharisha. Ni rahisi kwa wale Waislamu wachache katika jamii wanaojizatiti kufanya amali njema, kujiona kuwa wao ni bora kuliko jamii iliyowazunguka. Pia wale wanaojitahidi kutenda mema na kuwafanyia wengine mema, hutokea kuwa watu hufurahia mwenendo wao na kuanza kuwasifu. Sifa hizi huwapandisha kichwa na kujiona kuwa ni watu muhimu, wakaanza kuwatangazia watu kuwa wao ni muhimu na wakajionyesha katika mwendo wao.

Kundi la Harakati litakapotumbukia katika majivuno na kujifaharisha, lifahamu kuwa limeshashindwa na kazi na badala ya kutarajia kutengenekewa, litarajie kuharibikiwa na kuhiliki. Kundi la Harakati litaepukana na majivuno na kujitkuza endapo kila Mwanaharakati na kundi la Harakati kwa ujumla, litajitahidi kufanya yafuatayo:

kwanza, kuwa na Ikhlas – kufanya kazi ya Da'awah kwa ajili ya Allah (s.w) tu kwa kutarajia kupata Radhi yake na malipo bora ya Akhera.

Pili, kila Mwanaharakati na kundi la Harakati kwa ujumla lijifanyie muhasaba (lijihesabu na kujitathmini). Muislamu mwenye tabia ya kujihesabu kabla ya kuhesabiwa hujigundua udhaifu wake na makosa yake. Mtu mwenye kujiona makosa yake na udhaifu wake mara kwa mara kamwe hawezi kujiona bora na wa maana kuliko wengine. Daima atajiona si lolote wala si chochote mbele ya wengine na mbele ya Allah (s.w) na atajitahidi kutembea kwa unyenyekevu katika ardhi.

Tatu, jambo linalosaidia sana katika kumuepusha Muislamu na majivuno na kujitkuza katika ardhi, ni kujenga tabia ya kuwaangalia watu wema na wacha-Mungu waliomzidi katika kutenda wema. Muislamu atakapojilinganisha na watu watendao

wema na wacha-Mungu, daima atajiona kuwa hajafanya wema wowote wa kumfanya ahisi kuwa bora kuliko wengine. Tumehimizwa katika Qur-an (83:26) tushindane katika mema na tuharakie mambo mema. Wala tusitosheke kwa mema machache tunayoyafanya.

7. Kujiepusha na Ria

Ria ni ugonjwa mwingine unaoweza kumtoa mtu katika Uislamu na kumtumbukiza katika **ushirikina** na **unafiki**. Muislamu anatakiwa afanye kila kitendo chema kwa ajili ya Allah (s.w) kwa matarajio ya kupata malipo kutoka Kwake tu na wala asifanye wema ili kujionyesha kwa watu. Mtu anayefanya wema kuwaonyesha watu, hayuko tayari kufanya wema pale ambapo hapana watu wa kumuona au kumsifu. Muislamu anatakiwa akumbuke daima kuwa yuko pamoja na Allah (s.w) kila wakati, naye ndiye mlipaji kwa kila analolifanya na anayajua hata yale ya siri yaliyoko katika nafsi yake.

Kundi la Harakati halina budi kujiepusha na kujiweka mbali na ria. Halina budi kufanya mambo yake kwa siri kila iwezekanavyo. Ikibidi Mwanaharakati au kundi la Harakati lifanye shughuli zake hadharani, halina budi kujizuia na hisia za kujioa na kujitkuza kwa kutangaza mazuri yake linaloifanyia jamii.

Katika juhudzi za kujiepusha na ria, kila Mwanaharakati ajitahidi kuficha amali zake njema ambazo hazina lazima ya kuonekana. Kila mara Mwanaharakati atathmini hisia zake kuwa anafurahia na kupanda kichwa anaposifiwa na watu wakati inapobidi afanye wema hadharani, au anafurahia zaidi akifanya amali zake bila ya kuonekana na watu? Iwapo Mwanaharakati atagundua kuwa nafsi yake inapendelea kusifiwa na watu, basi ajirudi haraka na kutubia kwa Mola wake. Hali kadhalika, iwapo Mwanaharakati atakuwa hafanyi vizuri shughuli zake njema anapokuwa faraghani kama anavyozifanya akiwa hadharani, ajirudi haraka na kujihesabu kuwa amefanya ria na atubu haraka kwa Mola wake.

Hali kadhalika, kundi la Harakati nalo halina budi kujiепusha na ria kwa kuhakikisha kuwa linayafanya hadharani mambo yale tu ambayo ni lazima kudhihirishwa kwa watu. Shughuli nyine zote za kundi zifanyiwe faraghani. Hata yale ya hadharani, kundi la Harakati lijitatidi kutafuta namna ya kujificha na lijitatidi kutokana na tabia ya kuumuka na kufanya kazi kwa bidii linaposifiwa na lenye kukata tamaa na kuzorota linapolaumiwa na kutukanwa. Kundi la Harakati lililosalimika na ria huwa na Msimamo mmoja nyakati zote likiwa limesifiwa au limeshutumiwa.

8. Kuwa na Subira.

Kama tulivoona kwa Mwanaharakati binafsi, Kundi la Harakati nalo linawajibika kuwa na subira kwa:

- (i) Kutokuwa na haraka katika kutoa maamuzi. Maamuzi yatolewe baada ya kuliangalia jambo kwa kina na kupata ushauri wa kutosha.
- (ii) Kutokuwa na haraka katika kupata mafanikio ya harakati. Ni kazi inayohusu mabadiliko ya jamii ambayo kwa kawaida yake hayapatikani kwa muda mfupi. Nabii Nuhu (a.s) alilingania watu wake kwa muda wa miaka 950, bila kufikia lengo lilokusudiwa la kusimamisha Uislamu katika jamii yake. Nabii Musa aliandaliwa kuwakomboa Bani Israil na udhalimu wa Fir aun tangu akiwa mimbani.
- (iii) Kubakia na msimamo bila ya kuyumbishwa na hila na vitimbwi vyaa maadui.
- (iv) Kuwa tayari kupambana na magumu mbali mbali kwa kurejea aya zifuatazo: (2:214), (3:142), (29:2-3) na (33:23).
- (v) Kuvumilia maudhi ya kila namna kutoka kwa maadui wa Uislamu.
- (vi) Kusubiri juu ya misukosuko ya kawaida itakayolifika kundi na wanakundi.

9. Kuwa na Hekima

Kama ilivyo kwa mwanaharakati binafsi, kundi la Harakati linalazimika kuendesha Harakati kwa hekima, kwa kufanya mambo ya sawasawa yanayolandana na Qur'an na Sunnah, kwa namna ya sawa sawa kwa wakati wa sawa sawa katika mazingira muafaka.

Vile vile ni katika hekima kwa kundi la Harakati kuyafahamu vyema matatizo yanayoikabili jamii ya Waislamu hata isiweze kusimamisha Uislamu, kuchukua njia sahihi ya kuyatatua, kwa kuzingatia wakati na mazingira.

Kundi la Harakati litakapo jita hidi kwa kadiri itakavyowezekana kusifika kwa sifa hizi tisa(9), hapanashaka kwa taufiq ya Allah(s.w), litakuwa lile kundi aliloagiza Allah(s.w) (Qur'an 3:104) lililoweza kulingania kheri, kuamrisha mema na kukataza mabaya katika jamii.

Kuanzisha kundi la harakati kama alivyofanya Mtume(s.a.w)

Tukirejea historia tunaona kuwa Mtume (s.a.w) kabla ya Utume aliandaliwa Ki-il-hamu tangu utotonu na alipambika na tabia njema isiyo na mfano wake katika jamii yake. Alipopewa amri ya kulingania Uislamu alianza na familia yake, kisha kwa marafiki na jamaa zake wa karibu. Wale walioukubali Uislamu katika jamaa na rafiki zake hao nao waliulingania Uislamu kwa familia zao, rafiki na jamaa zao wa karibu. Mtume (s.a.w) alianzisha darasa duara la kuwafunza Uislamu kinadharia na kimatendo wale wote waliosilimu katika nyumba ya Bwana Arkam bin Abi-Arqam. Darasa hili la Mtume (s.a.w) lilizaa kundi madhubuti lililokuwa chachu ya kusimamisha Dola ya Kiislamu iliyo fanya Dini ya Allah (s.w) kuwa juu ya mifumo yote ya maisha katika kipindi cha miaka 23 tu. Hivyo kwa kufuata Minhaji hii ya Mtume (s.a.w), tutaanzisha kundi la Harakati lililo madhubuti kwa kufuata Hatua zifuatazo:

- (i) Mtu binafsi kusoma elimu sahihi juu ya Uislamu kwa kufuata mtaala wa: Maarifa ya Uislamu, Darasa la Watu Wazima, Juzuu 1-7 (IPC).
- (ii) Mtu binafsi kuipipamba na Sifa za Mwanaharakati (kuingiza elimu sahihi katika matendo).
- (iii) Kuiendea familia - mke/mume, watoto, wazazi na wale wote waliochini a malezi ya familia.
- (iv) Kuwafikishia ujumbe wa Uislamu marafiki na jamaa wa karibu na kuwashawishi nao waufikishe ujumbe huo kwa familia zao, rafiki na jamaa zao wa karibu.
- (v) Kuanzisha Darasa Duara litakalo wakusanya na kuwaelimisha juu ya Uislamu kinadharia na kimatendo wale wote uliowalingania na kuupokea ujumbe wa Uislamu. Darasa Duara likiendeshwa na kuongozwa inavyostahiki huwa ndio chimbuko la kundi madhubuti la Harakati. Darasa Duara huanzia ngazi ya familia kisha mtaa hadi kufikia ngazi ya taifa kulingana na ukuaji wakundi la Harakati.

Nini Darasa Duara?

Darasa Duara ni darasa linaloendeshwa kwa mtindo wa semina. Panakuwa na mada inayowasilishwa na mmoja wa wana darasa au kiongozi wa darasa, kisha mada hiyo huchangiwa na kujadiliwa na wanadarasa mpaka ielevweke vyema kwa kila mwana darasa. Baada ya mada kueleweka. Wanadarasa hupitisha maazimio ya utekelezaji wa mada hiyo katika maisha ya kila siku. Kisha kufuatia tathmini ya utekelezaji wa maazimio haya katika darasa linalofuata kabla ya kuanza mada mpya. Hivi ndivyo Mtume (s.a.w) alivyowalea maswahaba zake kama tunavyojifunza kwa Ibn Masoud kuwa, wao (Maswahaba) hawakuwa wanapokea aya kumi mpya alizokwu akiwasomea Mtume (s.a.w) kabla hawajahakikisha zile kumi walizosomewa awali wameziingiza katika matendo ya maisha yao ya kila siku. Mtume (s.a.w) naye alikuwa makini katika kufuatilia utekelezaji wa yale aliyowafunza maswahaba wake.

Kazi za Darasa Duara.

Darasa Duara linakazi kubwa nne zifuatazo:

- (i) Kuwapatia wanadarasa ujuzi sahihi juu ya Uislamu.
- (ii) Kusimamia utekelezaji wa kila kilichosomwa.
- (iii) Kujenga udugu na mshikamano mionganini mwa wanadarasa. Kwa kukutana mara kwa mara, wanadarasa huwa hadhiri juu ya lengo kuu la kusimamisha Uislamu na kupata hisia za udugu na umoja wao. Hivyo kuhurumiana na kushirikiana huwa ni ada yao.
- (iv) Kukuza uchumi. Wanadarasa kwa kujua kuwa nyenzo kuu za kusimamishia Uislamu katika jamii ni mali na nafsi hujiwekea ada ya kutoa sehemu ya kipato chao kwa mwezi au kwa kila mkutano wa darasa kwa ajili ya mfuko wa kuendeleza harakati.

Mtaala wa Darasa Duara

Darasa Duara zenyе lengo la kuandaa vikundi vya harakati vyenye lengo la kusimamisha Uislamu katika jamii, hazina budi kutumia **mtaala mmoja** utakaowezesha vikundi vyote vya harakati katika jamii kuwa na muono na muelekeo mmoja. Inapendekezwa kwa wanaharakati wa Tanzania na nchi zinazotumia lugha ya Kiswahili wafuate mtaala wa “Maarifa ya Uislamu, Darasa la Watu Wazima Juzuu 1-7, ulioandaliwa kwa kufuata mtaala wa Mtume (s.a.w) kwa lengo la kuawezesha Waislamu kusimamisha Uislamu katika jamii na kuuhami usiangushwe baada ya kusimama. Kama alivyofanya Mtume(s.a.w) na maswahaba wake.

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ وَإِلَهُدِي وَدِينِ الْحَقِّ لِنُظْهِرَهُ وَعَلَى الَّذِينَ كُلَّهُمْ
 وَكَفَنَ بِاللَّهِ شَهِيدًا ﴿٢٨﴾ مُحَمَّدٌ رَسُولُ اللَّهِ وَالَّذِينَ مَعَهُ أَشَدَّاءُ عَلَى
 الْكُفَّارِ رُحْمَاءُ بَيْنَهُمْ رُكَّعًا سُجَّدًا يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِنْ اللَّهِ
 وَرِضْوَانًا سِيمَاهُمْ فِي وُجُوهِهِمْ مِنْ أَثْرِ السُّجُودِ ذَلِكَ مَثَلُهُمْ
 فِي التُّورَةِ وَمَثَلُهُمْ فِي الْإِنْجِيلِ كَرَزْعَ أَخْرَاجَ شَطْفَهُ وَفَازَرَهُ
 فَاسْتَغْلَظَ فَلَسْتَوَى عَلَى سُوقِهِ يُعْجِبُ الْرُّرَاعَ لِيَغِيظَ بِهِمُ الْكُفَّارَ
 مُحَمَّدٌ رَسُولُ اللَّهِ وَالَّذِينَ مَعَهُ أَشَدَّاءُ عَلَى الْكُفَّارِ رُحْمَاءُ بَيْنَهُمْ
 تَرَنُهُمْ رُكَّعًا سُجَّدًا يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِنْ اللَّهِ وَرِضْوَانًا سِيمَاهُمْ فِي
 وُجُوهِهِمْ مِنْ أَثْرِ السُّجُودِ ذَلِكَ مَثَلُهُمْ فِي التُّورَةِ وَمَثَلُهُمْ فِي الْإِنْجِيلِ
 كَرَزْعَ أَخْرَاجَ شَطْفَهُ وَفَازَرَهُ فَاسْتَغْلَظَ فَلَسْتَوَى عَلَى سُوقِهِ يُعْجِبُ
 الْرُّرَاعَ لِيَغِيظَ بِهِمُ الْكُفَّارَ وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ عَامَنُوا وَعَوْلَوْا الصَّنِيعَتِ
 مِنْهُمْ مَغْفِرَةً وَأَجْرًا عَظِيمًا ﴿٢٩﴾


“Yeye ndiye aliye mntuma (Aliyemleta) Mtume wake kwa uongofu na Dini iliyo ya haki, ili aishindishe juu ya dini zote. na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi”. “Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na walio pamoja naye ni wenye nyoyo thabiti mbele ya makafiri na wenye kuhurumiana wao kwa wao. utawaona wakiinama kwa kurukuu na kusujudu(pamoja), wakitafuta sadhila za Mwenyezi Mungu na radhi yake. alama zao zi katika nyuso zao kwa taathira (athari)ya kusujudu. Huu ndio mfano wao katika Taurati. na mfano wao katika Injili(umetajwa hivi): kuwa wao ni kama mmea uliota matawi yake; kisha matawi hayo yakautia nguvu, ukawa mnene ukasimama

sawasawa juu ya kigogo chake, ukawafurahisha walioupanda; ili awakasirishe makafiri kwa ajili yao. Mwenyezi Mungu amewaahidi walioamini na kutenda mema katika wao msamaha na ujira mkubwa (48:28-29)

Uongozi wa Darasa Duara

Kwa kuwa Darasa Duara ni darasa la kudumu lenye kutarajiwa kuwaandaa wana darasa kuwa wanaharakati wa kusimamisha Uislamu, halina budi kuwa na uongozi imara utakaoliweka darasa katika nidhamu inayostahiki. Msonge wa uongozi wa darasa utakuwa kama ifuatavyo:

UONGOZI WA DARASA DUARA



Tanbihi: Shura ni mkusanyikao wa Amir, Katibu, Mhazini na Wajumbe watakaoteuliwa na darasa. Kama darasa ni lawatu wachache, Shura itakuwa ni wana darasa wote.

Kazi za Viongozi wa Darasa Duara

Shura: Ndio chombo cha kutoa sera na maamuzi ya mwisho ya darasa:

Amir: Atakuwa na shughuli zifuatazo:

- (i) Kuendesha darasa kama Mwenyekiti.
- (ii) Kuratibu shughuli zote za darasa.
- (iii) Kuchunga nidhamu ya wana darasa.
- (iv) Kung'amua wana darasa wenye nidhamu na ari kubwa ya kusimamisha Uislamu katika jamii.
- (v) Kuwa msimamizi mkuu wa utekelezaji wa yote yaliyoazimiwa katika darasa.

Katibu: Atakuwa na shughuli zifuatazo:

- (i) Kuweka rikodi ya mahudhurio.
- (ii) Kunukuu viini vikuu vya mada na majadiliano na maazimio yaliyofikiwa mwisho wa somo.
- (iii) Kuandika kumbukumbu za vikao vya Shura,
- (iv) Kufanya kazi nyingine za uandishi.
- (v) Kumshauri Amir.

Mhazini: Atafanya kazi zifuatazo:

- (i) Kukusanya Zakat na Sadaka.
- (ii) Kukusanya michango maalumu kama vile $2\frac{1}{2}\%$ ya kipato cha kila mwanadarasa cha mwezi kwa ajili ya Harakati.
- (iii) Kununua vifaa vya darasa vinavyohitajika.
- (iv) Kuweka mahesabu ya mapato na matumizi ya darasa.
- (v) Kutoa ripoti ya mapato na matumizi kwa Amir na Shura kila itakapohitajika.
- (vi) Kufanya kazi nyingine ye yeyote itakayohusiana na mapato na matumizi ya darasa.

Zoezi la Nne

1. (a) Ni lipi kundi la harakati ?
(b) Kwa kurejea Qur'an bainsiha Umuhimu wa kuwepo kundi la Harakati.
2. "*Na wawepo katika nyininyi watu wanaolingania kheri(uiislamu) na wanaomrsisha mema na kukataza maovu na hao ndio watakaotengenekewa*" (3:104)
 - (a) Kwa mujibu wa aya hii inaonesha kuwa si kila muislamu atajiunga na kundi la Harakati. Kwa nini?
 - (b) Ni zipi kazi kuu za kundi la Harakati ?
3. Chambua sifa za kundi la Harakati.
4. Toa hoja tano (5) za msingi kuonesha kwanini makundi mengi yanayojiita ya "harakati" yanamasbaratika baada ya miaka michache tu ya kuundwa kwake.
5. *Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na walio pamoja naye ni wenye nyoyo thabiti mbele ya makafiri na wenye kuhurumiana wao kwa wao. utawaona wakiinama kwa kurukuu na kusujudu(pamoja),wakitafuta fadhila za Mwenyezi Mungu na radhi (yake). Alama zao zi katika nyuso zao kwa taathira (athari) ya kusujudu. huu ndio mfano wao katika Taurati. Na mfano katikia Injili(umetajwa hivi): kuwa (wao) ni kama mmea uliota matawi yake; kisha (matawi hayo) yakautia nguvu, ukawa mnene ukasimama sawasawa juu ya kigogo chake, ukawafurahisha walioupanda; ili Awakasirishie makafiri kwa ajili yao. Mwenyezi Mungu amewaaahidi walioamini na kutenda mema katika wao msamaha na ujira mkubwa.* (48:29)

- (a) Toa sifa za kundi al Harakati aliloliunda Mtume (s.a.w) linalobainishwa katika aya hii.
- (b) Kwa kurejea historia,bainisha mbinu alizozitumia Mtume(s.a.w) katika kuliandaa, kulijenga na kulidumisha kundi hili la Harakati lilopongezwa na Allah(s.w) katika aya hii.
6. Eleza hatua kwa hatua utakayoanzisha kundi la harakati litakalofanana lile alilolitaja Allah(s.w) katika Qur'an (48:29)



Sura ya Tano

MBINU ZA KULINGANIA NA KUSIMAMISHA USIALMU KATIKA JAMII

Dhana ya kulingania Uislamu

“**Da’awah**” ni neno la kiarabu lenye maana ya Wito. “Da’aaa ila llaah” “kuwaita watu kwa Allah”

وَمَنْ أَحْسَنْ قَوْلًا مِّمَّنْ دَعَا إِلَى اللَّهِ وَعَمِلَ صَالِحًا

وَقَالَ إِنِّي مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿٤١﴾

“Na ni nani asemaye kauli bora zaidi kuliko (yule) aitaye kwa Mwenyezi Mungu, na (mwenyewe) akafanya vitendo vizuri na kusema (kwa maneno yake na vitendo vyake) Hakika mimi ni mionganoni mwa Waislamu” (41:33)

Hivyo tunaweza kusema, Da’awah kwa mujibu wa harakati za kusimamisha Uislamu katika jamii, ni kitendo cha kulingania Uislamu kwa watu au kuwaita watu waje kwenye Uislamu. Kulingania Uislamu kwa watu ni kufikisha Uislamu sahihi kwa watu ambao hawajaufahamu ili waufahamu na wahamasike kiasi cha kuwa tayari kuufuata katika maisha yao ya kila siku na hatimaye kuusimamisha katika jamii.

Hivyo “**Da’iyah**” au mlinganiaji atakuwa amefanikiwa katika kazi ya “Da’awah” pale atakapokuwa amewafikishia watu **ujumbe sahihi wa Uislamu** utakaowawezesha kufuata Uislamu vilivyo katika kila kipengele cha maisha yao na kuwapa ari na hamasa ya kuutawalisha katika jamii.

Dhana ya kusimamisha Uislamu katika Jamii

Uislamu utakuwa umesimama katika jamii pale waumini katika jamii hiyo watakapoweza kumuabudu Mola wao katika kila kipengele cha maisha yao ya kibinagsi na ya kijamii. Yaani pale waumini watakapoweza kukiendea kila kipengele cha maisha yao ya kibinagsi na kijamii kwa kufuata barabara mwongozo wa Qur'an na Sunnah. Kwa mujibu wa Qur'an, Uislamu utakuwa umesimama pale waumini watakapoweza kutekeleza amri ya Allah (s.w) ifuatayo:

يَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَدْخُلُوا فِي الْسَّلَمِ كَافَةً وَلَا تَرْكُوا
خُطُواتِ الشَّيْطَانِ إِنَّهُ وَلَكُمْ عَذْوَنٌ مُّبِينٌ
۲۰۸

Enyi mlioamini! Ingieni katika hukumu za Uislamu zote, wala msifuate nyayo za Shetani, kwa hakika yeye kwenu ni adui dhahiri. (2:208)

Jukumu la kulingania na kusimamisha Uislamu katika Jamii ni Amana Kuu

Jukumu la kulingania na kusimamisha Uislamu katika jamii ni jukumu zito kwani ndiyo amana kuu aliyokabidhiwa binaadamu na Mola wake kama tunavyojifunza katika Qur'an:

إِنَّا عَرَضْنَا الْأُمَانَةَ عَلَى الْأَسْمَنَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَالْجِبَالِ فَأَبَيْنَ أَنْ يَحْمِلُنَّهَا
وَأَشْفَقُنَّ مِنْهَا وَحَمَلَهَا إِنْسَنٌ إِنَّهُ وَكَانَ ظَلُومًا جَهُولًا
۷۷

"Kwa yakini sisi tuliidhahirisha amana (amri) yetu kwa mbingu, ardhi na milima, vikakataa kuichukuwa na vikaogopa, lakini mwanaadamu akaichukua. Bila shaka yeye ni dhalimu mkubwa Mjinga sana" (33:72)

Mwanaadamu anakuwa mjinga kutokana na kule kutojitambua kwake kuwa amebeba amana nzito. Anakuwa

dhalimu kwa sababu ametunukiwa vipaji mbalimbali vya akili, utambuzi binafsi (self consciousness) wa hali ya juu, elimu na Uhuru wa kufanya alitakalo pamoja na neema nyingine mbali mbali kama Allah (s.w) anavyoainisha katika aya mbali mbali za Qur'an zikiwemo zifuatazo:

﴿ وَلَقَدْ كَرِمَنَا بَيْتَ إِادَمَ وَحَمَلْنَاهُمْ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ وَرَزَقْنَاهُمْ ﴾

﴿ مِنَ الظِّبَابِتِ وَفَضَلْنَاهُمْ عَلَىٰ كَثِيرٍ مِّمْنُ خَلْقَنَا تَقْضِيَّاً ﴾
٧٦

"Na hakika Tumewatukuza wanaadamu na tukawapa vya kupanda barani na baharini na Tumewaruzuku vitu vizuri vizuri, na Tumewatukuza kuliko wengi katika wale Tuliowaumba, kwa utukufu ulio mkubwa (kabisa)." (17:70)

﴿ لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ فِي أَحْسَنِ تَقْوِيمٍ ﴾
٩٥

"Hakika Tumemuumba mwanaadamu kwa umbo lililo bora kabisa" (95:4)

﴿ هُوَ الَّذِي خَلَقَ لَكُمْ مَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا ثُمَّ آسَتَوْا إِلَى السَّمَاءِ ﴾

﴿ فَسَوَّنُهُنَّ سَبْعَ سَمَوَاتٍ وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴾
٢٩

"Yeye ndiye aliyekuumbieni vyote vilivyomo katika ardhi (kabla hajakuumbeni ili mkute kila kitu tayari), tena akakusudia kuumba mbingu; na akazifanya mbingu saba. Naye ndiye ajuaye kila kitu". (2:29)

Mwanaadamu amekirimiwa na Mola wake vipaji na neema nyingine kuliko viumbwe wengine, ikiwemo mbingu, ardhi na milima (majabali), ili aweze kubeba amana ya kusimamisha Uislamu katika jamii. Mwanaadamu atakapo amua kuvitumia vipaji na neema hizo kwa kufikia malengo mengine kinyume na kusimamisha Ukhilifa wa Allah (s.w) katika ardhi, atakuwa mwizi wa fadhila na atakuwa hamdhulumu yejote ila nafsi yake.

Kusimamisha Ukhalifa wa Allah (s.w) katika ardhi ni jukumu zito na ameliweka hili bayana wakati alipokuwa anamkabidhi Mtume (s.a.w) jukumu hili la kuutawalisha Uislamu juu ya Dini zote (Mifumo yote ya Maisha); pale alipomwambia:

إِنَّا سَنُقِي عَلَيْكَ قَوْلًا شَقِيلًا

“Hakika sisi tutakuteremshia kauli nzito” (73:5)

Hivyo mwanaharakati yejote aliyeazimia kuchukua jukumu hili la kuusimamisha Uislamu katika jamii hanabudi kuwa na ujuzi sahihi juu ya Uislamu na juu ya Mbinu za kuulingania.

Mbinu za Kulingania Uislamu

Mbinu za Msingi za kulingania na kusimamisha Uislamu katika jamii zimeainishwa katika aya ifuatayo:

أَدْعُ إِلَى سَبِيلِ رَبِّكَ بِالْحِكْمَةِ وَالْمُوعِظَةِ الْحَسَنَةِ وَجَدِيلُهُمْ بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ يَعْمَلُ مَنْ ضَلَّ عَنْ سَبِيلِهِ وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ

“Waite (watu) katika njia ya Mola wako kwa hikima na mawaidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola Wako ndiye anayemjua aliyepotea katika njia yake, Naye, ndiye Anayewajua walioongoka”. (16:125)

Kutokana na aya hii tunajifunza Mbinu zifuatazo:

1. Kuwepo Mlinganiaji Mwenye sifa stahiki

Mlinganiaji au mwitaji watu kwa Dini ya Allah (s.w) atakayeweza kuifanya kazi hii kwa ufanisi ni yule atakaye kuwa na sifa zilizoainishwa katika aya ifuatayo:

وَمَنْ أَحْسَنْ قَوْلًا مِّنْ دَعَا إِلَى اللَّهِ وَعَمِلَ صَالِحًا

وَقَالَ إِنِّي مِنَ الْمُسْلِمِينَ

“Na ni nani asemaye kauli bora zaidi kuliko (yule) aitaye (watu) kwa Mwenyezi Mungu, (mwenyewe) akawa anafanya vitendo vizuri na kusema (kwa maneno yake na vitendo vyake) “Hakika mimi ni mionganoni mwa Waislamu”. (41 :33)

Kutokana na aya hii tunajlfunza kuwa mlinganiaji hanabudi kuwa na sifa za msingi zifuatazo:

- (i) Awe na ujuzi sahihi juu ya Uislamu
- (ii) Awe ni mfano wa kuigwa katika kuufuata Uislamu katika kukiendea kila kipengele cha maisha yake ya kibinafsi na ya kijamii kwa kadiri ya uwezo wake. Yaani mlinganiaji awe ni mwenye kujipamba na vipengele vyote vya tabia njema kama vilivyo ainishwa katika Qur'an na Sunnah

Kwa ujumla, ili mlinganiaji aweze kuwaleta watu kwenye Uislamu kiasi cha kuwa tayari kuufuata na kuusimamisha katika jamii, hanabudi kujipamba na Sifa za Mwanaharakati zilizoainishwa katika Qur'an na Hadithi sahihi za Mtume (s.a.w) ambazo ni:

- Ujuzi sahihi juu ya Uislamu.
- Imani thabiti na kuwa na msimamo.
- Tabia njema ya kiutendaji.
- Lengo kuu la maisha liwe ni kusimamisha Uislamu katika jamii.
- Kutarajia malipo kutoka kwa Allah (s.w) tu .
- Kuwa na Hekima.
- Kuwa na Subira. (Rejea Sifa za Mwanaharakati sura ya tatu).

Mlinganiaji wa Uislamu atakapoamua kulingania bila ya kujipamba na sifa stahiki zilizoorodhesha, si tu hatafanikiwa kuwashawishi watu kuwa Waislamu na kuwajengea ari na hamasa

ya kuufuata Uislamu katika maisha yao ya kila siku na hatimaye kuusimamisha katika jamii, bali pia amekamiwa na Mola wake kupata adhabu iumizayo.

يَأَيُّهَا الَّذِينَ ظَمَّنُوا لِمَ تَقُولُونَ مَا لَا تَفْعَلُونَ ﴿٧﴾ كَبُرُّ مَفْعَلًا عَنْدَ اللَّهِ
أَنْ تَقُولُوا مَا لَا تَفْعَلُونَ ﴿٨﴾

“Enyi Mlioamini! Mbona (kwanini) mnasema msiyoyatenda? Ni chukizo kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu kusema msiyoyatenda” . (61 :2-3)

2. Kuwepo Kundu la walinganiaji lenye sifa stahiki

Kazi ya kulingania na kusimamisha Uisiamu katika Jamii, ni jukumu zito, kama tulivyoona katika Qur'an(73:5), hivyo inahitajia kuwa na nguvu za pamoja. Mitume wa Allah (s.w) pamoja na kuandaliwa na kuletewa Wahyi, hawakuweza wenywewe kuilingania na kuusimamisha Uislamu katika jamii, bali walisaidiana na waumini waliowakubali. Tangu mwanzo wa Utume Wake, katika kipindi cha Makka, Mtume (s.a.w) alishirikiana mno na waumini wa mwanzo kuilingania Uislamu kiasi kwamba katika kipindi cha miaka mitatu ya mwanzo (ya kulingania kwa siri), Uislamu ulifika katika kila kaya ya kabila la Quraish. Pia Mtume (s.a.w) kwa kushirikiana na Waumini ulinganizi wa Uislamu ultanuka kwa kasi kikubwa sana baada ya Mkataba wa Hudaybiya pale Mtume (s.a.w) alipowakusanya waumini na kuwahutubia kama ifuatavyo:

“Enyi Watu! Allah amenitura kuwa Rehema kwa Wanaadamu na kuwa Mtume wa Ulimwengu mzima. Kwa hiyo linganieni Uislamu kwa niaba yangu na Allah atakurehemuni. Kwa hiyo nakuusieni msifarikiane kama (watu wa) Isa mwana wa Maryamu”.

Katika khutuba hii tunaona Mtume (s.a.w) akiwausia waumini kuwa na mshikamano, na kuwatahadharisha juu ya mifarakano. Walinganiaji watakafarakana, kila mlinganiaji atawaita watu waje kwenye Uislamu wa mrengo wake. Matokeo ya faraka za walinganiaji ni Uislamu kugawanyika katika madhehebu mbali mbali, jambo ambalo halipo na halikubaliki katika Uislamu. Allah (s.w) anatukumbusha katika Qur'an:

﴿مُنِيبِينَ إِلَيْهِ وَأَتَقْوَهُ وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَلَا تَكُونُوا مِنَ الْمُشْرِكِينَ
٢٣﴾
منَ الَّذِينَ فَرَّقُوا دِينَهُمْ وَكَانُوا شَيْعَاتٍ كُلُّ جُزْءٍ بِمَا لَدَيْهِمْ فَرِحُونَ

“Nyenyekeeni Kwake na Mcheni, na simamisheni Sala, wala msiwe katika washirikina. “Katika wale walioitenga dini yao na wakawa makundi makundi; kila kikundi kinafurahia kilicho nacho”. (30:31-32)

Waislamu ni **Umma mmoja** na dini yao ni **Moja** iliyo asisiwa chini ya misingi ya Qur'an na Sunnah. Ili kulingania Uislamu **Mmoja** utakaopelekea kupatikana kwa **Umma mmoja** wenye nguvu ya kusimamisha Uislamu katika jamii walinganiaji hawanabudi kufuata **Mtaala mmoja** unaotokana na Qur'an na Sunnah. Maswahaba wa Mtume (s.a.w) walioandalowiwa kwa **Mtaala** huu walishikamana na kuwa Umma Mmoja wenye nguvu kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

مُحَمَّدٌ رَسُولُ اللَّهِ وَالَّذِينَ مَعْهُ وَأَشْدَاءُ عَلَى الْكُفَّارِ رُحْمَاءُ بَيْنَهُمْ
 تَرَاهُمْ رُكَّعًا سُجَّدًا يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِنْ اللَّهِ وَرِضْوَانًا سِيمَاهُمْ فِي
 وُجُوهِهِمْ مِنْ أَثْرِ السُّجُودِ ذَلِكَ مَثَلُهُمْ فِي الْتَّوْرَةِ وَمَثَلُهُمْ فِي الْإِنْجِيلِ
 كَزَرَاعٍ أَخْرَاجَ شَطْعَهُ فَقَارَرَهُ فَاسْتَغْلَظَ فَاسْتَوَى عَلَى سُوقِهِ يُعْجِبُ
 الْرُّرَاعَ لِيَغِيظَ بِهِمُ الْكُفَّارُ وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ ظَمِنُوا وَعَمِلُوا الْصَّلِحَاتِ
٢٩ مِنْهُمْ مَعْفِرَةٌ وَأَجْرًا عَظِيمًا

Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na walio pamoja naye ni wenyenyo thabiti mbele ya makafiri na wenyenye kuhurumiana wao kwa wao. Utaona wakiinama kwa kurukuu na kusujudu (pamoja), wakitafuta fadhila za Mwenyezi Mungu na radhi (yake). Alama zao zi katika nyuso zao, kwa taathira (athari) ya kusujudu. Huu ndio mfano wao katika Taurati. Na mfano wao katika Injili (umetajwa hivi): Kuwa (wao) ni kama mmea uliota matawi yake; kisha (matawi hayo) yakautia nguvu; ukawa mnene ukasimama sawasawa juu ya kigogo chake, ukawafurahisha waliupanda; ili awakasirisha makafiri kwa ajili yao. Mwenyezi Mungu amewaaahidi walioamini na kutenda mema katika wao msamaha na ujira mkubwa.” (48:29).

Hivyo, kwa kuwa lengo la kulingania Uislamu ni kupata umma mmoja wenyenye nguvu ya kuamrisha mema na kukataza maovu na hatimaye kusimamisha Uislamu katika jamii, suala la kulingania lazima lifanywe ki umma kama Allah (s.w) anavyohimiza:

وَلْتَكُنْ مِنْكُمْ أُمَّةٌ يَدْعُونَ إِلَى الْخَيْرِ وَيَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَاونَ عَنِ
١٤ الْمُنْكَرِ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ

“Na wawepo katika nyinyi umma(kundi la watu)wanaolingania kheri (Uislamu) na wanaao amrisha mema na wanaokataza maouvu. Na hao ndio watakaotengenekewa” (3:104)

Vikundi vya harakati vilivyooundwa kwa kutekeleza agizo hili la Allah (s.w) havinabudi kujipamba na sifa zilizo ainishwa katika Qur'an na Sunnah.

Miongoni mwa sifa za msingi zilizoainishwa ni hizi zifuatazo:

- Kila mwanakundi binafsi awe amejipamba na sifa za Mwanaharakati.
- Wanakundi wawe na mshikamano wa udugu na upendo.
- Wawe ni wenye kushauriana.
- Pawe na nidhamu.
- Kujikosoa na kujitathmini.
- Kujiepusha na ria.
- Kujiepusha na majivuno na kujiona.
- Kuwa na Hekima.
- Kuwa na Subira .

(Rejea Sura ta Nne ya juzuuhii)

Vikundi vya kulingania Uislamu vyenye kujipamba na sifa hizi za msingi, hatakama vitakuwa katika mazingira yaliyotofautiana kijiografia au kisiasa, vitakuwa vinalingania Uislamu mmoja ule ule alioulingania Mtume (s.a.w) na maswahaba zake, na hatima ya ulinganizi huu ni kupata Umma mmoja wenye nguvu kwa ulimwengu mzima.

3. Wawepo Wenye Kulinganiwa

.....اذْهُنِي سَبِيلِ رَبِّكَ

“Waite katika njia ya Mola Wako “ (16:125)

Kwa mujibu wa aya hii, ni akina nani wanaotakiwa waitwe kwa Allah (s.w)? Kwa uoni wetu wanaotakiwa waitwe kwa Allah (s.w) ni watu wa aina tatu:

- (i) Watu ambaao hawajafikiwa kabisa na ujumbe wa Uislamu
- (ii) Watu walioingia katika Uislamu kwa kuzaliwa au kufuata mkumbo kwa ajili ya kupata maslahi fulani kama vile kuoa au kuolewa bila ya kujuu chochote juu ya Uislamu wao.
- (iii) Waislamu wanaoujua na kuufuata Uislamu wa mapokeo (uliofundishwa kinyume na Qur'an na Sunnah) usio wawezesha kusimamisha Ukhaliifa katika ardhi na kumuabudu Allah (s.w) ipasavyo katika kila kipengele cha maisha ya kibinagsi na kijamii.

Mlinganiaji, kama tulivoona katika utangulizi, lengo lake haliishii tu kwenye kuufikisha Uislamu sahihi kwa watu, bali atakuwa amefikia lengo la ulinganiaji pale atakapo wawezesha wale anaowalingania kuufahamu Uislamu kwa usahihi wake kiasi cha kupata ari na hamasa ya kuutekeleza katika kila kipengele cha maisha binagsi na kufanya jitihada za makusudi za kuusimamisha katika jamii. Hivyo walinganiaji mahiri, hawanabudi kuigawanya jamii ya watu wanayoilingania katika makundi haya matatu na kutoa “dose” stahiki kwa kila kundi. Kihalisia katika midani ya kulingania, kundi la kwanza ni jepesi kulingania likifuatiwa na la pili. Kundi la tatu ambalo linaongozwa na ‘masheikh’ na ‘wanazuoni’ waliokhiyari kutumia elimu ya mwongozo (ya Qur'an na Sunnah) waliyonayo kwa maslahi machache ya maisha ya kidunia, ni katika kundi gumu katika kulilingania. Kuhusu

‘masheikh’ na ‘wanazuoni’ wa Kiislamu wenye mrengo huu wa kutaka watu wawatukuze na kuwafuata kwa ajili ya maslahi yao binafsi, Allah (s.w) anatutahadharisha tuwaepuke katika aya zifuatazo:

وَأَقْلِلْ عَلَيْهِمْ تَبَأَ الَّذِي عَانِيَتَنَا فَإِنْسَلَخَ مِنْهَا فَاتَّبَعَهُ الشَّيْطَانُ
 فَكَانَ مِنَ الْغَالِوِينَ ﴿١٧٦﴾ وَلَوْ شِئْنَا لَرَفَعْنَاهُ بِهَا وَلَكِنَّهُ وَأَخْلَدَ إِلَى
 الْأَرْضِ وَأَثْبَعَ هَوْنَهُ فَمَثَلُهُ كَمَثَلِ الْكَلْبِ إِنْ تَحْمِلُ عَلَيْهِ يَأْلَهُتْ أَوْ
 تَشْرُكُهُ يَأْلَهُتْ ذَلِكَ مَثَلُ الْقَوْمِ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِعَائِدَتَنَا فَلَاقُصُصِ
 الْقَصَصَ لَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ ﴿١٧٧﴾ سَاءَ مَثَلًا الْقَوْمُ الَّذِينَ كَذَّبُوا
 بِعَائِدَتَنَا وَأَنفَسَهُمْ كَانُوا يَظْلِمُونَ ﴿١٧٨﴾ مَنْ يَهْدِ اللَّهُ فَهُوَ الْمُهَدِّدِ
 وَمَنْ يُضْلِلْ فَأُولَئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿١٧٩﴾

“Na wasomee habari za wale tuliowapa aya zetu (kuzijua), kisha wakajivua nazo (wasizifuate). Na shetani akawaandama, wakawa mionganoni mwa waliopotea”.

“Na kama tungelitaka tungeliwanyanya kwazo, lakini wao waligandamana na ardhi (kutaka ukubwa wa Kidunia wakayatupa ya Akhera) na wakayaafuata matamanio yao. Basi hali yao ni kama hali ya mbwa; ukimpigia kelele (hukimbia na huku) anahema, na ukimwacha pia huhema. Hiyo ndiyo hali ya watu waliozikadhibisha Aya zetu. Basi simulia hadithi, huenda wakatafakari”. Uovu ulioje wa mfano wa wanaozikadhibisha Aya zetu na wakajidhulumu nafsi zao (wenyewe Wanapigiwa mfano na mbwa!) Atakaowaongoza Mwenyezi Mungu ndio watakaoongoka; na atakaowaachia kupotea (kwa kuwa hawafuati anavyoamrisha, hao) ndio watakaopata khasara. “(7:175-178)

أَتَخَذُوا أَحْبَارَهُمْ وَرُهْبَنَهُمْ أَرْبَابًا مِّنْ دُونِ اللَّهِ وَالْمَسِيحَ أَبْنَ مَرْيَمَ
وَمَا أُمِرْتُ إِلَّا لِيَعْبُدُوا إِلَهًا وَاحِدًا لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ سُبْحَانَهُ عَمَّا يُشَرِّكُونَ

“Wamewafanya wanavyuoni wao na watawa wao kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu, na (wamemfanya) Masihi mwana wa Maryamu (pia Mungu), hali hawakuamrishwa isipokuwa kumuabudu Mungu mmoja, hakuna anayestahiki kuabudiwa ila Yeye. Ametakasika na yale wanayomshirikisha nayo. “(9:31)

﴿يَتَأَيَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّ كَثِيرًا مِّنَ الْأَحْبَارِ وَالرُّهْبَانِ لَيُكُلُّونَ أَمْوَالَ

النَّاسِ بِالْبَطْلِ وَيَصْدُونَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ﴾

“Enyi mliaoamini Wengi katika makasisi (wanavyuoni wa Mayahudi na Manasara) na watawa (wao) wanakula mali za watu kwa batili na kuwazuilia njia ya Mwenyezi Mungu
“(9:34)

مَثَلُ الَّذِينَ حُمِلُوا التَّوْرَةَ ثُمَّ لَمْ يَحْمِلُوهَا كَمَثَلُ الْجَمَارِ يَحْمِلُ
أَسْفَارًا بِئْسَ مَثَلُ الْقَوْمِ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِعَلَيْتِ اللَّهَ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ

الظَّالِمِينَ ﴿٦﴾

“Mfano wa wale waliopewa Taurati, kisha hawakuichukua (kwa kuitumia) ni kama punda anayebeba vitabu vikubwa (bila kupata nafuu kwavyo). Ni mbaya kabisa mfano wa watu waliozikadhibisha Aya za Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhalimu”. (62:5)

Aya hizi, kwa ujumla zinatutaka tuwe macho na **wanazuoni** au **masheikh** wanaotaka kusimamisha himaya zao badala ya kusimamisha Uislamu katika jamii. Mara nyingi masheikh na wanazuoni wa aina hii ambao wanafananishwa na Mbwa na Punda,

wanashirikiana na utawala wa Kitwaghut katika kuzima harakati za kulingania na kusimamisha Uislamu katika jamii.

4. Kulingania kwa Hekima

Hekima ni kipengele cha tabia njema chenye maana pana. Hekima kwa ujumla ni kufanya jambo la sawa sawa kwa namna ya sawa sawa kwa wakati wa sawa sawa na katika mazingira ya sawa sawa katika kuendea lengo husika. Kwa mnasaba wa kulingania Uislamu kwa lengo la kuusimamisha katika jamii hekima itakuwa imetumika pale:

- (1) Uislamu utakapolinganiwa kwa usahihi wake kwa kutumia mtaala wa Qur'an na Sunnah.
- (2) Kisha ukafundishwa kwa kutumia mbinu stahiki zinazolandana na mwongozo wa Qur'an na Sunnah.
- (3) Kisha ukafundishwa kwa kuzingatia wakati uliopo, wakati wa sayansi na teknolojia, wakati wa utandawazi, n.k.
- (4) Na kisha ukazingatia mazingira yaliyopo, ikiwa ni pamoja na kujua historia ya Uislamu wa watu wa eneo husika; maadui wa Uislamu na mbinu zao dhidi ya Uisiamu, mila na desturi za watu unao walingania, umri wao, kiwango chao cha elimu ya mazingira na elimu ya mwongozo n.k.

Ni vema kusisitiza kuwa hekima si woga au kuchelea matatizo au kuepa majukumu. Mara nyingi wanafiki wamesingizia kutumia hekima, kumbe wanaogopa au wanachelea kukabili ana na magumu au wanaepa majukumu yanayo wakabili katika mchakato wa kusimamisha Uislamu katika jamii. Ni kweli kwamba kazi ya kulingania na kusimamisha Uislamu katika jamii si jambo jepesi, bali ni jambo linalohitaji ujasiri, kujitoa muhanga na subira kama Allah (s.w) anavyotukumbusha mara kwa mara katika Qur'an (rejea 2:214; 3:142; 9:16; 47:31)

5. Kulingania kwa Mawaiidha mazuri

Kwa mnasaba wa kulingania Uislamu kwa lengo la kuusimamisha katika jamii, mawaiidha mazuri ni yale yaliyobeba sifa zifuatazo:

- (i) Yanayotokana na ujumbe halisi wa Qur'an na Sunnah. Yasiwe yale yanayotokana na simulizi za watu. Yaani usiwe ni ujumbe wa mapokeo. Kwa maana nyine yasitoke kwa sheikh au mwanazuoni fulani bali yashehenezwe na ushahidi wa Qur'an na Hadith sahihi za Mtume (s.a.w) na hasa ukizingatia kuwa wahyi kwa njia ya Jibril umekomea kwa Mtume (s.a.w). Kwahiyo kila muumini wa kweli ana fursa ya kutumia vipawa alivyopewa katika kuipambanua Qur'an na Hadith ili aweze kuitekeleza viliyvo.
- (ii) Yale yanayowezesha kuitambua nafasi au hadhi ya Muislamu katika jamii na kulitambua fika lengo la kuumbwa binaadamu.
- (iii) Yanayo mjenga Muislamu na kumpa ari na hamasa ya kuufuata Uislamu katika kukiendea kila kipengele cha maisha yake ya kibinafsi na kumpa ari na hamasa ya kufanya jitihada za makusudi za kusimamisha Uislamu katika jamii.
- (iv) Yanayomuwezesha mtu kuwa na mtazamo sahihi wa Uislamu juu ya dhana mbali mbali za maisha ya kibinafsi na kijamii. Yaani mawaiidha mazuri ni yale yanaonesha mtazamo sahihi kwa mujibu wa Qur'an na Hadith sahihi, juu ya elimu, dini, imani, uchumi,siasa, utamaduni n.k.
- (v) Yaliyoepukana na laghawi. Yaani mawaiidha mazuri ni yale yaliyoepukana na porojo au hadithi za "paukwa pakawa", ambazo huwafanya watu waishie kwenye kuangua vicheko bila ya kuondoka na ujumbe wowote utakao pelekea kuongeza ufanisi katika kuufuata Uislamu kibinafsi na kijamii.

(vi) Yaliyotolewa kwa kutumia lugha ya msikilizaji. Ni katika uzembe na ukosefu wa hekima kuwafikishia watu ujumbe kwa lugha wasiyoifahamu. Kwa mfano, ni uzembe wa hali ya juu kutumia lugha ya kiarabu kuwafikishia ujumbe watu wasiojuwa kiarabu. Ulinganiaji wa namna hiyo ni kama kutwanga maji kwenye kinu. Ni katika Sunnah ya Allah (s.w) kuwafikishia watu ujumbe wa Uislamu kwa lugha zao kupitia kwa Mtume anayetokana na wao kama tunavyojifunza katika Qur'an:

وَمَا آرْسَلْنَا مِنْ رَسُولٍ إِلَّا بِلِسَانٍ قَوْمَهُ لِيُبَيِّنَ لَهُمْ فَيُضَلُّ اللَّهُ مَنْ يَشَاءُ
وَيَهْدِي مَنْ يَشَاءُ وَهُوَ أَعْزِيزُ الْحَكِيمُ



'Hatukumpeleka Mtume yejote isipokuwa kwa lugha ya watu wake ili apate kuwabainishia (vizuri). Kisha Mwenyezi Mungu anamuacha kupotea amtakaye (kwa kuwa mwenyewe hataki kuongoka) na kumuongoza amtakaye (kwa kuwa mwenyewe yuko tayari kuiendea njia ya uongofu).

Naye ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima." (14:4)

Kwa mnasaba wa aya hii ilibidi Mtume (s.a.w) ashushiwe Qur'an kwa lugha ya Kiarabu cha Kiquraish ili apate kuwabainishia jamaa zake wa karibu (Maquraish) ambao walipaswa kusaidiana naye kuufikisha ujumbe huo kwa walimwengu wote. Mtume (s.a.w) angeshushiwa Qur'an kwa lugha isiyo ya kiarabu, ingelikuwa ni sababu tosha ya jamaa zake kumkataa kama Allah (s.w) anavyotubainishia:

وَلَوْ جَعَلْنَاهُ فِرْعَانًا أَعْجَمَيَا لَقَالُوا لَوْلَا فُصِّلَتْ عَائِدَةٌ هُنَّ عَاجِمُونَ وَعَرَبُونَ
فُلُّ هُوَ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا هُدًى وَشَفَاءٌ وَالَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ فِي ءَادَانِهِمْ وَقُرْ
وَهُوَ عَلَيْهِمْ عَمَّى أُولَئِكَ يُتَادُونَ مِنْ مَكَانٍ بَعِيدٍ



Na lau kama tungalifanya Qur'an kwa lugha isiyo ya Kiarabu wangalisema: "Kwa nini Aya zake hazikupambanuliwa? Lo! Lugha isiyokuwa ya Kiarabu na (Mtume) Muarabu! (Mambo gani haya)!" Sema: "Hii (Qur'an) ni uwongofu na poza kwa wale walioamini; na wale wasioamini umo uzito katika masikio yao; na hiyo (Qur'an) ni giza kwao. (Hawasikii. Kama kwamba) hao wanaitwa, na hali ya kuwa wako mbali kabisa. "(41:44)

Kwa mnasaba wa ujumbe wa aya hii, nasi watu watatushangaa kuwafikishia ujumbe wa Uislamu kwa lugha wasiyoifahamu. Mtume (s.a.w) mwenyewe aliwahimiza maswahaba zake alipowatuma kutoa Da'awah kwa watu mbali mbali wasiokuwa waarabu kuwa wajifunze lugha zao na wawafikishie ujumbe wa Uislamu kwa lugha zao. Hivyo watu kutokuwa waarabu au kutojua kiarabu isiwe sababu ya kuwafanya wasifikasiwe na ujumbe sahihi wa Uislamu.

6. Kujadiliana na watu kwa namna iliyo bora

Mlinganiaji anatakiwa atumie lugha ya upendo na mvuto itakayoweza kuvuta nyoyo na usikivu wa watu anaowingania. Asiwalazimishie watu ujumbe bali awavutie kwa kutoa hoja zenye mashiko madhubuti kama Allah (s.w) anavyo tuelekeza:

لَا إِكْرَاهٌ فِي الدِّينِ قَدْ تَبَيَّنَ الرُّشْدُ مِنَ الْغَيِّ فَمَن يَكُفُّرُ بِالظَّغْفُوتِ
وَيُؤْمِنُ بِاللَّهِ فَقَدِ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَى لَا أَنْفِصَامَ لَهَا وَاللَّهُ سَمِيعٌ



"Hakuna kulazimishwa (mtu kuingia) katika dini. Uongofu umekwisha pambanuka na upotofu. Basi anayemkataa twaaghieu na akamwamini Mwenyezi Mungu, bila shaka yeye ameshika kishiko chenye nguvu kisichovunjika. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua. "(2:256)

Kwa mujibu wa aya hii, mlinganiaji anawajibika kuubainisha ujumbe wa Uislamu kwa kudhihirisha uongofu na upotofu kwa hoja madhubuti zinazoingia akilini kwa mlinganiwaji.

Katika kujadiliana mlinganiaji, ajiepushe na jazba na mabishano. Tunafundishwa katika Qur'an kuwa tukizungumza na watu ambao hawataki kuelewa bali wanataka kubishana tu, tusiendelee kujadiliana nao bali tuagane nao kwa amani.

وَعَبَادُ الرَّحْمَنِ الَّذِينَ يَمْشُونَ عَلَى الْأَرْضِ هُوَنَا وَإِذَا حَاطَبُهُمْ

الْجَنِيلُونَ قَالُوا سَلَامًا ﴿٢٣﴾

'Na waja (wema) wa Rahman ni wale wanaotembea katika ardhii kwa unyenyekevu na wajinga wakisema nao, huwajibu, 'Salama' (25:63)

7. Kutowakatia tamaa unaowalingania

Mlinganiaji anatakiwa awe na subira na amfanye Nabii Nuhu (a.s) kiigizo chake. Nabii Nuhu (a.s) kwa kutumia mbinu mbali mbali alilingania watu wake, bila ya kuwakatia tamaa kwa muda wa miaka elfu moja kasoro hamsini (950).

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا نُوحًا إِلَى قَوْمِهِ فَلَبِثَ فِيهِمْ أَلْفَ سَنَةٍ إِلَّا خَمْسِينَ

عَامًا فَأَخَذْنَاهُمُ الظُّوقَانَ وَهُمْ ظَالِمُونَ ﴿١٤﴾

'Na bila shaka tulintuma Nuhu kwa watu wake na akakaa nao miaka elfu kasoro hamsini (wasikubali kufuata) basi tufani liliwafikia (wakaghariki) na hali walikuwa madhalimu". (29:14)

Kinyume chake tusiwakatie watu tamaa kama alivyofanya Nabii Yunus (a.s) aliyeamua kuwakimbia watu wake baada ya kuona wamekataa kumfuata. Kwa kosa hili alipata mkasa wa kumezwa na samaki na akarejea kwa Mola wake kwa kuleta toba ya kweli baada ya kutambua kosa lake kama tunavyo jifunza katika Qur'an:

وَذَا الْتُّونِ إِذْ ذَهَبَ مُغْلِظِبًا فَظَرَّ أَنْ لَنْ تَقْدِرَ عَلَيْهِ فَتَادَى فِي الظُّلْمِ
 أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ سُبْحَانَكَ إِنَّكَ كُنْتَ مِنَ الظَّالِمِينَ ﴿٦﴾ فَاسْتَجَبْنَا
 لَهُ وَنَجَّيْنَاهُ مِنَ الْقُمْرِ وَكَذَلِكَ شَجَرَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٧﴾

“Na (Mtaje) Dhun-Nun (Yunus) alipoondoka hali amechukiwa, na akadhani ya kwamba hatutamdhikisha. Basi (alipozongwa) aliita katika giza (akasema): “Hakuna ababudiwaye isipokuwa wewe, Mtakatifu; hakika mimi nilikuwa mionganoni mwa wenyewe kudhulumu (nafsi zao)”. Basi Tukampokelea na Tukamuokoa katika huzuni iLe, Na namna hiyo ndivyo Tuwaokoavyo walioamini”. (21:87-88)

Jukumu la mlinganiaji ni kufikisha ujumbe wa Uislamu kwa hekima, kwa mawaidha mazuri na kwa kujadiliana kwa namna iliyo bora na jukumu la kumuongoza mlinganiwaji au kumuachia kupotea liko kwa Allah (s.w) kamaaya inavyosisitiza:

إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ بِمَنْ ضَلَّ عَنْ سَبِيلِهِ وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ ﴿١٥﴾.....

“... Hakika Mola wako ndiye anayemjua aliye potea katika njia yake, Naye ndiye anayewajua walioongoka” (16:125)

8. Kuwafahamu maadui wa Uislamu na mbinu zao

Pamoja na kuzijua hizi mbinu saba (7) za kulingania Uislamu ni muhimu pia kuwajua fika maadui wa Uislamu na mbinu zao. Kumjua adui yako vilivyo ni nusu ya ushindi. Maadui wa Uislamu walioainishwa katika Qur'an ni

- Makafiri na Washirikina
- Mayahudi na Wakristo
- Wanafiki
- Shaitwaani.

● Makafiri na Washirikina.

Tunajifunza katika Qur-an kuwa makafiri na Washirikina daima wako mbioni katika kutaka kuizima nuru ya Allah (s.w) na wanachukia mno kuuona Uislamu unasimama kama zinavyobainishaaya zifuatazo:

يُرِيدُونَ لِيُطْفَأُوا نُورَ اللَّهِ بِأَفْوَاهِهِمْ وَاللَّهُ مُتِمٌ ثُورِهِ
وَلَوْ كَرِهَ الْكَافِرُونَ

Wanataka kuizima nuru ya Mwenyezi Mungu kwa vinywa vyao, na Mwenyezi Mungu atakamilisha nuru yake, ijapokuwa makafiri watachukia. (61:8)

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ وَبِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُنَظِّهِرَهُ عَلَى الْدِينِ كُلِّهِ
وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ

Yeye ndiye aliyemtuma Mtume wake kwa Uongofu na kwa dini ya haki ili kuifanya ishinde dini zote japo washirikina watachukia. (61:9)

Kwa nini Makafiri na Washirikina wanachukia kuuona Uislamu unasimama katika jamii? Sababu Uislamu unaamrisha mema na kukataza maovu katika jamii na unasimamisha haki. Makafiri na washirikina kwa kufuata matashi ya nafsi zao, huzuua mema na huamrisha maovu na wameunda mifumo ya maisha ambayo humfanya kila mwenye uwezo mkubwa wa kiafya, kielimu, kiuchumi, kimadaraka; amdhulumu mwenye uwezo mdogo. Ni kwa msingi huu, tunafahamishwa katika Qur-an kuwa katika historia yote ya mwanaadamu, walioongoza katika kuupiga vita Uislamu ni viongozi wa jamii za kikafiri na kishirikina.

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَا فِي كُلِّ قَرْيَةٍ أَكْبَرَ مُجْرِمِيهَا لِيَمُكْرُرُوا فِيهَا وَمَا
يَمْكُرُونَ إِلَّا بِأَنفُسِهِمْ وَمَا يَشْعُرُونَ

Na kadhalika tulijaalia kila mji wakuu wao ndio waovu. Ikawa humo wanafanya hila (na vitimbi nya kuzuilia watu na dini ya Mwenyezi Mungu) wala hawafanyi hila isipokuwa nafsi zao lakini hawatambui. (6:123)

Wakuu hawa waliochukua nafasi ya Allah (s.w) ya kuwatungia watu wa jamii zao sheria na mwongozo wa maisha, walijiweka juu ya jamii zao na kujihalalishia kuidhulamu jamii. Hofu kubwa ya wakuu hawa wa jamii za kikafiri na kishirikina ni kwamba, wakiuachia Uislamu ukisimama katika jamii, watakosa maslahi yao, kwani haki itasimama na hawatampata tena wa kumkandamiza wala kumnyonya. Hivyo hamu yao kubwa ni kuuzuia Uislamu usisimame katika jamii zao ili wawe na uhakika wa kuendeleza dhuluma bila ya kipingamizi. Allah (s.w) anatuhadharisha juu ya hila zao katika aya ifuatayo:

وَلَا يَرَأُونَ يُقْتَلُونَ كُمْ حَتَّىٰ يَرُدُّو كُمْ
 عَنِ الدِّينِ كُمْ إِنْ أَسْتَطَعُوْ وَمَنْ يَرْتَدِدْ مِنْكُمْ عَنِ الدِّينِ
 فَيُمْتَأْنِي وَهُوَ كَافِرٌ فَأُولَئِكَ حَبِطْتُ أَعْمَالُهُمْ فِي الدُّنْيَا
 وَالآخِرَةِ وَأُولَئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَلِيلُونَ



“..... Wala hawataacha kupigana nanyi mpaka wakutoeni katika dini yenu kama wakiweza. Na watakaotoka katika dini yao katika nyinyi, kisha wakafa makafiri, basi hao ndio ambao amali zao zimeharibika katika dunia na akhera. Nao ndio watu wa Motoni, humo watacaa milele. (2:217)

Hivyo Waislamu wanatakiwa watambue wazi kuwa makafiri na washirikina ni maadui zao na kamwe wasiwafanye wapenzi wao na marafiki zao kama Allah (s.w) anavyotutahadharisha:

لَا يَتَّخِذُ الْمُؤْمِنُونَ الْكَافِرِينَ أَوْ لِيَاءً مِنْ دُونِ الْمُؤْمِنِينَ وَمَنْ يَفْعَلُ ذَلِكَ فَلَيْسَ مِنَ اللَّهِ فِي شَيْءٍ إِلَّا أَن تَتَقَوَّلُ مِنْهُمْ تُقْنَةٌ وَيُحَدِّرُ كُمُّ اللَّهُ نَفْسَهُ وَإِلَى اللَّهِ الْمُصِيرُ

Walioamini wasiwafanye makafiri kuwa wapenzi wao badala ya Waislamu wenziwao. Na atakayefanya hivyo, basi hatakuwa na chochote mbele ya Allah. Ila (ikiwa mnafanya nao urafiki wa juu juu, tu hivi) kwa ajili ya kujilinda na shari zao. Na Mwenyezi Mungu anakuhadharisheni na adhabu yake. Na marejeo ni kwa Allah (s.w). (3:28)

يَتَأْيَهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَوَلَّوْا قَوْمًا غَضِيبَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ قَدْ بِإِسْوَانِ الْآخِرَةِ كَمَا يَبِسُ الْكُفَّارُ مِنْ أَصْحَابِ الْقُبُوْرِ

Enyi mlionamini msifanye urafiki wa ndani na watu ambao Mwenyezi Mungu amewakasirikia na wamekata tamaa na akhera kama walivyokwisha kata tamaa makafiri waliomo makaburini. (60:13).

Pia Waislamu wanatahadharishwa na Mola wao kuwa wasiwatii wale wote wanaoongoza kinyume na uwongozi wa Allah (s.w):

وَلَا تُطِعْ الْكَافِرِينَ وَالْمُنْتَفِقِينَ وَدُعْ أَذْنَهُمْ وَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ وَكَفَى بِاللَّهِ وَكِيلًا

Na usiwatii makafiri na wanafiki wala usijali udhia wao, na mtegemee Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa mlinzi. (33:48)

وَإِن تُطِعْ أَكْثَرَ مَنْ فِي الْأَرْضِ يُضْلُلُوكَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ إِن يَتَّبِعُونَ إِلَّا الظُّنُنَ وَإِنْ هُمْ إِلَّا يَخْرُصُونَ

Na kama ukiwatii wengi katika waliomo ulimwenguni watakupoteza na njia ya Mwenyezi Mungu. Hawafuati ila dhana tu, na hawakuwa ila ni wenye kuzua tu. (6:116)

اللَّهُ وَلِيُّ الَّذِينَ ءامَنُوا يُخْرِجُهُم مِّنَ الظُّلْمَاءِ إِلَى النُّورِ
وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَوْلِيَأُهُمُ الظَّاغِنُونَ يُخْرِجُونَهُم مِّنَ النُّورِ إِلَى
الظُّلْمَاءِ إِلَّا كَمَا أَصْحَبُ اللَّارِطُهُمْ فِيهَا خَلِيلُونَ



Mwenyezi Mungu ni Mlinzi wa wale walioamini. Huwatoa katika giza na huwaingiza katika nuru. Lakini waliokufuru walinzi wao ni matwaghuti (wachupaji mipaka ya Allah). Huwatoa katika nuru na huwaingiza katika giza. Hao ndio watu wa motoni, humo watadumu. (2:257)

Mbinu za Makafiri na Washirikina

Mbinu wanazozitumia makafiri katika kuuhujumu Uislamu na Waislamu ni nyingi mno. Mbinu zao ni pamoja na kueneza propaganda za uongo dhidi ya Uislamu, kuwapakazia Waislamu na Uislamu kuwa ni dini ya kikatili, dini ya Ugaidi, dini ya watu wasioendelea, n.k. Huweka programu mbali mbali za kijamii zinazofisidi Uislamu na utamaduni wake. Kama mfano tu, Bwana Cleon aliyewahi kuwa Mkurugenzi wa idara ya usalama (C.I.A) ya Marakani aliorodhesha mbinu za kueneza ukafiri na kuua itikadi nyingine na kuziweka katika kumbukumbu ya maktaba ya Congress. Baadhi ya mbinu zilizoorodhesha ni hizi zifuatazo:

- (i) Kudhibiti mashule ambapo hisia za kidini zitafutwa katika mitaala na vitabu vya kiada.
- (ii) Kudhibiti magazeti na Television.
- (iii) Kuharibu utamaduni na mila za jamii.
- (iv) Kuanzisha ghasia za wafanyakazi katika serikali zinazoamini kuwepo kwa Mwenyezi Mungu.

- (v) Kuvuruga maadili mema kwa kusamabaza picha, filamu, vitabu, majarida na magazeti yenyeye watu walio uchi ili kuchochaea zinaa.
- (vi) Kuondosha sheria zote zinazokataza ufuska au maandishi machafu.
- (vii) Kupiga vita taasisi ya familia.
- (viii) Kuhimiza watoto walelewe katika vituo vya watoto ili wasiathiriwe na mafunzo na malezi ya wazazi wao.
- (ix) Kuwafanya watu waione tabia ya uasherati na kulawitiana kuwa ni jambo la kawaida.
- (x) Kufuta swala au ishara yoyote ya Ibada maalumu katika shule.

Hizi ni baadhi tu ya mbinu zilizoandaliwa na zinazotumiwa na makafiri katika kuwahujumu Waumini. Ukiziangalia kwa makini mbinu hizi utaona kuwa makafiri si maadui wa mchezo na ni hatari iliyoje kuwafanya marafiki. Ndio maana katika aya chungu nzima Allah (s.w) ametukataza tusiwatii makafiri.

يَأَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِن تُطِيعُوا الَّذِينَ كَفَرُوا يَرُدُّو كُمْ عَلَىٰ أَعْقَبِكُمْ

فَتَنَقِّلُهُمْ خَسِيرِينَ

Enyi mlio amini! Ikiwa mtawatii waliokufuru watakurudisheni nyuma (katika ukafiri) na mtakuwa wenye kukhasirika. “(3:149)

Lengo la Makafiri ni kuwafanya waumini wawe makafiri kama wao.

● Mayahudi na Wakristo

Uadui wa Ahalal-Kitaabi (watu wa Vitabu) – Mayahudi na Wakristo dhidi ya Uislamu na Waislamu unabainishwa wazi katika aya zifuatazo:

الَّمُ شَرِ إِلَى الَّذِينَ أَوْتُوا نَصِيبًا مِّنَ الْكِتَابِ يَشْتَرُونَ الْضَّلَالَةَ
وَيُرِيدُونَ أَن تَضْلِلُوا النَّاسَ

Huwaoni wale waliopewa sehemu ya (kukifahamu) Kitabu (cha Mwenyezi Mungu Mayahudi na Manasara)? Wanakhiari upotofu (upotevu) na wanakutakieni mpotee njia (ya kheri). (4:44)

وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِأَعْدَائِكُمْ وَكَفَى بِاللَّهِ ذِيَّالْكُفَّارِ

Na Mwenyezi Mungu anawajua vyema maadui zenu. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa mlinzi, na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa msaidizi. (4:45)

يَتَأَيَّهُ إِلَّا الَّذِينَ ظَاهَرُوا لَا تَتَخِذُنَّوْا بِطَانَةً مِّنْ دُونِكُمْ
لَا يَأْلُونَكُمْ خَبَالًا وَدُوْا مَا عَيْثُمْ قَدْ بَدَتِ الْعَضَاءُ مِنْ
أَفْوَاهِهِمْ وَمَا تُحْفِي صُدُورُهُمْ أَكْبَرُ قَدْ بَيَّنَا لَكُمُ الْآيَاتِ إِنْ كُنْتُمْ
 تَعْقِلُونَ

Enyi mlionmini! Msiwafanye wasiri wenu watu wasiokuwa katika nyinyi: hao hawataacha kukufanyieni ubaya. Wanayapenda yale yanayokudhuruni. Bughudha (yao juu yenu) inadhihirika katika midomo yao. Na yanayofichwa na vifua vyao ni makubwa zaidi. Tumekubainishieni dalili (zote) ikiwa nyinyi ni watu wa kufahamu. (3:118)

هَتَّا نُتْمُ أُلَاءِ تُحِبُّونَهُمْ وَلَا يُحِبُّونَكُمْ وَنُؤْمِنُونَ بِالْكِتَابِ كُلِّهِ
وَإِذَا لَقُوْكُمْ قَالُواْ ءَامَنَّا وَإِذَا خَلَوْاْ عَضُوًّا عَلَيْكُمُ الْأَنْتَامِلَ مِنَ الْغَيْظِ فُلْ
مُوْثُواْ بِعَيْظَكُمْ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِذَاتِ الْصُّدُورِ

١١٩

Oh! Nyinyi mnawapenda (maadui zenu hao), hali wao hawakupendeni! Nanyi mnaamini vitabu vyote (chenu na vya). Na wanapokutana nanyi husema, “Tumeamini”. Lakini wanapokuwa peke yao wanakuumieni vyanda kwa uchungu (wa kukuchukieni). Sema: “Kufeni kwa uchungu wenu (huo); hakika Mwenyezi Mungu anayajua (hata) yaliyomo vifuanî.” (3:119)

إِنْ تَمْسَسْكُمْ حَسَنَةٌ تَسُوْهُمْ وَإِنْ تُصِبْكُمْ سَيِّئَةٌ يَفْرُحُوْ
بِهَا وَإِنْ تَصْبِرُوْا وَتَتَقَوْلُوْ لَا يَضْرُرُكُمْ كَيْدُهُمْ شَيْءٌ إِنَّ اللَّهَ
بِمَا يَعْمَلُونَ مُحِيطٌ

١٢٠

Ikikupateni kheri huwasikitisha. Na ikikupateni shari wanaifurahia. Na kama nyinyi mkisubiri na mkamcha Mungu hila zao hazitakudhuruni kitu. Hakika Mwenyezi Mungu anayajua vizuri yote wanayoyatenda. (3:120)

Kwanini Mayahudi na Wakristo wanauchukia sana Uislamu na Waislamu? Wanauchukia Uislamu kwa sababu Qur-an inawaumbua kuwa hawaftati viliyyo mafundisho ya Mitume wao na Vitabu vya wanavyodai kuvifuata, bali wamechanganya haki na batili kwa ajili tu ya kutafuta maslahi ya maisha ya dunia. Qur-an inawalingania mara kwa mara na kuwaita kwenye Uislamu kama kweli wanadai kuwa wanafuata mafundisho ya Mitume na Vitabu vya Mwenyezi Mungu. Allah (s.w) anawalingania:

يَبْيَنِي إِسْرَائِيلَ أَذْكُرُو وَنَعْمَتِي الَّتِي أَنْعَمْتُ عَلَيْكُمْ وَأَوْفُوا بِعَهْدِي
 أُوفِ بِعَهْدِكُمْ وَإِيَّنِي فَارْهَبُونِ ﴿٤١﴾

*Enyi kizazi cha Israili (Nabii Yaaqub! Yaani Mayahudi!)
 Zikumbukeni neema zangu nilizokuneemesheni; na tekelezeni
 ahadi yangu (ya kuwa akija Mtume mtamfuata), nitatekeleza
 ahadi yenu (ya kukupeni Pepo); na niogopeni mimi tu.(2:40)*

وَعَامِنُوا بِمَا أَنْزَلْتُ مُصَدِّقًا لِمَا مَعَكُمْ وَلَا تَكُونُوا أُولَئِكَافِرٍ بِهِ
 وَلَا تَشْتَرُوا بِغَایَاتِي ثَمَنًا قَلِيلًا وَإِيَّنِي فَاتَّقُونِ ﴿٤١﴾

*Na aminini niliyoyateremsha ambayo yanasadikisha yaliyo
 pamoja nanyi, wala msiwe wa kwanza kuyakataa. Wala
 msiyauze maneno yangu kwa ajili ya thamani ndogo tu (ya
 kilimwenguni); na niogopeni Mimi tu.(2:41)*

وَلَا تَلِسُوا الْحَقَّ بِالْبَطْلِ وَتَكْتُمُوا الْحَقَّ وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٤٢﴾

*Wala msichanganye haki na batili, na mkaficha haki, na hali
 mnajua.(2:42)*

وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَءَاشُوا الْرَّكُوْةَ وَأَرْكَعُوا مَعَ الْرِّكَعَيْنِ ﴿٤٣﴾

*Na simamisheni Swala (Enyi Mayahudi) na toeni Zaka na
 inameni pamoja na wanaoinama (yaani kuweni
 Waislamu).(2:43)*

* أَتَأْمُرُونَ الْإِنْسَانَ بِالْبَرِّ وَتَنْسَوْنَ أَنْفُسَكُمْ وَأَنْتُمْ تَتَلَوَّنَ الْكِتَابَ أَفَلَا
 تَعْقِلُونَ ﴿٤٤﴾

*Je! Mnawaamrishwa watu kutenda mema na mnajisahau
 nafsi zenu, hali mnasoma Kitabu (cha Mwenyezi Mungu
 kuwa kufanya hivyo ni vibaya)? Basi je, hamfahamu?
 (2:44)*

Allah (s.w) anawabainishia Mayahudi na Wakristo kuwa, kama hawataifuata Taurati, Injili na Qur-an katika kuendesha maisha yao ya kibinagsi na ya kijamii, watakuwa wamekufuru kama walivyokufuru makafiri wengine.

إِنَّ أُولَئِكَ النَّاسُ بِإِيمَانِهِمْ لَلَّذِينَ أَتَبَعُوهُ وَهَذَا الظَّبْءُ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَاللَّهُ

وَلِسْتُ أَنَا مُؤْمِنَ

Watu wanaomkurubia zaidi Ibrahimu ni wale waliomfuata yeye (katika zama zake) na Mtume huyu (Muhammad) na waliomwamini (Mtume huyu). Na Mwenyezi Mungu ndiye Mlinzi wa wenye kuamini. (3:68)

Kwa kuzifahamu vyema chuki zao na uadui wao dhidi ya Uislamu na Waislamu, Allah (s.w) ametukataza kuwatii na kuwafanya Mayahud na Wakristo rafiki zetu.

*يَتَأَيَّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَخِذُوا أَلْيَهُودَ وَالنَّصَارَى أَوْ لِيَاءَ بَعْضَهُمْ
أَوْ لِيَاءَ بَعْضٍ وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ مِنْكُمْ فَإِنَّهُ مِنْهُمْ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهُدِي الْقَوْمَ

الظَّالِمِينَ

Enyi Mlioamini! Msiwafanye Mayahudi na Wakristo kuwa marafiki (wa kuwapa siri zenu); wao kwa wao ni marafiki. Na mionganoni mwenu atakayefanya urafiki huo nao, basi huyo atakuwa pamoja nao. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongozi (njia ya kheri) watu madhalimu. (5:51)

*يَتَأَيَّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَخِذُوا الَّذِينَ أَتَخَذُوا دِينَكُمْ هُرُزًا وَلَعِيَا
مِنَ الَّذِينَ أَوْثَوْا الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِكُمْ وَالْكُفَّارَ أَوْ لِيَاءَ وَأَنْقُوا اللَّهَ

إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ

Enyi mlionamini! Msiwafanye marafiki wale walioifanyia mzaha na mchezo dini yenu mionganini mwa wale waliopewa kitabu kabla yenu na mionganini mwa makafiri (wengine). Na mcheni Mwenyezi Mungu kama nyinyi ni wenye kuamini. (5:57)

يَتَأْيِهَا الَّذِينَ ظَاهَرُوا إِنْ تُطِيعُوْ فَرِيقًا مِنَ الَّذِينَ أَوْتُوا الْكِتَابَ يَرُدُّوْ كُمْ

بَعْدَ إِيمَانِكُمْ كَفَرُوْنَ

Enyi mlionamini! Mkiwatii baadhi ya wale waliopewa Kitabu, watakurudisheni kuwa makafiri baada ya Uislamu wenu. (3:100)

Mbinu za Mayahudi

Mbinu za Mayahudi tunazipata vizuri tukidurusu “The Protocols of The Elders of Zion” yaani “Mikakati ya Wazee wa Kizayuni (Mayahud)” zilizofafanuliwa vizuri na Bwana Henry Ford katika kitabu chake “The International Jew”. Mbinu hizi zimeainishwa kama ifuatavyo:

- (i) Kuunda mashirika ya kijasusi ya siri na dhahiri ili kupata taarifa muhimu.
- (ii) Kutumia propaganda ili kuondosha mshikamano wa kiiislamu kwa kutumia majina mabaya kama vile siasa kali, ugaidi n.k.
- (iii) Kuziondoa madarakani serikali wasizozitaka kwa mtazamo wao.
- (iv) Kutumia propaganda kupandikiza chuki na kuvuruga ukweli kuhusu jambo Fulani.
- (v) Kuchochea chokochoko na chuki za kidini hasa baina ya Waislamu na Wakristo. Pia baina ya Waislamu kwa Waislamu. Ndio waasisi wa Twarika, madhehebu na vikundi mbali mbali vyta Waislamu vinavyo hasimiana hivi leo.
- (vi) Kuchochea hisia za kibaguzi ndani ya nchi moja kama vile Kashmir, Palestine, Lebanon n.k.

- (vii) Kuzidhibiti taasisi kubwa za kimataifa zitakazotumika kusimamia maslahi ya Waislamu Ulimwenguni kote.
- (viii) Kuvuruga na kubomoa maadili ya jamii kupitia mifumo ya elimu.
- (ix) Kumiliki vyombo vyote vya habari
- (x) Kusababisha umaskini kwa wananchi hasa katika nchi za ulimwengu wa tatu.
- (xi) Kupiga vita taasisi ya familia na kuyafanya maisha ya ndoa kuwa si kutu cha maana.

Mbinu za Wakristo

Mbinu kubwa wanayoitumia Wakristo ni kuwaghilibu Waislamu kwa kuunga nao urafiki wa kinafiki ili waweze kupenyeza mila zao ndani ya jamii ya Waislamu. Jamii ya Waislarnu wa leo imeathiriwa mno na mila za Kikristo baada ya Waislamu kuwakumbatia Wakristo, licha ya tahadhari aliyatupa Allah (s.w):

وَلَنْ تَرْضَىَ عَنْكَ الْيَهُودُ وَلَا النَّصَارَىَ حَتَّىَ تَتَبَعَ مِلَّتَهُمْ قُلْ
 إِنَّ هُدَىَ اللَّهِ هُوَ الْهُدَىٰ وَلَمَّا آتَيْنَاهُمْ بَعْدَ الَّذِي جَاءَكُمْ مِنَ الْعِلْمِ
 مَا لَكُمْ مِنَ اللَّهِ مِنْ وَلِيٍّ وَلَا نَصِيرٍ



Hawatakuwa radhi juu yako Mayahudi wala Wakristo mpaka ufuate mila yao. Sema: "Hakika uongozi wa Mwenyezi Mungu ndio uongozi (khasa). Na kama ukifuata matamanio yao baada ya yale yaliyokufikia ya ujuzi (wa kweli) hutapata msaidizi yoyote wala mlinzi kwa Mwenyezi Mungu". (2:120)

Miongoni mwa mbinu na mikakati ya Wakristo, dhidi ya Uislamu inadhihirika vizuri kwenye taarifa ya utafiti uliofanywa na Profesa A. B. Kasozi wa huko Canada na kuchapishwa 1989. Miongoni mwa mengi yaliyomo katika taarifa hiyo ni kwamba Wakristo kuanzia 1900 waliandaa mkakati wa kuhakikisha kuwa Uislamu unatoweke barani Afrika.

Kufikia mwaka 1970 wakaanzisha mradi mkubwa waliouita “Islam in Africa Project” yaani “**Mradi wa kuua Uislamu Afrika**” na Mkurugenzi wake mkuu akawa Nairobi, Kenya. Mradi huu kwanza ulifanya kazi ya kuwatafiti Waislamu na udhaifu wao ili kujua namna ya kuwamaliza. Wakagundua kuwa udhaifu mkubwa wa Waislamu ni:

- (i) Kutojua Uislamu wao na kutofuata Qur'an na Sunnah.
- (ii) Kuridhika na kukaa mijini tu na kutofanya Da'awah vijijini.

Wao, Wakristo, wakaingia vijijini na kueneza Ukristo. Hivyo Uislamu ambao ulikuja Afrika Mashariki tangu karne ya tisa, leo unashindana na hata kuzidiwa nguvu na Ukristo uliokuja Afrika Mashariki miaka elfu baadaye.

Mbinu kubwa iliyopangwa na kutumiwa Afrika ilikuwa kuwaelekeza Mapadri wote wajisingizie kuwa ni marafiki wa Waislamu. “Wote ni ndugu.” Halafu bila kuwagutua Waislamu, waeneze mafundisho ya Ukristo polepole kwa Waislamu hasa kwa kupitia shule na hospitali. Lengo lilikuwa ni kuwafanya Waislamu waritadi.

Kampeni hiyo imefikia hatua kubwa sana hivi leo kiasi ambacho Waislamu bila hata kujijua wanawafuata Wakristo katika mambo mengi. Zimezuka siku hizi “Ibada” za pamoja za madhehebu yote. Yaani Waislamu na Wakristo wanashirikiana Ibada kuombea kitu fulani, Waislamu wanaume na wanawake wanavaa kama Wakristo, huna namna ya kumjua yupi Muislamu na yupi Mkristo. Hivyo huwezi kujua yupi umtolee “Assalaam Alaykum”. Katika harusi ndio kabisa. Binti wa Kiislamu anakuwa kama Mkristo halisi. Leo mpaka katika mazishi utakuta Waislamu wanamweka hadharani maiti mwenzao Muislamu na kuwaalika watu wote waliokusanyika hapo wake kwa waume waje,

kumkashifu maiti huyo eti wanatoa heshima za mwisho! Hapana shaka yote hayo wamewaiga wakristo.

Imefikia hadi mwezi wa Ramadhani badala ya Muislamu kumfuturisha Muislamu mwenzake kama alivyosisitiza sana Mtume (s.a.w) huwafuturisha wakristo ambao hawakufunga kana kwamba hakuna Waislamu waliofunga.

Na katika kuhakikisha kuwa tunawafuata wakristo katika kila jambo, yupo Muislamu mmoja tena Al-haj, akafikia hadi kujipa jukumu la kuandaa karamu ya kusherehekeea Noeli na yeze ndiye aliyewaalika Wakristo waende kula sikukuu! Kwa sababu ni kiongozi maarufu, picha yake ikawekwa ukurasa wa mbele wa gazeti la Sunday News! Hayo ni mafanikio ya maadui ambao Waislamu wamehadharishwa nao lakini hawasikii.

Mfano mwingine wa mikakati yao tunauona katika mpango wa kuhujumu Uislamu ulioandalika katika ile semina ya Nairobi ya Septemba 23, 1989.

Semina hiyo ambayo ilikuwa na mada moja kuu – “Kukabiliana na Uislamu” ilihudhuriwa na washiriki 989 toka mikoa yote ya Kenya isipokuwa mkoa wa Pwani (Mombasa).

Msemaji Mkuu katika semina hiyo alikuwa Prof. Hafkean ambaye ni Profesa katika mambo ya Kiislamu Afrika na muanzilishi wa “Miradi ya Kiislamu Afrika” (Islam Projects in Africa).

Profesa Hafkean alizungumza kwa kirefu imani na tabia za Waislamu na namna Wakristo wanavyoweza kuwavuruga Waislamu nchini Kenya. Katika jumla ya mikakati aliyoibainisha Profesa Hafkean iliyoandalika kupambana na Uislamu ni pamoja na:

- (i) Kwamba wadhamini wa chuo Kikuu cha Daystar Nairobi wametenga kiasi cha Paundi Milioni 56 sawa na kiasi cha shilingi 1.97 bilioni kuwasaidia vijana wa Kiislamu wanaoritadi.

- (ii) Kujenga zahanati na kuweka huduma nyingine muhimu za kijamii katika maeneo yenye Waislamu wengi.
- (iii) Kuwafundisha wachungaji lugha ya Kiarabu.
- (iv) Vitabu vya Kikristo vichapishwe kwa lugha ya Kiarabu.

Naye Mchungaji James Beggs wa kituo cha Kikristo cha kimataifa Nairobi alitoa mada juu ya kuhubiri Ukristo kwa Waislamu ambayo alitoa ushauri ufuatao:

- (i) Mapasta wawatemelee Waislamu kuwavuta katika Ukristo.
- (ii) Kutumia majasusi na wapasha habari (informers) kuchunguza habari za Waislamu.
- (iii) Kutumia tofauti zilizopo kati ya Sunni na Shia kuwavuruga Waislamu.

Dr. Tokobah ambaye ni katibu wa “Association of Evangelical Fellowship” ya Madagascar na Afrika Mashariki aliwafahamisha washiriki wa semina hiyo kuwa yapo makanisa na vyama vya Kikristo huko Marekani ambayo viko tayari kutoa misaada ya kuanzisha biashara ndogo ndogo kwa vijana wanaoritadi.

“Miradi ya Uislamu katika Afrika” (Islam projects in Africa) ina lengo la kuyastawisha makanisa kusini mwa jangwa la Sahara kuwasoma na kuwaelewa Waislamu ili waweze kuwavuta kwa urahisi katika Ukristo.

● **Wanafiki**

Wanafiki ni maadui wakubwa wa Uislamu na Waislamu kwa sababu wao ni maadui wa ndani. Wanafiki ni wale wanaodai kuwa ni Waislamu lakini nyoyoni mwao na katika matendo yao wanaukanusha Uislamu, na kuupiga vita. Sifa za wanafiki zimeainishwa katika aya nyingi za Qur-an (rejea Juzuu 3) zifuatazo ni baadhi tu ya sifa zao:

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَقُولُ عَامَنَا بِاللَّهِ وَبِالْيَوْمِ الْآخِرِ وَمَا هُمْ بِمُؤْمِنِينَ ﴿٨﴾

Na katika watu, wako (wanafiki) wasemao: “Tumemwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho”; na hali ya kuwa wao si wenye kuamini.(2:8)

يُخَدِّعُونَ اللَّهَ وَالَّذِينَ عَامَنُوا وَمَا يَخْدَعُونَ إِلَّا أَنفُسَهُمْ

وَمَا يَشْعُرُونَ ﴿٩﴾

Wanatafuta kumdanganya Mwenyezi Mungu na wale walioamini, lakini hawadanganyi ila nafsi zao; nao hawatambui.(2:9)

يُخَدِّعُونَ اللَّهَ وَالَّذِينَ عَامَنُوا وَمَا يَخْدَعُونَ إِلَّا أَنفُسَهُمْ

وَمَا يَشْعُرُونَ ﴿١٠﴾

Nyoyoni mwao mna maradhi, na Mwenyezi Mungu amewazidishia maradhi) Basi watakuwa na adhabu iumizayo kwa sababu ya kule kusema kwao uwongo.(2:10)

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ لَا تُقْسِدُوا فِي الْأَرْضِ إِنَّمَا نَحْنُ مُصْلِحُونَ ﴿١١﴾

Na wanapoambiwa “Msifanye uharibifu ulimwenguni.” Husema: “Sisi ni watengezaji.” (2:11)

أَلَا إِنَّهُمْ هُمُ الْمُقْسِدُونَ وَلَكِنْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿١٢﴾

Hakika wao ndio waharibuji, lakini hawatambui.(2:12)

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ عَامَنُوا كَمَا عَامَنَ النَّاسُ فَقَاتُوا أَنْوَاعُ الْمُؤْمِنِينَ كَمَا عَامَنَ السَّفَهَاءُ لَا إِنَّهُمْ هُمُ الْسَّفَهَاءُ وَلَكِنْ لَا

يَعْلَمُونَ ﴿١٣﴾

Na wanapoambiwa: “Aminini kama walivyoamini watu,” husema: “Oh! Tuamini kama walivyoamini wale wapumbavu?” Hakika wao ndio wapumbavu lakini hawajui.(2:13)

وَإِذَا لَفُوا الَّذِينَ ءَامَنُوا قَالُواْ ءَامَنَا وَإِذَا خَلَوْ إِلَى شَيْءٍ طَبِيعُهُمْ قَالُواْ
 إِنَّا مَعْكُمْ إِنَّمَا نَحْنُ مُسْتَهْزِئُونَ (١٤)

Na wanapokutana na walioamini husema: “Tumeamini”; na wanapokuwa peke yao kwa mashetani wao husema: “Hakika sisi tu pamoja nanyi, tunawacheza shera tu.” (2:14)

اللَّهُ يَسْتَهْزِئُ بِهِمْ وَيَمْدُهُمْ فِي طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُونَ (١٥)

Mwenyezi Mungu atawalipa shere yao na kuwawacha katika upotofu wao wakitangatanga oyoo. (2:15)

أُولَئِكَ الَّذِينَ أَشْتَرُوا الْضَّلَالَةَ بِالْهُدَىٰ فَمَا رَبَحْتَ تِجَارَتُهُمْ
 وَمَا كَانُوا مُهَتَّدِينَ (١٦)

Hao ndio waliokhari upotofu kuliko uongofu; lakini biashara yao haikupata faida wala hawakuwa wenye kuongoka. (2:16)

إِنَّ الْمُنْتَفِقِينَ يُخَدِّعُونَ اللَّهَ وَهُوَ خَدِيرٌ عَهُمْ وَإِذَا قَامُوا إِلَى الْأَصْلَوةِ قَامُوا
 كُسَالَىٰ يُرَأُونَ الْثَّالِثَ وَلَا يَذَرُونَ اللَّهَ إِلَّا قَلِيلًا (١٧)

Wanafiki hutaka kumdanganya (hata) Mwenyezi Mungu. Naye atawaadhibu kwa sababu ya kudanganya kwao (huko). Na wanaposimama kuswali husimama kwa uvivu, wanaonyesha watu (kuwa wanawali) wala hawamtaji Mwenyezi Mungu ila kidogo. (4:142)

مُذَبِّدِينَ بَيْنَ ذَلِكَ لَا إِلَى هَتْوَلَاءِ وَلَا إِلَى هَتْوَلَاءِ وَمَنْ يُضْلِلِ اللَّهُ فَلَنْ
 تَجِدَ لَهُ وَسِيلًا (١٨)

Wanayumbumba baina ya huku (kwa Waislamu na huko kwa makafiri). Huku hawako wala huko hawako. Na ambaye Mwenyezi Mungu amemhukumu kupotea, huwezi kumpatia njia (ya kuhisabika kuwa mwongofu). (4:143)

الْمُنَافِقُونَ وَالْمُنَافِقَاتُ بَعْضُهُم مِّنْ بَعْضٍ يَأْمُرُونَ بِالْمُنْكَرِ وَيَنْهَاوْنَ عَنِ الْمَعْرُوفِ وَيَقْبِضُونَ أَيْدِيهِمْ نَسْوَاتٌ لِلَّهِ فَنِسِيَاهُمْ إِنَّ الْمُنَافِقِيَنَ هُنَّ مِنَ الْفَسِيلِ فُونَ

Wanaume wanafiki na wanawake wanafiki, wote ni hali moja; huamrisha yaliyo mabaya na huyakataza yaliyo mazuri, na kuizulia mikono yao (hawasaidii mambo ya kheri); wamemsahau Mwenyezi Mungu (wamepuuza amri Zake); na Yeye pia amewasahau Hakika wanafiki ndio wavinjao amri. (9:67)

وَعَدَ اللَّهُ الْمُنَافِقِينَ وَالْمُنَافِقَاتِ وَالْكُفَّارَ نَارَ جَهَنَّمَ خَلِدِينَ فِيهَا هِيَ حَسْبُهُمْ وَلَعَنْهُمُ اللَّهُ وَلَهُمْ عَذَابٌ مُّقِيمٌ

Mwenyezi Mungu amewaaahidi wanafiki wanaume na wanafiki wanawake na makafiri, moto wa jahannamu kukaa humo daima. Huo unawatosha (kuwaadhibu); na Mwenyezi Mungu amewalaani; nao wana adhabu itakayodumu. (9:68)

إِذَا جَاءَكُ الْمُنَافِقُونَ قَالُوا نَشَهُدُ إِنَّكَ لَرَسُولُ اللَّهِ وَاللَّهُ يَعْلَمُ إِنَّكَ لَرَسُولُهُ وَاللَّهُ يَشْهُدُ إِنَّ الْمُنَافِقِينَ لَكَذِبُونَ

Wanapokujia wanafiki, husema: “Tunashuhudia ya kuwa kwa yakini wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu.” Na Mwenyezi Mungu anajua kuwa wewe ni Mtume wake na Mwenyezi Mungu anashuhudia ya kuwa hakika wanafiki ni waongo. (63:1)

أَتَخَذُوا أَيْمَانَهُمْ جُنَاحًا فَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ إِنَّهُمْ سَاءَ مَا كَلَّوْا يَعْمَلُونَ

Wamevisanya viapo vyao ndizo ngao za kujikingia, wakajikinga na kupitishwa njia ya Mwenyezi Mungu. Kwa hakika ni mabaya kabisa waliyo kuwa wakifanya. (63:2).

ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ عَامَلُوا نُسُمَّ كُفَّارًا فَطَبَعَ عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ فَهُمْ لَا يَقْنَعُونَ ﴿٦٣﴾

Na hayo ni kuwa waliamini, kisha wakakufuru; kwa hiyo muhuri umepigwa juu ya nyoyo zao; kwa hivyo hawafahamu lolote.(63:3)

Katika aya hizi chache juu ya tabia ya wanafiki tunajifunza kuwa:

- (i) Wanafiki wanadai kuwa ni waumini wa Allah (s.w) na siku ya Mwisho lakini si kweli kwa sababu wanakanusha maamrishi ya Allah na hawaogopi adhabu ya Akhera.
- (ii) Wanafanya uharibifu katika ardhi huku wakidai kuwa wanatengeneza.
- (iii) Hushirikiana na Makafiri katika kuwadhihaki na kuwapiga vita Waislamu.
- (iv) Huiendea swala kwa uvivu.
- (v) Hawamtaji Allah ila kidogo tu.
- (vi) Hufanya mema kwa ria.
- (vii) Hawana msimamo, wakati mwingine kwa ajili ya maslahi hujifanya kuwa pamoja na Waislamu na wakati mwingine hujikomba kwa Makafiri na kushirikiana nao katika kuwapiga vita Waislamu. Kwa tabia yao hii, hawaaminiki kwa Waislamu wala kwa Makafiri.
- (viii) Wanafiki huamrisha yaliyo mabaya na kukataza yaliyo mazuri.
- (ix) Huficha maovu yao kwa viapo.
- (x) Hujifanya kuwa Waislamu safi kwa maneno yao laini ya kujikomba na kwa mavazi yao ya Kiislamu.

Je, Waislamu tulio wengi hivi leo hatuna sifa za wanafiki zilizobainishwa katika Qur-an na Sunnah? Je, wengi hatujiiti Waislamu safi lakini hatuko tayari kusimamisha Dini ya Allah (s.w) katika jamii? Je, baadhi ya Waislamu wenye nyadhifa katika dola

hawasaidiani na Matwaghuti katika kuukandamiza Uislamu na Waislamu na kuhakikisha kuwa Uislamu hausimami katika jamii? Je, baadhi ya viongozi wa Waislamu hawashirikiani bega kwa bega na dola za Kitwaghuti katika kuuhujumu Uislamu na Waislamu? Kwa ujumla, ukiichunguza jamii yetu hii ya Waislamu, utaona kuwa wengi wanaojiita Waislamu ni wanafiki wanaouhujumu Uislamu kwa njia moja au nyingine.

Waislamu walio wengi katika jamii hii ni wanafiki kwa sababu ya kutoufahamu vyema Uislamu. Waislamu wengi hawafahamu Uislamu uliofunuliwa katika Qur-an na Sunnah ya Mtume (s.a.w), bali wengi ni Waislamu wa kufuata mkumbo. Wengi Uislamu wao ni ule wa kufuata Masheikh bila ya kujua kuwa wengi katika hao masheikh wameitumia dini kama bidhaa ya kufanya biashara kwa ajili ya maslahi ya dunia. Juu ya Masheikh, Allah (s.w) anatutanabahisha katika aya ifuatayo:

* يَتَأْيِثُهَا الَّذِينَ ظَاهَرُوا إِنَّ كَثِيرًا مِنَ الْأَحْبَارِ وَالرُّهْبَانُ لَيَأْكُلُونَ أَمْوَالَ

..... النَّاسُ بِالْبَطْلِ وَيَصْدُونَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ

Enyi mliaoamini! Wengi katika Makasisi (wanazuoni) na Mayahudi na Watawa (viongozi wa wakristo) wanakula mali za watu kwa batwili na kuwazulia njia ya Mwenyezi Mungu..... (9:34)

Je, wengi wa Masheikh wetu hawana tabia hii ya Masheikh wa Kiyahudi na Kinaswara? Je, hatuoni, Waislamu hivi leo wamegawanyika katika makundi mbali mbali, yaliyoundwa na Masheikh kwa ajili tu ya kuwa na watu wa kuwanyonya? Je, hatuoni leo hii Waislamu wakigombana na kufarakana kutokana na vitu ambavyo si vya msingi kabisa wa Dini ambavyo vimepachikwa na Masheikh kwa ajili tu ya maslahi ya dunia?

Ni dhahiri kuwa Masheikh wetu walio wengi wana mwenendo ule ule wa Makasisi na Mapadri wa kuwanyonya wafuasi wao na

kuwapoteza na njia ya Allah (s.w) kwa kutumia nafasi zao. Allah (s.w) anatutanabahisha na Masheikh wa aina hii katika aya ifuatayo:

وَإِنْ مِنْهُمْ لَفَرِيقًا يَلْوُنَ الْسِنَّتَهُمْ بِالْكِتَابِ لِتَحْسِبُوهُ مِنَ الْكِتَابِ وَمَا
هُوَ مِنَ الْكِتَابِ وَيَقُولُونَ هُوَ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ وَمَا هُوَ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ
وَيَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبُ وَهُمْ يَعْلَمُونَ

Na mionganini mwao kuna baadhi yao wanapinda ndimi zao kwa (kusoma) kitabu ili mpate kuyafikiri (maneno) yao hayo kuwa ni ya Kitabu (cha Allah), na wanasema: “Haya yametoka kwa Mwenyezi Mungu”, na hali hayajatoka kwa Mwenyezi Mungu; na wanamsingizia Mwenyezi Mungu uwongo na hali wanajua. (3:78).

Sheikh mcha-Mungu anayestahiki kuitwa Sheikh na kufuatwa na watu ni yule anayewaelekeza watu kufuata Qur-an na Sunnah, Allah (s.w) anatufahamisha:

مَا كَانَ لِبَشَرٍ أَنْ يُؤْتِيهِ اللَّهُ الْكِتَابَ وَالْحُكْمُ وَالْبُيُّوْثَةُ ثُمَّ
يَقُولُ لِلنَّاسِ كُوْنُوا عِبَادًا لِّي مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلَكِنْ كُوْنُوا رَبِّنِيْشَنْ بِمَا
كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ الْكِتَابَ وَبِمَا كُنْتُمْ تَدْرُسُونَ

Haiwi kwa mtu ambaye Mwenyezi Mungu amempa Kitabu na hukumu na unabii aseme kuwaambia watu: Kuweni wa kuniabudu mimi badala ya Mwenyezi Mungu (peke yake). Bali (atawaambia): “Kuweni wenyewe kumuabudu Mwenyezi Mungu. Kwa sababu mnafundisha kitabu na kwa sababu mnakisoma (3:79)

Je, Masheikh walio wengi leo hawawang’ang’anizi watu kufuata maoni yao na vitabu vyao badala ya Qur-an na Sunnah? Bado Waislamu walio wengi kwa kutoifahamu Qur-an na Sunnah wamewafuata Masheikh wakapotea njia kama walivyopotea Mayahudi

na Wakristo kama Allah (s.w) anavyotukumbusha katika Qur-an:

أَتَخَذُوا أَحْبَارَهُمْ وَرُهْبَانِهِمْ أَرْبَابًا مِّنْ دُونِ اللَّهِ وَالْمَسِيحَ أَبْنَى مَرْيَمَ
وَمَا أُمِرْتُ إِلَّا لِيَعْبُدُوا إِلَهًا وَاحِدًا لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ سُبْحَانَهُ وَعَمَّا يُشْرِكُونَ

(٣١)

Wamewafanya wanavyuoni wao, na watawa (Mapadri) wao kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu, na (wamemfanya) Masihi mwana wa Maryamu (pia Mungu), hali hawakuamrishwa isipokuwa kumuabudu Mungu mmoja, hakuna anayestahiki kuabudiwa ila Yeye. Ametakasika na yale wanayomshirikisha nayo. (9:31)

Waislamu, hatuna budi kufahamu kuwa hapana udhuru wowote tutakaotoa mbele ya Allah (s.w) juu ya kupotezwa kwetu na masheikh waovu. Wao wana malipo yao mbele ya Allah (s.w) na sisi wenye kukubali kupotezwa na wao pia tuna malipo yetu. Kuhusu malipo ya Masheikh waovu tunafahamishwa:

إِنَّ الَّذِينَ يَشْتَرُونَ بِعَهْدِ اللَّهِ وَأَيْمَانِهِمْ ثَمَنًا قَلِيلًا أُولَئِكَ لَا خَلَقَ لَهُمْ

Hakika wale wanaouza ahadi ya Mwenyezi Mungu na viapo vyao kwa ajili ya thamani ndogo ya kilimwengu, hao ndio hawatakuwa na sehemu ya kheri katika akhera, (3:77)

Kuhusu malipo ya wale wenye kufuata Masheikh kibubusa bila ya kutumia nuru ya Qur-an na Sunnah, tunafahamishwa katika aya zifuatazo:

إِذْ تَبَرَّأَ الَّذِينَ أَتَبْغُوا مِنَ الَّذِينَ أَتَبَغُوا وَرَأَوْا الْعَذَابَ وَتَقَطَّعَتْ بِهِمْ
الْأَسْبَابُ

(Wakumbushe wakati) wanaofuatwa watakpowakataa wale waliowafuata, na hali ya kuwa wamekwisha kuionna adhabu, yatakatika mafungamano yao. (2:166).

وَقَالَ الَّذِينَ أَتَبَعُوا لَوْ أَنْ لَتَأْكِرْهُ فَنَتَبَرَّأُ مِنْهُمْ كَمَا تَبَرَّغُوا
مِنَ الَّذِي لَكُمْ يُرِيهِمُ اللَّهُ أَعْمَلَهُمْ حَسَرَاتٍ عَلَيْهِمْ وَمَا هُمْ بِخَدْرٍ جِينَ

﴿١٦﴾ مِنَ النَّارِ

Na watasema wale waliofuata laiti tungeliweza kurudi (duniani) tukawakataa kama wanavyotukataa. Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu atakavyowaonyesha vitendo vyao kuwa majuto yao, wala hawatakuwa wenye kutoka motoni. (2:167).

Mbinu za wanafiki.

Wanafiki kwa mujibu wa Qur'an ni wale watu wanaojiita Waislamu kinadharia lakini kimatendo mwenendo wao ni sawa na ule wa Mayahud, Wakristo, Makafiri, Washirikina na Mashetani kulingana na mazingira na maslahi ya kidunia. Hawa, pamoja na kujiita Waislamu si Waislamu kama Allah (s.w) anavyobainisha katika Qur'an:

﴿٨﴾ وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَقُولُ إِيمَانًا بِاللَّهِ وَبِالْيَوْمِ الْآخِرِ وَمَا هُمْ بِمُؤْمِنِينَ
يُخَدِّعُونَ اللَّهَ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَمَا يُخَدِّعُونَ إِلَّا أَنفُسُهُمْ وَمَا يَشْعُرُونَ

"Na katika watu, wako (wanafiki) wasemao: 'Tumemwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho' na hali ya kuwa wao si wenye kuamini. Wanatafuta kumdanganya Mwenyezi Mungu na wale walioamini, lakini hawamdaganyi ila nafsi zao; nao hawatambui'. (2:8-9).

Tabia ya wanafiki na mbinu zao katika kuuhujumu Uislamu na Waislamu zimeelezwa kwa kirefu katika Qur'an katika aya na sura mbali mbali na imeshushwa sura maalum ya wanafiki – "**Suratul-Munaafiqun**".

Kwa muhtasari, mionganini mwa tabia na mbinu za Wanafiki dhidi ya Uislamu ni hizi zifuatazo kwa mujibu wa Qur'an:

- (i) Hutenda kinyume cha imani wanaodai kuwanayo.
- (ii) Hujaribu kumdanganya Mwenyezi Mungu na waumini wakidhani kuwa yaliyo nyoyoni mwao hayajulikani.
- (iii) Hufanya uharibifu katika jamii huku wakidai kuwa wanatengeneza.
- (iv) Huwaona waumini wa kweli kuwa ni wajinga kwa kufuata kwao Uislamu inavyotakikana.
- (v) Huwacheza shere Waislamu.
- (vi) Hujiona kuwa wao ni bora kuliko waumini.
- (vii) Hujikomba kwa viongozi wa kitwaaghuut.
- (viii) Huwfanya Makafiri, Washirikina, Mayahudi na Wakristo kuwa marafiki wao wa ndani badala ya Allah, Mtume wake na waumini.
- (ix) Huyapenda zaidi maslahi ya dunia kuliko ya akhera.
- (x) Hukataa kuhukumiwa na sheria za Allah (s.w).
- (xi) Hutumia kiapo kama kifuniko cha maovu yao.
- (xii) Huchanganya haki na batili/Uislamu na ukafiri.
- (xiii) Huendea swala kwa uvivu.
- (xiv) Hawamtaji Allah (s.w) ila kidogo tu.
- (xv) Huchochea fitna baina ya Waislamu.
- (xvi) Huchukia Waislamu wanapofikwa na kheri na kufurahia wanapofikwa na shari.
- (xvii) Hawako tayari kutoa mali zao katika njia ya Allah (s.w) na wakitoa chochote hutoa kwa ria.
- (xviii) Huwazuia watu kutoa katika njia ya Allah (s.w).
- (xix) Huzifanya stihizai (shere) aya za Qur'an.
- (xx) Wakifikwa na mtihani humdhania Allah (s.w) dhana mbaya.
- (xxi) Huamrisha maovu na kukataza mema.
- (xxii) Husema uwongo na kuvunja ahadi.
- (xxiii) Wakipewa amana huhini.
- (xxiv) Wakighadhibika huchupa mipaka na kudhihirisha chuki zao dhidi ya Uislamu na Waislamu.

- (xxv) Huwavunja moyo na kuwakatisha tamaa waumini wa kweli ili wawe makafiri sawa na wao.
- (xxvi) Hufanya hiyana katika mambo ya kheri na kuchagua mambo mepesi mepesi.
- (xxvii) Wanawaogopa na kuwachelea watu zaidi kuliko Allah(s.w)
- (xxviii) Hushirikiana na Makafiri, Washirikina, Mayahudi na Wakristo dhidi ya Uislamu na Waislamu.

Wanafiki ni kundi la hatari zaidi kuliko makundi mengine ya maadui kwa sababu ni kundi lililo mionganoni mwa Waislamu. Hili ndilo kundi linalotumika kufarakanisha Waislamu. Kwa mfano ukirejea historia, utaona kuwa Dola ya Kiislamu aliyoiasisi Mtume (s.a.w) na kuendelezwa na Abubakar (r.a) ‘Umar (r.a) ilisambaratishwa na kikundi cha Wanafiki kilichoongozwa na Abdullah bin Sabaa na kupelekeea kuuliwa kwa ‘Uthman (r.a) na Ally (r.a) na kuiacha jamii katika mgawanyiko wa makundi ya Waislamu yaliyohasimiana na kutwangana wao kwa wao. Kutokana na hatari ya kundi hili, Allah (s.w) analikamia adhabu kali zaidi kuliko ile ya makafiri wengine katika aya ifuatayo:

﴿إِنَّ الْمُنَذِّرِينَ فِي الدُّرُجَاتِ لَا يُشَفَّلُونَ وَلَنْ تَجِدَ لَهُمْ نَصِيرًا﴾
[145]

“Bila shaka Wanafiki watakuwa katika tabaka ya chini kabisa katika Moto. Hutamkuta kwa ajili yao msaidizi (yoyote)”. (4:145).

● Sheitwaani

Maadui wote waliozungira – makafiri na washirikina, Mayahudi na Wakristo na wanafiki – ni maadui wa wazi. Shetani ni adui aliyejificha na daima anapania kumpoteza mwanaadamu na njia ya Allah (s.w) kwa njia ya ushawishi na ulaghai. Iblis, kiongozi wa Mashetani, alimlaghai hata baba yetu Adam (a.s) na mama yetu Hawa, mpaka wakamuasi Mola wao. Allah (s.w) anatutahadharisha juu ya adui yetu huyu katika aya zifuatazo:

يَذَّبَّحُ إِدَمْ لَا يَقْتَنِنُكُمْ الشَّيْطَانُ كَمَا أَخْرَحَ أَبَوَيْكُمْ مِّنَ الْجَنَّةِ يَنْزِعُ
عَنْهُمَا لِبَاسَهُمَا لِيُرِيهِمَا سَوْءَاتِهِمَا إِنَّهُ يَرْكُمُ هُوَ وَقَبِيلُهُ وَمِنْ حَيْثُ لَا
تَرَوْنَهُمْ إِنَّا جَعَلْنَا الشَّيْطَانَ أُولَئِكَ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ

٢٧

Enyi wanaadamu! Shetani asikutieni katika matata, kama alivyowatoa wazee wenu katika Pepo, akawavua nguo zao ili kuwaonyesha tupu zao. Hakika yeye pamoja na wafuasi wake wanakuoneni, na hali ya kuwa hamuwaoni. Bila shaka sisi tumewajaalia Mashetani kuwa marafiki wa wale wasioamini. (7:27)

﴿يَتَأَلَّهُ إِلَيْهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّبَعُوا حُطُوطَ الشَّيْطَانِ وَمَنْ يَتَّبِعُ حُطُوطَ
الشَّيْطَانِ فَإِنَّهُ وَيَأْمُرُ بِالْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ﴾

Enyi mliaoamini – msifuate nyayo za Shetani, na atakayefuata nyayo za shetani (atapotea) kwani yeye huamrisha mambo ya aibu na maovu..... (24:21).

﴿يَتَأَلَّهُ إِلَيْهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَذْخُلُوا فِي الْسَّلَمِ كَافَةً وَلَا تَتَّبِعُوا
حُطُوطَ الشَّيْطَانِ إِنَّهُ لَكُمْ عَذُّوٌ مُّبِينٌ﴾

٢٨

Enyi mliaoamini! Ingieni katika Uislamu wote, wala msifuate nyayo za shetani, kwa hakika kwenu ni adui dhahiri. (2:208)

Kufanya jambo lolote lile kinyume na maamrisho na makatazo ya Allah (s.w) ndio kufuata nyayo za shetani na kumfanya shetani rafiki. Kwa maana pana, Shetani ni yejote yule au chochote kile kinachokushawishi kuvunja maamrisho ya Allah (s.w). Kwa maana hii Mashetani si katika majini tu bali hata watu wanaweza kuwa mashetani endapo watajiingiza katika kuwapoteza watu katika njia ya Allah (s.w). Hebu tuzingatie aya ifuatayo:

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ عَدُواً شَيْطَنَ الْأَنْسِ وَالْجِنِّ يُوحِي بِعَضُّهُمْ
إِلَى بَعْضٍ زُخْرُفَ الْقَوْلِ غُرُورًا وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ مَا فَعَلُوا فَذَرْهُمْ وَمَا

 يَقْتَرُونَ

Na namna hii tumemfanyia kila Nabii maadui (na ni) mashetani katika watu na majini. Baadhi yao wanawafunulia wenziwao maneno ya kupamba-pamba ili kuwadanganya (na kuwapoteza). Na kama Mola wako angalipenda wasingalifanya hayo. Basi waache na uwongo wao. (6:112)

Katika Qur'an tunajifunza kuwa Shetani ni katika watu na majini ambao huwalaghai watu kwa maneno ya kupamba pamba ili waache kuufuata Uislamu kama ulivyoelekezwa katika Qur'an na mafundisho ya Mtume (s.a.w) na badala yake wafuate njia ya hao mashetani (matwaghuuti). Tunatahadharishwa katika Qur'an kuwa wale wasioamini Akhera watatekwa nyara na mashetani, watawafanya marafiki, watawatii na kufuata utaratibu wa maisha waliowapambia. Tunafahamishwa katika aya hizi kuwa dawa ya kumwepuka Shetani ni kufuata hukumu zote za Qur'an, yaani kuendesha maisha yote kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah. Endapo Muislamu atatokea kuteleza au kuhisi kuteleza kidogo na kutoka nje ya Qur'an na Sunnah, basi mara tu anapogundua hivyo ajikinge kwa Allah (s.w) na Shetani na arejee haraka katika njia iliyonyooka kama tunavyoelekezwa katika Qur'an:

 وَإِمَّا يَنْرَغِنَكَ مِنَ الشَّيْطَنِ نَرْزَعُ فَاسْتَعِذُ بِاللَّهِ إِنَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ

Na kama wasiwasi wa shetani ukikusumbua, basi jikinge kwa Mwenyezi Mungu. Bila shaka yeeye ndiye asikiaye na ajuaye. (7:200)

إِنَّ الَّذِينَ تَقَوَّلُوا إِذَا مَسَّهُمْ طَيْفٌ فَمِنَ الشَّيْطَنِ تَذَكَّرُوا فَإِذَا

هُمْ مُبْصِرُونَ ﴿٢١﴾

Wale wanaomuogopa (Allah) zinapowagusa pepesi za Shetani mara hukumbuka, tahamaki wamekwisha ona njia. (7:201).

وَقُلْ رَبِّ أَعُوذُ بِرَبِّكَ مِنْ هَمَزَاتِ اللَّهِيَّاطِينِ ﴿٤٧﴾
وَأَعُوذُ بِرَبِّكَ رَبِّكَ أَنْ يَحْضُرُونَ ﴿٤٨﴾

Na sema: Mola wangu! Najikinga kwako na wasiwasi wa shetani, na najikinga kwako, Mola wangu ili wasinihuudhurie. (23:97-98)

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ ﴿١﴾ مَلِكِ النَّاسِ ﴿٢﴾ إِلَهِ النَّاسِ ﴿٣﴾ مِنْ شَرِّ
الْوَسْوَاسِ الْخَنَّاسِ ﴿٤﴾ الَّذِي يُوَسْوِسُ فِي صُدُورِ النَّاسِ ﴿٥﴾ مِنَ الْجِنَّةِ
وَالنَّاسِ ﴿٦﴾

Sema: Najikinga kwa Bwana Mlezi wa watu, Mfalme wa watu, Mola wa watu, Na shari ya mwenye kutia wasiwasi mwenye kurejea nyuma. Atiaye wasiwasi nyonyoni mwa watu. (Ambaye ni) katika majini na watu. (114:1-6)

Mbinu za Sheitwaani

Allah (s.w) katika aya nyingi za Qur'an ametuzindua tena na tena kuwa shetanl ni adui yetu mkubwa kabisa na wa dhahiri hivyo tujiepusho naye na katu tusimfanye rafiki. Hila nyingi anazozitumia Shetani katika kuwapoteza watu zimetajwa katika aya zifuatazo:

وَلَقَدْ خَلَقْنَاكُمْ ثُمَّ صَوَرْنَاكُمْ ثُمَّ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةِ أُسْجِدُوا لِأَدَمَ فَسَجَدُوا

إِلَّا إِبْلِيسَ لَمْ يَكُنْ مِنَ السَّاجِدِينَ ﴿١١﴾

Na hakika tulikuumbeni kisha tukakutieni sura kisha tukawaambia Malaika: ‘Msujudieni Adam Basi wakasujudu isipokuwa Iblis hakuwa mionganoni mwa waliosujudu .. (7:11)

قَالَ مَا مَنَعَكَ أَلَا تَسْجُدَ إِذْ أَمْرَتُكَ قَالَ أَنَا خَيْرٌ مِنْهُ خَلَقْتَنِي مِنْ

نَارٍ وَخَلَقْتَهُ مِنْ طِينٍ ﴿١٢﴾ قَالَ فَاهْبِطْ مِنْهَا فَمَا يَكُونُ لَكَ أَنْ تَتَكَبَّرَ

فِيهَا فَأَخْرُجْ إِنَّكَ مِنَ الصَّدِّيقِينَ ﴿١٣﴾

(Mwenyezi Mungu) akasema: ‘Nini kllichokuzuua kumsujudia nilipokuamrisha? Akasema: ‘Mimi ni bora kuliko yeye. (Mimi) umeniumba kwa moto, naye umemuumba kwa udongo’. Akasema (Mwenyezi Mungu): basi shuka huko haikufai kufanya kiburi humo. (Haya) toka. Hakika wewe u mionganoni mwa wadhalilifu .. (7:12-13)

قَالَ أَنْظِرْنِي إِلَى يَوْمٍ يُبَعَّثُونَ ﴿١٤﴾ قَالَ إِنَّكَ مِنَ الْمُنْظَرِينَ

Akasema: ‘Nipe muda (nisife) mpaka siku watakapofufuliwa (viumbe)’ Akasema (Mwenyezi Mungu): “Utakuwa mionganoni mwa waliopewa muda (lakini si mpaka wakati huo)”. (7:14-15)

قَالَ فِيمَا آتَيْتَنِي لَقَدْنَ لَهُمْ صِرَاطُكَ الْمُسْتَقِيمَ ﴿١٥﴾ ثُمَّ لَمْ يَتَّبِعُوهُمْ مِنْ

بَيْنِ أَيْدِيهِمْ وَمِنْ خَلْفِهِمْ وَعَنْ أَيْمَانِهِمْ وَعَنْ شَمَائِيلِهِمْ وَلَا تَجِدُ أَكْثَرَهُمْ

شَكِيرِينَ

Akasema: “Kwa kuwa umenihukumia upotofu (upotevu) basi nitawakalia (waja wako) katika njia yako iliyonyooka(ili niwapoteze)”. Kisha nitawafikia kwa mbele yao na nyuma

yao na kuumeni (kuliani) kwao na kushotoni kwao, katika wao hutawakuta (hutawaona) ni wenyewe kushukuru”.(7: 16-17)

قَالَ أَخْرُجْ مِنْهَا مَدْعُوًّا مَدْحُورًا لَمَنْ تَبِعَكَ مِنْهُمْ لَأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنْكُمْ

أَجْمَعِينَ

Akasema (Mwenyezi Mungu): “Toka humo, hali ya kuwa ni mwenye kudharauliwa na mwenye kufukuzwa. Atakayekufuata mionganoni mwao, (nitamtia motoni) niijaze Jahannamu kwa nyinyi nyote..(7:18)

وَبَيْتَادُمْ أَسْكُنْ أَنْتَ وَزَوْجُكَ الْجَنَّةَ فَكُلَا مِنْ حَيْثُ شَئْتُمَا وَلَا تَقْرَبَا

هَذِهِ الشَّجَرَةِ فَتَكُونَا مِنَ الظَّالِمِينَ

(Kisha Mwenyezi Mungu akasema kumwambia nabii Adam): “Na wewe Adam! Kaa peponi pamoja na mkeo, na kuleni mnapopenda, lakini msiukaribie mti huu msije kuwa mionganoni mwa waliodhulumu (7:19)

فَوَسُوسْ لَهُمَا الشَّيْطَانُ لِيُبَيِّدِي لَهُمَا مَا وُدِرَى عَنْهُمَا مِنْ سَوْءَاتِهِمَا

وَقَالَ مَا نَهَدْكُمَا رَبُّكُمَا عَنْ هَذِهِ الشَّجَرَةِ إِلَّا أَنْ تَكُونَا مَلَكَيِّينَ

أَوْ تَكُونَا مِنَ الْخَالِدِينَ

Basi shetani naye ni yule (Iblis) aliwatia wasi wasi ili kuwadhihirishia aibu zao walizofichiwa, akasema: “Mola wenu hakukukatazeni mti huu ila (kwa sababu hii): msije kuwa Malaika au kuwa mionganoni mwa wakaao milele (wasife) .”.(7:20)

وَفَاسِمَهُمَا إِذْنِي لَكُمَا لِمَنِ الْمُصْحِّينَ

Naye akawaapia (kuwaambia): “Kwa yakini mimi ni mmoja wa watoao shauri njema kwenu”..(7:21)

فَذَلِّلُهُمَا بِغُرْوِ^{٢٢} فَلَمَّا دَآفَ الشَّجَرَةَ بَدَتْ لَهُمَا سُوءَ اتْهَمَاهَا وَطَفْقًا يَخْصِفَانِ
عَلَيْهِمَا مِنْ وَرَقِ الْجَنَّةِ وَنَادَاهُمَا رَبُّهُمَا أَلَّمْ أَنْهَكُمَا عَنْ تِلْكُمَا الشَّجَرَةِ
وَأَفْلَلَ لَكُمَا إِنَّ الشَّيْطَنَ لَكُمَا عَدُوٌّ مُبِينٌ

Basi akawateka (wote wawili) kwa khadaa (yake). Na walipouonja mti ule aibu zao ziliwadhihirikia na wakaingia kujibandika majani ya (miti ya huko) Peponi. Na Mola wao akawaita (akawaambia): “Je, sikukukatazeni mti huu na kukuambieni kwamba shetani ni adui yenu aliye dhahiri?”.(7:22)

قَالَ رَبُّنَا ظَلَمْنَا أَنفُسَنَا وَإِنْ لَمْ تَغْفِرْ لَنَا وَتَرْحَمْنَا لَنَكُونَنَّ مِنَ

الْخَسِيرِينَ

Wakasema “Mola wetu! Tumehulumu nafsi zetu; na kama hutusamehi na kuturehemu, bila shaka tutakuwa miongoni mwa wenyewe khasara (kubwa kabisa)”.(7:23)

قَالَ آهِبِطُوا بَعْضُكُمْ لِيَعْضِنْ عَدُوًّا وَلَكُمْ فِي الْأَرْضِ مُسْتَقْرٌ وَمَتَّعٌ إِلَيْ

جِينِ

Akasema (Mwenyezi Mungu) “Shukeni (katika ardhi), nyinyi kwa nyinyi ni maadui. Na makao yenu yatakuwa katika ardhi, na starehe yenu , mpaka muda (niutakao mimi mwenywewe Mwenyezi Mungu). (7:24)

قَالَ فِيهَا تَحْيَوْنَ وَفِيهَا تَمُوتُونَ وَمِنْهَا تَخْرُجُونَ

Akasema (Mwenyezi Mungu): “Mtaishi humo na mtafia humo, na mtatolewa humo” (mtafufuliwa kwenda akhera kulipwa)..(7:25)

يَدَبَّيْنَ ءَادَمَ قَدْ أَنْزَلْنَا عَلَيْكُمْ لِبَاسًا يُوَارِى سُوءَ اتِّكُمْ وَرِيشًا وَلِبَاسٍ

الْتَّقْوَى ذَلِكَ خَيْرٌ ذَلِكَ مِنْ عَائِدَتِ اللَّهِ لَعَلَّهُمْ يَذَّكَّرُونَ

(Anasema Mwenyezi Mungu kuwaambia wanaadamu tangu hao wa zamani huko): Enyi wanaadamu! Hakika tumekuteremshieni nguo zifichazo tupu zenu na nguo za pambo; na nguo za utawa (yaani kumcha Mungu) ndizo bora". Hayo ni katika ishara za (neema za) Mwenyezi Mungu ili wapate kukumbuka.(7:26)

يَدْبَيْتَ عَادَمَ لَا يَقُتِّنَنَّكُمُ الْشَّيْطَانُ كَمَا أَخْرَجَ أَبْوَيْكُمْ مِّنَ الْجَنَّةِ يَنْزَعُ
عَنْهُمَا لِبَاسَهُمَا لِيُرِيهِمَا سَوْءَاتِهِمَا إِنَّهُ وَيَرَكُمْ هُوَ وَقَبِيلُهُ وَمِنْ حَيْثُ لَا
تَرَوْنَهُمْ إِنَّا جَعَلْنَا الشَّيْطَانَ أُولَئِكَ لِلَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ

٢٧

"Enyi wanaadamu. Shetani (Iblisi) asikutieni katika matata. Kama alivyowatoa wazee wenu katika Pepo; akawavua nguo zao ili kwaonyesha tupu zao. Hakika ye ye pamoja na khabila yake wanakuoneni, na hali ya kuwa hamuwaoni". Bila shaka sisi tumewajaalia shetani kuwa marafiki kwa wale wasioamini. (7:27).

Tukizingatia aya hizi kwa makini mambo yafuatayo yanajitokeza:

Kwanza, Shetani alilaaniwa kwa sababu ya kukataa kutii amri ya Allah (s.w). Na alikataa kwa sababu alijidhani kuwa yu bora kuliko binaadam. Ubora huo aliuhusisha na kabila lake. Yaani ye ye ni jinni na viumbe wa kabila la majini wameumbwa kwa moto na viumbe wa kabila la binadamu wameumbwa kwa udongo. Moto, alihisi **iblisi**, ni bora kuliko udongo, hivyo alikataa kutii amri ya Mola wake.

Mtu kulitokuza kabila lake, au rangi yake, au nasaba yake au taifa lake na wakati huo huo kulibenza kabila, rangi, nasaba au taifa la mwenzake ni katika mwenendo wa shetani. Ni kibri kisichokuwa na msingi wowote na matokeo ya fikra hizi za kishetani yamekuwa ni chuki, bughudha na umwagaji damu usiokwisha katika dunia. Watu wengi wamedhulumiwa na wanaendelea kuteseka na hata

kuuliwa kwa sababu ya baadhi ya watu kujiona kuwa kwa asili yao wao ni bora na hivyo watumikiwe.

Shetani akishafanikiwa kupandikiza fikra hizi mionganoni mwa Waislamu basi hata kama watakuwa wengi viyi wingi wao utakuwa si hoja. Chuki, uadui na uhasama mionganoni mwao havitakwisha na katu hawatakuwa na nguvu wala umoja. Waislamu wa rangi hii watawadharau Waislamu wenzao wa rangi nyingine, au kabilia jingine au nchi nyingine.

Na kwa kutumia hizo hisia za utaifa Waislamu wa nchi moja wanaweza kuchochewa na kujikuta wanawaua Waislamu wenzao. Hivyo kila Muislamu na ajihadhari sana na mwenendo huu wa shetani wa kujiona bora kwa sababu ya rangi, kabilia, utaifa, n.k.

Pili, Shetani amepewa na Allah (s.w) muda wa kuishi hadi siku ya Kiyama.

Na katika kipindi hicho amekula kiapo kuwa atafanya kila hila ya kumpotosha binaadamu ili aonyeshe kuwa binaadamu hana utukufu wowote, na kwamba nimwasi na hana shukrani kama alivyo yeye.

Tatu, Mtu kuona aibu na haya ni katika maumbile ya binaadamu. Hisia hizi hujidhihirisha kwa mara ya kwanza mtu anapoona haya kuonesha sehemu zake za siri kwa mtu mwingine. Hivyo mbinu mojawapo ya shetani ni kuwaondolea watu haya, hadi waone ni jambo la kawaida na la maendeleo kukaa uchi hadharani na hata kufanya machafu hadharani.

Nne, Udmaifu mkubwa kuliko mwingine wowote alionao binaadamu ni ile silka yake yakutamani ngono na udhaifu huu ndio silaha kubwa anayoitumia Shetani katika kuwaangamiza. Hivyo hila ya kwanza ni ya kuwaondolea binaadamu haya na kuwashawishi watembee uchi. Hilo likishatimia jamii hiyo

itajiangamiza yenyewe kwa ufuscak utakaotokea. Ni hila hiyo ya shetani ndiyo inayowapeleke baadhi ya watu kudhani kuwa maendeleo hayawezi kupatikana sharti kwanza wanawake watupe shungi zao na hijabu. Na ili kuyaweka mawazo vizuri kabla ya kujadiliana mambo muhimu ya kitaifa baadhi ya vikao hutanguliwa na vikundi vyaa wanawake walionusu uchi wakinengua jukwaani!

Tano, Binaadamu kwa umbile lake hayuko tayari kukubali kirahisi wito wa kufanya maovu. Kwa sababu hiyo siku zote jambo hata likiwa ovu hupambwa kwa sifa nzuri na ndipo watu hulitenda. Hata kama imethhibitika kuwa pombe inaharibu afya ya mwili na akili na hivyo kuditimiza jamii, matangazo ya pombe katu hayasemi: Kunywa pombe ili uharibu haraka afya yako ya mwili na akili, bali yatasema: “Baada ya kazi ngumu burudisha mwili wako kwa pombe kadhaa ili uwe mwenye afya, nguvu na furaha tele!” Hizi ni hila za shetani.

Sita, Binaadamu kwa umbile lake pia anatamani sana kufikia daraja ya juu kuliko aliyonayo sasa, au kutamani kudumu milele. Ndiyo maana Shetani alimdaganya, Nabii Adamu (a.s) kuwa atakuwa Malaika na ataishi milele akiiasi amri ya Allah(s.w). Hila hiyo hiyo yaendelea kutuumiza hata leo kwani shetani huwarubuni watu kwa kuwafanya waamini kuwa yanayopendekezwa na shetani kama wizi, dhuluma, mauaji, riba, n.k. yatawapatia maisha ya juu ya anasa na fahari.

Saba, Binadamu anapomwasi Allah (s.w), Allah (s.w) humwumbua na kuyaweka wazi maovu yake.

Zoezi la Tano

1. “*Na ni nani asemaye kauli bora zaidi kuliko (yule) aitaye kwa Mwenyezi Mungu, na (mwenyewe), akafanya vitendo vizuri na kusema au Hakika mini ni miongoni mwa waislamu.*” (41:33)
 - (a) Toa mafunzo matatu ya msingi yatokanayo na aya hii.
 - (b) Kutokana na aya hii (41:33) nini maana ya **Da’awah ?**
 - (c) Tofautisha kutoa **Da’awah na kuwaidhi,**
2. “*Kwa yakini sisi tulizidhahirisha amri zetu na makatazo yetu, (tukaziuliza) mbingu na ardhi na milima vikakataa kuichukua (ahadi hiyo) na vikaiogopa, lakin mwanaadamu akaichukua bila shaka yeye ni dhalimu mkubwa, mjinga sana.*” (33:72)
 - (a) Bainisha amana aliyokabidhiwa mwanaadamu na mola wake.
 - (b) “Bila shaka yeye (mwanaadamu) ni dhalimu mkubwa mjinga sana”, kwa nini ?
3. *Waite (watu) katika njia ya Mola wako kwa hikima na mavidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora Hakika Mola wako ndiye anayemjua aliyepotea katika njia yake, Naye ndiye anayewajua walioongoka.* (16:125)

Toa mafunzo matano yatokanayo na aya hii.
4. Kwa kurejea Qur'an (16:125), eleza kwa muhtasari juu ya
 - (a) Hikima katika Da’awah.
 - (b) Mawaiida mema.
 - (c) Kujadiliana kwa namna iliyo bora.

5. Ili kulingania kwa hekima, jamii ya Tanzania tunaweza kuigawanya katika makundi matatu. Bainisha makundi hayo na mbinu utakazo zitumia katika kuliendea kila kundi.
6. Bainisha makundi ya maadui wa Uislamu na waislamu yaliyoainishwa katika Qur'an na bainisha mbinu zinazotumiwa na kila kundi katika kuuhujumu Uislamu na waislamu hivi leo.



Sura ya Sita

MIPANGO KATIKA HARAKATI ZA KIISLAMU

Maana ya Mipango (Planning)

Tunaweza kusema mipango ni utaratibu wa kuendea lengo husika kwa ufanisi kwa kufuata hatua baada ya hatua. Kuweka mipango ni kutengeneza njia ya kumfikisha mtu mahali anapokusudia kwenda kwa wepesi. Ukiwa njiani kuelekea uendako, waweza kupotea njia na kuelekea usikokusudia au waweza kufika mahali ukadhani umefika kumbe bado kutokana na kutokuwa na mpango wa safari.

Umuhimu wa kuweka mipango


Watalamu wa fani ya mipango wana msemo “Ikiwa unashindwa kupanga, basi unapanga kushindwa”. maana yake ni kwamba ukishindwa kuweka mipango ya jambo lolote unalokusudia kulifanya, umeamua kushindwa kufanya jambo hilo. Hekima ya msemo huu ni kuwa, iwapo utafanya mambo bila ya kuweka mipango madhubuti, waweza kupoteza nguvu bure bila ya kupata matunda tarajiwa. Lakini endapo utapanga mipango yako vyema kabla ya kujitosa katika utekelezaji, kwanza utabakia katika lengo na pili hutafuja juhudhi na nguvu zako katika mambo ambayo hayako katika mpango wako.

Kwa muhutasari tunaona kuwa kuweka mipango katika kufanya mambo yetu ni muhimu kwa sababu zifuatazo:

Kwanza, kuweka mipango hutufanya tuwe makini katika kuweka malengo. Kwa kuwa na mipango tutahakikisha kuwa tunaweka malengo yanayotekelvezek. Lengo lolote tunaloliweka ni lazima tuliweke kwenye mizani ya kiutekelezaji na tukiona halitekelezeki tunaliacha.

Pili, kuweka mipango katika mambo yetu hutuepusha na ubadhirifu wa kiasi kidogo tulichonacho cha mali na nguvu kazi inayohitajika sana katika kuendea malengo yetu. Pale ambapo hamna mipango, tunaweza kutumia nguvu kazi na mali yetu kuendea malengo ambayo siyo na kwa hiyo kutopata matunda tarajiwa.

Tatu, kuweka mipango hutupa fursa ya kutathmini utendaji wetu na kwahiylo kutuungezea ufanisi. Kuweka mipango si jambo la kufanyika mara moja na kupita bali ni hatua yenye kuendelea. Baada ya kuuweka mpango kwenye fikra na maandishi hufuatia utekelezaji, kisha tathmini ya utekelezaji huo. Tathmini hiyo hupelekeea kuweka mipango mipyä kufuatia utekelezaji wa awali. Mipango madhubuti na endelevu inaweza kuwakilishwa na mchoro ufuatao:



Nne, kwa kutoa fursa ya kutathmini utekelezaji, mipango pia inatuepusha na matatizo au makosa yanayojitekeza katika utendaji.

Tano, kuweka mipango huwafanya watu wawajibike ipasavyo. Kwa mfano, kama msikiti au taasisi ya Kiislamu

haikuweka mipango inayoonesha inataka ifikie malengo gani katika kipindi cha miaka mitano ijayo, ni wazi kuwa miaka hiyo mitano itapita bila ya kufanyika lolote na bila kuhisi vibaya kwamba hakuna mafanikio yaliyopatikana, kwani tangu hapo hapakuwa na malengo ya kufanya lolote. Lakini jaalia kwa mfano, waumini wa msikiti wa Mwanza Mabatini wanampango wa kuwa na (a) Shule safi ya awali, (b) Zahanati yenye kuendeshwa kwa maadili ya Kiislamu na (c) Mfuko wa fedha wa kuwasaidia vijana na akina mama wa Kiislamu kuanzisha biashara ndogo ndogo katika kipindi cha miaka mitano. Ni lazima viongozi na waumini watahangai kuhakikisha malengo hayo yanafikiwa. Kwa kuwa na mpango huu zitapatikana faida zifuatazo:

- (i) Waumini watakuwa na kigezo cha kupima utendaji wa viongozi wao kama wanafaa au laa.
- (ii) Waumini hawatapoteza muda wao, nguvu na mali zao katika mambo yasiyowapelekea kwenye lengo na watajua nguvu na uwezo wao kuliko kubakia kila siku katika nadharia.
- (iii) Aidha, ni katika utekelezaji wa malengo yaliyowekwa watafahamika Waislamu wa kweli (watekelezaji) na wale washabiki tu wa kupiga takbiria zisizo na utendaji.

Aina ya mipango

(1) Mipango ya muda mfupi

- Utekelezaji wake huchukua mwaka 1 -3
- Utekelezaji wake pia huchangia kufikia malengo ya mpango wa muda mrefu.

(2) Mipango ya muda mrefu:

- Utekelezaji wake huchukua zaidi ya miaka 3
- Hugawanywa katika mipango ya muda mfupi mfupi

Hatua za kufuata katika kupanga

1. Kuweka matarajio (vision) na mikakati (njia) ya kufikia matarajio hayo.
 - Matarajio ya waislamu ni kusimamisha Uislamu katika jamii
 - Muelekeo na njia tunayotakiwa tupite ni ile ya kuwaelimisha waislamu wakaijua na kuifuata Qur'an katika kila kipengele cha maisha yao kupitia:
 - Shule za awali hadi vyuo vikuu vyaa kiislamu
 - Darasa duara – kwa watu wazima
 - Darasa za watoto
 - Vitabu, magazeti, T.V. Radio
2. Kuweka malengo
 - Malengo yawe wazi – yaeleze kwa uwazi unakusudia kufanya nini ?
 - Yawe yanayopimika kwa urahisi na yawe yenye kutekelezeka.
 - Malengo yaendane na matarajio (vision).
3. Kufanya utafiti juuya "Hali halisi" na namna inavyoweza kuathiri kufikiwa kwa malengo yako. Mambo ya kuyaangalia katika utafiti huu ni:-
 - (i) Kuyatambua mambo ambayo yanaweza kukupa nguvu dhidi ya washindani wako kama vile
 - Mtandao mpana
 - Elimu ya kutosha
 - kuwa na taarifa muhimu
 - (ii) Kuzijua fursa zilizopo na namna fursa hizo zinavyo weza kuchangia katika kulifikia lengo kwa ufanisi.
 - (iii) Kuzingatia kanuni na sheria za serikali.
 - (iv) Kuijua hali ya uchumi wa nchi.

- (v) Kuzingatia teknolojia iliyopo.
4. Kuainisha mbinu zitakazo tumika
- Onesha lengo la kila kazi na mbinu zitakazo tumika kuhakikisha kuwa kazi hiyo inafanikiwa.
 - Si lazima mbinu moja katika kila kazi bali mbinu zitumike kulingana na mazingira na wakati.
5. Kuweka vigezo vyta tathmini kwa kila kazi kwa muda maalumu.
- Faida za tathmini
 - (i) Kuona kwamba tunafanikiwa kufikia malengo yetu.
 - (ii) Kung'amua makosa au mapungufu yanayotokea na kuyarekebisha.
 - Vigezo vyta tathmini visiwe vyta ujumla jumla bali ni vema viangalie mambo kwa kina

Vigezo vyta mpango madhubuti

Mpango madhubuti ni ule unaojibu kwa usahihi maswali yafuatayo:

- (i) Ni lipi lengo la mpango huu ?
- (ii) Nini umuhimu wa lengo hilo?
- (iii) Nani wahusika katika utekelezaji wa mpango huo ?
- (iv) Lengo hilo litafikiwaje ?
- (v) Lengo linatarajiwa kufikiwa lini (muda) ?
- (vi) Wapi mpango huo utafanyika (location)?
- (vii) Gharama kiasi gani itahitajika?
- (viii) Jamii ya waislamu kwa ujumla itafaidikaje?

Lengo la maswali haya ni kumuongoza mpangaji asije akafanya jambo lisilo na manufaa kwa Waislamu. Au akawa na mipango mizuri ya maendeleo lakini ikawa haitekelezeki kwa sababu hakuzingatia uwezo wa kifedha na watendaji alionao.

Tuchukulie mfano wa jumuiya ya Kiislamu ilioamua kujenga shule ya awali zahanati na kuwa na mfuko wa kuwasaidia vijana na akina mama. Tuangalie utekelezaji wa mipango hiyo kwa kujibu maswali manane.

- (1) Nini lengo la mipango hiyo:
 - (a) Shule ya awali: kuwapa watoto malezi bora ya Kiislamu.
 - (b) Zahanati: kutoa huduma za afya kwa Waislamu na watu wengine.
 - (c) Mfuko wa Misaada ya kiuchumi: kuwapa vijana na akinamama wa Kiislamu nguvu za kiuchumi ili waweze kujitegemea.
- (2) Kwanini malengo hayo ni muhimu?
Kujenga jamii yenyeye maadili ya Kiislamu na inayojitegemea kwa huduma za afya na kiuchumi.
- (3) Nani watekelezaji na watakaonufaika na mipango hiyo:
 - (a) Shule ya awali: Watoto wa Waislamu waishio jirani na shule.
 - (b) Zahanati: Waislamu na watu wengine.
 - (c) Mfuko wa misaada: Vijana na akinamama wa Kiislamu wenye kuupigania Uislamu lakini wasio na kipato cha kumudu maisha yao.

Katika kujibu swali hili, jumuiya inayohusika ni lazima pia ionyeshe watu watakaohusika kusimamia kila mradi na majukumu ya kila mmoja wao.

- (4) Vipi au malengo yatafikiwaje? Hapa ni lazima ionyeshwe mipango yote ya kiutekelezaji mfano:

Utafutaji wa kiwanja. Ukusanyaji wa fedha, ununuzi wa vifaa, upatikanaji wa wataalamu na usimamizi kwa ujumla.

Kama watu watajenga kwa kujitolea kufyatua tofali n.k. ilezwe au kama atatafutwa mkandarasi ilezwe pia na wapi fedha za kumlipa zitatoka.

- (5) Lini? Ili kufuatilia utekelezaji, ni lazima ilezwe shughuli zitaanza na kukukamilika lini. Lini shule itaanza kujengwa na lini itakamilika. Zahanati itaanza kujengwa lini na lini itaanza kufanya kazi, na lini fedha za mfuko wa misaada zitaanza kuchangwa na lini mikopo itaanza kutolewa.
- (6) Wapi – ni lazima ionyeshwe shule na zahanati zitajengwa wapi, Ardhi itapatikana wapi na taratibu zote za kumiliki zifuatwe.

Kwa upande wa mfuko wa misaada ilezwe fedha zitahifadhiwa wapi Mfano Benki ya Taifa ya biashara, Benki ya CRDB na n.k.

- (7) Kwa gharama gani? Gharama za kila mradi zionyeshwe, mfano:
 - (a) Shule – milioni 50.
 - (b) Zahanati milioni 20.
 - (c) Mfuko wa misaada milioni 30.
- (8) Nini faida ya kufanya yote haya? utapatikana msingi na mazingira mazuri ya kuusimamisha Uislamu.

Kama tulivyotaja awali, kuwa na mipango kama hii, ndiyo njia pekee ya kujua wapi watu wanaelekea na hatua waliyopiga katika maendeleo. Bila kuwa na mipango, Imamu wa Msikiti au Katibu wa Jumuiya hatajua majukumu yake. Ataamua kufanya lolote analoona linafaa kwa sababu hana dira. Aidha. Waumini nao hawatakuwa na mahali maalum pa kupeleka mali zao na nguvu

zao. Kila mmoja atafanya ajualo na awezalo. Matokeo yake ni kukosekana kwa mshikamano, kupoteza nguvu na juhudzi za bure na kukosekana kwa maendeleo kwa ujumla.

Mfano halisi ni hali ya Misikiti yetu na jumuiya zetu hivi leo. Kwa vile Misikiti haina mipango yoyote ya maendeleo, Imamu huishia kuongoza swala na maamuma kuswali na kutawanyika. Hakuna lolote linalofanyika kuwaletea maendeleo ya elimu, uchumi na afya katika eneo lao.

Kubwa linalofanyika ni kutoa mawaida na kuamsha hamasa bila ya kuweka mipango ya kutafsiri mawaida na hamasa hizo katika vitendo vya kimaendeleo. Watu wamekuwa kana kwamba wanasubiri maendeleo yao yashuke toka mbinguni au kuletwa na watu wengine.

Kisa cha kuokolewa Nabii Nuhu (a.s) na gharka pamoja na wale aliokuwa nao katika safina kina funzo kubwa juu ya mipango. Tunafahamu kuwa baada ya wale waliokufuru kukataa kabisa kuukubali ujumbe alioleta Nabii Nuhu; Mwenyezi Mungu alishaangamiza na kuwaokoa wale wachache walioamini.

..... فَنَجَّيْنَاهُ وَمَنْ مَعَهُ وِفِي الْفُلُكِ وَجَعَلْنَاهُمْ خَلَتِيفَ وَأَغْرَقْنَا^{٦٣}
..... الَّذِينَ كَذَّبُوا بِيَوْمِنَا

“... Basi tukamwokoa yeye na waliokuwa naye katika jahazi. Na tukawafanya wao ndio waliobakia ulimwenguni. Na tukawazamisha wale waliozikadhibishaaya zetu.....” (10:73)

Tunajua kwamba Mwenyezi Mungu atakapo jambo huliambia liwe na likawa.

إِنَّمَا أَمْرُهُ إِذَا أَرَادَ شَيْئاً أَنْ يَقُولَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿٤٢﴾

Hakika amri yake anapotaka chochote (kile kitokee) ni kukiambia: “Kuwa”; basi mara moja huwa. (36:82)

Kwa ukweli huo Mwenyezi Mungu angeweza kutoa amri ya gharika iwaangamize wale waovu na kwa Rehema zake, waongofu wasalie bila kupata taabu ya kutengeneza Jahazi. Lakini tukisoma katika Qur-an (11:37-41) tunaona jinsi Mwenyezi Mungu alivyoweka mpango (plan) ya kuwaokoa walioamini na baadhi ya viumbe ili uhai uendelee baada ya gharika. Mwenyezi Mungu katika hatua ya awali alimwambia Nuhu:

﴿ وَقَالَ أَرْكَبُوْا فِيهَا بِسْمِ اللّٰهِ مَجْرِهَا وَمُرْسِلَهَا إِنَّ رَبِّي لَغَفُورٌ ﴾

رَحِيمٌ

Na unda jahazi mbele ya macho yetu na (iwe sawa) na amri yetu.

Wala usiniseemeze kuwasamehe wale waliodhulamu nafsi zao.

Kwa yakini wao watazamishwa. (11:37)

Ilipofika siku ya gharika; Mwenyezi Mungu aliamrisha ardhi itowe maji kisha akamwamrisha Nabii Nuhu (a.s) awapakie jahazini waliopata Nusura yake:

حَتَّىٰ إِذَا جَاءَ أَمْرُنَا وَفَارَ الشَّنُورُ فُلِّنَا أَحْمَلُ فِيهَا مِنْ كُلِّ زَوْجٍ يَنْ أَشْنَىٰ
وَأَهْلَكَ إِلَّا مَنْ سَبَقَ عَلَيْهِ الْفَوْلُ وَمَنْ ءَامَنَ وَمَا ءَامَنَ مَعَهُ إِلَّا قَلِيلٌ

Hata ilipofika amri yetu, ardhi ikaanza kufoka maji tulimwambia: “Pakia humo (jahazini) jozi moja katika kila (wanyama); jike na dume, na (wapakie) watu wako wa nyumbani kwako isipokuwa wale ambao imewapitia hukumu (ya Mwenyezi Mungu). Na wachukue wote walioamini”. (11:40)

﴿ وَقَالَ أَرْكَبُوْا فِيهَا بِسْمِ اللّٰهِ مَجْرِهَا وَمُرْسِلَهَا إِنَّ رَبِّي لَغَفُورٌ ﴾

رَحِيمٌ

Na akasema (Nuhu): “pandeni humo kwa jina la Mwenyezi Mungu kuwe kwenda kwake na kusimama kwake. Hakika Mola wangu ni msamehevu na mrehemevu. (11:41)

Ukichunguza kisa hiki Mwenyezi Mungu aliweka mpango madhubuti wa kuwaokoa waja wake wema pindi atakapoleta gharika ili uhai uendelee. Pengine tutathmini mpango huu kwa mujibu wa vigezo vyta mpango madhubuti au kwa kujibu yale maswali manane:

- (1) Nini ulikuwa mpango wa Mwenyezi Mungu?

Jibu: Kuwasafirisha viumbe teule na waumini mahali pa salama.

- (2) Kwanini zoezi hilo lilikuwa muhimu?

Jibu: Ili maisha yaweze kuendelea baada ya mafuriko.

- (3) Nani walikuwa walengwa?

Jibu: Nabii Nuhu (a.s), waumini na baadhi ya wanyama (viumbe).

- (4) Vipi lengo hilo litafikiwa?

Jibu: Usafiri wa majini kwa kutumia safina.

- (5) Lini?

Jibu: Mwanzo wa mafuriko mpaka mwisho wa mafuriko.

- (6) Wapi?

Jibu: Mashariki ya kati katika mji alioishi Nabii Nuhu na watu wake.

- (7) Kwa gharama ya kiasi gani?

Jibu: Nuhu na waumini walijitolea kuchonga jahazi.

- (8) Faida gani itapatikana baada ya zoezi hilo?

Jibu: Ardhi itakuwa na viumbe hai tena baada ya gharika na waumini watamuabudu Mola wao ipasavyo katika kila kipengele cha maisha yaani watasimamisha ukhalifa katika ardhi.

Kama tulivyosema awali; Mwenyezi Mungu akitaka jambo huliambia tu liwe na likawa. Lakini katika tukio hili anaandaa mpango wa kuwaokoa watu wema kwa kumwamuru Nabii Nuhu aunde jahazi. Hapana shaka kuwa lipo fundisho kubwa kwetu Waislamu.

Kama tunalalamika kuwa hatuna elimu, kama tunalalamika kuwa hatuna hospitali, kama tunalalamika kuwa hali yetu kiuchumi na kisiasa ni mbaya; matatizo yote haya hayawezi kuondoka kwa kulalamika tu au kwa kuomba dua tu. Yataondoka tu kwa sisi wenyewe kuweka mipango madhubuti inayoteklezeka, na kujitolea kwa hali na mali kuitekeleza. Bila mipango, bila utendaji na bila ya kujitolea na kushikamana katika kujenga na kuendesha taasisi za sekta mbali mbali za maendeleo, tusitarajie kupiga hatua mbele kutokana na hali yetu duni ya sasa.

Mipango ya Kistratejia (Strategic Planning)

Mipango ya kistratejia (strategic plans) ni ile mipango inayopelekea kufikia lengo kuu ambayo hujiбу maswali matatu yafuatayo:

Tuko wapi? Tunakusudia kwenda wapi? Tutafikaje huko?

Mtu anayepanga mambo yake kwa mbinu, huangalia kule anakokwenda kisha akaanza kutafakari kinyumenyume jinsi ya kufika. Kwa hiyo kila mbinu au mpango atakaouweka anahakikisha kuwa unamsogeza hatua fulani katika kuliendea lengo kuu.

Lengo kuu la Waislamu ni **kuusimamisha Uislamu** wao na wenyewe **kuwa Makhalifa** katika jamii. Waislamu wanalahimika kuweka malengo na mipango mbali mbali katika kuliendea lengo kuu.

Kwa mfano mipango ya Kistratejia kwa Waislamu wa Tanzania sasa ni kuwaelimisha Waislamu ili (a) Waujue Uislamu kwamba ndio mfumo pekee sahihi wa maisha wanaopaswa kuufuata. (b) Kujua hadhi yao kama Makhalifa wa Allah (s.w) hapa ardhini. (c) Waweze kujenga na kuendesha taasisi muhimu za Kiislamu, kusimamia elimu, uchumi, maadili na masuala mbali mbali ya kijamii. (d) Waweze kushikamana na kuwa tayari kujitoa muhangaa kuupigania Uislamu kwa mali na nafsi zao.

Kwa kuwa na mpango wa Kistratejia Waislamu wanatakiwa:

Kwanza kushikamana wote katika kuendea mpango huo. Hata kama itakuwepo tofauti ndogo ndogo mionganini mwao au mionganini mwa jumuiya na taasisi zao, wasiruhusu vivunje mshikamano wao katika kuendea lengo hili.

Pili, wasipoteze rasilimali zao ikiwa ni akili zao, nguvu zao na mali zao katika jambo lisilowapeleka katika mpango huu wa Kistratejia.

Tatu, wasikubali kutolewa katika agenda yao. Mara nyingi maadui wamekuwa wakiwachezea Waislamu kwa kuwaletaa agenda ambazo zinawashughulisha badala ya kutizama mipango yao. Kwa mfano wanaweza kuja na agenda ya kuwa na Kadhi, Waislamu wakapoteza muda kulumbana juu ya umuhimu wa kuwa na Kadhi na nani awe Kadhi. Inapotokea jambo kama hilo, Waislamu wanatakiwa wajiuilize je, linawasaidiaje kukamilika kwa mpango wao wa kistratejia. Kama haliwasaidii lolote, waliache kama lilivyo na waunde kikundi cha watu wachache kulishughulikia, huku nguvu kubwa ikiendelea na mpango uliopo.

Nne, wawe tayari kusamehe au kutoa sadaka baadhi ya haki, maslahi na fursa zao kwa ajili ya manufaa makubwa ya lengo lao la kistratejia.

Mkataba wa Hudaibiya unatoa ufanuzi na mafunzo makubwa juu ya nukta hizi.

Mkataba wa Hudaibiya

(Dhul-Qa'dah 6, A.H/March 628)

Tangu kuingia kwake Madinah, Mtume (s.a.w) na Masahaba wake hawakupata amani angalau kwa mfululizo wa miezi michache. Wakati mwengine ilikuwa hapana mwezi unaopita bila ya kuwa katika mapigano ya vita na maadui wa Uislamu.

Kukosekana kwa amani ilikuwa ni kikwazo kikubwa sana kwa kazi ya kuufikisha ujumbe wa Uislamu kwa watu. Katika mwezi wa Dhul-Qa'dah 6 A.H. akiwa na Waislamu 1400 Mtume (s.a.w) alifunga safari kuelekea Makkah kufanya U'mrah.

Maquraish walipopata habari waliweka vizuizi katika njia zote za kuingilia Makkah kumzuia Mtume (s.a.w) na masahaba wasipenye kuingia Makkah. Mtume alilazimika kupiga kambi sehemu iitwayo Hudaibiya.

Baada ya mjadala mrefu baina ya Waislamu na Maquraish, pande zote mbili ziliafikiana kuweka mkataba wa amani wa miaka kumi wenye masharti yafuatayo:

- (1) Waislamu watarudi Madinah bila kufanya Umrah.
- (2) Waislamu wanaweza kurudi mwakani (7:A.H.) kufanya Umrah lakini wakae siku tatu.
- (3) Wakija Makkah, wasije na silaha ila panga zikiwa ndani ya ala.
- (4) Waislamu hawataenda nao Madinah Waislamu wanaoishi Makkah na wala hawatamzuia ye yeyote mionganoni mwao anayetaka kubakia Makkah.
- (5) Kama ye yeyote atatoroka kwenda Madinah kusilimu, Waislamu hawana budi kumrudisha (wasimpokee) lakini ye yeyote kutoka Madinah akitoroka kwenda Makkah Maquraish watampokea.

- (6) Makabila ya Waarabu yatakuwa huru kufanya itifaki (urafiki) na upande wowote ule yanayoupendelea.
- (7) Pasiwe na vita kwa kipindi cha miaka 10 baina ya Waislamu na Maquraish na baina ya washirika (Allies) wa Waislamu na washirika wa Maquraish.
- (8) Hapana ruhusa ya kutengua hata shuruti moja katika hizi kabla ya miaka 10 kupita.

Kwa ujumla Waislamu hawakufurahishwa na baadhi ya masharti ya mkataba hasa sharti la tano (5). Waliona kuwa wamedhalilishwa na kuonewa.

Aidha Maquraish walionesha tabia ya dharau kwa Mtume (s.a.w), walikataa asitajwe kama Mtume wa Mwenyezi Mungu bali, itajwe kuwa ni mkataba baina ya Muhammad bin Abdillahi na Maquraish (waliwakilishwa na Suhail bin ‘Amr). Si hivyo tu, bali kabla hata mkataba haujatiwa sahihi alitokea Abu Jandal bin Suhail bin ‘Amr akakimbilia kwa Waislamu. Yeye alisilimu Makka na sasa anakimbia mteso. Suhail alimkamata na kumcharaza bakora kisha kumrudisha Makkah akaendelee kuteswa. Waislamu walimhurumia na kuomba asihusishwe na kifungu cha tano (5) cha mkataba lakini Suhail alikataa vinginevyo mkataba wa amani uvunjike. Mtume (s.a.w) alimsihi Abu Jandal afanye subira na arudi Makkah.

Amani iliyopatikana baada ya mkataba wa Hudaibiya ilirahisisha maingiliano kati ya makafiri wa Makkah na Waislamu wa Madina. Kabla ya mkataba, Waislamu wa Madina na makafiri wa Makkah walikuwa na uhasama mkubwa. Hapakuwa na maingiliano ya kidugu wala kirafiki. Lakini baada ya mkataba huo watu wa Makkah walizuru Madinah kwa ajili ya biashara na kuwatemebelea ndugu zao. Katika maingiliano haya Maqraysh walipata fursa ya kushuhudia ubora wa maisha ya jamii ya Kiislamu na walivutiwa sana na tabia na maadili ya Waislamu. Pia

waislamu wa Madina walikuwa huru kutembelea Makka na kufanya Da'awah. Maingiliano haya yalipelekea watu wengi sana kusilimu wakiwemo majemedari wa Kiquraish, Khalid bin Walid na Amr al-'As na Suhail bin Amri(aliye saini mkataba)

Kwa upande mwingine hali ya amani ilimpa fursa Mtume (s.a.w) kulingania Uislamu kwa watu wa karibu na wa mbali. Ni katika kipindi hiki Mtume (s.a.w) alituma wajumbe kwa watu mbali mbali wakiwemo watawala na wafalme. Matokeo ya kazi hiyo ni watu wengi sana kusilimu hata ikabidi baadaye Maquraish wavunje mkataba.

Baada ya maelezo hayo, hebu tujiulize maswali yafuatayo:

- (1) Nini lilikuwa lengo kuu la Waislamu?
- (2) Nini ulikuwa mpango au jambo la kistratejia kwao kwa wakati ule?

Lengo kuu lilikuwa kusimamisha Uislamu

Jambo muhimu(strategic Issue) walilokuwa nalo Waislamu ilikuwa ni kuufikisha ujumbe wa Uislamu kwa watu. Lakini hali ya vita na uhasama ilikwamisha kazi hiyo. Kwa hiyo ili mpango huu wa kistratejia wa kufikisha Uislamu kwa watu ufanikiwe, ilibidi Waislamu wanunue amani kwa gharama yoyote. Ndio ukaona Mtume (s.a.w) hakujali kutokutajwa yeye katika mkataba kama Mtume. Aidha alikubali kifungu cha tano cha mkataba japo kilionekana kuwadhalilisha Waislamu na akawa tayari kuacha Abu Jandal arudishwe Makkah.

Asingekuwa Mtume (s.a.w) anaangalia na kupanga mambo yake kistratejia angeng'ang'ania mkataba umtaje kama Mtume wa Allah au kufutwa kwa kipengele cha 5 ambapo maafikiano yasingefikiwa. Lakini kwa kuangalia mbali alikuwa tayari kusamehe au kutoa muhanga baadhi ya mambo kwa ajili ya faida kubwa zaidi.

Tumeeleza awali kuwa Mtume (s.a.w) aliondoka Madinah kwenda Makkah kufanya Umra, lakini Maquraish wakamzuia. Kufanya Umra japo ni Ibada lakini haikuwa ndio jambo la kistratejia la kuufanya Uislamu usimame, kwa kujua hilo Mtume (s.a.w) alikuwa tayari kujikosa Umra hiyo lakini ajenge mazingira ya kumwezesha kuufikisha ujumbe wa Uislamu kwa watu.

Je, ni wangapi mionganoni mwetu, wenyewe mtizamo huo? Hatufarikiani katika Misikiti na taasisi kwa tofauti ndogo tu ambazo tangu hapo hazina msaada wowote katika kulifiki lengo? Jumuiya ngapi zimesambaratika kutohana na migogoro isiyokuwa na msingi?

Uoni na Mwelekeo (Vision na Direction)

Katika kuweka mipango, ni lazima kwanza mtu ajue analolenga kufikia na njia anayokusudia kupita. Tunakolenga Waislamu ni kusimamisha Uislamu katika jamii. Mwelekeo na njia tunayopita ni ile ya kuwaelimisha Waislamu wakaijua na kuifuata Qur-an katika kila kipengele cha maisha yao. Darasa za Misikitini zinazoratibiwa vizuri, madrasa za watoto na watu Wazima, shule za msingi na sekondari za Kiislamu, uchapishaji na usambazaji wa vitabu na kadhalika ni katika njia za kutupeleka tunakokusudia kufika. Aidha programu kama kuandaa miadhara, semina, itikafu, na kuanzisha taasisi za Kiislamu za kushughulikia mambo mbali mbali ni mionganoni pia mwa njia za kuendea kwenye lengo.

Kuwa na uoni huu ni muhimu kwani wakati mwengine watu waweza kufanikiwa kuwa na vitu kama shule safi za watoto (Chekechea) au sekondari za Kiislamu wakidhani ndio wamefika. Akili zao na juhudhi zao zote zikaishia kuziangalia shule hizo, wasiwe na mpango mwengine wa kusonga mbele. Au watu waweza kuwa na utaratuibu wao mzuri wa kutoa miadhara, kuendesha Itikafu na kadhalika wakaona imetosha. Na madhali hawazuiliwi na mamlaka yoyote kufanya shughuli hizo wakatosheka, bila kufikiria kwamba:

- Baada ya kutoa ujumbe kwenye muhadhara nini kifuate.
- Baada ya mja kukandamiza nafsi yake akaweza kukaa Itikafu, afanye nini baada ya hapo.
- Baada ya Muislamu kuzitekeleza Ibada maalumu kama Swala, Funga, Zakka na Hijja, afanye nini tena katika maeneo mengine kama uchumi, huduma za jamii, siasa na kadhalika.

Kwa kutokujua wanakolenga na kwa kukosa mwelekeo, Waislamu wengi wamekuwa wakipoteza muda na rasilimali zao katika mambo ambayo hayawaletei maendeleo yoyote. Aidha, wengine wamekuwa wakitosheka na Ibada ndogo ndogo wanazofanya bila ya kujua kuwa ipo kazi kubwa inayowangojea ya **kusimamisha Uislamu** katika jamii.

Zoezi la Sita

1. (a) “*Ukiwa unashindwa kupanga, basi umepanga kushindwa*”.
-
- Fafanua msemo huu.
(b) Toa sababu tano(5) za msingi, kwa nini ni muhimu kuweka mipango katika mchakato wa kuendea Harakati za kiislamu.
2. (a) Ainisha vigezo vyta mpango madhubuti.
(b) Kwa kutumia vigezo vyta mpango madhubuti onesha kuwa:
 - (i) Nabii Yusufu (a.s) kuwa kiongozi Misr ni mpango madhubuti wa Allah(s.w)
 - (ii) Nabii Musa (a.s) kuwakomboa Bani Israil kutokana na makucha na Firauni ni mpango madhubuti wa Allah(s.w).
 - (iii) Safari ya Hijrah ya Mtume(s.a.w) na Abubakar Swiddiq(r.a) ni mpango madhubuti.
3. Bainisha mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa mpango.
4. (a) Ni upi mpango wa kistratejia?
(b) Ainisha lengo kuu la waislamu na ainisha mipango ya kistratejia itakayowawezesha waislamu kufikia lengo hilo katika miaka ishirini na tatu(23) ijayo.



Sura ya Saba

UONGOZI BORA KATIKA HARAKATI ZA KIISLAMU

Nani Kiongozi ?

Kiongozi ni yule anayewaelekeza watu kuendea lengo husika bila ya kutumia nguvu au yule anayewatoa watu pahala na kuwafikisha pahala pengine panapotarajiwa na wote bila ya kutumia nguvu. Katika mchakato wa uongozi, kiongozi bora **huelekeza, hufafanua na huhamasisha** watu waongoze kuendea njia sahihi itakayowafikisha pahali tarajiwa.

Nani mtawala ?

Mtawala ni yule anayetumia nguvu kuwatoa watu pahali na kuwapeleka anakotaka yeche kwa manufaa yake au ya kikundi kidogo cha watawala wenzake.

Dhana ya uongozi kwa mtazamo wa Uislamu.

Katika Uislamu, kila muislamu anawajibika kuwa kiongozi:

- (i) Kila muislamu anawajibika kuwa Da'iyah ambaye analazimika kujua namna ya kumuongoza mtu mmoja mmoja,familia, taasisi, n.k.
- (ii)Mtume (s.a.w) ameweka bayana kuwa kila muislamu ni kiongozi kwa mujibu wa Hadith ifuatayo:

"Abdullah bin Umar(r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "kila mmoja ni mchunga(kiongozi) na kila mmoja ataulizwa juu ya wale aliowaongoza. Imamu (kiongozi wa jamii) ni mchunga wa watu anaowangoza na ataulizwa juu ya yao,mwanaumume ni kiongozi wa familia yake na ataulizwa juu ya watu wa familia yake. Mwanamke ni malikia wa nyumba ya mume wake na watoto na ataulizwa juu ya vitu hivyo. Sikilizeni! Hakika

kila mmoja ni mchunga (kiongozi) na ataulizwa juu ya wale aliwachunga (aliowaongoza) (Bukhari na Muslimu).

- (iii) Kila muumini anawajibika kuwa khalifa wa Allah(s.w) katika jamii.

..... وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلَائِكَةِ إِنِّي جَاعِلٌ فِي الْأَرْضِ خَلِيفَةً

"Wakumbushe wakati Mola wako alipowaambia Malaika ,nitaleta katika ardhi Khalifa" (2:30)

- Khalifa ni yule anayeongoza katika ardhi kwa niaba ya Allah(s.w) au yule anayesimamisha sharia za Allah(s.w) katika kukiendea kila kipengele cha maisha ya kibinafsi na ya kijamii.

Aina za Uongozi

Kuna aina mbili kuu za uongozi kwa mujibu wa Qur-an:

اللَّهُ وَلِيُّ الَّذِينَ آمَنُوا يُخْرِجُهُم مِّنَ الظُّلْمَاتِ إِلَى النُّورِ وَالَّذِينَ كَفَرُوا أُولَئِكَ أَعْذُّهُمُ الظُّلْفُوتُ يُخْرِجُونَهُم مِّنَ النُّورِ إِلَى الظُّلْمَاتِ أُولَئِكَ أَصْحَابُ الشَّارِطِ هُمْ فِيهَا خَلِيلُونَ

"Allah ni kiongozi wa walioamini, huwatoa katika giza na kuwaingiza katika nuru.Lakini waliokufuru viongozi wao ni Matwaghut. Huwatoa katika nuru na kuwaingiza katika giza. Hao ndio watu wa Motoni, humo watakaa milele." (2:257)

Kutokana na ujumbe wa aya hii, tunajifunza kuwa pamoja na mifumo mingi ya Uongozi, kuna aina kuu za Uongozi:

- (i) Uongozi wa Allah (s.w).
(ii) Uongozi wa Twaghut.

Uongozi wa Allah (s.w)

Allah (s.w) huwaongoza waumini kupitia vitabu vyake pamoja na kauli na matendo ya Mitume wake.

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلًا إِلَيْكُمْ بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنْزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ
لِيَقُولُوا إِنَّا نَنْهَاكُمْ بِالْقِسْطٍ وَأَنَّا أَنْزَلْنَا الْحَدِيدَ فِيهِ بَأْسٌ شَدِيدٌ وَمَنْفِعٌ لِلنَّاسِ
وَلَيَعْلَمَ اللَّهُ مَنْ يَنْصُرُ وَرَسُولُهُ وَالْغَيْبُ إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ

٢٥

“Kwa hakika Tuliwapeleka Mitume wetu kwa dalili wazi wazi na Tukaviteremsha vitabu na uadilifu pamoja nao, ili watu wasimamie uadilifu...” (57:25)

Uongozi wa Allah (s.w) huwatoa watu kutoka kwenye maisha ya ukafiri na ushirikina yaliyozingirwa na maovu ya namna mbali mbali na dhuluma (**maisha ya giza**) na kuwapeleka kwenye maisha ya uadilifu ambapo kila mtu hupata haki yake. Haya ndiyo maisha ya Uislamu ambayo yamezingirwa na furaha na amani. Haya ndiyo **maisha ya Nuru**.

Uongozi wa Kiislamu unaofuata mwongozo wa Allah (s.w) huvielekeza vipawa, nguvu, mali na muda wa waumini vitumike katika kumuaudu Allah (s.w) katika nyanja zote za maisha ndani ya saa 24 kwa lengo la kuwanufaisha viumbwe wote. Hili ndilo kusudio kuu la uongozi wa Kiislamu ambalo Allah (s.w) analibainisha kwa kumfahamisha Mtume (s.a.w).

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِلْعَالَمِينَ

“Na hatukukutuma ila uwe Rehema kwa viumbwe vyote. (21:107)

Uongozi wa Twaghuti

Uongozi wa Kitwaghuti hupatikana katika mifumo ya maisha au dini zilizobuniwa na watu. Uongozi wa Kitwaghuti msingi wake hasa ni maoni na mapendekezo ya watu wanaokanusha kuwepo kwa Allah (s.w) na Siku ya Malipo.

Uongozi wa Kitwaghuti husimamia batili na dhulma na matokeo yake ni kuenea ujisadi katika ardhi. Uongozi wa kitwaghuti hufanya ujisadi huku ukijitangaza kuwa unasimamia amani, usalama na maendeleo ya watu. Tabia hii ya uongozi wa Kitwaghuti Allah (s.w) anaiweka wazi katika aya zifuatazo:

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ لَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ قَالُوا إِنَّمَا نَحْنُ مُصْلِحُونَ
﴿١﴾
أَلَا إِنَّهُمْ هُمُ الْمُفْسِدُونَ وَلَكِنْ لَا يَشْعُرُونَ
﴿٢﴾

*Na wanapoambiwa: "Msifanye uharibisu ulimwenguni" Husema
"Sisi ni watengezaji." (2:11)*

أَلَا إِنَّهُمْ هُمُ الْمُفْسِدُونَ وَلَكِنْ لَا يَشْعُرُونَ
﴿٣﴾

Hakika wao ndio waharibisu, lakini hawatambui. (2:12)

Sifa za kiongozi wa kiislamu

Katika Uislamu kiongozi hachaguliwi kwa kufanya kampeni ya kuomba kura kwa mujibu wa Hadith zifuatazo:

"Abdul-Rahmaan bin Sanurah(r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: usiombe uongozi kwa sababu utakapo pewa uongozi kwa kuomba utaachiwa peke yako jukumu la uongozi, na kama umepewa bila kuomba utasaidiwa katika uongozi huo."
(Bukhari na Muslim)

Katika Hadith nyingine aliyosimulia Abu Mussa, Mtume (s.a.w) amesema:-

"Hatumchagui kwenye uongozi huu yejote anayeomba wala hachaguliwi yule aliyemroho wa uongozi". (Bukhari na Muslim)

Katika Uislamu mtu huwa kiongozi kwa kuchaguliwa na watu na kubebeshwa jukumu hili kwa ajili ya Allah:

"*Abu Hurairah amesema Mtume wa Allh amesema: utawaona watu hawapendi kabisa kazi ya uongozi mpaka uchaguzi utakapo waangukia (kwa kubebeshwa)". (Bukhari na Muslim)*

Sifa za msingi za kiongozi wa kiislamu

Zifuatazo ni sifa za msingi za kiongozi wa kiislamu

(i) Aliyebora kuliko waumini wengine, yaani aliyezidi kwa Ucha-Mungu

يَتَأْكُلُهَا النَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَاكُمْ مِنْ ذَكَرٍ وَأُنْثَى وَجَعَلْنَاكُمْ شُعُوبًا وَفَبَأَيْلَلَ
..... لِتَعَارِفُوا إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَنْتُنَّكُمْ

"Enyi watu! Hakika tumekuumbeni (nyote) kwa yule mwanamumeme(mmoja; Adamu) na (yule) mwanamke (mmoja; Hawwa). Na tumekufanyeni mataifa na makabila (mbalimbali) ili mjuane (tu basi; siyo mkejeliane). Hakika ahishimiwaye sana mionganoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule amchaye Mungu zaidi katika nyinyi....." (49:13)

(ii) Aliye bora katika wacha-mungu ni yule aliye zidi kwa elimu

إِنَّمَا يَخْشَى اللَّهَ مِنْ عِبَادِهِ الْعَالَمُتُؤْمِنُوْا

"..... kwa hakika wanomugopa Mwenyezi Mungu mionganoni mwa waja wake ni wale wataalamu(35:28)

يَرْفَعُ اللَّهُ الْأَذْلِينَ ءَامِنُوا مِنْكُمْ وَالْأَذْلِينَ
..... أُوْثُوا الْعِلْمَ دَرَجَاتٍ

"..... Mwenyezi Mungu atawainua wale walioamini mionganoni mwenu, na waliopewa elimu watapata daraja zaidi....." (58:11)

.....إِنَّ اللَّهَ قَدْ بَعَثَ لَكُمْ طَالُوتَ مَلِكًا قَالُوا أَتَيْ كُوْنُ لَهُ
 الْمُلْكُ عَلَيْنَا وَنَحْنُ أَحَقُّ بِالْمُلْكِ مِنْهُ وَلَمْ يُؤْتَ سَعَةً مِنَ الْمَالِ قَالَ إِنَّ اللَّهَ
 أَصْطَفَهُ عَلَيْكُمْ وَرَادَهُ بِسُطْنَةٍ فِي الْعِلْمِ وَالْجِسْمِ وَاللَّهُ يُؤْتِنِي مُلْكُهُ وَمَنْ
 يَشَاءُ وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلَيْهِمْ

"..... Mwenyezi Mungu amemchagua(Twalut) juu yenu na
 amemzidishia wasaa wa elimu na kiwiliwili. Na Mwenyezi Mungu
 humpa usfalme wake amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni mwenye
 wasaa mwenye kujua ". (2:247)

(iii)Mwenye afya(siha) nzuri - Rejea Qur'an (2:247)

(iv)Mwenye tabia njema kuliko wengine

"Abu Hurairah ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) amesema Mwenye
 imani iliyopea katika waislamu ni yule mwenye tabia njema,na
 aliyembora katika nyinyi ni yule anayemtendea wema
 mkewe"(Tirmith)

Sifa za ziada za kiongozi bora ni hizi zifuatazo

(v) Huruma

Kiongozi awe mnyenyeketu,mpole,mwenye huruma ambaye
 huwahurumia wale anaowaongoza na mwenye kuwapendelea lile
 analolipendelea nafsi yake. Kiongozi anatakiwa daima kuwa yeye
 ni mtumishi wa wale waliomuweka katika uongozi, awaheshimu
 kama mtumishi anavyomuheshimu bwana wake. Wakati huo huo,
 kiongozi anatakiwa ajiweke katika nafasi ya ulezi ambayo hana
 budi kuwahurumia wale anaowalea. Kiongzi wa Kiislamu daima
 anatakiwa azingatie usia wa Allah (s.w) ufuatao:

وَهُوَ الَّذِي جَعَلَكُمْ خَلَّيْفَ الْأَرْضِ وَرَفَعَ بَعْضَكُمْ فَوْقَ بَعْضٍ فَرَحِبْتُ
تَبْلُوْكُمْ فِي مَا ءاَتَيْتُكُمْ إِنَّ رَبّكَ سَرِيعُ الْعِقَابِ وَإِنَّهُ وَلَغُورٌ رَّحِيمٌ

Naye ndiye aliyekujaalieni kuwa Makhaliqa (viongozi) katika ardhi. Na amewanyanya baadhi yenu juu ya wengine daraja kubwa kubwa ili akufanyieni mtihani kwa hayo aliyokupeni. Hakika Mola wako ni mwepesi wa kuhisabu na hakika yeye ni mwinci wa kusamehe, mwinci wa kurehemu. (6:165)

Kutokana na aya hii tunajifunza kuwa kiongozi anatakiwa mara zote afahamu kuwa wadhifa wa uongozi alionao ni mtihani kwake. Allah (s.w) amemuinua daraja na kumfanya kiongozi juu ya wengine ili kumfanya mtihani kuwa atashukuru neema hiyo aliyyotunukiwa na Mola wake kwa kutekeleza wajibu wake ipasavyo na kuchunga mipaka ya Allah (s.w) katika kazi hiyo au atakufuru ajipe uungu kwa kuchupa mipaka ya Allah na kuwageuza watumwa wake wale waliomchagua na kumfanya kiongozi wao. Kiongozi anatakiwa awe msaada na rehema kwa wale anaowaongoza na wala asiwe mzigo na tatizo kwa raia zake hao. Mtume (s.a.w) kila alipowachagua sahaba zake kuwa viongozi wa sehemu mbali mbali daima alikuwa akiwausia kuwa watu wa msaada na wenye huruma na upole kwa ria zao.

(vi) *Uadilifu*

Kiongozi wa Kiislamu anatakiwa awe muadilifu. Kipimo cha kiongozi mzuri ni uadilifu. Kiongozi wa Kiislamu akiwa muadilifu huwa Khalifa wa Allah (s.w) na akiwa si muadilifu huwa Khalifa wa Shetani. Uadilifu unasisitizwa mno katika Qur-an kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

..... ﴿ إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُ بِالْعُدْلِ ..﴾

Kwa hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha uadilifu..... (16:90)

Kiongozi muadilifu ni yule anayechunga haki za watu anaowaongoza. Yeye ni mchunga na mgawaji wa haki. Hana budi kuhakikisha kuwa yeye mwenyewe hachukui haki zake mpaka ahakikishe kuwa kila mtu amepata haki yake. Mtume (s.a.w) aliwaamuru wale aliowapa kazi ya uongozi wasivae kivazi kizuri zaidi kuliko watu wengine, wasifunge milango yao wakati watu wanawahitajia haki zao au wanataka kutoa madukuduku yao.

Kiongozi wa Kiislamu anatakiwa awe muaminifu na mkweli na asithubutu kujilimbikizia mali kwa kutumia madaraka yake ya uongozi. Amir au kiongozi wa juu wa Serikali ya Kiislamu anatakiwa achukue mshahara au posho kutoka kwenye mfuko wa serikali (Baitul-Mali) kiasi kile tu kinachotosheleza mahitaji muhimu ya chakula, mavazi na makazi kwa yeye mwenyewe na familia yake. Kiongozi wa Kiislamu anatakiwa akumbuke daima kuwa uongozi katika Uislamu si kitega uchumi kama ulivyo uongozi wa Kitwaghuti. Mtume Muhammad (s.a.w) ambaye ndiye kiongozi wa Ummah huu wa mwisho na kiigizo chetu kwa mwenendo na uongozi wake bora, aliishi maisha rahisi.

Abu bakar (r.a) aliyechaguliwa kushika uongozi wa Umma wa Kiislamu mara baada ya kutawafu Mtume (s.a.w), alifuata nyayo za Mtume (s.a.w) kwa kila kitu. Maisha yake yalikuwa rahisi mno. Umar (r.a) aliyechaguliwa kuwa kiongozi wa serikali ya Kiislamu baada ya Abu Bakar alifuata vyema nyayo za Mtume (s.a.w) na Abu Bakar. Pamoja na kuwa Umar alikuwa kiongozi wa dola kubwa ya Kiislamu iliyoenea mashariki ya kati yote na kupanuka hadi Spain, aliishi maisha rahisi sana. Umar (r.a) alikuwa na kawaida ya kuzunguka usiku ili kujua matatizo ya watu wake.

Kinyume chake viongozi wa Kitwaghuti, huchukua madaraka ya uongozi wanayopewa na jamii zao kama kitega uchumi chao kwa ajili ya kujinufaisha wao binafsi. Huifuja watakavyo na humpa

yejote wamtakaye kwa upendeleo mali ya jamii ambayo imepatikana kwa kukung'uta mifuko ya masikini. Muda mfupi baada ya kiongozi wa Kitwaghuti kukabidhiwa madaraka ya uongozi wa ngazi ya juu katika jamii, utamuona ana gari zuri jipya ana nyumba nzuri mpya na mabadiliko ya kila namna katika matumizi yake ya kimaisha pamoja na familia yake. Kama mambo yenye ni haya, kwa nini watu wengine katika jamii ya Kitwaghuti wasiupupie uongozi kwa hali na mali au kwa kufa na kupona? Kwa nini mtu aliyeonja uongozi katika serikali ya Kitwaghuti asing'ang'anie kubakia humo kwa gharama yoyote ile? Kwa nini mapinduzi ya mara kwa mara na mauaji yasitegemewe katika jamii za Kitwaghuti ambapo watu wanashindania uongozi kwa lengo la kujinufaisha wao binafsi na familia zao? Haya yote ni matunda machungu yanayotarajiwa katika jamii kutokana na uongozi uliokosa uadilifu.

Kiongozi muadilifu hana budi kuhakikisha kuwa wanyonge katika jamii wanapata haki zao na wenye mali wanatoa haki za wanyonge. Abu Bakar, katika khutuba yake ya kwanza baada ya kuchaguliwa kuwa Khalifa wa kwanza wa Mtume (s.a.w) alisisitiza:

“Mnyonge mionganini mwenu ni mwenye nguvu katika uongozi wangu mpaka apate haki zake; na mwenye nguvu mionganini mwenu atakuwa dhaifu katika uongozi wangu, mpaka akipenda Allah nichukue haki za watu anazodaiwa.....”³

Vile vile ni katika uadilifu kwa kiongozi kuhakikisha kuwa kila mtu mkosaji anahukumiwa kwa mujibu wa sharia bila ya upendeleo au uonevu wowote. Kiongozi hatamchelea yejote katika kuitisha hukumu. Katika Uislamu watu wote ni sawa mbele ya sharia na hakuna aliye juu ya sharia hata akiwa Amir (Rais) wa nchi.

(Prof: Shibli Muman al-Farooq - The life of
Omar the Great uk.61)

(vii) *Subira*

Kiongozi katika dola ya Kiislamu anatakiwa awe mwenye subira, mvumilivu na mstahimilivu. Kiongozi atekelze wajibu wake ipasavyo na asitarajie kupendwa na kufurahiwa na watu wote. Waumini wa kweli tu ndio watakaomfurahia na kumsaidia atakapowaongoza kwa mujibu wa Qur-an na Sunnah. Lakini wanafiki, wenyewe husuda, wapenda vyeo na sifa na maadui wote wa Uislamu hawawezi kamwe kumfurahia kiongozi wa Kiislamu muadilifu. Kiongozi wa Kiislamu hana budi kukumbuka kuwa anafanya kazi ile ile ya Mtume (s.a.w). Arejee historia ajikumbushe maudhi na vitimbi vya kila namna alivyofanyiwa Mtume wa Allah na makafiri wa Makkah na Mayahudi na Wanafiki wa Madina. Kisha katika uongozi wake anapokumbana na matatizo ya kutukanwa, kusingiziwa, kupuuzwa n.k. ajiulize: “Je haya yaliyonifika yanaweza kulinganishwa na yale yaliyomfika Mtume wa Allah” Pia kiongozi wa Kiislamu anayejithadi kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Qur-an na Sunnah, hana budi kukumbuka kuwa malipo ya kazi yake yapo kwa Allah (s.w) na ndiye pekee anayewajibika kumuogopa na kutaka radhi yake.

(viii) *Uoni wa mbali*

Kiongozi ni lazima awe na mtazamo wa mbali, ajue anakoipelea jamii ya Waislamu na aweze kubuni program za kuifikisha jamii huko. Hapa tunakusudia kuwa kiongozi wa Kiislamu awe na lengo la kusimamisha Uislamu katika jamii au ajue namna ya kulifikia lengo hilo. Hii ni pamoja na kuweza kutambua vikwazo na hatari zilizo mbele yao na kubuni mbinu na program za kukabiliana nazo.

(ix) *Uwezo wa Kubuni Mipango*

Kiongozi wa Kiislamu awe na uwezo wa kubuni mipango inayotekelzeza na mbinu bora za kufikia yale anayoyaona mbele.

(x) *Uwezo wa Kuunganisha Nguvu Kazi*

Kiongozi wa Kiislamu anatakiwa awe na uwezo wa kuunganisha nguvu kazi na yale yote yanayohitajika kufanikisha

mipango yenyе kуupelekeea kufikia lengo kuu la kusimamisha Uislamu katika jamii.

(xi) *Utegemezi kwa Allah (s.w)*

Kiongozi na wale anaowaongoza wawe na tabia ya kumtanguliza Allah (s.w) kwa kila walifanyalo kwa kumtegemea ye ye na kuchunga maamrisho na makatazo yake.

(xii) *Msimamo katika Kuendea Lengo*

Kiongozi wa Kiislamu anatakiwa awe na msimamo thabiti katika kuendea lengo na wala asisukumwe na maslahi binafsi iwe ya vitu au sifa. Kiongozi asiyeyumbishwa na maslahi binafsi hujijenеa mazingira ya kuaminika hivyo kupata watu wengi zaidi kwa kushiriki katika kazi ya Da'awah.

(xiii) *Mwenye kuzingatia maelekezo ya Shura*

Ni muhimu kwa kiongozi wa Kiislamu kuzingatia maelekezo ya shura katika uongozi wake. Asimamie utekelezaji wa maamuzi ya shura na pale maamuzi hayo yatakapokuwa hayatekelezeki, ayarudishe kwenye shura.

(xiv) *Mwenye Kujiamini*

Kiongozi wa Kiislamu anatakiwa awe na uwezo wa kujenga mazingira ambayo yatamruhusu kila mtu kutoa mawazo yake kwa uhuru. Hili haliwezi kupatikana iwapo kiongozi hajiamini. Kiongozi atajiamini iwapo atadumu katika Ucha-Mungu na uadilifu.

(xv) *Uwezo wa Kuainisha Matatizo na Kuyatafutia Ufumbuzi*

Kiongozi ni lazima awe na uwezo wa kutambua matatizo yanayoikabili jamii yake. Hili ni muhimu kwa sababu kulitambua tatizo ni hatua muhimu sana katika kuendea utatuvi wake. Hatua hii huanza kwa kulifafanua tatizo. Katika kuainisha tatizo ni

lazima kwanza kujiuliza. Ni jambo gani limetokea na lisilo la kawaida? Hali ya kawaida au inayokubalika ilitakiwa iweje na kilichobadilika nini?

Ni vizuri tatizo liainishwe vizuri kabla ya kufanya juhudii yoyote ya kulitatu. Vinginevyo yawezekana hatua zitakazochukuliwa zisisaidie kitu. Kwa upande mwingine, iwapo hatua hii itafanyika vizuri, huenda mengi yadhaniwayo ni matatizo yakasawazika.

Katika hatua hii ni muhimu vile vile kuyaweka matatizo katika daraja mbali mbali kutegemeana na uzito wa hasara au athari zake. Kutohana na fursa na uwezo uliopo, tatizo lenye athari kubwa lianze kushughulikiwa. Lakini pia ni muhimu kuangalia gharama na madhara yanayoandamana na ufumbuzi utakaotolewa.

Juhudi na uangalifu ufanywe kuchagua hatua ambazo pamoa na unaafuu wake katika gharama, hazina athari mbaya kwa programu nyingine au jamii kwa ujumla. Muhimu hapa ni kwamba, kupatikana kwa ufumbuzi wa tatizo moja, kusijezalisha mengine na pengine makubwa zaidi.

(xvi) *Mwenye Kujali Muda*

Kiongozi wa Kiislamu anatakiwa awe anajali matumizi ya muda wake. Kila sekunde aitumie kwenye mambo yenyewe manufaa kibinafsi na kijamii.

(xvii) *Mwenye Kulenga Matokeo*

Muislamu hafanyi mambo mradi tu anafanya. Kila analolifanya lazima awe na matarajio fulani. Hivyo kiongozi lazima awe mdadisi juu ya yale anayolenga. Kabla hajafanya lazima ajiulize; tunataka kupata nini na je inawezekana? Nini matokeo, gharama na udhaifu wake?

(xviii) *Mwenye kutegemea umadhubuti wa mtu na kuepa mapungufu na udhaifu wake*

Kiongozi aliye bora hujaribu kadiri ya uwezo wake kuwalea watu na kuenda nao ili kila mmoja atoe mchango wake kulingana na uwezo wake. Na katika kwenda nao huwanasihi na kuhakikisha kuwa udhaifu wa kila mmoja wao hauwi kikwazo kwa shughuli za Da'awah.

(xix) *Mwenye kukamata mambo machache muhimu na kudumu nayo katika utekelezaji*

Kiongozi bora ni yule anayechagua mambo machache muhimu ya msingi na kudumu nayo katika utekelezaji. Mambo muhimu anayoyachagua ni yale ya kistratejia (strategical) ambayo yatatupa msingi na njia ya kuendea lengo kuu la kusimamisha Uislamu katika jamii.

Zoezi la Saba

1. (a) Tofautisha kiongozi na mtawala
(b) Ni upi mtazamo wa Uislamu juu ya dhana ya kiongozi?
 2. Kwa kurejea Qur'an ainisha aina kuu mbili za uongozi hapa ulimwenguni.
 3. (a) Kwa kurejea Qur'an, bainisha sifa kuu nne za msingi za kiongozi wa kiislamu.
(b) Pamoja na sifa hizo za msingi zilizobainisha katika swali la3(a), chambua sifa zingine kumi (10) za ziada anazostahiki kuwa nazo kiongozi bora wa Kiislamu.
-

Sura ya Nane

MWONGOZO WA KUJIFUNZA NA KUUJUA UISLAMU KWA WEPESI

Utangulizi:

Kutafuta **Elimu sahihi ya Mwongozo** (Maarifa ya Uislamu) ni jambo lenye thamani kubwa lisilo na mfano wa kulinganishwa. **Elimu sahihi ya Mwongozo** ni ile elimu inayomuwezesha mtu kumjua Mola wake vilivyo na kumuabudu inavyostahiki katika kila kipengele cha maisha yake ya kibinagsi na kijamii na kumpa ari na hamasa ya kuutawalisha Uislamu katika jamii.

Elimu sahihi ya Mwongozo ilioingizwa kwenye utekelezaji ndiyopekee inayomuwezesha binaadamu kupata radhi za Allah (s.w) na kuishi kwa furaha ya milele huko akhera.

Kutokuwa na elimu sahihi ya Mwongozo ni sababu tosha ya kumfanya mtu aghadhibikiwe na Mola wake na kuishi maisha ya khofu na huzuni hapa duniani na kustahiki adhabu kali huko akhera.

Kuuja Uislamu sahihi na kuutekeleza ni **jambo jepesi** kama Allah (s.w) anavyosisitiza:

..... وَمَا جَعَلَ عَلَيْكُمْ فِي الدِّينِ مِنْ حَرَجٍ مُّلِّهَ أَبِيكُمْ إِبْرَاهِيمَ
..... *Wala Hakuweka juu yenu mambo mazito katika dini. (Nayo Dini hii) ni Mila ya baba yenu Ibrahimu... ”* (22:78)



وَنُيَسِّرُكَ لِلْيُسْرَى

“Nasi tutakusahalishia Dini iliyo nyepesi” (87:8).

Kutokana na aya hizi, Uislamu ni mwepesi kuujua kwa anayetaka kuujua na pia ni mwepesi kuutekeleza kwa kuwa ni dini nayolandana na maumbile binaadamu:

فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلَّذِينَ حَنِيفُا فَطَرَ اللَّهُ الَّتِي فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَا لَا تَبْدِيلَ
لِخَلْقِ اللَّهِ ذَلِكَ الَّذِينَ أَقْرَئُوا النَّاسَ لَا يَعْلَمُونَ

“Basi uelekeze uso wako katika Dini iliyo sawasawa – ndilo umbile Mwenyezi Mungu alilowaumbia watu: (yaani Dini hii ya Kiislamu inawafikiana barabara na umbo la binaadamu). Hakuna mabadiliko katika maumbile ya viumbe vya Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo Dini iliyo haki, lakini watu wengi hawajui” (30:30).

Yapo mambo kadhaa yakizingatiwa yatamuwezesha Muislamu kuujua Uislamu kwa usahihi na kuutekeleza kwa wepesi. Baadhi ya mazingatio hayo ni haya yafuatayo:

- (i) Kujiwekea ratiba ya kujisomea Maarifa ya Uislamu.
- (ii) Kusoma kwa lengo kwa kufuata Mtaala.
- (iii) Kusoma kwa njia ya mjadala (Darasa Duara).
- (iv) Kujiunga na Elimu ya Kiislamu kwa Posta(E.K.P)
- (v) Kusoma Qur'an kwa mazingatio.

Kuweka ratiba ya kujisomea.

Watu kwa kujua thamani ya **elimu ya mazingira** huipinda katika kuitafuta, hutoa gharama kubwa na kutumia muda mwingi. **Elimu ya Mwongozo** ambayo ndiyo dira ya maisha ya binaadamu ya hapa duniani na akhera inapaswa iwe na thamani kubwa zaidi kwani elimu ya mazingira bila ya kufuata mwongozo wa Allah (s.w) huangamiza badala ya kunufaisha.

Pamoja na ukweli huu Waislamu waliowengi hufanya jitihada ndogo sana katika kujifunza Uislamu na mara nyingi hawapati nafasi kabisa. Kwa kujua thamani ya kusoma elimu ya mwongozo kwa ajili ya Allah (s.w) hatunabudi kusoma kwa

nidhamu na kujiwekea ratiba ya kila siku kwa kuzingatia yafuatayo:

1) Katika siku Muislamu ajiwekee saa moja hadi mbili za kujisomea Maarifa ya Uislamu.

Wakati mzuri wa kujisomea ni baada ya kazi – baada ya swala ya Alasiri hadi Magharibi. Wakati mwingine mzuri wa kujisomea na kufanya Ibada nyingine uliosisitizwa katika Qur'an na Hadith za Mtume (s.a.w) ni theluthi ya mwisho ya usiku kati ya saa 8 na saa 11 alfajiri kwa kuwa katika muda huo kuna utulivu mkubwa kama Allah (s.w) anavyo tuarifu:-

إِنَّ تَائِيْنَةَ الْيَوْمِ هِيَ أَشَدُّ وَطْأَةً وَأَقْوَمُ قِيَالًا ﴿١﴾ إِنَّ لَكَ فِي النَّهَارِ سَبْعًا
طَوِيلًا ﴿٢﴾

"Hakika kuamka usiku (na kufanya Ibada) kunawafikiana zaidi na moyo na maneno yanatuwa zaidi. Hakika mchana una shughuli nyingi" (73:6-7).

Jambo muhimu kwa mwenye kuamka usiku kwa ajili ya kujisomea na kufanya Ibada nyingine ni kulala mapema mara tu baada ya swala ya Ishai.

2) Kujitahidi kujiepusha na lagh-wi.

Lagh-wi ni shughuli au jambo lolote lile lisilo mpelekeea au linalomsahaaulisha mja kuendea lengo la kuumbwa kwake na kusimamisha Uislamu katika jamii. Wenye akili ni wale wanaobakia na dhikri (kumzingatia) Allah (s.w)muda wote wa saa 24:

إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَآخْتِيلِ الْيَلِ وَالنَّهَارِ
 لَآيَاتٍ لِّأُولَئِكَ الْأَذَّيْبِ ﴿١٩١﴾ الَّذِينَ يَذْكُرُونَ اللَّهَ
 قِيَمًا وَقُعُودًا وَعَلَى جُنُوبِهِمْ وَيَتَفَكَّرُونَ فِي خَلْقِ السَّمَاوَاتِ
 وَالْأَرْضِ رَبَّنَا مَا خَلَقْتَ هَذَا بَطِّلًا شَبَحْتَنَا فَقِنَا عَذَابَ النَّارِ ﴿١٩٢﴾

“Hakika kuumbwa mbingu na ardhi na mfauatano wa usiku na
 mchana ziko hoja (za kuonyesha kuwapo Mwenyezi Mungu
 Mmoja) kwa wenyewe akili”. “Ambao humkumbuka Mwenyezi
 Mungu wakiwa wima na wakikaa na wakilala. Na huzingatia
 umbo la mbingu na ardhi (kisha wakasema) Mola wetu
 Hukuviumba hivi bure , utukufu ni wako basi tuepusha na
 adhabu ya Moto ” (3:190-191)

Miongoni mwa sifa kuu za Waumini ni kujiepusha na lagh-wi.

قُدُّ أَفْلَحَ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١﴾ الَّذِينَ هُمْ فِي صَلَاتِهِمْ حَشِّعُونَ ﴿٢﴾ وَالَّذِينَ هُمْ
 عَنِ الْلُّغُوِ مُعْرِضُونَ ﴿٣﴾

“Hakika wamefuzu waumini. Ambao katika Swala zao huwa ni
 wanyenyekemu. Na ambao hujiepusha na mambo ya upuuzi (lagh-
 wi)” (23:1-3).

Pia miongoni mwa sifa za waja wa Rahmani ni pamoja:

وَالَّذِينَ لَا يَشَهِّدُونَ الرُّزُورَ وَإِذَا مَرُوا بِاللَّغْوِ مَرُوا إِكْرَاماً ﴿٧٧﴾

“Na wale ambao hawashuhudii shahada za uwongo, na
 wanapopita penye upuuzi (lagh-wi) hupita kwa heshima (yao)”
 (25:72).

Kujisomea kwa lengo kwa kufuata mtaala.

Lengo kuu la kusoma **Maarifa ya Uislamu** liwe ni
 kumuwezesha msomaji amjue Mola wake vilivyo na amuabudu

inavyostahiki katika kukiendea kila kipengele cha maisha yake ya kibinafsi na ya kijamii na kumuwezesha kusimamisha Uislamu katika jamii. Ili kufikia lengo hili hatunabudi:

- 1) Kuusoma Uislamu kama mfumo wa maisha unaohusiana na maisha ya mtu binafsi, familia na jamii kwa ujumla.Yaani Muislamu anatakiwa awe na maarifa na ujuzi utakao muwezesha kuishi Kiislamu kama mtu binafsi, kama mwanafamilia na kama mwana jamii.
- 2) Kufuata minhaji/mtaala utakaotuwezesha kuufuata Uislamu wote – Qur'an (2:208), ulioandaliwa kwa kuzingatia mwongozo wa Qur'an na Sunnah na mazingira ya jamii husika.Kwa hapa Tanzania tuna Mihutasari ya Maarifa ya Uislamu kuanzia ngazi ya Elimu ya awali hadi Vyuo vya Ualimu na Vyuo Vikuu.Pia tuna muhutasari wa "darasa la watu wazima" unao wakilishwa na juzuu saba (7).
- 3) Kusoma kila mada ya Muhtasari kwa lengo la kuiingiza katika utendaji ikiwa ni pamoja ya kuifikisha(kuifundisha) kwa wengine.

Kusoma kwa njia ya Mjadala (darasa duara).

Baada ya kila mtu kujisomea mwenyewe ni vema ajumuike na wenzake katika Darasa Duara.Darasa Duara linaendeshwa kwa mtindo wa semina ambapo kuna mchokoza mada kisha wanasemina/wanadarasa wote hupata fursa ya kutoa michango yao fikra juu ya mada ilijojadiliwa au kuuliza maswali ili kupata kuielewa vizuri mada.Baada ya mada kueleweka vizuri wanadarasa hupitisha maazimio ya utekelezaji kisha uongozi wa darasa hufuutilia utekelezaji wa maazimio hayo.Katika darasa linalofuatia jambo la kwanza, kabla ya kuanza mada mpya, ni kutathmini utekelezaji wa maazimio ya darasa lililopita. Ni vyema darasa duara lifanyike angalau mara moja kwa wiki kwa muda usiopungua saa tatu.

Kujiunga na Elimu ya Kiislamu kwa Posta (E.K.P).

Elimu ya Kiislamu kwa Posta (Elimu ya Masafa – Distance Learning) ni mfumo wa kujifunza Maarifa ya Uislamu, ambapo mwalimu yuko mbali na mwanafunzi na huwasiliana kwa njia ya Posta, Simu, Mtandao n.k. Kwa Tanzania, E.K.P inaendeshwa bure na Islamic Propagation Centre (I.P.C). E.K.P. inaendeshwa kwa kufuata Muhtasari wa “**Darasa za Watu Wazima**” unaowasilishwa na Juzu (Vitabu) saba zifuatazo:

- Juzu 1: Lengo la Maisha ya Mwanadamu.
- Juzu 2: Nguzo za Uislamu.
- Juzu 3: Qur'an na Sunnah.
- Juzu 4: Familia ya Kiislamu.
- Juzu 5: Jamii ya Kiislamu.
- Juzu 6: Historia ya Kuhuisha Uislamu.
- Juzu 7: Kuhuisha Uislamu katika Jamii.

Malengo ya ujumla ya E.K.P. ni haya yafuatayo:

- (a) Kuwawezesha wasomaji kuusimamisha Uislamu katika jamii na kuutekeleza vivilyo katika kila kipengele cha maisha yao.
- (b) kuwaandaa wanafunzi wa Sekondari kwa Mtihani wa kidato cha nne (4) (CSEE) wa Somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu hasa wale wasiopata fursa ya kufikiwa na walimu wa somo hili.
- (c) kuwaandaa walinganiaji wa Uislamu na walimu wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu kwa shule za msingi na sekondari.

Utaratibu wa kujiunga na mafunzo haya ni kujaza fomu maalumu ambayo imeeleza mambo yote muhimu yanayohusiana na mafunzo.

Kusoma Qur'an kwa Mazingatio.

Kusoma Qur'an kwa mazingatio ni faradhi ya tatu aliyopewa Mtume (s.a.w) (na kwahiyo Waislamu wote) baada ya faradhi ya kusoma kwa ajili ya Allah(s.w) na kisimamo cha Usiku (Qiyamullayl).

يَتَأْتِيهَا الْمُرْرِيلُ ① فَمِنْ الْأَلْيَلِ إِلَّا قَلِيلًا ② نِصْفَهُ ۝ أَوْ أَنْقُضُ مِنْهُ قَلِيلًا ۝
أَوْ زِدْ عَلَيْهِ وَرَتِيلٌ الْفُرْعَانَ تَرْتِيلًا ۝

“Ewe ulijejifunika maguo! Simama usiku (kucha kufanya ibada); ilu muda mdogo (tu hivi). Nusu yake au ipunguze kidogo. Au izidishe – na soma Qur'an viliyvo” (73:1-4).

Kusoma Qur'an kwa mazingatio ni kusoma Qur'an kwa kuzingatia ujumbe utokanao kwa lengo la kuutekeleza vilivyo katika maisha ya kila siku. Wale wanaosoma aya za Qur'an bila ya kuzizingatia na kuziingiza katika utendaji Allah (s.w) anawalinganisha na punda (Qur'an (62:5)); mbwa (Qur'an (7:175-176)) na wanyama kwa ujumla (Qur'an: 7:179). Kinyume chake, Allah (s.w) anawapenda wale ambao wanaposoma au kukumbushwa aya za Qur'an, hawaziangukii kwa uziwi na upofu (Qur'an: 25:73). Pia mionganoni mwa sifa za waumini ni wale ambao wanaposomewa aya za Allah huwazidishia Imani(Qur'an8:2-4) Kwa muhtasari ili tuweze kuongozwa na Qur'an pamoja na kuzingatia hukumu za usomaji hatunabudi kufanya yafuatayo:

- (a) Kuwa na yakini kuwa Qur'an ni ujumbe usio na shaka kutoka kwa Allah (s.w) (Qur'an 2:2).
- (b) Kuisoma kwa mazingatio na kujitahidi kupata ujumbe unaotokana na kila aya.
- (c) Ili kupata ujumbe wa kila aya au kila Sura ya Qur'an ni wajibu wetu kusoma tafsiri na sherehe za wanazuoni mbali mbali walijitahidi kutafsiri Qur'an katika lugha tunayoimudu. Qur'an imetafsiriwa katika lugha mbali mbali zikiwepo Kiswahili na Kiingereza.

- (d) Baada ya kupata kwa uwazi ujumbe wa Qur'an hatuna budi kuyaingiza maagizo ya Mola wetu katika utendaji huku tukimfanya Mtume (s.a.w) kiigizo chetu.
- (e) Kuisoma Qur'an mara kwa mara kuanzia mwanzo (Suratul Fatha) hadi mwisho (Suratul An-Naas) na msomaji awe na kalamu na daftari ya kuandika kila analoona ni muhimu au geni linalotaka kudhibitiwa – Hata Mtume (s.a.w) alisomewa Qur'an (4:41), akaiona kama ngeni kwake.
- (f) Tunaposoma Qur'an, tudhibiti kila tunachokipitia. Kama vile sifa zote ambazo kila mtu anataka asifike nazo. Na vile kuzidhibiti sifa zote ambazo anatakiwa mtu ajiepushe nazo. Tunaposoma Qur'an tudhibiti mambo ambayo Qur'an inasema kuwa kwa mambo hayo ndio kunapatikana mafanikio, na kwamambo hayo mengine ndio kunapatikana kuharibikiwa (maangamizo).
- (h) Tuwe na tabia ya kuirejea Qur'an kila tunapokabiliwa na tatizo lolote la kibinagsi au la kijamii.

Tusiridhike kujifanyia au kufuata mkumbo katika kuendea mambo yetu ya kibinagsi au ya kijamii bila ya kuangalia kwanza Allah (s.w) kasema nini au kaagiza nini juu ya jambo hilo au Mtume wake (s.a.w) ambaye ndiye Mfasiri Mkuu wa Qur'an, ameliendeaje jambo hilo huku tukizingatia usia wa Mtume (s.a.w) alioutoa mwezi 9 Dhul-Haj, 10A.H katika uwanja wa Arafa pale alipokuwa anawaaga Waislamu na kusema:

"Nimekuachieni vitu viwili ambavyo mkishikamana navyo hamtapotea abadan; navyo ni Kitabu cha Allah (Al-Qur'an) na Sunnah ya Mtume Wake".

Zoezi la Nane

1. (a) Ni ipi elimu sahihi ?
(b) Tofautisha na kufananisha **elimu ya mwongozo** na
elimu ya mazingira
2. Kwa kurejea Qur'an onesha kuwa elimu ya mwongozo ni nyepesi kuliko waislamu wengi wanavyoidhania.
3. Kama Da'ee(mlinganiaji) waelekeze wageni katika Uislamu (waliosilimu)namna watakavyo jifunza na kuutekeleza Uislamu kwa wepesi.
4. Eeleza ni vipi utaiendea Qur'an kwa lengo la kuifanya mwongozo wa maisha yako ya kila siku.



Sura ya Tisa

MBINU ZA KUFUNDISHA UISLAMU KWA LENGO LA KUMUANDAA KHALIFA.

Utangulizi:

Elimu ya **mwongozo** na ya **mazingira** imeambatanishwa na jukumu la mwanaadamu la kusimamisha Ukhilifa katika ardhi. Tunajifunza katika Qur'an kuwa kabla Allah (s.w) hajamuumba binaadamu aliwatangazia Malaika kusudio lake la kuleta Khalifa katika ardhi.

وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلَائِكَةِ إِنِّي جَاعِلٌ فِي الْأَرْضِ خَلِيفَةً
فَالْأُولُوُّ أَتَجْعَلُ فِيهَا مَنْ يُفْسِدُ فِيهَا وَيَسْفِكُ الدِّمَاءَ وَنَحْنُ نُسْبِعُ
بِحَمْدِكَ وَنُقَدِّسُ لَكَ قَالَ إِنِّي أَعْلَمُ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢٣﴾

"(Wakumbushe watu khabari hii;) Wakati Mola wako alipowaambia Malaika: "Mimi nitaleta katika ardhi." (Nao ndio wanaadamu). Wakasema (Malaika): "Utaweka humo watakaofanya uharibifu humo na kumwaga damu, hali sisi tunakututkuza kwa sifa Zako na kukutaja kwa utakatifu Wako?" Akasema (Mwenyezi Mungu): "Hakika Mimi nayajua msiyoyajua" (2:30).

Kwa mujibu wa aya hii Malaika walipatwa na wasiwasi/mashaka kuwa hapana kiumbe atakaye stahiki cheo hicho cha Ukhilifa isipokuwa wao. Allah (s.w) aliwatoa Malaika wasiwasi na kuwahakikishia kuwa Binaadamu anaweza kuwa Khalifa kwa nyenzo ya elimu na kuwa wao hawanauwezo wa kuwa Makhalifa:-

وَعَلِمَ عَادَمُ الْأَسْمَاءَ كُلُّهَا ثُمَّ عَرَضَهُمْ عَلَى الْمَلَائِكَةَ فَقَالَ أَنْبِيُونِي بِاسْمَيْهِمْ هَوْلَاءِ إِنْ كُنْتُمْ صَدِيقِينَ ﴿٢﴾ قَالُوا سُبْحَنَكَ لَا يَعْلَمُ لَنَا إِلَّا مَا عَمِلْنَا إِنَّكَ أَنْتَ الْعَلِيمُ الْحَكِيمُ ﴿٣﴾ قَالَ يَعْلَمُ أَنْبِيَاهُمْ بِاسْمَاهُمْ فَلَمَّا أَنْبَاهُمْ بِاسْمَاهُمْ قَالَ اللَّمْ أَقْلُ لَكُمْ إِنِّي أَعْلَمُ غَيْبُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَأَعْلَمُ مَا تُبَدِّدُونَ وَمَا كُنْتُمْ تَكْثُمُونَ ﴿٤﴾ وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةَ أَسْجُدُوا إِلَّا فَسَجَدُوا إِلَّا إِلِيلِيسْ أَبْنِي

Na (Mwenyezi Mungu) akamfundisha (Nabii) Adam majina ya vitu vyote, kisha Akaviweka mbele ya Malaika, na Akasema (kuwaambia Malaika): “Niambieni majina ya vitu hivi ikiwa mnasema kweli (kuwa nyinyi ndio wajuzi wa mambo)”. Wakasema (Malaika): “Utakatifu ni Wako! Hatuna ilimu isipokuwa ile Ulyotufundisha; bila shaka Wewe ndiye Mjuzi na ndiye Mwenye hikima.” Akasema (Mwenyezi Mungu): “Ewe Adam! Waambie majina yake”. Alipowaambia majina yake alisema (Mwenyezi Mungu): “Sikukwambieni kwamba Mimi ninajua siri za mbinguni na za ardhi; tena najua mnayoyadhihirisha na mliyokuwa mnayaficha?” Na (wakumbushe watu khabari hii): Tulipowaambia Malaika: “Msujidieni Adam;” (yaani mwadhimisheni kwa ile ilimu yake aliyopewa). Wakamsujidia wote isipokuwa Iblis, akakataa na akajivuna; na (tokea hapo) alikuwa katika makafiri” (2:31-34).

Mbinu za kumuandaa Khalifa

Zipo mbinu kadhaa za kuwaandaa wanafunzi Waislamu wainukie kuwa Makhalifa wa Allah (s.w) (watawala wa jamii kwa niaba ya Allah (s.w)). Baadhi ya mbinu hizo ni hizi zifuatazo:

- (i) Kuliweka bayana lengo la Elimu.
- (ii) Kutumia lugha nyepesi inayofahamika kwa mwanafunzi.
- (iii) Kufafanua somo/mada kwa Aya na Hadith.
- (iv) Kutoa na kutumia mifano na vielelezo vya Kiislamu.
- (v) Kuleta Mazingatio ya Allah (s.w) kupitia mada mbali mbali za elimu ya mazingira.
- (vi) Kukosoa nadharia potofu.

(i) Kuliweka Bayana Lengo la Elimu.

Mwalimu kabla hajaanza kufundisha somo lake ni muhimu kwanza awaweke sawa wanafunzi wake juu ya nafasi na lengo la elimu katika Uislamu. Ukizingatia historia iliyobainishwa katika Qur'an elimu imechukua nafasi mbili zifuatazo:

(1) Takrima ya kwanza aliyotunukiwa binaadamu na Mola wake.

Neema ya kwanza aliyotunukiwa Adam (a.s) baada tu ya kuumbwa kwake ni kuelimishwa na Mola wake.

..... وَعَلِمَ عَادَمَ الْأَسْمَاءَ كُلَّهَا

“Na Mwenyezi Mungu akamfundisha Adam Majina ya vitu vyote ...” (2:30).

“**Majina ya vitu vyote**” katika aya hii inaashiria fani zote za **elimu ya mazingira** ambazo anahitajia mwanaadamu hapa ulimwenguni. Kisha Adam (a.s) na mkewe Hawwah waliposhushwa kuanza maisha ya Ukhilifa hapa duniani waliahidiwa **elimu ya Mwongozo**.

..... قُلْنَا أَهْبِطُوا مِنْهَا جَمِيعًا فَإِمَّا يَأْتِيَنَّكُمْ مِّنْ هُدًى فَمَنْ تَبِعَ هُدًى إِلَيَّ فَلَا
خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْرُجُونَ ﴿٢٨﴾

Tukasema; “Shukeni humo nyote; na kama ukikufikieni uwongozi utokao Kwangu, basi watakaofuata uwongozi Wangu huo haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika” (2:38).

(2) Amri ya kwanza aliyopewa Mtume (s.a.w) na kwahiyo watu wote wa **Ummah** wake ni kutafuta Elimu:-

..... أَقْرَأْ بِاسْمِ رَبِّكَ الَّذِي خَلَقَ ① خَلَقَ الْإِنْسَانَ مِنْ عَلْقٍ ② أَقْرَأْ وَرَبِّكَ
الْأَكْرَمُ ③ الَّذِي عَلَمَ بِالْقَلْمَنِ ④ عَلَمَ الْإِنْسَانَ مَا لَمْ يَعْلَمُ

“Soma kwa jina la Mola wako aliyumba. Ambaye amemuumba mwanaadamu kwa ‘Alaq (kitu chenye kuning’inia). Soma na Mola wako ni karimu sana. Ambaye amemfundisha (mwanaadamu) kwa kalamu amemfundisha mwanaadamu (chungu ya) mambo aliyokuwa hayajui” (96:1-5).

Kwa mujibu wa aya hii **“kusoma kwa jina la Mola”** ina maana ya kusoma kwa lengo la kutafuta radhi za Allah (s.w) au kwa lengo la kumuabudu Allah (s.w) ipasavyo na kusimamisha Ukhilifa katika jamii. Amri ya kujielimisha inahusu Elimu ya Mazingira (majina ya vitu vyote) na Elimu ya Mwongozo (Maarifa ya Uislamu). Elimu sahihi ni ile iliyosomwa “kwa jina la Mola”, iwe ni ya Mazingira au Maarifa ya Uislamu. Elimu yoyote itakayosomwa si kwa jina la Mola haitakuwa sahihi hata ikiwa ni Maarifa ya Uislamu kama tunavyojifunza katika Hadith:

*“Abu Hurairah amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) amesema:
‘Anayetafuta elimu isiyokuwa kwa ajili ya kutafuta radhi za Allah
(s.w), hasomi kwa lengo lolote lile ila la kupata maslahi ya hapa
duniani tu. Hivyo siku ya kiyama hatapata hata harufu ya pepo’.
(Ahmad, Abu Daud, Ibn Majah).*

Elimu iliyosomwa kwa lengo lake imepewa nafasi ya kwanza kwa sababu:

- (1) Ndiyo pekee inayomuwezesha mwanaadamu kumjua Mola wake viliyvo na kumuabudu inavyostahiki na kwahiyo kufikia lengo la kuumbwa - Qur'an (51:56).
- (2) Ndiyo nyenzo pekee ya kuwainua waumini daraja, Qur'an (58:11), na kuwa Makhilifa wa Allah katika jamii.

(ii) Kutumia Lugha Nyepesi Inayofahamika kwa Wanafunzi.

Mwalimu anapofundisha somo lolote lisilokuwa lugha, lengo lakesikufundishalugha inayotumika kufundishia bali lengo lake ni kumuwezesha mwanafunzi kubaini dhana (concepts) za mada husika. Hivyo ni wajibu wake kutumia lugha nyepesi na inayofahamika kwa wanafunzi wake.

Ni katika maelekezo ya Allah (s.w) kuwa tunapofikisha ujumbe wa msingi kwa watu tuufikishe kwa lugha zao, kwani Yeye Mwenyewe (s.w) ndivyo anavyofanya katika kuwafikishia ujumbe Waja wake.

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ رَّسُولٍ إِلَّا بِلِيْسَانٍ قَوْمِهِ لِتَبَيَّنَ لَهُمْ فَنِعْمَالُ اللَّهِ مَنْ يَشَاءُ
وَيَهْدِي مَنْ يَشَاءُ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

(4)

“Na hatukumpeleka Mtume yejote isipokuwa kwa lugha ya watu wake ili apate kuwabainishia. Kisha Mwenyezi Mungu anamuacha kupotea Amtakaye (kwa kuwa mwenyewe hataki kuongoka), na humuongoza Amtakaye. Naye ni Mwenye nguvu (na) Mwenye hikima” (14:4).

Kwa mnasaba wa aya hii ni jambo la busara na hekima kwa hapa Tanzania kuwafundisha watu Maarifa ya Uislamu kwa Kiswahili au,kwa lugha ya kabile husika ikibidi, kuliko kutumia kiarabu au lugha nyingineyo ya kigeni isiyofahamika vyema kwa wanafunzi unaowafundisha.

Ukirejea historia jamii yetu ya Waislamu kuwa hivi ilivyo, imechangiwa kwa kiasi kikubwa, kwa kutumia lugha ya kiarabu, isiyojulikana kwa watu, kuwa ndio lugha pekee ya kufundishia Uislamu. Mpaka hivi leo kuna baadhi ya Waislamu, tena wanachuoni, wanaoamini kwamba mtu hawezি kupata Elimu ya Mwongozo (Maarifa ya Uislamu) bila kutumia lugha ya kiarabu.

(iii) Kufafanua mada kwa aya au Hadith

Mwalimu Muislamu anawajibika kuzibaini aya za Qur'an na Hadithiza Mtume (s.a.w) zinazolandana na kila mada ya somo lake. Kwa mfano, Mwalimu wa "Biology" anapofundisha mada ya "Cell" ya wanayama na ya mimea na kuonesha kuwa asilimia 75% ya sehemu za "cell" ni maji, ni vema akalithibitisha hilo kwa aya ifuatayo:

أَوَلَمْ يَرَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَنَّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ كَانَتَا رَتْقًا فَفَتَّقْنَاهُمَا
وَجَعَلْنَا مِنَ الْمَاءِ كُلًّا شَرْبًا حَتَّىٰ أَفْلَأَ يُؤْمِنُونَ ﴿٢١﴾

"Je! Hawakuona wale waliokufuru ya kwamba mbingu na ardhi vilikuwa vimeambatana, kisha tukaviumbunga (Tukavipambanua). Na Tukafanya kwa maji kila kitu kilicho hai. Basi je, hawaamini?" (21:30).

Aya hii inasisitiza kuwa kila kitu kilicho hai kimeumbwa na Allah(s.w) kutokana na maji.

Takriban kila mada kuu tunayoisoma katika elimu ya mazingira (Biology, Chemistry, Physics, Geography, History, Luga, Biashara, Siasa, n.k.), ina aya ya Qur'an au Hadith inayoifafanua.

(iv) Kutoa na kutumia mifano na vielelezo vya Kiislamu.

Mwalimu Muislamu ajijengee tabia ya kutumia vielelezo na mifano hai ya maisha ya Kiislamu katika kukazia mada anayoifundisha pale panapohitaji mifano au vielelezo. Kwa mfano Mwalimu wa Hisabati anayefundisha mada ya "Uwiano" (ratios), atoe mifano na maswali ya kugawa Mirath kwa wenye mafungu; kama vile:

“Baada ya Amina bint Hassan kufariki na kuacha shs. 20,000,000 na warithi wafuatao:

- (i) Mumewe – $\frac{1}{4}$ ya mali ya urithi,
- (ii) Mama mzazi – $\frac{1}{6}$ ya mali ya urithi,
- (iii) Watoto watatu wa kiume watakaogawana mali itakayobakia baada ya kutoa fungu la baba na bibi yao; mgawie kila muhusika haki yake ya urithi.

(v) Kuleta Mazingatio ya Allah (s.w) Kupitia Mada Unazo Fundisha.

Mwalimu Muislamu anatakiwa ajitahidi kuwawezesha wanafunzi wake kumjua Allah (s.w) na kumcha ipasavyo kupitia mada mbalimbali za somo lake. Kwani Allah (s.w), anatufahamisha kuwa, watu wanaozama katika fani mbalimbali za elimu ya mazingira, ndio wanaoweza kumfahamu vilivyo na kumuabudu inavyostahiki:

الَّمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ أَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجْنَا بِهِ ثَمَرَاتٍ مُّخْتَلِفَةً لَوْنُهَا
وَمِنَ الْجِبَالِ جَدَدٌ بَيْضٌ وَحُمُرٌ مُّخْتَلِفُ الْوَانُهَا وَغَرَابِيبُ سُودٌ
وَمِنَ النَّاسِ وَالدَّوَابِ وَالْأَنْعَمِ مُخْتَلِفُ الْوَانُهُ وَكَذَلِكَ إِنَّمَا يَحْشِى اللَّهُ
مِنْ عِبَادِهِ الْعَلَمَتُو إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ غَفُورٌ

Je! Huoni kwamba Mwenyezi Mungu ameteremsha maji toka mawinguni! Na kwayo Tumeyatoa matunda yenyе rangi mbali mbali. Na katika milima imo mistari myeupe na myekundu yenyе rangi mbali mbali, na (mingine) myeusia sana. Na katika watu na wanyama wanaotambaa na wanyama (wengine), pia rangi zao ni mbali mbali. Kwa hakika wanaomwogopa Mwenyezi Mungu mionganini mwa waja Wake ni wale wataalamu (wanavyouini). Bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Msamehevu” (35:27-28)

Aya hizi zinasisitiza kuwa mtu akizama kitaaluma katika fani mbali mbali za elimu ya Mazingira anayakinisha kuwepo Allah (s.w) kwa upeo mkubwa.

(vi) Kukosoa Nadharia Potofu

Mfumo wa elimu wa Kikafiri upo pale kwa lengo la kuwaongoza watu kutoka kwenye nuru (Uislamu) na kwenda kwenye giza (Ukfiri) – Qur'an (2:257). Kwa kujua hili Mwalimu Muislamu awe makini katika kufuata mitaala ya kitwaghuti iliyopo pamoja na vitabu nya kiada masomo mbali mbali.

Pale ambapo katika vitabu nya kiada imetumika mifano au vielelezo vinavyokwenda kinyume na Uislamu, Mwalimu Muislamu hanabudi kuubainisha na kuukosoa upotofu ule na kutoa mifano au vielelezo mbadala vyenye muelekeo wa Kiislamu.

Kwa mfano katika mitaala ya mfumo wa elimu wa Tanzania, katika somo la Historia, inafundishwa nadharia ya Charles Robert Darwin inayodai kuwa asili ya mwanaadamu ni Sokwe. katika kufundisha mada hii ya “asili ya mwanaadamu” (The Origin of Man), Mwalimu Muislamu hanabudi kukosoa nadharia hiyo kwa kutumia hoja na kisha kuonesha asili sahihi ya mwanaadamu kwa kurejea Qur'an.

Pia historia ya Tanzania bara na visiwani imepotoshwa ili mchango wa Uislamu na Waislamu wakupigania uhuru usionekane badala yake ioneokane kuwa ukoloni uliombatana na ukristo ndio uliowaokoa watanzania kutokana na utumwa ulioendeshwa na waaarabu waliokuwa ni waislamu.

Zoezi la Tisa

1. Kwa kurejea Qur'an onesha kuwa elimu ya mwongozo na mazingira imeambatanishwa na jukumu kuu la mwanaadamu la kuwa Khalifa katika ardhi.
2. (a) "Soma kwa jina la Mola wako aliyeumba" (96:1)

Nini maana ya "Soma kwa jina la Mola wako" ?

- (b) Ni vipi utafundisha elimu ya mazingira kwa lengo la kuumuandaa Khalifa wa Allah(s.w)
3. (a) Ni vipi utaleta mazingatio ya Allah(s.w.) katika kufundisha somo la "**geography**" katika kiwango cha sekondari.
(b) Katika kufundisha somo la lugha ya kiingereza au kiswahili, toa mifano miwili na vielelezo viwili vyatikiislamu.
4. Eleza ni vipi utawaandaa wanafunzi wako kusoma kwa lengo la kuwa makhalifa wa Allah(s.w) katika jamii.



سُبْحَانَكَ لَا يَعْلَمُ لَنَا إِلَّا مَا عَلِمْتَنَا إِنَّكَ أَنْتَ الْعَلِيمُ الْحَكِيمُ


..... Utukufu ni wako (Allah)! Hatuna elimu isipokuwa ile uliyotufundisha, bila shaka wewe (Allah) ndiye mjuzi na ndiye mwenye hikima(2:32)